Kiswahili

السواحلية

Maktaba ya Kielimu ya Sheikh Dkt. Haytham Sarhan

المكتبة العلمية للشيخ د. هيثم سرحان

Mkusanyiko wa vitabu na maelezo ya kielimu ya Sheikh Dkt. Haytham bin Muhammad Sarhan, unaojumuisha vitabu vitatu muhimu:

1. Sharhi ya Masomo Muhimu kwa Kila Muislamu
2. Huu Ndio Uislamu
3. Vigawanyo na Misingi (Kanuni) za Kitabu cha Al-Qawl Al-Mufid katika Sharhi ya Kitabu cha Tawhid

Mkusanyiko huu unalenga kuwasaidia Waislamu kujifunza misingi ya dini ya Kiislamu, Aqidah sahihi, Tawhid, ibada na mafundisho muhimu ya Kiislamu kwa njia rahisi, iliyo wazi na yenye mpangilio mzuri.

Sheikh Dkt. Haytham bin Muhammad Sarhan alikuwa mwalimu katika Msikiti wa Mtume (Al-Masjid an-Nabawi) na Msikiti wa Quba. Kwa sasa, yeye ni msimamizi wa kielimu wa taasisi ya masomo ya mbali ya Mahad Sunnah (معهد السنة).

معهد السنة
Mahad Sunnah

Tovuti Rasmi:
mahadsunnah.com

MAFUNZO MUHIMU KWA UMMAH MZIMA

SHEIKH ABDULAZIZ BIN ABDILLAHI BIN BAAZ

USHEREHESHAJI WA MAFUNZO MUHIMU KWA UMMAH MZIMA

MTUNZI

SHEIKH ABDULAZIZ BIN ABDILLAHI BIN BAAZ
(Allah amrehemu na amweke pahala pema peponi)

MSHEREHESHAJI

SHEIKH HAITHAM BIN MUHAMMAD JAMIL SARHAN
(Aliyekuwa mwalimu kwenye chuo cha Haram kwenye Msikiti wa Mtume Madinah na pia msimamizi wa tovuti ya elimu ya Attasseel)
http://attasseel-alelmi.com
(Allah amsamehe na wazazi wake na waliohusika katika uandalizi wa kitabu hiki)

Chapa hii imetolewa kama waqf kwa ajili ya Allah
Kimechapishwa kwa udhamini wa Fatuma bint Jeilan bin Farihah (Allah amrehemu)

KIMEFASIRIWA KWA KISWAHILI NA
SULEIMAN MUHAMMED
Mwanafunzi Mkenya wa Chuo Kikuu cha Madinah, KSA.

CHAPA CHA KWANZA

Haki zote zimehifadhiwa

Anayetaka kutoa chapa au kukifasiri kwa lugha nyingine kwa lengo la kukigawanya bure baada ya kupata idhini kutoka kwa mtunzi basi awasiliane na

islamtorrent@gmail.com

Kitengo cha Ujumbe

Sharh ya Utangulizi wa Mtunzi

Amesema Sheikh Abdulaziz bin Abdillahi bin Baaz, Allah amrehemu:

Bismillahi Rahmani Rahim

Shukrani zote ni zake Allah Mola wa walimwengu, na mwisho mwema ni kwa wacha Mungu. Kisha rehema na amani zimwendee Mja wake na Mtume Wake nabii wetu Muhammad, na waliomfuata na Sahaba zake kwa jumla.

Baada ya hayo:

Hakika haya ni maneno yaliyofupishwa katika kubainisha baadhi ya mambo yanayolazimu ummah wote kuyatambua katika Uislamu, nimekiita:

MAFUNZO MUHIMU KWA UMMAH WOTE

Namuomba Allah anufaishe nacho Waislamu na aitakabali kutoka kwangu, hakika yeye ni Mkwasi Mkarimu.

Abdulaziz bin Abdillahi bin Baaz

Mbona tunakisoma kitabu cha Mafunzo Muhimu?

Tunakisoma kwa sababu ni muhimu kama alivyokiita Mtunzi na Maulamaa wengi wakakihusia kusomwa.

Na yeyote akiuliza: Hiki ni kitabu cha ummah mzima, na mimi ni mwanafunzi wa elimu ya dini, cheo changu kiko juu kuliko waliobaki katika jumla ya ummah.

Jibu: Tutamuuliza kilichoko ndani ya kitabu hiki. Akishindwa kulijibu basi jumla ya ummah waliobaki ni bora kumliko yeye. Na yampasa mwanafunzi wa elimu awe mnyenyekevu na wala asiwe ni mwenye kiburi kwenye elimu na maulamaa. Na afuate mkondo wa maulamaa waliobobea.
Na katika (Sahih Bukhari): Amesema Mujahid: ***Hatopata elimu mwenye haya na mwenye kiburi***.

Ni yapi yaliyomo katika kitabu cha Mafunzo Muhimu?

- Njia za wema waliotangulia katika kuisoma Kur'ani, kuihifadhi, kuizingatia na kuitendea kazi
- Kubainisha Uislamu, Imani, Ihsani, Tauhidi na aina za Shirki
- Kubainisha Sala
- Kubainisha Wudhuu
- Kusifika kwa nidhamu za kidini na kuwa na tabia na adabu njema za Kiislamu
- Kutahadhari na Ushirikina na aina za Maasi
- Maandalizi ya maiti, kumswalia na kumzika.

Mbona maulamaa wengi huanza uandishi wao kwa: Bismillahi Rahmani Rahim?

Kuiga mfumo wa Kur'ani Tukufu, Manabii na Mitume, rehema na amani ziwe juu yao	Kuitekeleza hadith inayosema: "***Kila jambo lenye zao ambalo halitaanza kwa jina la Allah basi limeporomoka***" Japo hadith yenyewe ni dhaifu.	Kuiga Maulamaa wema waliotangulia, Allah awarehemu.	Kwa matarajio ya kupata mema na baraka kwa kuanza kwa jina la Allah aliyetukuka.

SOMO LA KWANZA

SURATUL FATIHAH NA SURAH ZINGINE FUPI

Suratul Fatihah na surah zingine fupi, kuanzia Suratul Zalzala mpaka Suratu Naas kwa udhibiti, kurekebisha usomaji, kuhifadhi na kusherehesha yanayopaswa kufahamika.

UFAFANUZI

Maanake aihifadhi – kama walivyokuwa wema waliotangulia – kila siku aya kumi pamoja na kusoma tafsiri zake kuanzia tafsiri za mukhtasar kwa mfano Tafsiri ya Abdurahman Saadiy, Allah amrehemu na amsamehe madhambi yake. Ajifunze nacho na akitendee kazi.

MWANAFUNZI ANAFAA KUANZA KWA TAFSIRI IPI?

Mwanafunzi wa elimu ya dini anahusiwa aanze kwa ((Taisiril Karimi Rahman fii Tafsiri kalaamil Mannan)) cha Sheikh Abdurahman bin Nassir As-Saadiy, Allah amrehemu.

MBONA MWANAFUNZI ANAFAA KUANZA NACHO?

- Maulamaa wengi wamekihusia na wakakifanyia uchambuzi mwingi
- Kimefanywa mukhtasar basi kinaendana na hali ya yule anayeanza
- Sentensi zake ni nyepesi na wazi, hakuna uzito ndani yake
- Kinasaidia kuifanyia Kur’ani kazi kwa uwezo wa Allah
- Mtunzi wa kitabu hicho amezingatia sana pande ya Tauhidi

AINA ZA WATU KATIKA KUAMILIANA NA KUR'ANI

Watu wamegawanyika katika kuamiliana na Kur'ani makundi matatu

WAADILIFU

Hiki ni kikundi kinachodumu katika kuisoma Kur'ani, kuhifadhi, kuzingatia na wanamuomba Allah kuwawezesha kuitekeleza kwa vitendo.

Na hii ndio ilikuwa hali ya wema waliotangulia

WASIOZINGATIA

Hawa ni wale wanaosoma na kuhifadhi bila mazingatio wala vitendo

WALIOIHAMA

Hiki ni kikundi kilichoihama Kur'ani.

Na kuihama Kur'ani inakuwa kwa mambo yafuatayo:

- Kutoisoma
- Kutohifadhi
- Kutozingatia
- Kutofanyia kazi
- Kutojitibu nayo kwa maradhi ya

Anasema Allah, "**Na atasema mtume (siku ya kiyama): ewe Mola wangu, hakika ya kaumu yangu waliihama hii Kur'ani.**" na amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, akiashiria kiongozi wa kikundi cha watu walioenda kinyume na mafunzo yake, "*hakika katika kizazi chake watatoka watu wanaosoma Kur'ani na wala haivuki kinywa chao. Watawaua Waislamu na kuwaacha wale wanao abudu masanamu. Na hakika watatoka katika Uislamu kama vile mshale utoka kwenye upinde. Lau ningefikia zama zao ningewapiga vita vikali.*"

Chemichemi kutoka kwa kitabu cha Tafsiri cha Sheikh Abdurahman bin Nassir As-Saadiy, Allah amrehemu na masuali juuya hayo.

[TAFSIRI YA SURATUL FATIHAH]

(Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah)

(1). Bismillahi Rahmani Rahim. (2). Alhamdu Lillahi Rabbil Alamin. (3). Arrahmani Rahim. (4) Maliki yaumid diin. (5). Iyyaka na'budu wa iyyaka nasta'iin. (6). Ihdinaa swiratwal mustaqim. (7). Swiratwa ladhina an amta aleihim, ghairil magh-dhubi aleihim wa la dhwaalliin.

(**Aya 1**): Surah hii imeanza kwa kila jina lake Allah. Kwa sababu Allah ni neno linalokusanya majina yote mazuri yake Allah. Jina **Allah** linamaanisha anayestahiki kupwekeshwa kwenye ibada, kutokana na sifa za ukamilifu anazozimiliki katika uungu Wake. (**Ar-Rahmani Ar-Rahim)** haya ni majina mawili Yake Allah ambayo yanaonyesha kuwa Allah ametakasika na anasifika kwa upana wa rehema inayopenya kwa kila kiumbe kilichoko hai. Na akaiwekea fungu bora maalum aliyowaandikia waja Wake waumini walioiga mienendo ya Manabii an Mitume; hawa watapata fungu maalum ya rehema ambayo imeandaliwa rasmi kwa ajili yao.

Na utambue kwamba miongoni mwa misingi waliokubaliana wema waliotanguliwa na wanazuoni wote ni; kuiamini majina yake Allah na sifa Zake na kanuni za sifa hizo. Kwa mfano: wanaamini kuwa Allah ni mwenye rehema, mwenye kurehemu; anasifika kwa rehema kwa kila kiumbe, basi kutokana na hayo athari na matokeo ya rehema Zake tunapata neema. Na vile vile kwa majina Yake yaliyobaki.

Husemwa katika jina Lake, **Mjuzi wa yote:** Allah ni mwenye elimu wa kila kitu. **Mweza:** mwenye uwezo juu ya kila jambo.

(**Aya 2**): *Alhamdu Lillahi* **(Shukrani zote ni Zake Allah):** Ametukuka na ametakasika Allah kwa kila sifa ya ukamilifu, na kwa matendo Yake ambayo yako baina ya fadhila na uadilifu; ametakasika Allah kwa kila namna.

Rabbil Alamin **(Mola wa walimwengu):** Rabb inamaanisha Mola. Rabb kwa asili ya lugha ya Kiarabu inamaanisha mlezi. Kwa hiyo Allah ni Mlezi wa vyumbe vyote; kwa kuviumba, kuviandaa, kuvineemesha kwa neema kubwa ambazo lau zingekosekana, ingepelekea kukosekana maisha. Kila neema inatoka kwa Allah. Na malezi ya Allah kwa vyumbe vyake yamegawanyika aina mbili:-

1. **Malezi ya Jumla:** Haya ni malezi ambayo Allah amewapa vyumbe wote; kwa kuwaumba, kuwaruzuku na kuwaongoza kwa kila lenye maslahi kwao katika maisha yao ya Duniani.
2. **Malezi Maalum:** Haya ni malezi maalum kwa wanaomcha Allah: Allah anawalea malezi maalum katika Imani, kuwajaalia ufaulu, kuwapa ukamilifu wa Imani na kuwaepusha na misukosuko, dosari na vizuizi baina Yake na wao. **Uhalisia wa Malezi Maalum:** Kuwawezesha katika kila kheri na kuwaepusha na kila shari. Na huenda hii ndio siri katika dua za Manabii kutumia kwao neno Rabb**;** kwa sababu haja zao zote zilikuwa katika malezi maalum. Basi *Rabbil Alamin* inaonyesha kumpwekesha Allah katika *uumbaji, uendeshaji, neema, ukwasi wake Allah na ufakiri wa vyumbe kwa kila njia.*

(**Aya 4**): *Maliki yaumid diin* **(Mfalme wa Siku ya Malipo):** Malik inamaana ya mfalme. Hii inaonyesha kuwa Allah anasifika kwa ufalme bila mipaka; ufalme ambao ana uwezo wa kuamrisha, kukataza, kulipa na kuadhibu bila mipaka. Anatawala katika ufalme Wake kwa uhuru mkamilifu wa utawala. Kisha Allah akaegemeza ufalme kwa siku ya malipo (Kiyama) ambayo ni siku watakayolipwa wanadamu kwa kila walilotenda ya mema na uovu. Ni siku ambayo itadhihirika kwa vyumbe wote ukamilifu wa ufalme Wake Allah, uadilifu Wake, Hukumu Zake na mwisho wa umiliki wa vyumbe. Siku hiyo watakuwa hali sawa wafalme na raia, watumwa na waliokuwa huru; wote watanyenyekea utukufu Wake Allah wakisubiri malipo ya yale waliyoyatenda, wakitarajia thawabu Zake Allah, wakihofia adhabu Yake. Ndiposa Allah akaegemeza ufalme Wake kwa kutaja siku ya malipo.

(**Aya 5**): *Iyyaka na'budu wa iyyaka nasta'iin* **(Ni Wewe tu tunakuabudu na ni Wewe tu tunakutaka msaada):** Maanake: Tunakupwekesha ewe Allah kwa ibada na kutaka msaada. Kwa sababu katika ufundi wa lugha ya Kiarabu, neon **Iyyaka** inapotangulizwa mbele ya kitendo inakuwa na maana ya kupwekesha kitu kwa hicho kitendo.

Ibada ni neno linalokusanya kila jambo ambalo Allah analipenda na analiridhia kutokana na vitendo na kauli zilizo wazi na zilizofichika.

Kumtaka Allah msaada ni kumtegemea Allah katika kuleta manufaa na kuzuia madhara pamoja na kuwa na imani ya kufikia hayo malengo.

Kutekeleza ibada na kumtaka Allah msaada ndio njia ya kuweza kupata furaha na kuongoka kutokana na aina zote za shari; hakuna njia ya kuongoka isipokuwa kwa kutekeleza ibada na kumtaka Allah msaada. Na ibada inakuwa yenye mazingatio ikifanywa kutokana na mafunzo ya Mtume, rehema na mani ziwe juu yake, na ikikusudiwa radhi Zake Allah pekee. Kwa kuzingatia haya mawili, ibada inakuwa ibada sahihi. Kisha Mtunzi akataja kumtaka Allah msaada baada ya kutaja ibada, pamoja na kuwa inaingia kwenye ibada, kwa sababu mja anahitaji msaada wa Allah katika kila ibada; na akiukosa msaada wa Allah hatoweza kufikia matakwa yake katika kutekeleza maamrisho na kuepuka makatazo.

(**Aya 6**): *Ihdinsa Swiratwal mustaqiim* **(Tuongoze kwenye njia iliyonyooka):** Maana ya aya: tuonyeshe, tueongoze na utuwezeshe kwenye njia iliyonyooka; njia iliyonyooka ni njia iliyo wazi na yenye kumpeleka mja kwa Allah na pepo Yake, na hii inakuwa kwa kuijua haki na kuitendea kazi. Tuongoze kwenye njia na tuongoze ndani ya njia. Kuongozwa kwenye njia ni ni kushikamana na dini ya Uislamu na kuikufuru dini zingine zote. Na kuongozwa ndani ya njia ni kuongoka katika mambo yote ya kidini, kielimu na vitendo. Na hii aya ni dua iliyokusanya vyote vya muhimu na yenye manufaa zaidi. Ndio maana imewajibika juu ya kila mwanadamu kumuomba Allah katika kila rakaa ya swala yake kwa udharura wake. Na hii njia ni

(**Aya 7**): *Swiratwa ladhina an amta aleihim* **(Njia ya wale uliowaneemesha):** njia ya walioneemeshwa katika manabii, wakweli, mashahidi na wema.

Ghairil **(sio njia ya wale)** *magh-dhubi aleihim* **(uliowakasirikia):** wale waliojua haki na wakaiwacha kama Mayahudi na mfano wao. Na wala sio njia ya *Adh-dhwalliin* **(waliopotea):** wale waliowacha haki kwa ujahili na upotovu kama Wakristo na mfano wao.

Hakika ya hii surah, pamoja na ufupisho wake, imekusanya mambo ambayo surah nyingine za Kur'ani hazijakusanya. Ndani yake mnapatikana aina tatu za Tauhidi: **1**. Kumpwekesha Allah katika Malezi Yake kama ilivyoko kwenye kauli Yake *Rabbil alamin***. 2.** Kumpwekesha Allah katika uungu Wake – ibada Yake –kama ilivyo kwenye kauli ***Yake Iyyaka na'budu wa iyyaka nasta'iin*. 3.** Kumpwekesha Allah katika majina Yake na sifa Zake; kumthibitishia sifa za ukamilifu ambayo amejithibitishia na amemthibitishia bila ya kuzigeuza, kuzipinga, kuzishabihisha wala kuzitolea namna. Na hii tumeipata kwenye kauli Yake *Alhamdu***.**

Pia surah hii imebeba ndani yake uthibitisho wa utume katika kauli Yake *Ihdinas Swiratwal mustaqiim***.** Maana hili haliwezi timia bila Mtume wa kuelekeza kwenye njia hii ilinyooka.

Pia ndani yake kuna uthibitisho wa malipo ya matendo kama ilivyo kwenye kauli Yake *Maliki yaumid diin***,** na hakika ya malipo yatakuwa kwa uadilifu.

Pia imepatikana ndani yake uthibitisho wa Qadar na kwamba mja ni mtendaji.

Pia imewaponda watu wote waliozama katika uzushi na upotovu kwa kauli Yake *Ihdinas Swiratwal mustaqiim;* kwa sababu ndio njia kuijua haki na kuitendea kazi na yeyote mzushi na mpotovu yupo kinyume na haya.

Pia imepatikana ndani yake maamrisho ya kuipwekesha dini kwa Allah katika kumuabudu Yeye pekee na kumtaka Yeye pekee msaada kama ilivyo kwenye kauli Yake *Iyyaka na'budu wa iyyaka nasta'iin***.**
Shukrani zote zimrudie Allah, Mola wa walimwengu.

[TAFSIRI YA AYATUL KURSI]

*Allahu laa ilaha illa huwal Hayyul Qayyum, laa ta'khudhuhu sinatu wa laa naum. Lahu maa fis samawati wa maa fil ardh. Man dha ladhii yashfa^u ^indahu illa bi idhnih. Ya^lamu ma baina aidiihim wa maa khalfahum. Wa laa yuhitwuuna bishein min ^ilmihi illa bimaa shaa. Wasia^ kursiyyuhus samawati wal ardh. Wa laa yauduhu hifdhuhumaa wa huwal ^Aliyyul ^Athwiim (***Baqarah 255***).*

Ameelezea Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuwa hii aya ndiyo aya kubwa katika Kur'ani; kutokana na maana za Tauhidi, ukubwa wa Allah na sifa za ukamilifu zinazopatikana ndani yake. Ameelezea Allah kuwa: *Allah* ambaye anastahiki maana zote za Uungu, na kuwa hakuna apasaye haki ya kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye Allah pekee Yake; basi kuabudu miungu mingine hiyo ni ibada potovu. Na ya kuwa Yeye Allah ni *Al-Hayyu* ambaye anamiliki sifa zote za maisha kamilifu kama kusikia, kuona, uwezo, kutaka na sifa zingine zinazohusiana na Dhati Yake, kama vile Yeye ni *Al-Qayyum* sifa ambayo inabeba sifa zote za vitendo; kwa sababu *Al-Hayyu* ni Yule anayejitegemea mwenyewe wala hana haja kumtegemea kiumbe yeyote. Ameumba viumbe waote vyote na akavipa kila wanavyohitaji katika maisha. Allah ni qayyum ambaye amtakasika katika vitendo vyake na ameepukana na sifa za upungufu, ndio maana akasema *laa ta'khudhuhu sinatu* (hasinzii) *wa laa naum* (haimchukui usingizi). Sifa ya kusinzia na kulala ni sifa mbili zinazompata kiumbe ambaye hupatwa na udhaifu, unyonge na uchovu na wala hazimpati mwenye sifa ya Utukufu, Ukubwa na Uwezo.

Kisha Allah akaelezea kuwa anamiliki yote yaliyomo mbinguni na ardhini, kila kitu ni mtumwa wa Allah na milki yake wala hakuna hata kimoja kinachoepuka kutoka kwa ufalme Wake kama anavyosema katika Kur'ani (*Kila aliye mbinguni na ardhini atamjia Allah siku ya Kiyama akiwa mja*). Allah ndiye mmiliki wa vyote vilivyomo. Yeye Allah pekee ndiye mwenye sifa ya ufalme, uendeshaji, uwezo na utukufu. Na katika ukamilifu wa ufalme Wake hakuna yeyote *yashf^u ^indahu* (**anayeweza kumtakia yeyote maombezi**) *illa biidhnihi* (**isipokuwa kwa idhini Yake**). Kila muombezi ni mwelekezi ni mja wa Allah na yupo katika ufalme Wake na wala hatokubaliwa kukadimisha maombezi yake ila kwa idhini Yake. Anasema Allah katika Kur'ani (*Hakika maombezi yote ni*

.
Nayo ni Yake ufalme wa mbingu na ardhi). Na Allah hatompa yeyote idhini ya maombezi isipokuwa yule aliyemridhia, na hatomridhia yeyote isipokuwa mwenye kumpwekesha katika Tauhidi na akawafuata Mitume Wake Allah. Basi asiyekuwa na hizi sifa hatopata fursa ya maombezi siku ya Kiyama.
Kisha Allah akaendelea kuelezea kuwa elimu Yake ni pana yenye kukusanya kila kitu na kuwa Yeye ni mjuzi wa yale yote yanayowahusu viumbe katika mambo ya mustakbali wao na yale *wa maa khalfahum* (**yaliyopita**) katika mambo yaliyopita yasiokuwa na mipaka; na wala hakuna lolote linalomponyoka (*Allah ni mjuzi wa yote yanayodhihirika machoni na yaliyofichika vifuani*) na wala hakuna kiumbe chochote kinachoweza kuitambua elimu na ujuzi wa Allah hata lepe *illa bimaa shaa* (**alichowajaalia Allah**) katika hayo; nayo ni yale aliyowavumbulia katika mambo ya sharia na Qadar (nacho ni kipande kidogo sana ukilinganisha na elimu ya Allah kama walivyomsifu malaika na Mitume (*Umetukuka. Hatuna elimu isipokuwa yale uliyotuelimisha*)
Kisha Allah akaelezea utukufu Wake na kuwa kursi Yake imepiku kwa ukubwa mbingu na ardhi, pamoja na kuwa amezihifadhi mbingu na ardhi na wote waliyomo ndani ya mbingu na ardhi amewahifadhi kwa njia na nidhamu ambazo amewajaalia. Lakini pamoja na hayo, haimshindi kuhifadhi mbingu na ardhi kwa sababu ya ukubwa Wake, utukufu Wake, uwezo Wake na upana wa hekima katika hukumu Zake, naye ni *Al-Aliyyu* (**Yupo juu**) katika dhati Yake na katika ukubwa Wake na Yupo juu ya viumbe wote na kila kilichopo kinamnyenyekea na kinajidhalilisha kwa *Al-Athwiim* (**Mtukufu**) aliyejumuisha sifa zote za kutakasika na kutukuka, ambaye nyoyo zinampenda, zinamtakasa nafsi na wanatambua wajuzi kuwa kila kitu pamoja na ukubwa wake ila kinanyenyekea kwake Allah.
Aya hii imekusanya maana kubwa ambayo inaifanya aya kubwa katika Kur'ani na ni haki ya kila mwenye kuisoma kwa mazingatio na ufahamu aijaze moyo wake kwa yakini, ujuzi na imani, na anakuwa amehifadhika kutokana na shari za shetani.

[TAFSIRI YA SURATU IDHAA ZULZILAT]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Madinah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Idhaa zulzilatil ardhu zilzaalahaa. (2). Wa akhrajatil ardhu athqaalahaa. (3). Wa qaalal insanu maa lahaa. (4). Yaumaidhin tuhaddithu akhbaarahaa. (5). Bianna rabbaka auhaa lahaa. (6). Yaumaidhin yasdurun naasu ashtaatan liyurau a^maalahum. (7). Famai ya^mal mithqaala dharratin khairai yarah. (8). Wa mai ya^mal mithqaala dharratin sharrai yarah.

(Aya 1-2): Anaelezea Allah kuhusu yale yatakayotokea Siku ya Kiyama na kuwa ardhi itatikiswa na kutetemeshwa kwa ushindo mkubwa utakaopelekea kuanguka kila jengo kilichopo ndani ya ardhi, na milima itaporomoka na kusawazishwa pasiwe na mnyanyuko wowote, *Wa akhrajatil ardhu athqaalahaa* (**Na itakapotoa ardhi mizigo yake**) katika maiti na madini.

(Aya 3): *Wa qaalal insaanu* (**atasema mwanadamu**) kwa anayoyaona katika hali ngumu ya dunia siku hiyo, *maa lahaa* (**ina nini**) leo dunia?

(aya 4-5): *Yaumaidhin tuhaddithu* (**siku hiyo itaelezea**) ardhi *akhbaarahaa* (**habari zake**) kwa iliyoshuhudia katika matendo ya wanadamu ya kheri na ya shari. Hakika ardhi itakuwa katika jumla ya mashahidi siku ya Kiyama. *Bianna rabbaka auhaa lahaa* (**kwa sababu Mola wako ameiamrisha**) ameiamrisha kuelezea vitendo vya waja.

(aya 6): *Yaumaidhin yasduru nnaasu* (**siku hiyo watu watatoka**) wametengana *liyurau a'maalahum* (**matendo yao**) waliyoyatenda ya mema na maovu.

(aya 7-8): *Famai ya'mal mithqaala dharratin khairan yarah. Wa mai ya'mal mithqaala dharratin sharran yarah* (**atakayetenda mema kadri ya punje basi atalipwa. Na atakayetenda uovu kadri ya punje basi atalipwa**) katika ya kheri na shari kwa sababu kila atakalofanya, kubwa na ndogo ataliona na atalipwa.

[TAFSIRI YA SURATUL AADIYAAT]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Wal aadiyaati dhwab-haa. (2). Falmuuriyaati qad-haa. (3). Falmughiiraati sub-haa. (4). Fa-atharna bihi naq'aa. (5). Fawasatna bihi jam-aa.
(6). Innal insaana lirabbihi lakanuud. (7). Wa innahu alaa dhaalika lashahiid.
(8). Wa innahu lihubbil khairi lashadiid. (9). afalaa ya'lamu idhaa bu'thira maa fil qubuur. (10).inna rabbahum bihim yaumaidhin lakhabiir.

(Aya 1): Ameapa Allah, aliyetukuka, kwa farasi; kwa yanayopatikana kwake ya dalili kubwa na neema zilizo wazi wakati wanapokabiliana na maadui; dalili na neema hizi zinaptika tu kwa farasi. Amesema, *wal aadiyaati dhwab-ha* (**naapa kwa farasi wendao mbio wakipumua**) farasi wanaowakabili maadui kwa kishindo.
(Aya 2): *Falmuuriyaati qad-haa* (**wakitoa moto kwa kupiga kwato zao chini**): kwa kwato zao wakikanyaga mawe wakitoa moto kwa kushambulia.
(Aya 3): *Falmughiiraati* (**wakishambulia**) adui *sub-haa* (**asubuhi**) na hili ni jambo la kawaida kuwa mashambulizi yanakuwa asubuhi.
(Aya 4-5): *Fa-atharna bihi* **(huku wakitimua)** kwa kuwashambulia maadui zao *naq-aa* (**vumbi**) na kuingia katikati ya majeshi ya maadui.
(Aya 6): Alichokiapia Allah ni *innal insaana lirabbihi lakanuud* (**hakika mwanadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola wake Mlezi**) mbanifu wa kheri. Katika maumbile yake mwanadamu nafsi yake hairuhusu kutekeleza haki na amana iliyo juu yake. Na hupata uzembe katika kutekeleza hayo isipokuwa yule ambaye Allah amemuongoza na kumuepusha na sifa hii ndiye atatekeleza haki.
(Aya 7): *Wa innahu alaa dhaalika lashahiid* (**na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo**) hakika ya mwanadamu ni shahidi juu ya tabia ya nafsi yake ya kutotekeleza haki na amana, wala hawezi likanusha. Kuna onyo kali kwa mwenye tabia hiyo.
(Aya 8): *Wa innahu* (**na hakika yeye**) mwanadamu *lihubbil khairi*(**katika kupenda mali**) yaani mali *lashadiid* (**ana nguvu**); ni mwingi sana wa kupenda mali. Na kupenda kwake mali zaidi ndio kumempelekea kutotekeleza haki na amana; ametanguliza matamanio yake juu ya majukumu yake ya kumridhisha Mola wake.
(Aya 9-10): Ndio maana Allah akasema kumuogopesha siku ya Kiyama *afalaa ya'lamu* (**kwani hajui**) huyu aliyeghurika *idhaa bu'thira ma fil qubuur* (**watakapofufuliwa walioko makaburini**) Allah atakapowatoa wafu makaburini kwa ufufuo *wa husswila maa fi ssuduur* (**na yakakusanywa yaliyomo vifuani**) yale yaliyokuwa yamesitiriwa nyoyoni katika mema na maovu yakawa dhahiri mbele ya viumbe wote.
(Aya 11): *inna rabbahum bihim yaumaidhin lakhabir* (**kwa hakika Mola wako Mlezi atakuwa na habari zao siku hiyo**) anayajua yaliyofichika na yaliyo wazi katika matendo ya mwanadamu na atawalipa kwa hayo siku ya Kiyama.

[TAFSIRI YA SURATUL QAARIAH]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Madinah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Alqaariah. (2). Malqaariah. (3). Wa maa adraaka malqaariah
(4). Yauma yakuunu nnaasu kalfaraashil mabthuuth. (5). Wa takuunul jibaalu kal-ihnil manfuush. (6). Fa ammaa man thaqulat mawaaziinuh.
(7). Fahuwa fii iishatin raadhwiyah. (8).wa ammaa man khaffat mawaaziinuh
(9). Faummuhu haawiyah. (10). Wa ma adraaka maa hiyah. (11). Naarun haamiyah

(Aya 1-3): *Alqaariah* (**inayogonga**) hii ni moja katika majina ya siku ya Kiyama. Imeitwa hivi kwa sababu inashtua kwa kugonga kwa matukio yake.

(Aya 4): *Yauma yakuunu nnaasu* (**siku ambayo watu watakuwa**) kwa sababu ya uzito wa siku hiyo *kalfaraashil mabthuuth* (**kama nondo waliotawanyika**) wakatapakaa hewani.

(Aya 5): Ama milima siku hiyo itakuwa *kal-ihnil manfuush* (**kama sufi zilizochambuliwa**) kwa udhaifu wake na kuelea hewani siku hiyo kwa amri ya Allah.

(Aya 6-7): *Fa ammaa man thaqulat mawaazinu* (**basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito**) kwa kuwa mema yake yakazidi maovu *fahuwa fii iishatin raadhwiya* (**huyo atakuwa katika maisha ya kupendeza**) ndani ya jannah.

(Aya 8-11): *Wa ammaa man khaffat mawaazinuh* (**na yule ambaye mizani yake itakuwa hafifu**) kwa kuzidi maovu yake kushinda mema *faummuhu haawiya* (**huyo maskani yake yatakuwa moto wa Haawiya**) makaazi yake. Haawiya ni katika majina ya jahanamu. Atatupwa ndani ya moto huo kwa uso wake ambao ni moto *haamiya* (**mkali**)

[TAFSIRI YA SURATU TTAKAATHUR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Alhaakumu ttakaathur (2). Hattaa zurtumul maqaabir
(3). Kallaa saufa ta'lamuun (4). Thumma kallaa saufa ta'lamuun.
(5). Kallaa lau ta'lamuun ilmal yaqiin. (6). Latarawunnal jahiim.
(7).Thumma latarawunnahaa ainal yaqiin. (8). Thumma latus-alunna yaumaidhin ani nnaiim.

(Aya 1): Anasema Allah huku akimkemea mwanadamu kwa kushughulika na mambo mengi na kuliacha jukumu lake la kumuabudu Allah; ambalo ni lengo la kuumbwa kwake *alhaakumu ttakaathur* (**kumekushughulisheni kutafuta wingi**); kuzidisha mali, watoto, marafiki, vyeo na mambo mengine yasiyo ya msingi.

(Aya 2): Kughafilika na kushughulika huku kumeendelea *hattaa zurtumul maqaaabir* (**mpaka mje makaburini/mfe**) basi hapo ndipo anagutuka na kukumbuka lengo lake. Allah ametumia neno ziara katika maisha ya barzakh (kaburini) kwa sababu ni kivukio kwenda maisha ya akhera kwa hesabu na malipo.

(Aya 3-6): Ndio maana akawapa ahadi kali *kallaa saufa ta'lamuun…….* (**Sivyo hivyo. Mtakujajua…..**) lau mwanadamu angelijua lililo mbele yake katika akhera basi angeliacha linalomshughulisha na kurudi kwenye ibada na matendo mema kwa wingi.

(Aya 7): *Thumma latarawunnahaa ainal yaqiin* (**tena bila shaka mtakuja liona kwa jicho la yakini**) kwa jicho la hakika

(Aya 8): *Thumma latus-alunna yaumaidhin ani nnaiim* (**tena bila shaka mtakuja ulizwa siku hiyo juu ya neema**) mlioneemeshwa nayo duniani. Je mlishukuru na mkatekeleza haki ya Allah pasina kuzitumia katika maasi? Au mlizikufuru na mkazitumia katika kumuasi Allah na wala hamkutekeleza haki za Allah katika neema hizo?

[TAFSIRI YA SURATUL ASR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Wal-asr. (2). Innal insaana lafii khusr. (3). Illa ladhiina aamanuu wa amiluu sswaalihaati wa tawaaswau bilhaqqi wa tawaaswau bisswabr

(Aya 1-3): Allah ameapa kwa asr (zama/muda) ambao ni usiku na mchana. Muda huu ndio pahala pa matendo ya mwanadamu. Allah amesema kuwa kila mwanadamu yupo kwenye aina zote za hasara isipokuwa mwenye sifa nne:-.

- **IMANI:** Anayemuamini Allah kwa yote aliyoamrisha kuaminiwa. Na imani haiwi bila ya elimu kwa sababu haitimii bila hiyo.
- **MEMA:** Anayetenda mema yaliyofichika na yaliyodhihirka katika kutekeleza haki za Allah na haki za waja za lazima.
- **KUHUSIANA HAKI:** Wakahusiana wenyewe kwa wenyewe katika jambo la haki ambalo ni imani na matendo mema.
- **KUHUSIANA SUBIRA:** Wakahusiana kufanya subira katika uchamungu, kutokana na maasi na katika mipango (Qadar) ya Allah.

Kwa kutekeleza mambo mawili ya mwanzo, mwanadamu atakuwa ameikamilisha nafsi yake na kwa kutenda mawili ya mwisho atakuwa amewakamilisha wenzake kuepuka hasara.

[TAFSIRI YA SURATUL HUMAZAH]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Wailun likulli humazatin lumazah. (2). Alladhii jama-a maalahu wa a-ddadah. (3). Yahsabu anna maalahu akhaladah. (4). Kallaa layumbadhanna fil hutwamah. (5). Wa maa adraaka mal hutwamah. (6). Naarullaahil muuqadah. (7). Allatii tattwaliu alal af-idah. (8). Innahaa aleihim mu'swadah. (9). Fii amadin mumaddadah.

(Aya 1): *Wailun likulli humazatin lumazah* (**Ole wake kila safihi msengenyaji**) hili ni onyo kali kwa wale wanaowaudhi na kuwaaibisha watu kwa vitendo na maneno. **Humaza** ni yule anayewaudhi watu kwa vitendo na **lumaza** ni anayeudhi kwa maneno.

(Aya 2): Na katika sifa za watu hawa, hawana linalowashughulisha zaidi ya kuchuma na kujumuisha mali huku wakipata furaha wanapozihesabu na wala hawazitumii katika yanayomfurahisha Allah.

(Aya 3): *Yahsabu* (**anadhani**) mwanadamu *anna maalahu akhladah* (**kuwa mali yake yatambakisha milele**) duniani. Ndio maana ikawa hamu yake kubwa ni mali na ubakhili na kuasahau kuwa haitomfaa katika maisha ya akhera na kwa hilo akawa ameiharibu akhera yake na mema yake.

(Aya 4-7): *Kallaa layumbadhanna* (**hakika huyo atavurumishwa**) kwa uso wake ndani ya *Hutwama* (**moto wa Hutwama**) ambao kwa ukali wake *tattwaliu alal af-idah* (**ambao unapanda moyoni**) inachoma mwili hadi ndani ya nyoyo.

(Aya 8): Pamoja na ukali wa joto la moto huu na hali ngumu ndani yake, watakuwa *innahaa aleihim mu'swadah fii amadin mumaddadah* (**hakiwa ndani ya moto huo watafungiwa kwenye nguzo zilizonyooshwa**) nyuma ya nguzo za milango yake wasiweze kutoka kwa hali yoyote ile.

[TAFSIRI YA SURATUL FIIL]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Alam tara kaifa fa-ala rabbuka bi-as-haabil fiil . (2). Alam yaj-al kaidahum fii tadhwliil. (3). Wa-arsala aleihim twairan abaabiil. (4). Tarmiihim bihijaaratim min sijjiil. (5). Faja-alahum ka-asfim ma'kuul.

(Aya 1-5): Je! Hukuona, katika mipango ya Allah na uwezo Wake mkubwa na dalili za kupwekeshwa Kwake na kusadikisha utume wa Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, alivyowafanya watu wa ndovu; ambao walikaribia Nyumba Yake tukufu na wakataka kuibomoa. Wakaandaa jeshi kubwa wakiwa na ndovu wakubwa kwenye jeshi lao kwa lengo la kuibomoa Kaabah. Wakaja kwa jeshi kubwa kutoka Yemen na Uhabeshi; jeshi ambalo halina mfano wake. Walipoukaribia Makkah – Waarabu hawakuwa na namna ya kukabiliana na jeshi hili – hapo Allah akawatumia ndege waliotapakaa wakiwa wamebeba mawe kutoka kwa moto. Wakaangushia mawe yale, yakakata miili ya kila aliyekuwepo kwenye jeshi lile, wakaganda na kuduwaa wakawa kama majani yaliyotafunwa yakatemwa. Na Allah akaizuia shari yao na kuwaadhibu kwa lengo lao bovu. Na kisa chao ni maarufu. Kilitokea mwaka ambao ndani yake alizaliwa Mtume Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake. Ikawa ni miongoni mwa mafunzo katika kulingania wale wenye malengo mabaya dhidi ya dini ya Allah.

[TAFSIRI YA SURATU QUREISH]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Li-iilaafi Quraish . (2). Iilaafihim rihlata sh-shitaai wa sswaiif. (3). Falya'budu u rabba haadhal baiit (4). Alladhii atw-amahum min juuin wa aamanahum min khauuf

(Aya 1-4): Wanasema wengi katika wanazuoni wa tafsiri: Allah aliangamiza jeshi la watu wa ndovu kwa sababu ya Qureish; amani yao na kuendeleza maslahi yao na nidhamu za safari zao kuenda Yemen msimu wa joto na kuenda ukanda wa Syria msimu wa baridi kwa lengo la kibiashara na kuchuma.

Basi Allah akawaangamiza waliowatakia shari na akaitakasa Nyumba Yake tukufu na kuiathimisha kwenye nyoyo zao. Ndio maana Allah akawaamrisha kumshukuru na kumpwekesha Allah kwenye ibada; Mola ambaye anawaruzuku kutokana na njaa na kuwaepusha na hofu. Kuepushwa kutokana na njaa na hofu ndio neema kubwa zaidi katika neema za dunia. Basi hatuna budi kumshukuru Allah kwa neema Zake zilizo wazi na zilizofichika.

[TAFSIRI YA SURATUL MAA^UUN]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Ara-aita lladhii yukadh-dhibu biddiin . (2). Fadhaalika lladhii yadu^ul yatiim.. (3). Wa laa yahudh-dhu alaa twa-aamil miskiin. (4). Fawailul lilmusswalliin. (5). Alladhiina hum an swalaatihim saahuun. (6). Alladhiina hum yuraa-uun. (7). Wa yamnauunal maa^uun.

(Aya 1): Anasema Allah huku akimkemea yule asiyetekeleza haki Zake na haki za waja *ara-aita lladhii yukadh-dhibu biddiin* (**Je. Umemwona anayekadhibisha malipo**); katika mambo ya kufufuliwa, hesabu, malipo na yale waliyokuja nayo Mitume.

(Aya 2): *Fadhaalika lladhii yadu^ul yatiim* (**huyo ndiye anayemsukuma yatima**) kwa kumfukuza kwa ukali bila kumhurumia. Hii ni kutokana na ugumu wa moyo kwa sababu hatarajii thawabu wala haogopi adhabu ya Kiyama.

(Aya 3): *Wa laa yahudh-dhu alaa twa-aamil miskiin* (**wala hahimizi kumlisha maskini**) na wala haihusii nafsi yake kutenda hilo.

(Aya 4-5): *Fawailul lilmusswalliin* (**basi ole wao wanaosali**) wale wanaopaswa kuhifadhi sala zao lakini wao *an swalaatihim saahuun* (**wanapuuza sala zao**) wamezipoteza, wamezichelewesha kutoka kwa muda wake na wakachelea katika kutimiza nguzo zake na mafunzo yake. Hili ni kutokana na kutozingatia maamrisho ya Allah. Kwa hiyo wakaipoteza sala ambayo ni ibada kubwa sana katika ibada za kimwili. Hawa watapata lawama na adhabu kali siku ya Kiyama.

(Aya 6-7): Allah amewasifu watu hawa kwa sifa ya kujionyesha katika ibada zao, ugumu wa moyo na kutokuwa na huruma kwa kauli yake *alladhiina hum yuraa-uun* (**ambao wanajionyesha**) katika ibada zao *wa yamnauunal maa^uun* (**na huku wanazuia msaada**); hawatoi chochote kile katika njia ya msaada wala zawadi wala mkopo. Hata vitu duni kama chumvi hawatoi kamwe.

Katika surah hii, Allah amehusia kuwalisha maskini, kuhusiana katika kulisha maskini, kusimamisha pamoja na kuhifadhi sala, kumpwekesha Allah katika ibada na kutojionyesha, kutenda mema na kusaidiana katika vitu vya haja na dharura.

[TAFSIRI YA SURATUL KAUTHAR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Innaa a'twainaakal kauthar . (2). Faswalli lirabbika wan-har. (3). Inna shaaniaka huwal abtar.

(Aya 1): Anasema Allah kumwabia Mtume Wake na kumkubusha neema Zake juu yake *innaa a'twainaakal kauthar* (**hakika tumekupa kheri nyingi**) na fadhila nyingi. Na katika kheri atakazompa siku ya Kiyama ni mto unaoitwa Kauthar: urefu wake ni mwendo wa mwezi mzima, upana wake ni mwendo wa mwezi mzima pia, maji yake ni meupe kushinda maziwa, matamu kushinda asali na vyombo vyake vya kunywea ni vingi mfano wa nyota angani. Atakayekunywa kutoka kwenye mto huo hatopata kiu kamwe.

(Aya 2): Na baada ya Allah kumtajia kheri na fadhila hizo, alimuamrisha kushukuru kwa kauli Yake *faswalli lirabbika wan-har* (**basi Sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi**). Allah alizitaja hizi ibada mbili kwa sababu ndizo ibada bora na kurbani bora; kwa sababu sala inapatikana ndani yake utulivu na unyenyekevu wa moyo na viungo na kuchinja kunapatikana ndani yake kujikurubisha kwa Allah kwa kitu bora anachokimiliki mwanadamu na kujiepusha na uroho na ubakhili.

(Aya 3): *Inna shaaniaka* (**hakika anayekuchukia**) na anayekukemea *huwal abtar* (**ndiye aliye mpungufu**) yaani amezuiliwa na kheri zote kwa kumchukia mbora wa viumbe ambaye amekamilika katika kumuabudu Mola wake.

[TAFSIRI YA SURATUL KAAFIRUUN]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Qul yaa ayyuhal kaafiruun . (2). Laa a'budu maa ta'buduun. (3). Wa laa antum aabiduuna maa a'budu. (4). Wa laa ana aabidum maa abadtum. (5). Wa laa antum aabiduuna maa a'budu. (6). Lakum diinukum wa liya diin

(Aya 1-6): Waambie makafiri kwa bayana kuwa *laa a'budu maa ta'buduun* (**siabudu mnachokiabuudu**) ili kujiepusha na ibada zenu fiche na za dhahiri *wa laa antum aabiduuna maa a'budu* (**wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu**) kwa kutompwekesha Allah katika ibada zenu. Kumuabudu kwenu pamoja na kumshirikisha na miungu mingine hakuitwi ibada.

Basi Allah akatenganisha baina ya vikundi hivi viwili kwa kauli Yake *lakun diinukum wa liya diin* (**nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu**).

[TAFSIRI YA SURATU NNASR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Madinah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Idhaa jaa-a nasrullaahi wal fat-h . (2). Wa-ra-aita nnaasa yadkhuluuna fii diinillaahi afwaajaa. (3). Fasabbih bihamdi rabbika wastaghfirhu, innahu kaana tawwaabaa.

(Aya 1-3): katika surah hii tukufu, kuna bishara, maamrisho kwa Mtume bishara likitimia, ishara na tanbihi kwa matokea ya hayo.

BISHARA: ni bishara ya nusra ya Allah kwa Mtume Wake na kufunguliwa kwa Makkah, na watu kuingia *fii diinillaahi afwaajaa* (**katika dini ya Allah kwa makundi**); watakuwa wengi sana katika waliozaliwa na waliosilimu baada ya kuwa maadui wa dini hii.

AMRI BISHARA IKITIMIA: Allah amemuamrisha Mtume Wake wakati bishara itatimia, azidishe shukrani, kusabihi na kumhidi Allah kwa neema hiyo.

ISHARA: hakika kutimia kwa bishara kunaashiria mambo mawili: (1) Nusra ya allah kwa dini itaendelea kwa kusabihi, kuhimidi na kuomba msamaha na kushukuru kwa wingi. Allah anasema, "*la-in shakartum la-aziidannakum*" (**Mkinishukuru nitawazidishieni**). Na hili lilitimia katika zama za makhalifa walioongoka na waliokuja baada yao katika ummah. Na hii nusra iliendelea hadi Uislamu ukafika pembe zote za dunia. Na ikaisha pindi ummah ulipoacha kutii maamrisho ya Allah na kutengana. Lakini nusra na kuhifadhi dini bado Allah amedhibiti. (2) Inaashiria kuwa kifo chake Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kilikuwa kimewadia. Kwa sababu katika Sunnah ya Allah ni kuwa hakuna kinachodumu katika walimwengu. Basi akaamrishwa kuhitimisha maisha yake kwa Sala na Hijja.

[TAFSIRI YA SURATUL MASAD]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Tabbat yadaa abii lahabin wa tabba . (2). Maa aghnaa anhu maaluhu wa maa kasaba (3). Sayaslaa naaran dhaata lahab. (4). Wamra'tuhu hammaalatal hatwab. (5). Fii jiidihaa hablun min masad.

Abu Lahab alikuwa ni ami yake Mtume. Na alikuwa mwenye maudhi na uadui mkubwa sana dhidi ya Uislamu na Waislamu; wala hakujali kuwa anahusiana na mtume kifamilia na ukoo. Basi Allah akamdunisha na kumdhalilisha hadi siku ya Kiyama kwa kusema: imeangamia mikono ya abu Lahab na kuzorota. Ambaye alikuwa akidhani kuwa mali aliyokuwa nayo itamnusuru siku ya Kiyama. Hakika ataingia jahanamu yeye na mkewe ambaye alishirikiana naye katika kumuudhi Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. Basi Allah akasema wataingizwa motoni yeye na mkewe ambaye atafungwa kamba shingoni kwa madhambi yake ambayo yatakuwa yamemzonga kama mbeba kuni.

[TAFSIRI YA SURATUL IKHLAAS]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Qul huwa Allahu ahad . (2). Allahu sswamad. (3). Lam yalid wa lam yuulad.
(4). Wa lam yakun lahu kufuwan ahad

(Aya 1): Waambie kwa kuamini na kuitikadi *huwa allahu ahad* (**Yeye Allah ni wa pekee**) ametukuka na anayepwekeshwa kwa kila kitu.

(Aya 2): *Allahu sswamad* (**Allah Mkusudiwa**) anayekusudiwa na kulengwa kwa mambo yote na haja zote za waja.

(Aya 3): Na katika ukamilifu wa sifa Zake *lam yalid wa lam yuulad* (**hakuzaa wala hakuzawa**) kwa sababu amejitosheleza.

(Aya 4): *Wa lam yakun lahu kufuwan ahad* (**wala hana anayefanana naye hata mmoja**) Katika majina yake, sifa Zake na katika vitendo Vyake. Ametukuka Allah.

Surah hii imekusanya Tauhidi ya kumpwekesha Allah katika majina Yake na sifa Zake.

[TAFSIRI YA SURATUL FALAQ]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Qul a-uudhu birabbil falaq . (2). Min sharri maa khalaq(3). Wa min sharri ghaasiqin idhaa waqab. (4). Wa min sharri nnaffaathaati fil uqad. (5). Wa min sharri haasidin idhaa hasad.

(Aya 1): Waambie kwa kujilinda kwa Allah *a-uudhu* (**najikinga**) na kujilinda kwa Mola wa mapambazuko.

(Aya 2): *Min sharri maa khalaq* (**na shari ya alivyoviumba**); hii inakusanya viumbe wote; majini, watu na wanyama. Lazima mwanadamu ajilinde kutokana na shari za viumbe hawa.

(Aya 3): *Wa min sharri ghaasiqin idhaa waqaba* (**na shari la giza la usiku liingiapo**) kwa sababu usiku unapowagubikka watu, roho na wanyama wabaya hupatikana kwa wingi.

(Aya 4): *Wa min sharri nnaffaathaati fil uqad* (**na shari ya wanaopulizia mafundoni**); shari za wachawi wanaopuliza kwenye mafundo yao ili kutekeleza uchawi wao.

(Aya 5): *Wa min sharri haasidin idhaa hasada* (**na shari ya hasidi anapohusudu**); Uhasidi ni kule kumtakia ndugu yako neema aliyonayo imwondokee kwa kila namna. Basi mwnadamu anahitaji kinga kutokana na shari hizi zote.

Surah hii imefunza kinga kutokana na aina zote za sharri ikiwemo uchawi na uhasidi.

[TAFSIRI YA SURATU NNAAS]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim
(1). Qul a-uudhu birabbi nnaas. (2). Maliki nnaas(3). Ilaahi nnaas. (4). Min sharril waswaasil khannaas. (5). Alladhii yuwaswisu fii sudduri nnaas. (6). Minal jinnati wa nnaas..

(Aya 1-6): Surah hii inafunza kutafta kinga kwa Allah kutokana na shari za shetani na fitina zake. Ambaye shetani huyu, sifa yake ni *yuwaswisu fii suddri nnaas* (**anayetia wasiwasi katika vifua vya watu**) kwa kuwapendezeshea shari na kuwapambia maovu na kuwahamasisha kutekeleza maovu yale. Kisha Allah akaelezea kuwa mashetani ni aina mbili; *minal jinnati wa nnaas* (**kutokamana na majini na wanadamu**)

Tunamshukuru Allah kwa kutujaalia kuikamilsha tafsiri ya baadhi ya surah za Kur'ani. Kisha rehema na amani zimwendee Mtume Wake.

MASUALI YA SURATUL FIIL

1. Surah hii ilishuka msimu wa Makkah au Madinah?
2. Ndani ya Surah hii, Allah ametaja uhatari wa kuifanyia uadui nyumba Yake. (sahihi / sio sahihi)
3. Alizaliwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, mwaka wa

   ○ Ndovu ○ Huzuni ○ Ukame
4. Allah aliwaadhibu jeshi kwa …….
5. Kila aliyepatwa na jiwe, alikuwa kama ……..

MASUALI YA SURATU QUREISH

6. Surah hii ilishuka msimu wa Makkah au Madinah?
7. Hii surah ina uhusiano na surah ipi?

○ Al-Fiil ○ Kaafiruun ○ An-Naas

8. Qureish walikuwa wakisafiri kwenda …….. msimu wa joto na …….. msimu wa baridi.

MASUALI YA SURATUL MAA^UUN

9. Surah hii ilishuka msimu wa……
10. Kuikadhibisha dini inamaanisha

○ Kufufuliwa na malipo

○ Kukanusha madeni ya watu

11. *Yadu^u* inamaanisha

○ Kumwacha

○ Kumfukuza na kumkataza kwa ukali

12. Yatima ni yule ambaye amefiwa na …… kabla ya kubaleghe.
13. Ni kusahau kupi kunahatarisha imani? …….
.....
14. Hukumu ya kutenda jambo kwa kujionyesha

    ○ Inaruhusiwa

    ○ Imeharamishwa
15. Katika surah hii Allah amehusia baadhi ya mambo, kwa mfano

    - ……..
    - ……..
    - ……..
    - ……..
    - ……..

16. Maa^uun inamaanisha …….

MASUALI YA SURATUL KAUTHAR

17. Surah hii ilishuka msimu wa ……

18. Al-Kauthar ni

- ○ Mto
- ○ Kheri na fadhila nyingi

19. Allah alitaja hizi ibada mbili: …… na …….. kwa sababu ndio ibada bora zaidi.

20. *Shaaniaka* inamaanisha

- ○ Anayekuchukia
- ○ Anayekudhalilisha
- ○ Yote mawili ni sahihi

21. Surah hii imefunza kuwa kumpeda Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuna ondoa hasara. (sahihi / sio sahihi)

22. Je, kwenye surah hii kuna dalili kuwa watakaonusuru dini watakuwa wengi?

MASUALI YA SURATUL KAAFIRUUN

23. Surah hii ilishuka msimu wa ……

24. Surah hii inasomwa katika rakaa ya kwanza baada ya suratul Fatihah katika swala ya

- ○ Sunnah ya Alfajr
- ○ Sunnah ya Maghrib
- ○ Sunnah ya Twawaaf
- ○ Witri
- ○ Sala zote ziizotajwa

25. Ibada iliyochanganyika na shirki ni ibada …….. (kamili/pungufu)?

26. Kafiri ni nani?

- ○ Kila aliyefikiwa na wito wa Uislamu na hakuamini
- ○ Watu wa Makkah pekee waliokataa Uislamu

MASUALI YA SURATU NNASRI

27. Surah hii ilishuka msimu wa ……..

28. Surah hii ndani yake kuna bishara, amri na ishara. (sahihi / sio sahihi)

29. Je, ndani ya surah hii kuna ishara ya kukaribia kifo chake, rehema na amani ziwe juu yake?

MASUALI YA SURATUL MASAD

30. Surah hii ilishuka msimu wa ……..

31. Abu Lahab alikuwa ni …….. yake Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.

32. Elezea maana ya maneno haya

Tabbat: …….

Maa kasaba: ……

Jiidihaa: ……..

Masad: …….

33. Ndani ya surah hii kuna dalili kuwa Abu Lahab na mkewe hawatasilimu. (sahihi / sio sahihi)

MASUALI YA SURATUL IKHLAAS

34. Surah hii ilishuka msimu wa ……..

35. Mbona surah hii imeitwa kwa jina la *Ikhlaas*?

36. Surah hii kuisoma ni sawa na kusoma …….. ya Kur'ani.

- ○ Robo
- ○ Thuluthi
- ○ Nusu

37. Surah inasomwa katika rakaa ya pili baada ya Fatihah katika swala gani?

- ○ Sunnah ya Alfajr
- ○ Sunnah ya Maghrib
- ○ Sunnah ya Twawaaf
- ○ Witri
- ○ Baada ya swala za faradhi
- ○ Yote ni sahihi

38. Surah hii imetaja aina gani ya Tauhidi? ……

39. Kumsingizia Allah mtoto ni

- ○ Kufru kubwa
- ○ Shirki ndogo

MASUALI YA SURATUL FALAQ

40. Surah hii ilishuka msimu wa …….

41. Surah hii inasomwa wakati gani?

- ○ Baada ya sala za faradhi
- ○ Wakati wa kulala
- ○ Nyakati zote mbili

42. Elezea maana na maneno haya:

Audhu: …….
Alfalaq: …….
Ghaasiq: ……
Waqab: …….
Haasid:…….

43. Surah hii inafunza kujikinga kutokana na kila kitu. (sahihi / sio sahihi)

MASUALI YA SURATU NNAAS

44. Surah hii ilishuka msimu wa …….

45. Inasomwa surah hii

- ○ Baada ya sala za faradhi
- ○ Wakati wa kulala
- ○ Nyakati zote mbili

46. Wanaotia wasiwasi ni ……. na ……

SOMO LA PILI

SOMO LA PILI: NGUZO ZA UISLAMU

Kubainisha nguzo tano za Uislamu; ya kwanza ni kushuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mtume Wake, kubainisha masharti ya shahada na kueleza maana ya baadhi ya maneno katika shahada.

Masharti ya Shahada ni:-

1. Elimu inayokanusha ujahili
2. Yakini inayokanusha shaka
3. Ikhlaas inayokanusha shirki
4. Ukweli unaokanusha kukadhibisha
5. Mapenzi yanayokanusha chuki
6. Utekelezaji unaokanusha utotekelezi
7. Kukubali kunakokanusha kupinga
8. Kuikufuru miungu yote inayoabudiwa kando na Allah.

Pia tutabainisha shahada ya kuwa Muhammad ni mtume Wake pamoja na masharti yake.

Kisha tutabainisha nguzo za Uislamu zilizobaki.

NGUZO ZA LAA ILAAHA ILLA

KUKANUSHA	KUTHIBITISHA
Kuikanusha miungu yote inayoabudiwa	Kumthibitishia ibada zote Allah na kumpwekesha katika ibada zote

MASHARTI YA SHAHADA (LAA ILAAHA ILLA ALLAH)

Umuhimu wa masharti ya shahada ni sawa na umuhimu wa meno kwenye ufunguo. Shahada ni ufunguo wa jannah na kama ilivyo kawaida ni kuwa ufunguo usiokuwa na meno hauwezi kuufungua. Na bishara njema zilizokuja kuelezea umuhimu wa shahada, hakika haziwezi kutimia mpaka kupatikane masharti haya manane:- ambayo ni

1. **ELIMU:** elimu iliyokamilika na kinyume chake ni ujahili. Asiyejua maana ya shahada basi shahada hii haitomfaa chochote. Inamlazimu kila anayetaka kuingia katika Uislamu aifahamu maana ya shahada (Laa ilaaha illa Allah). Anasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Atakayekufa huku akifahamu kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, ataingia jannah.*" (Ameipokea Muslim)
2. **YAKINI:** awe na yakini asilimia 100. Hakika ya shaka hata kama ni asilimia moja katika shahada au kupata wasiwasi katika shahada inamtoa mtu katika duara la Tauhidi. Amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Nashuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hakika mimi ni mtume Wake. Yeyote atakayekutana na Allah akishuhudia haya mawili pasina kuwa na shaka basi ataingia jannah.*" (Ameipokea Muslim)
3. **IKHLAAS:** kumpwekesha Allah ni wajibu. Atakayejionyesha katika ibada au kumshirikisha Allah na chochote katika ibada kwa mfano kuabudu sanamu, ibada hiyo haitomfaa kamwe. Amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Aliye bora zaidi kwa maombezi yangu siku ya Kiyama ni yule atakayetamka: Laa ilaaha illa Allah kwa ikhlaas kutoka moyoni mwake au kutoka kwa nafsi yake.*" (Ameipokea Bukhari)
4. **UKWELI:** Atakayetamka shahada kwa uongo – kama mnafiki – haitomfaa shahada hii, amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Hakuna yeyote anayeshuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mja Wake na mtume Wake kwa ukweli kutoka moyoni mwake isipokuwa mtu huyu Allah atamharamishia moto.*" (Ameipokea Muslim)
5. **MAPENZI:** Ampende Allah pekee wala asikipende pamoja na Allah chochote kile. Na ampende kila aliyeamrisha Allah kumpenda. Na kinyume chake ni chuki; ndio maana

ikawa kuchukia chochote alichokuja nacho Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kunamtoa Uislamuni hata kama atakifanyia kazi. Amesema Allah, "*Na miongoni mwa watu kuna wale wanaoifanya miungu na wakaipenda kama wanavyompenda Allah.*"

6. **UTEKELEZAJI:** Lazima kuifanyia kazi shahada. Yeyote ambaye hatoifanyia kazi shahada haitomfaa, amesema Allah, "*Hakika kwa haki naapa kwa Mola wako Mlezi. Hawatokuwa wenye kuamini hadi wakufanye hakimu kwa ugomvi unaotokea baina yao kisha wasipate moyoni dosari katika hukumu yako na waikubali kwa ukamilifu hukumu yako*."
7. **KUIKUBALI:** asiipinge shahada kwa maneno, vitendo au itikadi, anasema Allah, "*Hakika wao walikuwa wakiambiwa: hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, wanafanya kiburi huku wakisema: Haiwezekani sisi kuiacha miungu yetu kwa maneno ya mshairi wazimu*."
8. **KUIKUFURU MIUNGU:** Lazima aikufuru ibada ya miungu inayoabudiwa kando na Allah na azipwekeshe ibada zote kwa Allah pekee.

TANBIHI

LAZIMA MTU ATIMIZE MASHARTI HAYA KWA MANENO, VITENDO NA ITIKADI.

AINA ZA MAPENZI

MAPENZI PAMOJA NA ALLAH

Na hii ni shirki kubwa. Amesema Allah, "*Na miongoni mwa watu, kuna wale wanaopenda miungu kama mapenzi yao kwa Allah*"

KUMPENDA ALLAH

Na hii ni wajibu kwa kila mja bali ni moja katika shina kuu za imani. Amesema Allah, "*Muhammad ni mtume wa Allah. Na wale walioko naye ni wakali kwa makafiri na rahimu baina yao*"

Mapenzi haya yanakuwa katika mambo manne:-

MAPENZI YA KIMAUMBILE

Na hii imeruhusiwa kwa sharti: isipite mapenzi ya kumpenda Allah. Mfano wake: kumpenda mtoto au mke. Amesema Mtume, "*Hatoamini mmoja wenu mpaka anipende zaidi ya mwanawe, mzazi wake na watu wote.*"

KITENDO

Kitendo anachokiridhia Allah: nayo ni kila kilichokuja katika sharia kwa mfano Tauhidi

MTENDEA KAZI

Kama Manabii, Mitume, Malaika, Masahaba na kila anayempwekesha Allah.

ZAMA/MUDA

Zama/muda anaoupenda Allah kwa mfano Leilatul Qadri na thuluthi ya mwisho ya usiku.

SEHEMU

Sehemu anazozipenda Allah kama miji ya Makkah na Madinah yake Mtume.

MAANA YA **MJA** KATIKA SHAHADA INAYOSEMA: MUHAMMAD NI MJA WAKE NA MTUME WAKE

Haabudiwi kwa sababu yeye hana sifa yoyote katika uungu, mola wala pia hana sifa za ukamilifu kama za Allah.

Yeye ndiye mbora wa viumbe katika kumuabudu Allah basi anakuwa ametimiza sifa kamili ya kufanya ibada.

AINA ZA KUABUDU

JUMLA

Hii ni ibada ya ulezi wa viumbe (kumiliki na kuendesha) na kila kiumbe kinamnyenyekea katika hali hii. Allah anasema, "*Na hakika. Kila aliye mbinguni na ardhini atamjia Allah siku ya Kiyama akiwa mja*" Katika hii, anaingia Muumini na kafiri

HASA

Hii ni ibada ya kumcha Mwenyezi Mungu kijumla. Amesema Allah, "*Na waja wa Mwenyezi Mungu ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu*" Na ibada hii ni kwa kila aliyemfuata Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, katika mafunzo yake.

MAALUM

Hii ni ibada ya Mitume. Amesema Allah, "*Hakika alikuwa ni mja mwenye kushukuru*." Na hii ilikuwa ibada maalum kwa Mitume kwa sababu hakuna anayewashinda Mitume katika kumuabudu Allah.

MUKHTASAR WA HISTORIA YA MTUME MUHAMMAD, REHEMA NA AMANI ZIMWENDEE

NASABA YAKE	Muhammad bin Abdillahi bin Abdilmuttalib bin Hashim. Na Hashim ni kutoka kwa Qureish. Na Qureish ni kutoka kwa Waarabu. Na Waarabu ni katika kizazi cha Ismail bin Ibrahim, Allah awape salama.
KUZALIWA KWAKE	Alizaliwa mwaka wa ndovu kwenye mji wa Makkah mwezi wa tatu. Aliishi miaka sitini na mitatu (63); arbaini kabla ya unabii na ishirini na mitatu akiwa nabii mtume. Alizaliwa yatima; baba yake alifariki kabla ya kuzaliwa kwake; basi akawa katika malezi ya babu yake Abdulmuttalib na alipokufa babu yake, ami yake Abu Twalib ndiye alichukua majukumu ya kumlea.
WALIOMNYONYESHA	1. Mamake Amina bint Wahb 2. Thuwaibah, mjakazi wa ami yake Abu Lahab 3. Halima bint Abu Duwaib As-Saadiyyah
UTUME	Alitumwa kwa ajili ya viumbe wote; majini na wanadamu. Kila aliyefikiwa na wito wake na akafa bila ya kumuamini basi amekufa katika ukafiri.

WITO WAKE	Aliwalingania watu kwenye kumpwekesha Allah katika ibada Yake, tabia njema na akakataza ushirikina na tabia mbovu.
SAFARI YA ISRAA NA MI'RAJ	Allah alimsafirisha usiku kutoka Makkah hadi msikiti wa Aqsa kisha akamnyanyua hadi mbingu ya saba, akamzungumzisha kisha akamfaradhishia sala tano.
KUGHURA NA KIFO	Alighura kutoka mji wa Makkah kwenda mji wa Madinah. Na katika mji wa Madinah alifariki dunia na akazikwa humo; ndani ya chumba cha mkewe Aisha, Allah awe radhi naye.
KULINGANIA KWAKE	Allah alimkamilishia dini. Na yeye akalingania kiukamilifu kwa dini ya Allah, akatekeleza amana ya utume aliyopewa, akanasihi ummah, akapambana kwa njia ya Allah kwa kila namna; haiwezekani yeyote kuzidisha chochote katika dini hii.
VITA VYAKE MUHIMU	1. Badri 2. Uhud 3. Khandaq 4. Khaibar 5. Ufunguzi wa Makkah 6. Tabuk 7. Hunein
WATOTO WAKE SABA	- Qassim - Ibrahim - Abdullahi - Zeinab - Ruqaiyah - Ummu Kulthum - Fatuma **Wote walikufa akiwa hai isipokuwa Fatuma aliyefariki miezi sita baada ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.**

WAKE ZAKE	1. Khadija 2. Aisha 3. Sauda 4. Hafsa 5. Zeinab kutoka kabila la Hilal 6. Ummu Salama (Hind) 7. Zeinab bint Jahsh 8. Juweiriya bint Harith 9. Sofia bint Huyeiy 10. Ummu Habiba (Ramla) 11. Rihana bint Zeid 12. Maimuna bint Harith
UFUNUO WA KWANZA ALIOPEWA	Aya tano za mwanzo katika Suratul ^Alaq (Surah nambari 96 katika Kur'ani)
WALIOMWANI MWANZO	1. Katika wanaume : *Abubakar Siddiq* 2. Katika wanawake : *Mkewe Khadija* 3. Katika watoto : *Binamu yake (Ali bin Abi Twalib)* 4. Katika wajakazi : *Zeid bin Harith* 5. Katika watumwa : *Bilal bin Rabah*
HIJJA ZAKE NA UMRAH	Alifanya umrah nne, zote alikuwa anazifanya katika mwezi wa kumi na moja (Dhul Qaadah) na alifanya Hijja moja katika umri wake; inaitwa Hijja ya kuaga iliyofanyika mwaka wa 10 Hijri.
TABIA YAKE	Allah anamsifu akisema, "*Hakika wewe ni mwema wa tabia*". Anasema Aisha, Allah awe radhi naye, "**ilikuwa tabia yake ni Kur'ani.**"
UMUHIMU WA KUISOMA HISTORIA YAKE	Anasema Ibn Qayyim: *Ikiwa kufaulu duniani na akhera kumefungamanishwa na uongofu wake Mtume Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, ni wajibu kwa kila mmoja anayenasihi nafsi yake na kuipenda aitambue historia yake, rehema na amani ziwe juu yake, ili apate mazingatio kutoka kwa maisha yake.*

SOMO LA TATU

SOMO LA TATU: NGUZO ZA IMANI

Nguzo za Imani ni sita: Kumwamini Allah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Kiyama na kuiamini Qadar Yake; kheri yake na shari yake.

MAANA YA IMANI

Kutamka kwa ulimi, kukiri kwa moyo na kutenda kwa kiwiliwili na viungo. – imani huzidi na kupungua.

Dalili ya **KUTAMKA KWA ULIMI**	Dalili ya **KUTENDA KWA KIWILIWILI**	Dalili ya **KUTENDA KWA MOYO**	Dalili ya **KUZIDI IMANI**	Dalili ya **KUPUNGUA IMANI**
Hadith, "*Tawi la juu katika imani ni kutamka: Laa ilaaha illa Allah*"	Hadith, "*Tawi la chini katika imani ni kuondoa maudhi barabarani*"	Hadith, "*Na kuwa na haya ni katika matawi ya imani*"	Aya, "*Ni yupi kati yenu hili lilimzidisha imani*"	Hadith, "*Sijaona mpungufu wa akili na dini kama mwanamke...*"

SABABU ZINAZOMZIDISHIA MTU IMANI

Kuisoma Tauhidi hasa mlango wa Majina na Sifa za Allah.	Kuzidisha mambo ya ucha Mungu	Kuacha maasi na dhambi	Kutafakari katika maumbile ya Allah.

SABABU ZINAZOPUNGUZA IMANI YA MJA

- Kutoisoma Tauhidi hasa mlango wa Majina na Sifa za Allah.
- Kutofanya mambo ya ucha Mungu
- Kufanya maasi na dhambi
- Kutotafakari katika maumbile ya Allah.

NGUZO SITA ZA IMANI

- KUMWAMINI ALLAH
- KUAMINI MALAIKA WAKE
- KUAMINI VITABU VYAKE
- KUAMINI MITUME WAKE
- KUIAMINI SIKU YA MWISHO
- KUAMINI QADAR YAKE (KHERI NA SHARI)

NGUZO YA KWANZA YA IMANI: KUMUAMINI ALLAH

- Kuamini kuwepo Kwake.

  Ni hii inakuwa kwa mambo manne:-
  - **AKILI**
    Katika usalama wa akili, haiwezekani kupatikana viumbe bila muumbaji. Allah anasema, "*Au wameumbwa pasina chochote au wamejiumba*"
  - **HISIA**
    Pindi mtu anapozongwa na balaa au janga, kwa kawaida huinua mikono yake akielekea mbinguni akijua Allah anamsikiza.
  - **MAUMBILE**
    Hadith, "*Kila mzaliwa huzaliwa katika dini salama. Basi wazazi wake ndio humfanya Myahudi au Mkristo.*"
  - **SHERIA**
    Anasema Ibn Qayyim: ***hakuna aya katika Kur'ani isipokuwa inaonyesha Tauhidi***
- Kuamini Ulezi Wake

  (Uumbaji, Uendeshaji, Umiliki na Kuruzuku)
- Kuamini kustahiki Kwake ibada pasina miungu mingine.
- Kuiamini majina Yake na sifa Zake.

NGUZO YA PILI YA IMANI: KUAMINI MALAIKA WAKE

Malaika ni viumbe katika ulimwengu wa ghaibu. Allah amewaumba kwa nuru, wanamtii Allah na wala hawakiuki amri Zake. Wana nafsi kama alivyowasifu Allah kwa kauli Yake, "*Roho mtakatifu*", wana mwili kama alivyosema, "*Ametukuka aliyewaumba malaika na kuwafanya mitume wenye mbawa mbili-mbili, tatu-tatu, nne-nne, huzidisha katika uumbaji Wake anachokitaka*." Wana akili na nyoyo.

Malaika hawa tunawaamini kwa yale alotupa elimu Allah katika majina yao kama Jibril, Mikail na Israil, na katika sifa zao kama, "*Hawamuasi Allah anachowaamrisha na wao hutekeleza wanayoamrishwa.*" Na katika kazi zao.

BAADHI YA MALAIKA TULIOTAJIWA

Kuna Wabeba Arshi wanane, Jibril ambaye ni mhusika wa kushuka na ufunuo, Mikail ambaye ni mhusika wa hali ya anga na hewa. Tunawaamini wote na yote yaliyotajwa kuwahusu kwa ufupi na upana, kijumla na ufafanuzi.

NGUZO YA TATU YA IMANI: KUAMINI VITABU VYAKE

Ni lazima tuamini kuwa haya ni maneno ya Allah kiuhakika bila ya majazi na kuwa viliteremshwa wala havikuumbwa. Na lazima kuamini pia kuwa kila Mtume, Allah alimteremshia kitabu na tunaviamini kama alivyoelezea Allah kuhusu habari zao, majina yao na hukumu zao kijumla na ufafanuzi. Na pia tuamini kuwa Kur'ani ilishuka ikafuta vitabu vya awali kama Torati, Zaburi, Injili na nyaraka za Ibrahim na Musa.

NGUZO YA NNE YA IMANI: KUWAAMINI MITUME WAKE

Ni lazima tuamini kuwa Mitume ni viumbe ambao hawana sifa katika uungu na kuwa Mitume hawa ni waja wala hawapaswi kuabudiwa. Na tuamini kuwa Allah aliwatumiliza, akawapa ufunuo, akawapa miujiza ya kusadikisha wasemayo, na tuamini kuwa Mitume hawa walitekeleza amana ya utume, wakanasihi ummah, wakalingania na kueneza risala pamoja na kupambana katika njia ya Allah kuhakikisha mapenzi ya Allah yanatekelezwa.

Tunawaamini, na aliyotuelimisha Allah kuhusu sifa zao, habari zao na majina yao. Nabii wa kwanza alikuwa ni Adam na mtume wa kwanza alikuwa ni Noah na wa mwisho katika Manabii na Mitume alikuwa ni Muhammad, rehema na amani ziwe juu yao wote. Tunaamini pia kuwa sheria alokuja nayo mtume Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, ilifuta sheria zilizotangulia.

Na miongoni mwa Mitume, kuna wale Allah aliwanyanyua daraja zaidi ya waliobaki, nao ni Muhammad, Noah, Ibrahim, Musa na Isa, Allah awape salama.

NGUZO YA TANO YA IMANI: KUIAMINI SIKU YA MWISHO

Nguzo hii inamaanisha kuamini kila alichoelezea Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuhusu yale yatakayotokea baada ya kifo; kama mitihani ya kaburini, kupulizwa baraghumu,kufufuliwa watu, kupimwa vitendo katika mizani, kupewa kitabu cha matendo, kupita njia ya swiraat, kisima cha Mtume, maombezi, jannah, jahanamu, waumini kumuona Allah siku ya Kiyama na mengine mengi.

NGUZO YA SITA YA IMANI: KUIAMINI QADAR YAKE

Qadar ni mipangilio Yake Allah katika uumbaji. Na Qadar ina hatua nne:-

ELIMU

Tunaamini kuwa Allah alikijua kila kitu kwa upana kabla ya kuumba. Dalili ya hayo ni aya, "*Anajua yaliyokuwa kabla yao na yatakayokuwa kwenye mustakbali wao*"

UANDISHI

Tunaamini kuwa Allah, kabla ya kuumba, aliandika mipangilio ya kila kitu hadi siku ya Kiyama. Dalili ya hayo ni aya, "*Hakuna kilichofichika mbinguni wala ardhini isipokuwa kiko katika maandishi yaliyo wazi.*"

MATAKWA

Tunaamini kuwa kila alichokitaka Allah kinakuwa, na kila asichokitaka hakiwi, na kuwa mja pia kapewa matakwa yaliyo chini ya matakwa ya Allah. Anasema, "*Na wala hamtaki isipokuwa alichokitaka Allah.*"

UUMBAJI

Tunaamini kuwa mja ni kiumbe na vitendo vyake pia vimeumbwa, na vilivyomo vyote vimeumbwa. Anasema Allah, "*Allah ni muumbaji wa vyote*" "*Na Allah amewaumbeni na mtendavyo.*"

SOMO LA NNE

AINA ZA TAUHIDI NA AINA ZA SHIRKI

Kubainisha aina tatu za Tauhidi: kumpwekesha Allah katika Malezi, kumpwekesha Allah katika ibada na kumpwekesha Allah katika majina na sifa Zake:-

- **KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA MALEZI:** ni kuamini kuwa Allah ndiye muumbaji wa vitu vyote na mwendeshaji wa kila kitu na wala hana mshirika katika hayo.
- **KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA IBADA:** ni kuamini kuwa Allah ndiye apasaye kuabudiwa kwa haki na hana mshirika katika ibada. Na hii ndio maana halisi ya shahada. Ibada zote; swala, saum na zingine, anastahiki kupwekeshwa nayo Allah pekee na haifai kuielekeza ibada hiyo kwa miungu mingine.
- **KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA MAJINA NA SIFA ZAKE:** ni kuamini yote yalokuja kwenye Kur'ani na Sunnah kuhusiana na majina na sifa za Allah pasina kubadilisha maana wala kuzikanusha wala kuzitolea namna wala kuzifananisha na chochote katika viumbe. Anasema Allah, "*Hakuna mfano Wake chochote, na hakika Yeye ni mwenye kusikia na mwenye kuona.*"

Na baadhi ya wanazuoni wameigawanya Tauhidi kwa aina mbili; kwa kuingiza kumpwekesha Allah katika majina na sifa Zake katika kumpwekesha kwa ibada.

Shirki imegawanyika aina tatu:- shirki kubwa, ndogo na fiche.

- **SHIRKI KUBWA:** ni ile inayoporomosha amali zote za mja na kumdumisha jahanamu akifa katika hali hiyo, amesema Allah, "*Lau wangemshirikisha Allah na chochote ingeliporomoka amali yao.*" Na amesema pia, "*Haifai kwa washirikina kuitawala misikiti ya Allah hali ya kuwa wanaishuhudia nafsi zao katika ukafiri. Wao ni wale mema yao yameporomoka na ndani ya moto watadumu milele.*" Na atakaye kufa katika shirki kubwa hatosamehewa na ameharamishiwa jannah, asema Allah, "*Hakika ya Allah hamsamehe mwenye kumshirikisha na husamehe madhambi mengine kwa amtakaye*" pia anasema, "*Hakika atakayemshirikisha Allah basi huyo Allah amemharamishia jannah na makaazi yake ni motoni wala hatopata wa kumnusuru.*"

  Katika aina za shirki kubwa ni kuabudu maiti na sanamu, kutaka msaada kwao, kuwatolea nadhiri, kuwachinjia na mfano wa hizo.
- **SHIRKI NDOGO:** ni ile iliyotajwa katika Kur'ani au Sunnah kuwa ni shirki

lakini sio katika aina za shirki kubwa, kama kujionyesha katika ibada na kuapa na asiyekuwa Allah na mfano wake. Amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Kikubwa mno ninachowahofia ni shirki ndogo*" akaulizwa kuihusu akasema, "*Kufanya ibada kwa nia ya kujionyesha kwa watu.*" Na pia katika kauli yake, "*Atakayeapa kwa chochote kando na Allah basi amefanya shirki.*"

Shirki ndogo haimuondoi mtu katika Uislamu wala haitomdumisha mtu motoni akifa katika hali hiyo lakini inakanusha ukamilifu wa imani.

- **SHIRKI FICHE:** anasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuihusu, "*Je. Niwaelezeni ninachowahofieni kwenu zaidi ya masihi dajjal?*" wakasema tueleze ewe Mtume wa Allah, akasema, "*Shirki fiche: ni mtu kusimama katika sala yake kisha akaipamba kwa sababu ya wanaomtizama.*"

Pia shirki inatosheleza tu kugawanywa kwa aina mbili: kubwa na ndogo maana fiche inaingia ndani ya aina zote mbili; kubwa na ndogo.

- Inaingia kwenye Shirki Kubwa kama shirki ya wanafik; kwa sababu wanaficha ukafiri moyoni na wanadhihirisha Uislamu.
- Na inaingia kwenye Shirki Ndogo kama tulivyoona kwenye hadith iliyotangulia.

AINA ZA HARAMU

SHIRKI KUBWA
Ndiyo daraja ya juu katika haramu

SHIRKI NDOGO
Ndiyo inayofuata katika daraja ya pili za haramu

DHAMBI KUBWA
Ni kila dhambi yenye adhabu maalum na imehusishwa na laana na kutengwa mtendaji wake.

DHAMBI NDOGO
Ni kila kilichoharamishwa kisheria pasina adhabu maalum wala kufungamana na laana.

DHAMBI KUBWA

IDADI YAKE

Haina idadi maalum ila ina vidhibiti maalum vilivyotajwa

HUKUMU YA MTENDAJI

- Ni muumini mpugufu wa imani/ muovu kwa dhambi hilo
- Anapendwa kadri ya imani yake na anachukiwa kadri ya uovu wake.
- Haifai kuketi naye wakati wa kutekeleza ovu lile.

TARATIBU ZAKE
Zinatofautiana katika daraja na taratibu. Amesema Mtume, "*Je. Niwaambieni daraja ya juu katika dhambi kubwa….*"

HUKUMU YAKE
Ni lazima mja afanye tauba kwa kauli ya Mtume, "*Mpiga mayowe kwa kilio cha maiti asipotubu basi ……*"

TOFAUTI BAINA YA SHIRKI KUBWA NA SHIRKI NDOGO

SHIRKI KUBWA

1. Inamtoa mtu katika Uislamu
2. Inaporomosha amali zote
3. Inawajibisha mtu kudumu Jahanamu
4. Inahalalisha damu na mali ya mja (hili ni jukumu la kiongozi)
5. Inakuwa kwa dalili kuonyesha kuwa ni kubwa
6. Aitikadi kwenye sababu na kuacha mwenye kuleta sababu
7. Hatosamehewa mtu akifa kwa hali hii
8. Mja akitubu tauba yake inakubaliwa isipokuwa nyakati mbili:-
   - Jua likichomoza kutoka magharibi
   - Wakati wa kufa

SHIRKI NDOGO

1. Haimtoi mtu katika Uislamu
2. Haiporomoshi amali isipokuwa tu ile iliyopatikana ndani yake hiyo shirki
3. Haimdumishi mtu Jahanamu
4. Haihalalishi damu wala mali ya mja
5. Lazima ije dalili kuonyesha kuwa ni ndogo
6. Kuifanya sababu jambo ambalo Allah hajalifanya sababu
7. Kila kinachopelekea shirki kubwa basi hicho kitu ni shirki ndogo

SOMO LA TANO

IHSANI

Nguzo ya Ihsani ni moja: kumuabudu Allah ni kana kwamba unamuona na kama humuoni basi Yeye anakuona.

TABAKA MBILI ZA NGUZO YA IHSANI

IBADA YA USHAHIDI

Hii ni ibada kwa mapenzi kwa Allah. Na ibada hii ni maalum kwa Manabii na Mitume.

IBADA YA UCHUNGAJI

Hii ni ibada ya hofu na uoga ambayo kila Muislamu anakuwa nayo akijua kuwa Allah anatizama kila analolifanya.

MASUALI YA TAUHIDI

1. Daraja za Dini ni ngapi?

○ 3

○ 2

○ 5

2. Nguzo za Uislamu ni ngapi?

○ 5

○ 6

○ 7

3. Uislamu ni daraja la juu kuliko Imani…….. (sahihi / sio sahihi)

4. Nguzo za shahada ni ngapi?

○ 7

○ 8

○ 2

5. Masharti ya Shahada ni ngapi?

○ 8

○ 7

○ 5

6. Elimu katika shahada inamaanisha

○ Kuijua uhalisia wa jambo

○ Kujua kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah

7. Kukubali katika masharti ya shahada kunakusudiwa kukubali kwa

○ Maneno

○ Vitendo

○ Itikadi

○ Yote ni sahihi

8. Lau mtu akishuku kuwa Mayahudi ni makafiri. Je mtu huyu ni Muislamu au ametoka?

9. Kujionyesha katika shahada ni sawa na kujionyesha katika shirki ndogo?.....

10. Atakayetamka shahada kwa ulimi pasina kukiri moyoni. Mtu huyu ni

○ Mpwekeshaji

○ Muislamu lakini sio muumini

○ Kafiri ukafiri mkubwa

○ Dhaifu wa imani

11. Lau mtu atampenda Mtume mapenzi sawa na anayompenda Allah. Mtu huyu atakuwa

○ Amekufuru kufr kubwa

○ Amekufuru kufr ndogo

○ Ametenda dhambi katika dhambi kubwa

12. Aina za mapenzi ni ngapi?

○ 4

○ 3

○ 2

13. Kupenda pamoja na Allah ni

○ Shirki ndogo

○ Wajibu

○ Shirki kubwa

14. Aina za kuabudu ni ngapi?

○ 2

○ 3

○ 4

15. Jaza pengo

Alizaliwa Mtume Muhammad mwaka wa ……. Mji wa …… na aliishi miaka …….. ambayo ni …….kabla ya utume na …… katika unabii na utume.

16. Alitumilizwa kwa

○ Kabila lake

○ Watu wote

○ Viumbe wote; majini na wanadamu

17. Alighura kwenda mji wa

○ Uhabeshi

○ Madinah

○ Miji yote miwili ni sahihi

18. Alisafirishwa usiku kutoka …… kwenda msikiti wa…….

19. Alipigana vita kuu muhimu ……. (1/2/3/4/7)

20. Alikuwa na watoto …….

21. Alifanya Hijja ngapi katika umri wake? …….

22. Kusoma historia yake …… (ni lazima / inapendekezwa / haifai)

23. Nguzo za Imani ni ……

24. Kumuamini Allah kuna mambo mangapi? …… (3 / 4 / 5)

25. Dalili za kuonyesha kuwepo kwa Allah ni ngapi? ……. (3/4/ haina idadi)
26. Mikail ni malaika anayehusika na ……
27. Binadamu wana nyoyo lakini malaika hawana nyoyo…….. (sahihi / sio sahihi)
28. Ni vitabu vingapi vilitajwa majina yao? ……..
29. Allah alimshushia kila Mtume kitabu…… (sahihi / sio sahihi)
30. Nabii wa kwanza ni …….
31. Muhammad ni mtume lakini sio nabii……. (sahihi / sio sahihi)
32. Mitume bora ni wangapi? ……
33. Kuiamini siku ya mwisho inamaanisha
……
……
……
34. Hatua za Qadar ya Allah ni nne: 1 …….. 2……..3……..4……..
35. Je. Allah anajua vitu kabla ya kutokea?.....
36. Je. Kila anachokijua mwanadamu anakijua Allah?.....
37. Je. Kila anachokitenda mwanadamu anakijua Allah?.....
38. Je. Mwanadamu ana matakwa ya kujitegemea?.....
39. Je. Vitendo vya mwanadamu vimeumbwa?.....
40. Je. Tauhidi imegawanyika aina ngapi?.....
41. Taja tofauti tano baina ya shirki kubwa na shirki ndogo.
1 ……
2 ……
3 ……
4 ……
5 ……
42. Toa mifano tano ya shirki kubwa na tano ya shirki ndogo

SHIRKI KUBWA	SHIRKI NDOGO

43. Unafiki wa itikadi unamtoa mtu kwenye Uislamu…….. (sahihi / sio sahihi)
44. Ihsani ina nguzo moja. Nayo ni ……...

SOMO LA SITA

MASHARTI YA SALA

Masharti ya Sala ni tisa:-

1. Uislamu
2. Akili timamu
3. Upambanuzi
4. Kuondoa sifa zuizi
5. Kuondoa uchafu (najis)
6. Kusitiri uchi
7. Kuingia muda
8. Kuelekea Qiblah
9. Nia

SHARTI LA KWANZA: UISLAMU

Kinyume chake ni ukafiri. Lau mtu anayemtusi Allah au mshirikina atasali basi sala yake haitokubalika hadi alete tauba ya kikweli.

SHARTI LA PILI: AKILI TIMAMU

Kinyume chake ni wendawazimu au akili punguani. Na ulevi ni zaidi.

SHARTI LA TATU: UPAMBANUZI

Upambanuzi ni tofauti na kubaleghe. Maana ya upambanuzi ni uwezo wa kutofautisha na kupambanua utofauti baina ya vitu; yaani kuelewa suali na jawabu. Na upambanuzi hauna umri maalum lakini mara nyingi mtu katika umri wa miaka saba anakuwa mpambanuzi.

Ni wakati gani inasihi sala ya mtoto mdogo ambaye hajabaleghe? Akiwa na uwezo wa kupambanua baina ya vitu; kwa mfano kutofautisha baina ya maji na moto.

SHARTI LA NNE: KUONDOA SIFA ZUIZI (HADATH)

Sifa zuizi ni sifa ambayo ikipatikana kwa mja inamzuia kutekeleza ibada ya sala.

HADATH KUBWA
(Kama: janaba, hedhi na mengine**)**

Huondolewa kwa kuoga

HADATH NDOGO
(Kama: kukidhi haja, usingizi na mengine**)**

Huondolewa kwa kutawadha

SHARTI LA TANO: KUONDOA UCHAFU (NAJIS)

Kuondoa uchafu mwilini, nguoni au kwenye sehemu ya ibada. Lau atasali na najis huku akijua pamoja na kuwa na uwezo wa kuuonda pasina kughafilika basi sala yake haitokubalika.

Kuna aina tatu za najis:-

NAJIS NYEPESI

(**kwa mfano:** mkojo wa mtoto wa kiume ambaye hajaanza kula, maji ya shahawa na mkojo mwepesi wa uchovu)

Huondolewa kwa kunyunyizia maji bila kuosha

NAJIS YA WASTANI

(**kwa mfano:** mkojo)

Huondolewa kwa kukoshwa kwa maji sehemu yenye najis hiyo

NAJIS NZITO

(**kwa mfano:** mate ya mbwa)

Huondolewa kwa kukiosha kile chombo mara saba mojawapo ikiwa kwa kutumia mchanga

VITU AMBAVYO NI NAJIS

Mkojo na kinyesi cha mwanadamu, mkojo na kinyesi cha mnyama aliyeharamishwa kuliwa, wanyama wawindaji wote isipokuwa wale wagumu kuwaepuka kama paka, damu inayotiririka kwa wingi baada ya kuchinja, damu inayotoka kwenye tupu mbili, maiti zote isipokuwa maiti tatu: maiti ya mwanadamu, maiti ya wadudu wasiokuwa na damu yenye kutiririka, maiti ya panzi na maiti ya mnyama anayeishi kwenye maji.

SHARTI LA SITA: KUSITIRI UCHI

Uchi umegawanyika sampuli tatu:-

UCHI MWEPESI

Huu ni uchi wa mtoto aliye na miaka saba hadi kumi.

Lazima asitiri tupu zake mbili

UCHI MZITO

Huu ni mwili mzima wa mwanamke aliyebaleghe na aliye huru (sio mtumwa); mwili wake mzima ni uchi isipokuwa uso.

Lazima asitiri uso wake pia akiwa mbele ya wanaume wasiokuwa maharimu wake.

UCHI WA WASTANI

Ni uchi wa waliobaki (ukitoa uchi mwepesi na wa mwanamke)

Lazima asitiri mwili wake kuanzia magotini hadi kwenye kitovu. Inapedekezwa pia kusitiri mabega.

SHARTI LA SABA: KUINGIA MUDA WA SALA

Sala haikubaliki kabla ya kuingia muda wake na baada ya kuondoka muda wake isipokuwa kujumuisha kwa udhuru wa kisheria. Mtu akikusudia kuchelewesha sala kutoka kwa muda wake bila ya udhuru wa kisheria basi sala hiyo haitokubaliwa.

SHARTI LA NANE: KUELEKEA QIBLAH

Kuelekea Qiblah ni jambo la lazima isipokuwa katika sala za Sunnah mtu akiwa safarini juu ya kipando chake au katika hali yetu ya kisasa; mtu akiwa kwenye ndege. Na pia hana dhambi kwa asiyekuwa na uwezo wa kuelekea Qiblah kutokana na uoga au maradhi.

SHARTI LA TISA: NIA

Nia pahala pake ni moyoni na kuitamka nia ni katika mambo ya uzushi.
Akinuwia mtu kabla ya sala ya faradhi kwa muda basi sala yake ni sahihi.

TANBIHI MUHIMU

1. Haikubaliwi mtu kuacha sharti lolote kwa ujahili wala kusahau wala kusudi isipokuwa atakayesali na najis bila ya kujua basi huyo sala yake itakuwa sahihi.
2. Sharti linakuwa kabla ya ibada; nje ya ibada lakini lazima lipatikane hadi mwisho wa ibada husika.

SOMO LA SABA

NGUZO ZA SALA

Nguzo za Sala ni kumi na nne:-

1. Kusimama kwa uwezo
2. Takbiratul ihraam
3. Kusoma Fatihah
4. Kurukuu
5. Kusimama wima baada ya rukuu
6. Kusujudu kwa viungo saba
7. Kuinuka kutoka sijda
8. Kuketi baina ya sijda mbili
9. Utulivu katika kila kitendo
10. Utaratibu baina ya nguzo
11. Tashahhud ya mwisho
12. Kuketi kwaajili ya tashahhud hiyo
13. Kumsalia Mtume kwenye tashahhud ya mwisho
14. Salamu mbili

NGUZO YA KWANZA: KUSIMAMA KWA MWENYE UWEZO

SALA YA FARADHI

Kusimama ni nguzo katika sala ya faradhi na anasamehewa tu asiyekuwa na uwezo kabisa au uwezo wake akisimama utulivu wake unaondoka.

Akiwa na uwezo wa kusimama japo kidogo basi atasimama.

SALA YA SUNNAH

Inasihi sala yake akisali hali ya kuwa ameketi lakini atapata nusu ya thawabu ya yule aliyesali akiwa amesimama. Na akisali kwa kulala ubavuni basi atapata nusu ya thawabu ya aliyesali akiwa ameketi.

NGUZO YA PILI: TAKBIRATUL IHRAAM

Hii ni takbir ya kufunga sala. Na haikubaliki isipokuwa maneno haya: *Allahu akbar*

NGUZO YA TATU: KUISOMA SURATUL FATIHAH

Ni lazima kuisoma suratul Fatihah, kisomo kamili kwa utaratibu wa mpangilio wa aya zake, katika kila rakaa ya sala; iwe sala za kupaza sauti au kisiri. Na anasamehewa akimuwahi imam kwenye rukuu.

NGUZO YA TISA: UTULIVU KATIKA KILA KITENDO

Utulivu unatimia kwa kusoma nyiradi zote za sala inavyotakiwa.

TANBIHI MUHIMU

Nguzo zinakuwa ndani ya ibada na haikubaliwi kuiacha nguzo kwa ujahili wala kusahau wala kusudi, na wala haijazwi kwa sijdatu sahwi (sijda ya kusahau) na inamlazimu mtu kuirudia ile au kuileta nguzo ile aloiacha. Lakini akikumbuka muda baada ya kumaliza sala yake basi hapo anasamehewa.

SOMO LA NANE

VITU VYA WAJIBU KATIKA SALA

Vitu vya wajibu katika sala ni vinane:-

1. Takbir zote kando na ya ihraam
2. Kusema: *samia Allahu liman hamida* (kwa imam na maamuma)
3. Kusema: *rabbanaa wa lakal hamd* (kwa wote wawili)
4. Kusema: *subhana rabbiyal athwiim* katika rukuu
5. Kusema: *subhana rabbiyal a^laa* katika sijda
6. Kusema: *Rabbi ighfir lii* baina ya sijda mbili
7. Tashahhud ya mwanzo
8. Kuketi kwaajili ya tashahhud ya mwanzo

TANBIHI MUHIMU

Ni wajibu kusema: *subhana rabbiyal athwiim* katika rukuu kutumia maneno haya kisha inapendekezwa azidishe nyiradi zingine zilizopokelewa.

Na pia ni wajibu kusema: *subhana rabbiyal a^laa* katika sijda kutumia maneno haya kisha inapendekezwa azidishe nyiradi zingine zilizopokelewa.

SOMO LA TISA

KUBAINISHA TASHAHHUD

Tashahhud ni kusema: *Attahiyyaatu lillahi wa sswalawaatu wa ttwayyibaatu. Assalaamu aleika ayyuha nnabiy wa rahmatullahi wa barakaatuh. Assalaamu aleinaa wa alaa ibaadillahi sswaalihin. Ash-hadu an laa ilaaha illa Allah wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluh.*

Kisha anamsalia Mtume na kumuombea baraka kwa kusema: *Allahumma swalli alaa Muhammadin wa alaa aali Muhammadin kamaa swallaita alaa Ibrahima wa alaa aali Ibrahima innaka hamiidun majiid. Wa baarik alaa Muhammadin wa alaa aali Muhammadin kamaa baarakta alaa Ibrahima wa alaa aali Ibrahima innaka hamiidun majiid.*

Kisha anamuomba Allah amlinde kutokana na adhabu ya kaburini na adhabu ya motoni na kutokana na fitna za waliohai na waliokufa na kutokana na fitna ya masihi dajjal. Kisha anaomba dua yoyote atakayo na bora zaidi atumie zilizopokelewa kwa mfano: "*Allahumma ainniy alaa dhikrika wa shukrika wa husni ibaadatika. Allahumma inniy thwalamtu nafsiy dhulman kathiiran wa laa yaghfiru dhunuuba illa anta faghfir lii maghfiratan min indika wa-r-hamniy, innaka antal ghafuuru rahiim.*" (**Ewe Mol wangu hakika mimi niko katika utajo Wako na shukrani Zako na bora ya ibada Zako. Ewe Mola wangu, hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhulma nyingi na najua kuwa hakuna anayesamehe madhambi isipokuwa Wewe. Naomba unisamehe msamaha kutoka Kwako ambao haubakishi dhambi lolote na unirehemu kwani Wewe ndiye mwenye kurehemu.**)

Ama katika tashahhud ya mwanzo katika swala ya Dhuhur, Asr, Maghrib na Isha; atasimama baada ya kutoa shahada katika tashahhud na akimsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, itakuwa bora.

SOMO LA KUMI

SUNNAH ZA SALA

Miongoni mwa Sunnah za sala ni:-

1. Dua ya ufunguzi wa sala
2. Kuuwekelea mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto kwenye kifua wakati wa kusimama, kabla ya rukuu na baada ya rukuu.
3. Kunyanyua mikono miwili, huku umetawanya vidole, hadi urefu wa mabega au masikio wakati wa takbiratul ihram, kuenda rukuu, kutoka rukuu na kutoka tashahhud ya mwanzo kwa ajili ya kusimama rakaa ya tatu.
4. Kuzidisha nyiradi zaidi ya mara moja katika rukuu na katika sijda.
5. Kuleta nyiradi za ziada baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu.
6. Kusawazisha baina ya kichwa na mgongo katika rukuu
7. Kutenganisha baina ya viwiko na mbavu na baina ya tumbo na mapaja katika hali ya kusujudu.
8. Kuweka mikono juu kutoka kwa ardhi katika hali ya kusujudu. (kiwiko kisiguse ardhi)
9. Kuketi juu ya mguu wa kushoto uliotandazwa na kuusimamisha mguu wa kulia katika kikao cha tashahhud ya mwanzo.
10. Kuketi kikao cha *tawarruk* katika kikao chao tashahhud ya mwisho: kuketi kitako huku mguu wa kulia umesimama na kuupitiza mguu wa kushoto chini ya mguu wa kulia.
11. Kuashiria katika sala wakati wa tashahhud zote mbili kutumia kidole cha shahada kuanzia mwanzo wa tashahhud hadi mwisho na kukitikisa wakati wa dua.
12. Kumsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na kumtakia baraka kwenye tashahhud ya mwanzo.
13. Dua kwenye tashahhud ya mwisho.
14. Kupaza sauti kwa kisomo kwenye sala za AlFajr, Ijumaa, idi mbili, sala ya mvua na kwenye rakaa mbili za mwanzo za sala ya Maghrib na Isha.
15. Kuficha sauti kwa kisomo kwenye sala za Dhuhur, Asr, rakaa ya tatu ya sala ya Maghrib na rakaa mbili za mwisho kwenye sala ya Isha.
16. Kusoma surah nyingine baada ya suratul Fatihah.

DUA YA UFUNGUZI WA SALA

Inakuwa dua hii ya ufunguzi baada ya takbiratul ihraam kama ilivyopokelewa kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kwa maneno haya: "*Allahumma baaid bainiy wa baina khatwaayaai kamaa baa^adta bainal mashriq wal maghrib. Allahumma naqqiniy minal khatwaayaa kamaa yunaqqa th-thaubul ab-yadhu mina ddanas. Allahumma ighsilniy min khatwaayaai bilmaai wa th-thalji wal barad.*"

Au kauli hii: "*Subhaanaka Allahumma wa bihamdika, wa tabaaraka ismuka wa taala jadduka, wa laa ilaaha ghairuka.*"

SOMO LA KUMI NA MOJA

MAMBO YANAYOVUNJA SALA

Mambo yanayovunja sala ni manane:-

1. Kucheka
2. Kula
3. Kunywa
4. Kufichua uchi
5. Kuacha kuelekea Qiblah kipande kikubwa cha mwili
6. Harakati nyingi mutawalii
7. Kutenguka kwa twahara (hali ya usafi)
8. Kuzungumza kwa kusudi ndani ya sala pamoja na kuwa mtu anafahamu uharamu wake. (ama aliyesahau au hajui mafundisho hayo basi sala yake haijaharibika).

JAMBO LA NANE: KUZUNGUMZA KUSUDI PAMOJA NA KUJITAMBUA

Hairuhusiwi kuzungumza katika sala maneno yasiyohusiana na sala. Anaruhusiwa tu mtu kumkumbusha imam wakati imam kakosea au kasahau jambo katika sala.

HARAKATI KATIKA SALA

- Harakati ya lazima ambayo kukubalika kwa sala kunaitegemea kama kuondoa najis
- Harakati ambayo inapendekezwa kwa sababu inaleta ukamilifu wa ziada katika sala kama kuziba pengo katika safu.
- Harakati ambayo imeruhusiwa kama kujikuna kwenye ndevu kwa haja.
- Harakati ambazo zinachukiza pasina dharura kwa mfano kugeuza macho kando
- Harakati ambazo zimeharamishwa nazo ni harakati nyingi mfululizo pasina dharura kwa mfano: *kula*

TANBIHI MUHIMU

TOFAUTI BAINA YA SHARTI, NGUZO, WAJIBU NA SUNNAH KATIKA SALA

SHARTI	NGUZO	WAJIBU	SUNNAH
Inapatikana nje ya sala	Zinapatikana ndani ya sala		
Inaendelea hadi mwisho wa sala	Zinapatikana kwenye vipengele maalum katika sala		
Haisameheki kuacha kwa ujahili wala kusahau wala kusudi.		Inasameheka kuacha kwa ujahili na kusahau wala sio kwa kusudi	Inasameheka kuacha kwa ujahili, kusahau na kusudi.
Haina sijdatu sahwi (sijda ya kusahau)	Hailipwi kwa sijdatu sahwi	Hulipwa kwa sijdatu sahwi	/

SIJDATU SAHWI (SIJDA YA KUSAHAU KITU KATIKA SALA)

Hii sijda huletwa kwa sababu moja miongoni mwa sababu hizi tatu:-

KUZIDISHA

Kwa mfano mtu kuzidisha rukuu au sijda au kikao kwenye sala.

KUPUNGUZA

Kwa mfano mtu kupunguza jambo la wajibu katika mambo ya wajibu katika sala. Akaliacha kutoka sehemu yake.

SHAKA

Kama kutatasika mtu hajui amesali rakaa tatu ama nne.

Na shaka imegawanyika aina mbili:-

SHAKA BAADA YA KUMALIZA SALA

Aina hii ya shaka haizingatiwi kabisa isipokuwa awe na yakini.

SHAKA NDANI YA SALA

- Ikiwa ni shaka nyingi basi asiizingatie
- Ikiwa ni shaka chache, ajenge kwa lile alilo na yakini nalo
- Ikiwa shaka na yakini zimetoshana, basi achague ile ndogo (*kwa mfano hajui amesali rakaa tatu au nne wala hana jambo la kurajihisha moja yao basi inafaa aseme amesali rakaa tatu maana ndio yenye uhakika*)

MAELEKEZO MUHIMU

1. Akisahau mtu kusujudu sijda ya sahwi basi hana dhambi na sala yake ni sahihi
2. Mtu akiacha nguzo ya sala, hiyo sala haikubaliwi na lazima ailete nguzo ile na kisha asujudu sijda ya sahwi mwisho wa sala yake.
3. Akiacha mtu jambo ambalo ni wajibu katika sala na ashaondoka sehemu ya wajibu ile basi inamtosheleza kusujudu tu sijda ya sahwi mwisho wa sala yake.

MAFUNDISHO YA SALA KWA UFUPI

- Ajitwahirishe Muislamu nyumbani kwake na avalie mavazi nzuri.
- Aelekee msikitini – kwa miguu au kipando – kwa utulivu na taratibu wala asikimbie wala kutizama sana mambo ya dunia wala asinyanyue sauti yake.

- Akifika msikitini, avue viatu vyake na aviweke sehemu maalum ya kuweka viatu na aweke pia dunia sehemu hiyo ya viatu; asianze biashara ndani ya msikiti wala asitangaze msikitini kitu kilichopotea.
- Na autangulize mguu wake wa kulia katika kuingia msikitini na aseme dua hii: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillaah. Allahumma iftah lii abwaaba rahmatika.* Na wakati wa kutoka atangulize mguu wa kushoto na aseme: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillaah. Allahumma inniy as-aluka min fadhlika.*
- Wanaume waketi kwenye safu za mbele na wanawake bora ya safu zao ni safu zile za mwisho.
- Ikiwa sala tayari imeanza, basi alete takbiratul ihraam, afunge sala na amfuate imam atakapompata: Anahesabu rakaa kamili akimpata imam amesimama au katika rukuu. Na imam akitoa salamu basi asimame alipe yaliyompita.
- Lakini ikiwa ameingia msikitini na sala haijaanza, basi atasali sala za Sunnah au Sunnah ya kuingia msikitini.
- Wala haifai kuleta jambo la kushawishi kuashiria sala ianze. Kwa mfano kila wakati kutizama saa au kubuni kikohozi kama ishara.
- Inapendekezwa aweke sutra/kizuizi mbele yake akiwa anasali pekee lakini kama anasali nyuma ya imam basi imam ndiye sutra ya walioko nyuma yake.

- Na aweke miguu yake kama kiasi kilicho baina ya mabega yake bila kuzidisha wala kupunguza.

- Baada ya kutimiza masharti yote ya sala, aseme ***Allahu akbar*** huku akiinua mikono yake urefu wa wa mabega au masikio akiwa vidole vimeshikana na aelekeze sehemu ya ndani ya viganja Qiblah.

- Kisha auweke mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto kwa kubana au kutelekeza.



- Na aelekeze macho yake pahala pa kusujudu wala asitizame huku na kule.

- Kisha inapendekezwa asome dua ya ufunguzi katika rakaa ya mwanzo pekee na bora akitumia nyiradi tofauti tofauti za ufunguzi katika sala zake.
- Kisha ajilinde kwa Allah kwa kusema: ***Audhu billahi mina sh-shaitwani rrajiim***
- Kisha aseme: ***Bismillahi Rrahmani Rrahiim***
- Kisha aisome suratul Fatihah kamili kwa utaratibu na nidhamu ipasavyo.
- Kisha aisome surah nyingine baada ya Fatihah kadri ya uwezo.
- Kisha ainue mikono kama alivyoinua kwenye takbiratul ihraam na aseme: *Allahu akbar* kisha aende rukuu.
- Aishike magoti yake kwa viganja wala asikunje viwiko vyake na aunyooshe mgongo wake ausawazishe na kichwa.
- Aseme akiwa kwenye rukuu: *Subhana rabbiyal athwiim* mara moja au zaidi.

- Kisha anyanyuke kutoka rukuu huku akisema: *Samia Allahu liman hamida.* Ainuke pamoja na kunyanyua mikono yake urefu wa mabega au masikio.
- Akiwa amenyooka wima kabisa aseme: *Rabbanaa wa lakal hamd.*
- Kisha alete Takbir bila kunyanyua mikono na asujudu kwa viungo saba: *paji la uso, pua, viganja viwili, magoti mawili na miguu miwili.*
- Aweke mbali baina ya viwiko na tumbo na baina ya tumbo na mapaja.

- Na aseme akiwa amesujudu: *Subhana rabbiyal a^laa* mara moja au zaidi.
- Kisha aketi kama kikao cha tashahhud kama tulivyoelezea.



- Kisha asujudu tena kama sijda ya kwanza
- Kisha alete Takbir na asimame kwaajili ya kutekeleza rakaa ya pili bila ya kuleta dua ya ufunguzi.
- Akikamilisha sijda ya pili katika rakaa ya pili ataketi kikao cha tashahhud na kuleta tashahhud huku amefanya duara kidole chake cha gumba.
- Kama ni sala ya rakaa mbili basi atamsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na amuombe Allah amlinde kutokana na shari zote.
- Kisha atatoa salamu mbili; moja pande ya kulia na nyingine pande ya kushoto kwa kugeuza kichwa pande zote mbili wala sio kwa kugeuza mabega.

- Na ikiwa sala ni ya rakaa tatu au nne, basi baada ya tashahhud ya kwanza, atasimama ili kukamilisha rakaa zilizobaki.
- Ikiwa ni sala ya faradhi basi inapendekewa kuleta nyiradi za baada ya sala.

TANBIHI MUHIMU

- Kama ilivyotangulia kwenye masharti ya sala katika kusitiri uchi. Basi lazima ajisitiri isifichuke uchi isije haribika sala yake.

- Akisali mtu na imam, basi asimame upande wa kulia mwa imam na alilinganishe bega lake na la imam.

JEDWALI LA MUKHTASAR WA SALA

SALA	HUKUMU	MUDA WAKE	RAKAA	SIFA
Jumuah	Faradhi	Wakati wa sala ya Dhuhur	Rakaa mbili	Inasaliwa kwa kupaza sauti na kwa jamaa ya watu kuanzia watatu
Kusuuf	Faradhi kifaya (inatosheleza baadhi ya watu wakiisali)	Ikitokea kushikana jua na mwezi	Rakaa mbili	Inasaliwa kwa kupaza sauti na ina rukuu mbili kwa kila rakaa moja
Witri	Sunnah iliyosisitizwa	Baada ya sala ya isha hadi AlFajr	Kuanzia rakaa moja hadi kumi na moja.	Ikiwa rakaa moja au zaidi tashahhud itakua katika rakaa ya mwisho.
Sunnah ya Fajr	Sunnah iliyosisitizwa	Kabla ya sala ya Fajr	Rakaa mbili	Inasomwa rakaa ya kwanza baada ya Fatihah suratul Kaafiruun na rakaa ya pili Ikhlaas.
Sunnah ya Dhuhur	Sunnah	Rakaa nne kabla ya Dhuhur na rakaa mbili baada yake	4/2	Rakaa mbili kisha salamu kisha rakaa mbili tena
Sunnah ya Maghrib	Sunnah	Baada ya sala ya Maghrib	Rakaa mbili	Inasomwa rakaa ya kwanza baada ya Fatihah suratul Kaafiruun na rakaa ya pili Ikhlaas.
Sunnah ya Isha	Sunnah	Baada ya sala ya Isha	Rakaa mbili	
Taraweh	Sunnah	Baada ya sala ya Isha hadi Fajr	Kuanzia rakaa mbili hadi rakaa kumi	
Tahiyyatul Masjid	Wajib	Kuingia msikitini kabla ya kuketi	Rakaa mbili	
Dhuha	Sunnah	Kuchomoza jua hadi kabla ya kupinda	Kuanzia rakaa mbili hadi nane	
Istikhara	Sunnah	Muda wowote	Rakaa mbili	Anaomba dua ya istikharra kabla ya salamu
Istisqaa	Sunnah kwa haja	Baada ya kuchomoza jua wakati wa kiangazi	Rakaa mbili	Analeta Takbir saba baaada ya takbiratul ihraam na tano akiamka rakaa ya pili
Eid	Sunnah	Baada ya kuchomoza jua kadri ya urefu wa mkuki	Rakaa mbili na khutbah mbili	Analeta Takbir saba baada ya takbiratul ihram na tano akiamka rakaa ya pili

NYAKATI ZILIZOKATAZWA KUSALI

1. Kuanzia baada ya AlFajr hadi kuchomoza jua
2. Kuanzia Asr hadi Maghrib
3. Kusimama jua utosini hadi kupinda

MASUALI KUHUSU SALA

1. Masharti ya Sala ni ngapi?

- ○ 9
- ○ 11
- ○ 8

2. Upambanuzi ni nguzo au sharti ya Sala? …….

3. Je. Ni lazima kusafisha mwili, nguo na pahala pa Sala?

4. Najis ya nguruwe ni aina gani ya najis?

- ○ Nyepesi
- ○ Ya wastani

5. Je. Manii ni najis? ……

6. Tofauti baina ya kuosha na kunyunyizia. **Kuosha** ni …….. **Kunyunyizia** ni ……...

7. Maiti zote ni najis isipokuwa ……..

8. Mdudu asiyekuwa na damu yenye kutiririka maiti yake …….. najis (ni /sio)

9. Je. Damu inayobaki mishipani ni najis? ……..

10. Nguzo za Sala ni ngapi? ……..

11. Je. Mtu akiacha nguzo kwa kusahau, ataleta sijdatu sahwi pekee? ……..

12. Mambo ya wajibu katika Sala ni ngapi?

- ○ 8
- ○ 14
- ○ 9

13. Ni sheria kuuweka mkono wa kushot o juu ya mkono wa kulia kawaida? ……..

14. Mambo yanayovunja sala ni mambo ……

15. Kikao cha Tawarruk kinakua katika tashahhud ya ……. (mwanzo / mwisho)

16. Uradi baina ya sijda mbili ni: …….

17. Kiwiko kugusa ardhi katika sijda ni

- ○ Haramu
- ○ Sunnah
- ○ Inachukiza

18. Sababu za sijdatu sahwi ni ngapi?

- ○ 2
- ○ 3
- ○ 4

19. je shaka baada ya sala inaathiri? …….

20. Bainisha hukumu ya vitu vifuatavyo:-

JAMBO	HUKUMU YAKE
Sala ya mtu anayemtusi Allah	
Sala ya mlevi	
Sala ya mtu mwenye kifafa	
Sala ya mtoto	
Sala bila Wudhuu	
Sala kwa nguo yenye najis	
Mkojo wa ng'ombe	
Mkojo wa kunguru	
Sala hali ya kuwa mapaja yako wazi	
Sala kabla ya muda kwa kusahau	
Sala ndani ya ndege	
Sala kwa kuketi	
Kusahau kuisoma Fatihah katika sala	
Kumpata imam katika rukuu	
Kukimbilia sala	
Shaka nyingi kwenye sala	
Kushuku Wudhuu baada ya sala	
Kuzidisha rukuu kwa kusahau	
Kuiacha takbiratul ihraam	
Kuiacha tashahhud ya mwanzo	
Kuiacha tashahhud ya mwisho	
Kushuku amesali rakaa tatu au nne	
Shaka baada ya sala	
Shaka ndani ya sala	
Kusahau kuileta sijdatu sahwi	
Kusali uchi ukionekana bila kujua	
Kujitwahirisha nyumbani	
Biashara msikitini	
Kubadilisha sarafu msikitini	
Kuzungumza katika sala kwa kusahau	
Kumdiriki imam kwenye tashahhud	
Kujisitiri uchi katika sala	
Kutembeza macho katika sala	
Kusali kwa kasi	
Kumsalia Mtume	
Kuzidisha jambo katika sala	
Harakati nyingi katika sala	
Kuisahau Fatihah	
Sala ya Jumuah	

21. Elezea tofauti baina ya nguzo, sharti, wajibu na Sunnah katika sala.

SOMO LA KUMI NA MBILI

MASHARTI YA WUDHUU

Masharti ya Wudhuu ni kumi:-

1. Uislamu
2. Akili timamu
3. Upambanuzi
4. Nia
5. Asinuwie kuvunja Wudhuu hadi mwisho wa kutawadha
6. Kupatikana jambo linalowajibisha Wudhuu
7. Kukidhi haja
8. Maji yawe safi
9. Kuondoa kinachozuia maji kufikia ngozi
10. Kuingia muda wa sala kwa asiyekuwa msafi

SUNNAH ZA KIMAUMBILE

Katika mambo ya kimaumbile ambayo lazima kila Muislamu ayazingatie ni:-

(**LA KWANZA**): Kutahiriwa kwa watoto wa kiume.

(**LA PILI HADI LA TANO**): kupunguza masharubu, kukata kucha, kung'oa nywele za kwapa na kunyoa nywele za sehemu za siri. Anasema Anas, Allah awe radhi naye, "*Imeekwa kuwa kupunguza masharubu, kukata kucha, kung'oa nywele za kwapa na kunyoa nywele za sehemu za siri isipite siku arbaini.*" Basi haifai kusubiri hadi siku 40 ziishe.

(**LA SITA**): kufuga ndevu: kuzifuga ni wajibu na kuzinyoa ni katika dhambi kubwa.

(**LA SABA**): mswaki: inasisitizwa kupiga mswaki kila mara mtu anapotawadha, wakati wa sala, kuingia nyumbani, kusoma Kur'ani, kulala na inapobadilika harufu kinywani.

SOMO LA KUMI NA TATU

FARADHI ZA WUDHUU

Faradhi za Wudhuu ni sita:-

1. Kuosha uso pamoja na kusukutua na kuosha pua
2. Kuosha mikono miwili hadi kwenye viwiko
3. Kupangusa kichwa kwa mikono nyevunyevu pamoja na masikio
4. Kuosha miguu miwili hadi kwenye vifundo viwili vya miguu.
5. Taratibu katika kuosha viungo
6. Upesi katika kuosha viungo (aoshe kiungo kabla cha kabla yake kukauka)

Inapendekezwa kuosha uso, mikono miwili na miguu miwili mara tatu na vilevile katika kuosha pua na kusukutua. Lakini faradhi ni kuosha viungo vyote mara moja.

Na haipendekezwi kupangusa kichwa zaidi ya mara moja.

SOMO LA KUMI NA NNE

MAMBO YANAYOTENGUA WUDHUU

Mambo yanayovunja Wudhuu ni sita:-

1. Kinachotoka kwenye tupu mbili
2. Na kinachotoka mwilini katika vitu najis
3. Kupoteza fahamu kwa njia ya usingizi
4. Kugusa tupu mbili kwa kiganja bila ya kizuizi
5. Kula nyama ya ngamia
6. Kuritadi (kutoka katika Uislamu)

TANBIHI MUHIMU

Ama kumuosha maiti, kauli sahihi ni kuwa haitengui Wudhuu. Na hii ndio kauli ya wanazuoni wengi; kwa sababu hakuna dalili ya kudhibitisha hilo. Lakini lau mkono wa muosha maiti itaugusa utupu wa maiti bila kizuizi basi itamlazimu kutawadha. Na ni wajijbu kwa muosha maiti kutogusa utupu wa maiti isipokuwa kwa kizuizi.

Na vilevile kumgusa mwanamke hakutengui Wudhuu kabisa; ima amemgusa kwa matamanio au bila matamanio maadamu hajatokwa na manii. Na hii ndio sahihi katika kauli mbili za wanazuoni kwa sababu Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alikuwa akibusu wakeze kisha anaenda kusali pasina kutawadha.

Na makusudio ya aya namba 6 katika suratul Maidah inayosema *au laamastumu nnisaa* **(au mmewagusa wanawake)** makusudio ya kugusa kwenye ayah hii ni kuingiliana kwende tendo la ndoa. Hii ndio kauli ya Ibn Abbas na kikundi katika wema waliotangulia, Allah awe radhi nao.

MAFUNDISHO YA JINSI YA KUTAWADHA KWA UFUPI

- Akishanuwia Wudhuu basi aseme: *Bismillahi*
- Aoshe viganja viwili kabla ya kuvitumbukiza kwenye chombo cha maji
- Achukue maji kwa mkono wa kulia kuingiza mdomoni, asukutue na aoshe pua lake huku akitoa uchafu puani kwa kutumia mkono wa kushoto.
- Aoshe uso wake mara tatu kuanzia kidevu hadi mwanzo wa nywele za kichwani na kuanzia sikio hadi sikio la pili.
- Aoshe mikono miwili hadi kwenye viwiko mara tatu akianza na mkono wa kulia kisha kushoto.
- Kisha apanguse kichwa kuanzia mwanzo wa hadi mwisho
- Kisha atumbukize kidole cha shahada kwenye sikio aipanguse
- Kisha aoshe miguu yake miwili pamoja na vifundo mara tatu.

Kisha aseme anapomaliza Wudhuu wake: *ash-hadu an laa ilaaha illa Allahu wahdahu laa shariika lahu, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluh. Allahumma ij-alniy mina ttawwaabiina waj-alniy minal mutatwahhiriin.*

(**Nashuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake. Ewe Mola wangu, nijaalie niwe miongoni mwa wanaotubu na nijaalie niwe miongoni mwa waliotwahirika.**)

HUKUMU YA KUZIDISHA KIWANGO KILICHOPOKELEWA

Haifai kuzidisha kiwango kilichopokelewa katika Wudhuu. Kwa mfano kuzidisha zaidi ya mara tatu katika kuosha viungo au kuosha mkono hadi kwenye kwapa au kupangusa shingo.

MAMBO YANAYOAMBATANA NA NGUZO ZA UISLAMU

KWANZA: TWAHARA

KUTAYAMAM

Hii ni aina ya twahara mbadala ya maji kwa yule asiyekuwa na uwezo wa kutumia maji au amekosa maji au anahofia kuyatumia kwa sababu ya madhara ya kiafya. Inakuwa kwa kutumia mchanga.

SIFA YA KUTAYAMAM

Anuwie kisha aseme *Bismillahi* kisha apige ardhini kwa viganja viwili mara moja na apanguse uso wake na sehemu ya nje ya viganja vyake.

Wala haifai kunawa mikono kwa mchanga.



SIFA YA WAJIB YA GHUSL (KUOGA)

Anuwie kuoga na kuondoa hadith kubwa kisha aseme *Bismillahi* kisha aoge mwili mzima huku akihakikisha kuwa maji yameingia kila sehemu ya mwili; ikiwemo ndani ya nywele na asukutue pamoja na kuosha pua.

SIFA YA SUNNAH KATIKA KUOGA

Aoshe tupu mbili kisha viganja viwili kisha atawadhe kama anavyotawadha kwaajili ya sala kisha aingize maji kwenye nywele zitote kisha aoshe mwili wake upande wa kulia kisha kushoto kisha aoshe miguu.

MAMBO YANAYOWAJIBISHA KUOGA

1. JANABA: na inakuwa kwa kutokwa kwa manii kwa kuingiliana au mengine.
2. Kutokwa damu ya hedhi na damu ya uzazi
3. Kifo (isipokuwa aliyekufa katika jihad)
4. Mtu anaposilimu

MASHARTI YA KUPANGUSA SOKSI (KHUFEIN NA JAURABU)

Azivalie baada ya kutawadha Wudhuu kamili; yaani: kaosha miguu vyema katika Wudhuu wake.

Ziwe zimeundwa kwa vitu twaahir (vitu visivyokuwa najis)

Ziwe zimesitiri miguu kwa kiwango kikubwa

Iwe kupanguswa kwao ni katika hadath ndogo sio hadath kubwa.

Iwe muda wa kupangusa ni ule uliowekwa na sheria. Nayo ni: masaa ishirini na nne (**24**) kwa asiyekuwa msafiri kuanzia alipovunja Wudhuu akiwa nazo na masaa sabini na mbili (**72**) kwa msafiri kuanzia muda aliovunja Wudhuu akiwa amezivalia.

JINSI YA KUPANGUSA KWENYE SOKSI WAKATI WA KUTAWADHA

Aupitize mkono kutumia viganja kuanzia vidole vya mguu hadi karibu na muundi wa mguu; mkono wa kulia kwa mguu wa kulia na wa kushoto kwa mguu wa kushoto. Wala asipanguse sehemu ya chini ya miguu.

MASUALA YANAYOHUSIANA NA UPANGUSAJI WAKE

1. Ukiisha muda wa kupangusa au akazivua , basi Wudhuu wake unabaki wala hautenguki.
2. Inaruhusiwa kuzipangusa soksi zilizochanika au nyepesi.

ADABU ZA KUKIDHI HAJA

Inapendekezwa:-

- Anapoingia msalani, autangulize mguu wake wa kushoto na aseme: *Bismillahi. Allahumma inniy audhu bika minal khubthi wal khabaaith.*
- Na akitoka msalani autangulize mguu wa kulia na aseme: *Ghufraanaka.*

Ni **wajibu** ajisitiri wakati wa kukidhi haja na aende mbali na macho ya watu ikiwa katika jangwa

Na **sio ruhusa:-**

- Kukidhi haja barabarani au sehemu wanapoketi watu au chini ya kivuli cha mti wa matunda au sehemu ya kuwaudhi watu au kwenye maji yaliosimama.
- Kuelekea Qiblah au kuupa mgongo katika hali ya kukidhi haja.
- Kugusa utupu wake kwa mkono wa kulia.
- Kulitaja jina la Allah msalani.

Akishakidhi haja, achambe kwa maji safi au kwa kutumia mawe au mbadala. Na masharti ya kutumia mawe na mbadala ni:-

- Yawe mawe matatu au jiwe lenye pande tatu ili ajipanguse mara tatu.
- Yawe mawe/mbadala safi (yani karatasi au jiwe kavu)
- Isikuwe kujipangusa kwa kitu najis au chakula au mifupa au kinyesi.

Na ni ruhusa kukojoa hali ya kuwa amesimama kwa sharti; ule mkojo usimtonokee/rukie mwilini au kwenye nguo na asitiri uchi wake. Kwa dalili kuwa: *Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alifika kwenye makidhi ya kabila moja akakidhi haja ndogo hali ya kuwa amesimama.*

MASUALI KUHUSU TWAHARA

1. Masharti ya Wudhuu ni ngapi?

○ 9

○ 10

○ 8

2. Faradhi za Wudhuu ni

○ Viungo vinne

○ Viungo vinne pamoja na taratibu na upesi katika kuosha viungo

3. Mambo yanayotengua Wudhuu ni ngapi?

○ 6

○ 5

○ 8

4. Bainisha yafuatayo:-

    ○ Nyama ya ngamia:

    ○ Nyama ya kunguru:

    ○ Mngurumo tumboni:

    ○ Kujamba:

    ○ Kusinzia:

    ○ Kuosha maiti:

    ○ Kumgusa mwanamke:

5. Taja sifa ya Wudhuu:

……

……

……

6. Taja sifa za ghusl:

……

……

……

7. Taja hukumu ya kila lifuatalo:-

SUALA	HUKUMU
Kuitamka nia	
Kunuwia kwa Wudhuu wake sala moja	
Kutawadha kwa lengo la kusoma Kur'ani	
Kuvunja nia katikati ya Wudhuu	
Kuvunja nia baada ya Wudhuu	
Kutawadha huku anakula karoti	
Kutawadha kwa maji ya wizi	
Kutawadha kabla ya kukidhi haja	
Kupangusa sikio kwa maji mapya	
Kupangusa kichwa mara tatu	
Kuosha viungo mara tatu katika Wudhuu	
Kuosha viganja viwili katika Wudhuu	
Kulowesha ndevu	
Kujisugua katika Wudhuu	
Kuosha viungo vipasavyo kupanguswa	
Kuosha kichwa	
Kutumbukiza viganja kwenye chombo	
Kuanza kwa upande wa kulia katika Wudhuu	
Kuosha viungo zaidi ya mara tatu	
Kuosha miundi ya miguu	
Kusali baada ya kuogelea	
Kusali baada ya kuoga na bila kutawadha	

PILI: ZAKAH

AINA ZA ZAKAH:-

ZAKAH YA MALI

Hii ni nguzo ya tatu katika nguzo za Uislamu. Na ni wajibu kwa kila Muislamu aliye huru anayemiliki mali iliyofikia kiwango cha kutolewa. Na hakuna kulazimika zakah hadi itakapopitiwa na mwaka mzima isipokuwa mali inayotoka ardhini (mazao ya ukulima)

Na mali inayotolewa zakah ni ya aina nne:-

ZAKAH YA MWILI

Hii ni zakatul fitri inayotolewa baada ya kuumaliza mfungo wa Ramadhani.

Ni wajibu kutolewa kwa kila Muislamu; mkubwa kwa mdogo, kike kwa kiume, mtumwa na aliye huru.

HELA

Hii ni dhahabu, fedha na yanayotumika kama dhahabu na fedha katika miamala za kibiashara.

Kiwango cha kutoa zakah cha hela:-

Dhahabu: gramu 85

Fedha: gramu 595

MIFUGO

Hawa ni mifugo ambao huenda malishoni. Mifugo hawa ni: ngamia, mbuzi, kondoo na ng'ombe.

MAZAO YA ARDHI

Haya ni mazao yanayotoka ardhini katika mimea kwa mfano: mbegu na matunda.

BIDHAA ZA BIASHARA

Hiki ni kila kilichoandaliwa kwa makusudio ya kibiashara

WANAOPASWA KUPEWA ZAKAH

1. **FAKIRI:** huyu ni mtu ambaye hapati mahitaji yake ya dharura au anapata kisichomtosha.
2. **MASKINI:** huyu ni mwenye kupata mahitaji yake ila sio kiukamilifu.
3. **WAKUSANYA ZAKAH:** hawa ni wale waliotwikwa majukumu ya kukusanya, kuhifadhi na kuigawanya zakah kwa wanaostahiki. Na hawa sio lazima wawe maskini au fukara. Bali wanapewa hata kama ni matajiri.
4. **WALAINISHWA NYOYO:** hawa ni wale unaotarajiwa kusilimu kwao, kuzuia shari zao au kuhifadhi nguvu za imani yao.
5. **UTUMWA:-** hawa ni
   - Mtumwa Muislamu anayenunua uhuru wake kutoka kwa mola wake.
   - Kumwacha huru mtumwa Muislamu.
   - Mateka Muislamu

   Na wala haingii katika hawa, mtumwa alieachwa huru na mola wake kama zakah yake. Hili halifai.
6. **WANAODAIWA:** hawa ni
   - Aliyebeba gharama kwa lengo la kusuluhisha baina ya wagomvi.
   - Aliyebeba gharama kwa lengo la kukidhi mahitaji yake.

   Na wala haifai kumsamehe deni mdaiwa kwa lengo la kukusudiwa zakah.
7. **KWA NJIA YA ALLAH:** hii inakusudiwa chochote kinachofanywa kwa njia ya Allah ikiwemo kuwaandaa wapiganaji wa jihad na wanayoyahitaji kama silaha na mengine.
8. **MSAFIRI:** aliyekatikiwa na safari kwa kuishiwa nafaka yake ya safari. Huyu anapewa kitakachomwezesha kuikamilisha safari yake.

Inaruhusiwa kukipa kikundi kimoja katika hawa zakah, wala hairuhusiwi katika zakah kumpa tajiri wala mchumaji wala ahli zake Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, wala kizazi cha Bani Hashim na wajakazi wao wala kuwapa wale inayomlazimu lishe yao wala kafiri.

Inaruhusiwa katika sadaka ya kujitolea, kumpa yeyeto yule.

MAANA YA BAADHI YA MISAMIATI ZINAYOTUMIKA KATIKA ZAKAH

- **BINTUL MAKHAADH:** ni ngamia aliyetimiza mwaka mmoja
- **BINTU LABUUN:** ni ngamia aliyetimiza miaka miwili.
- **AL-HIQQAH:** ni ngamia aliyetimiza miaka mitatu.
- **AL-JADH^AH:** ni ngamia aliyetimiza miaka minne.
- **AT-TABI^AH KATIKA NG'OMBE:** huyu ni ng'ombe mwenye mwaka mmoja.
- **AL-MUSINNAH:** ng'ombe mwenye miaka miwili.

VIWANGO VYA KUTOA ZAKAH

AINA YA MALI	SHARTI LAKE	KIWANGO CHA MALI	KIWANGO KINACHOTOLEWA
MIFUGO WENYE LISHE HURU	Lazima ipitiwe na mwaka	Angalia jedwali ijayo	Angalia jedwali ijayo
MAZAO YA ARDHINI	Sio lazima ipitiwe na mwaka	Kilogramu 612	- Ushuru yake kama mavuno yalikuwa kupitia maji ya mvua - Nusu ya ushuru kama mavuno yalikuwa kupitia kunyunyiziwa kwa mikono. - Robo tatu ya ushuru kama mavuno yalikuwa kwa njia zote mbili.
HELA	Lazima ipitiwe na mwaka	**Dhahabu**: gramu 85 **Fedha:** gramu 595	Asilimia mbili na nusu (**2.5%**)
BIDHAA ZA BIASHARA	Lazima ipitiwe na mwaka	Italinganishwa na bei nafuu baina ya kiwango cha dhahabu gramu 85 au fedha gramu 595.	Asilimia mbili na nusu (**2.5%**)

VIWANGO VYA ZAKAH YA MIFUGO

MBUZI NA KONDOO		NGAMIA		NG'OMBE NA NYATI	
KIWANGO	**ZAKAH**	**KIWANGO**	**ZAKAH**	**KIWANGO**	**ZAKAH**
Kuanzia 40 hadi 120	Mbuzi mmoja	Kuanzia 5 hadi 9	Mbuzi mmoja	Kuanzia 30 hadi 39	Tabii^ah
Kuanzia 121 hadi 200	Mbuzi wawili	Kuanzia 10 hadi 14	Mbuzi wawili	Kuanzia 40 hadi 59	Musinnah
Kuanzia 201 hadi 300	Mbuzi watatu	Kuanzia 15 hadi 19	Mbuzi watatu	Kuanzia 60 hadi 69	Tabii^ah wawili
Zaidi ya 300	Mbuzi mmoja kwa kila mbuzi 100.	Kuanzia 20 hadi 24	Mbuzi wanne	Kuanzia 70 na zaidi	Katika kila 30 atatoa tabii^ah mmoja au katika kila 40 atatoa musinnah mmoja.
Haikubaliwi mbuzi kengeza, chongo, kipofu au mwenye aibu kubwa mwilini.		Kuanzia 25 hadi 35	Bint makhaadh		
Haikubaliwi walio chini ya kiwango cha miaka – wadogo zaidi		Kuanzia 36 hadi 45	Bint labuun		
		Kuanzia 46 hadi 60	Hiqqah		
		Kuanzia 61 hadi 75	Judh^ah		
		Kuanzia 76 hadi 90	Bint labuun wawili		
		Kuanzia 91 hadi 120	Hiqqah wawili		
		Kuanzia 121 hadi 129	Bint labuun watatu		
		Kuanzia 130 na zaidi	Katika kila ngamia 40 atatoa bint labuun mmoja au katika kila ngamia 50 atatoa hiqqah mmoja.		

MASUALI KUHUSU ZAKAH

1. Haikubaliki zakah mpaka ipitiwe na mwaka wa takwimu ya…….

○ Hijri

○ Miladi

○ Hakuna tofauti baina ya takwimu zote mbili

2. Ni mali ipi sio lazima ipitiwe na mwaka?

○ Madini

○ Mazao ya ardhini

○ Vyote viwili

3. Kiwango cha dhahabu kinachofaa kutolewa zakah ni

○ Gramu 200

○ Gramu 595

○ Gramu 85

4. Kiwango cha fedha kinachofaa kutolewa zakah ni

○ Gramu 85

○ Gramu 959

○ Gramu 595

5. Mifugo wanaotolewa zakah ni 1……2…….3……..4……5…….

6. Je inapaswa kutoa zakah katika matunda? ……

7. Mifugo wanaotolewa zakah ni wale

○ Wanaoenda malishoni huru

○ Wanaoletewa lishe zizini pasina kutoka

8. Elezea tofauti ya fakiri na maskini.

9. Fakiri anapewa katika zakah lishe inayomtosha

○ Mwaka mzima

○ Mwezi mzima

10. Wakusanya zakah ni …….

11. Kafiri anayeogopwa kwa shari zake kwa Uislamu anapewa zakah? ……

12. Je kusamehe deni kwa nia ya zakah inakubaliwa? ……..

13. Kujenga msikiti ni miongoni mwa sehemu zinazokubaliwa kutoa zakah? …….

14. Ni yupi katika wanyama hawa hatolewi zakah:-

○ Kuku ○ Paka

○ Farasi ○ Wote

15. Nyumba anayoishi mtu, kiwango cha kuitolea zakah ni ngapi?

- ○ Thamani ya dhahabu
- ○ Haitolewi zakah

16. Kila msafiri lazima apewe zakah?

- ○ Ndio
- ○ Hapana isipokuwa akiwa ni rafiki ya mkusanya zakah
- ○ Hapana

17. Taja kiwango cha zakah kwenye mali ifuatayo:-

MALI	ZAKAH
Dhahabu gramu 100	
Dhahabu gramu 200	
Dhahabu gramu 400	
Dhahabu gramu 80	
Fedha gramu 500	
Mbuzi 30	
Mbuzi 60	
Mbuzi 565	
Ngamia 4	
Ngamia 17	
Ngamia 449	
Ng’ombe 30	
Ng’ombe 49	
Ng’ombe 77	
Ng’ombe 99	
Milioni 20 Ksh.	
Kilogramu 255 za ngano	
Kilogramu 600 za mchele	

TATU: SAUM (KUFUNGA)

Saum katika asili ya kilugha inamaanisha ***kujizuia***

Katika Sheria inamaanisha ***kujizuia chakula, kinywaji na mambo yote yanayofuturisha kwa nia ya ibada kuanzia kuingia AlFajr hadi kuzama jua.***

NGUZO ZA SAUM

NIA

NIA YA SAUM YA FARADHI

Lazima mtu anuwie usiku kabla ya alfajiri ya siku ya funga ile. Na inatosheleza kunuwia mwanzo wa mwezi wa Ramadhani unapoingia.
Sehemu ya nia ni moyoni na wala haifai kuitamka maana itakuwa ni uzushi.

NIA YA SAUM YA SUNNAH

Inakubalika kunuwia wakati wowote ule wa mchana maadamu hajafanya chochote miongoni mwa vifuturishi.

KUJIZUIA NA VIFUTURISHI

AINA ZA SAUM

WAJIB

Ni aina tatu:-

1. Ramadhani
2. Kafara
3. Nadhiri

SUNNAH

Saum zote zisizokuwa za wajib.

MASHARTI YANAYOWAJIBISHA KUFUNGA

1 Uislamu
2 Akili timamu
3. Kubaleghe
4 Ukaazi (asiwe msafiri)
5 Afya
6 Kutokuwa katika hali ya kutokwa kwa damu ya hedhi au uzazi

AINA ZA MARADHI KATIKA SAUM

MARADHI YASIOTARAJIWA KUPONA

Anaingia katika kitengo hiki mzee mkongwe ambaye hawezifunga: hawa hawalazimishwi kufunga ila wanalisha maskini mmoja kila siku ya Ramadhani. Kulisha kuna njia mbili:

1. Kuwakusanya jumla ya maskini kadri ya idadi ya siku za Ramadhani ile (29 au 30) na kuwalisha wote kwa pamoja.
2. Au awape maskini wote hao kila mmoja wao chakula (kwa mfano mchele) na iwe kipimo chake gramu 610. Na akizidisha chochote ni bora.

MARADHI YANAYOTARAJIWA KUPONA

Anaingia katika kitengo hiki mwanamke katika siku za hedhi, damu ya uzazi, anayenyonyesha na msafiri. Watahesabu jumla ya siku ambazo hawakuzifunga kisha atazifunga akipata wasaa wa kufunga. Na akifa kabla ya kulitelekeza hilo deni la funga, basi litakuwa limemwondokea dhima lake.

KUINGIA MWEZI WA RAMADHANI KUNADHIBITIKA KWA KITU GANI?

Inaingia ima kwa kuonekana mbalamwezi au kukamilika mwezi wa Shabani siku 30.

MAMBO YANAYOVUNJA SAUM

1. Kula na kunywa kusudi (*akila au kunywa kwa kughafilika basi saum yake ni sahihi*)
2. Kumuingilia mwanamke kwa tendo la ndoa; ikiwa ni mchana wa saum ya Ramadhani basi inamlazimu kafara ya kumwacha mtumwa huru au kufunga siku sitini mfululizo au kulisha maskini sitini.
3. Kutokwa manii kwa kumpapasa mwanamke au kumbusu au kujichua.
4. Sindano za lishe au vinywaji au mfano wake.
5. Kutoa damu kwa njia ya hijama. Lakini kutoa damu ndogo kwaajili ya vipimo haina shida.
6. Kujitapisha
7. Kutokwa kwa damu ya hedhi au uzazi.

BAADHI YA YANAYORUHUSIWA KATIKA SAUM

Kumeza mate, kuonja chakula kwa ulimi kwa dharura, kuoga, kuswaki, marashi na kujipa baridi

BAADHI YA YANAYOPENDEKEZWA KATIKA SAUM

1 Kula daku
2 Kuchelewesha daku
3 Kuharakisha futari
4 Kufuturu kwa tende za rutab au tende za kawaida au maji na akikosa basi anuwie
5 Dua wakati wa kufuturu
6 Kuzidisha sadaka
7 Sala ya usiku
8 Kuisoma Kur'ani
9 Kutoingia katika ugomvi
10 Umrah
11 Itikafu msikitini
12 Kuutafuta usiku wa Leilatul Oadri

BAADHI YA YANAYOCHUKIZWA KATIKA SAUM

1. Kupitiliza katika kusukutua na kuingiza maji puani
2. Kuonja chakula kwa ulimi pasina haja

BAADHI YA YANAYOHARAMISHWA KATIKA SAUM

- Kumeza kikohozi (lakini haifuturishi)
- Kumbusu mwanamke kwa asiyeweza kuizuia hamu ya nafsi yake.
- Uongo na maneno ya kipuuzi
- Kutofaidika kielimu katika mafunzo ya saum
- Kuzinganisha siku mbili au zaidi za saum pasina kufuturu

SAUM ZA SUNNAH

- Kuzifunga siku sita za mwezi wa Shawwal kwa aliyekamilisha funga ya Ramadhani. Inapendekezwa azifunge kwa kufatanisha zote sita.
- Kufunga siku ya Arafa kwa yule ambaye hayuko kwenye ibada ya Hijja.
- Kufunga siku ya Ashuraa pamoja na siku kabla yake au siku baada yake.
- Kufunga kila siku ya Jumatatu na Alhamisi ya kila wiki.
- Kufunga siku tatu za kila mwezi wa Kiislamu (Tarehe 13, 14 na 15)
- Kufunga siku na kuacha siku.
- Kufunga mwezi wa Muharram.
- Kufunga siku tisa za mwanzo wa mwezi wa Dhul Hijja
- Kufunga mwezi wa Shabani (lakini asiufunge wote)

SAUM ZINAZOCHUKIZA

Kuifunga siku ya Ijumaa pekee au Jumamosi pekee au Jumapili pekee; lakini saum ya Sunnah ikiwiana na moja ya siku hizi basi ataruhusiwa kufunga.

SAUM ZINAZOHARAMISHWA

- Kuikhusisha mwezi wa Rajab kwa saum.
- Kufunga siku mbili za Eid (Eid kubwa na Eid ndogo).
- Kufunga siku ya shaka: siku asiyokuwa na uhakika kama mwezi umeonekana au la
- Kuzifunga siku tatu baada ya Eid kubwa (Tarehe 11, 12 na 13 za Dhul Hijja).
- Kufunga mwaka mzima

SHERIA ZA KULIPA DENI KWA ALIYEPITWA NA BAADHI YA MASIKU

- Inapendekezwa azifunge kwa kufatanisha
- Aharakishe kuzilipa pindi tu anapopata wasaa na uwezo wa kufunga
- Haifai kulicheleweshа deni hilo hadi Ramadhani ifuatayo bila ya dharura.
- Akicheleweshа hadi Ramadhani ifuatayo bila udhuru basi atapata dhambi

ZAKATUL FITRI (ZAKAH YA KUFUNGUA)

Inapozama jua siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani, ni wajibu juu ya kila Muislamu; mkubwa kwa mdogo, kiume kwa kike, mtumwa na aliye huru. Lazima atoe zakah yake na ya kila anayemtegemea yeye. Na anapaswa mtu kutoa kibaba cha chakula kinacholiwa kwenye mji wake.

Lengo la kuwekwa zakah hIi kwenye sharia ni:-

1. Kuziba mapungufu yaliyopatikana kwenye saum
2. Kuwasitiri na kuwakinaisha fukara na maskini ili wasiombe siku ya Eid.

MIDA YA KUTOA ZAKATUL FITRI

UNAORUHUSIWA
Kabla ya Eid kwa siku moja au siku mbili

UNAOPENDEKEZWA
Baada ya sala ya AlFajr siku ya Eid hadi kabla ya sala ya Eid.

UNAOHARAMISHWA
Baada ya sala ya Eid

KIWANGO CHA ZAKATUL FITRI

Kibaba cha chakula kinacholiwa kwenye mji wake na haipaswi kutoa pesa au vitu vingine ambavyo sio vyakula.

KIBABA ni kilogramu mbili na gramu arbaini (2 kg 40 grams)

SALA YA EID

Ni faradhi kwa kila mmoja ila mwenye udhuru. Inasaliwa sala hii ya Eid baada ya kuchomoza jua kadri ya urefu wa mkuki na muda wake unaisha linapoanza kupinda jua. Na atakayepitwa na sala hii haina kulipa. Na katika Sunnah, sala hii inafaa isaliwe kwenye uwanja; nje ya majengo. Inaruhusiwa kuisali msikitini kwa dharura ya mvua na dharura zingine.

Inafaa mtu ale tende kwa idadi ya witri au ale chochote kile kabla ya kusali eid, ajitwahirishe na kujisafisha, ajifukize kwa manukato mazuri au marashi, avalie mavazi mazuri na aelekee kwenye mswala kwa njia moja na akirudi arudi kwa njia nyingine. Na haina shida kupongezana kwa kusema ***Taqabbala Allahu minnaa wa minkum*** **(**Allah aitakabali amali yetu**).**

Na inapendekezwa katika Sunnah mtu kuzidisha Takbir kuanzia usiku ule wa Ramadhani kukamilika na kila baada ya sala za faradhi pia azidishe hadi kusali Eid.

TAKBIR YA EID

Allahu akbar, Allahu akbar. Laa ilaaha illa Allah. Allahu akbar, Allahu akbar wa lillaahil hamd.

Sala ya Eid inasaliwa rakaa mbili kabla ya khutbah: katika rakaa ya kwanza, analeta takbiratul ihraam kisha analeta takbir sita baadake. Na katika rakaa ya pili, analeta takbir tano baada ya Takbir ya wakati wa kusimama kutoka sijda ya pili kabla ya kusoma Fatihah.

MASUALI KUHUSU SAUM

1. Nguzo za saum ni ngapi?

○ 2

○ 3

○ 4

2. Saum ni wajibu kwa mtu mwenye sifa nne hizi:-
   1……
   2……
   3……
   4……
3. Kila mgonjwa haruhusiwi kufunga? ……..
4. Elezea hukumu ya mambo yafuatayo yanayohusiana na saum:-

JAMBO	HUKUMU YAKE
Kunuwia saum baada ya Alfajr	
Kufunga bila nia	
Saum ya mtoto	
Saum ya msafiri	
Saum ya mwanamke mwenye damu ya uzazi	
Saum ya mzee mkongwe	
Kula akiwa amefunga	
Sindano za lishe	
Dawa za maji za macho	
Sindano ya dawa	
Kutoa damu kwa njia ya hijama	
Kutapika	
Kumeza mate	
Kuonja chakula ili kujua kama kina chumvi	
Kulala mchana wa Ramadhani	
Kuoga mchana wa Ramadhani	
Kupumzika sehemu kwa nia ya ubaridi na upepo	
Kufukiza udi na ubani mchana wa Ramadhani	
Kupiga mswaki mchana wa Ramadhani	
Mtu anapaswa kula nini daku?	
Mtu anapaswa kufuturu kwa kitu gani?	
Sala ya Taraweh	
Umrah mwezi wa Ramadhani	
Kupitiliza katika kusukutua	
Kuunganisha saum siku mbili bila kufungua	

Kufunga siku sita za mwezi wa Shawwal	
Kufunga siku ya Arafa	
Kufunga siku ya shaka	
Kufunga siku ya Eid	
Kufunga siku tatu baada ya Eid kubwa (11, 12 na 13)	
Kufunga mwezi wa Muharram	
Kufungwa mwezi wa Rajab wote	
Kufunga mwaka	
Kufunga siku ya Ijumaa pekee	
Kuchelewesha deni ya saum hadi Ramadhani ifuatayo	

NNE: HIJJA

Hijja ni nguzo ya tano katika nguzo za Uislamu. Na ni ibada ya lazima kwa kila aliyetimiza masharti haya yote: Muislamu, akili timamu, aliye huru, mwenye uwezo. Na mwanamke anazidishiwa sharti lingine; awe na mahram wake akihitajia kusafiri kwa ibada ya Hijja..

Na **NGUZO ZA HIJJA** ni nne:-

IHRAAM

Hii ni nia anayoitia mtu wakati wa kuianza ibada ya hijja. Inakuwa sehemu maalum baadi ya kuvaliza mavazi ya ihram.

KUSIMAMA ARAFA

Kusimama katika uwanja wa Arafa siku ya tisa ya mwezi wa Dhul Hijja kuanzia kupinda kwa jua hadi kuchomoza kwa alfajiri siku ya Eid kubwa. Amesema Mtume, "*Hijja ni Arafa*"

TWAWAAF IFAADHWA

(Twawaaf ya ziara)

Inakuwa ruhusa kuifanya kuanzia baada ya kusimama Arafa.

SA^YI

Kukimbia baina ya milima ya Swafa na Marwa

AINA ZA KUITEKELEZA IBADA YA HIJJA

TAMATTU^

Hii ni kutia nia ya umrah kisha akatekeleza umrah kiukamilifu mwanzo katika miezi ya Hijja. Kisha anavalia tena mavazi ya ihraam na kutia nia ya Hijja ili kuingia kwenye ibada ya Hijja.

Na huyu inamlazimu kuchinja.

QIRAAN

Hii ni kutekeleza ibada ya umrah na Hijja kwa pamoja.

Huyu pia inampasa kuchinja.

IFRAAD

Hii ni kutekeleza ibada ya Hijja pekee.

MAMBO YANAYOWAJIBISHWA KATIKA KUTEKELEZA IBADA YA HIJJA

Atakayewacha moja katika mambo haya basi anailipa kwa kuchinja mbuzi na kuigawa baina ya maskini wa mji wa Makkah. Na haifai yeye kula katika nyama ile. Wajibu hizi ni:-

- Kuhirimia na kuvaa mavazi ya Ihraam kwenye miiqaat (sehemu maalum)
- Kusima kwenye uwanja wa Arafa hadi kuzama jua (kwa atakayesimama mchana)
- Kulala kwenye uwanja wa Muzdalifa
- Kulala kwenye uwanja wa Mina usiku kuanzia Eid hadi mwisho wa siku za kuchinja
- Kurusha mawe (jamaraat)
- Kunyoa nywele au kuzipunguza

Twawaf ya kuaga kwa anayetaka kuondoka Makkah hata lau ni baada ya mwezi. (isipokuwa mwanamke mwenye hedhi au damu ya uzazi)

NYAKATI NA SEHEMU ZA HIJJA NA UMRAH

NYAKATI

- Miezi ya Hijja ni:- Shawwal, Dhul Qa^adah na Dhul Hijja.
- Ibada ya Hijja ina mwezi wake maalum
- Ibada ya Umrah haina wakati maalum

SEHEMU

- **DHUL HULAIFAH:** ni kwa watu wa Madinah na watakaopitia Madinah.
- **JUHFA:** ni kwa watu wa kanda za Syria, Misri na watu wanaotoka magharibi.
- **QARNUL MANAAZIL:** kwa watu wa Najd
- **YALAMLAM:** kwa wanaotoka Yemen.
- **DHAATA IRQ:** kwa wanaotoka Iraq

MAMBO YANAYOPENDEKEZWA KATIKA KUTEKELEZA IBADA YA HIJJA

- Kuoga na kujifukiza marashi kabla kuhirimia na kuvaa mavazi ya Ihraam kwenye miiqaat (sehemu maalum)
- Kuvaa mashuka mawili (shuka na kikoi) meupe ya ihraam kwa wanaume.
- Kukata kucha na baadhi ya nywele (kama kuna haja) kabla ya kuvaa mavazi na kabla ya kutia nia ya ihraam.
- Kuleta talbiya kuanzia kunuwia ihraam hadi kuanza kurusha mawe (jamaraat)
- Twawaaf ya Kufika (Kwa qaarin na ifraad)
- Kutembea upesi katika twawaaf ya Kufika
- Kupitisha ncha za shuka chini ya kwapa la kulia katika twawaaf ya Kuingia.
- Kutanguliza katika kujumuisha baina ya sala ya Maghrib na sala ya Isha.
- Kulala kwenye uwanja wa Mina usiku wa Arafa
- Kuibusu Hajarul Aswad (*jiwe nyeusi kwenye nguzo ya kulia ya Kaabah*)
- Kusimama kwenye uwanja wa Muzdalifa kwenye sehemu shiari tukufu kuanzia alfajiri hadi kupambazuka.

MAMBO YANAYOKATAZWA BAADA YA IHRAAM

Ni mambo tisa:-

Kunyoa nywele za kichwa na mwili, kukata kucha, kufunika kichwa kwa kitu kilichoshikana na kichwa kwa wanaume, nguo linalotenganisha viungo kwa wanaume, wanawake kuvaa nikabu na glavu, kujifukiza marashi au kutumia sabuni zenye manukato, kuwinda na kuwaua wanyama wa porini, kufunga ndoa au kufungisha ndoa, kufanya tendo la ndoa au kuhamasishana hisia bila kufanya tendo.

Atakayefanya haya kwa kusahau au kutojua au kulazimishwa basi hana dhambi isipokuwa atakayewinda au kumuua mnyama mwitu basi atalipa fidia sawa na alichokiua.

Ama atakayefanya mambo haya kwa kusudi basi kuna hali nne zitakazozingatiwa:-

KISICHOKUWA NA FIDIA

Kufunga au kufungisha ndoa. Na pia kuhamasisha hisia bila tendo la ndoa pasina kutokwa na manii. Haya yanahitaji tauba wala hayana fidia.

CHENYE FIDIA MFANO WAKE

Kuwinda au kumuua mnyama mwitu.

Basi mtu huyu atalipa fidia mfano wa kile alichokiua au kukiwinda. Waadilifu wawili watakitathmini alichokiua.

CHENYE FIDIA NZITO

Kufanya tendo la ndoa.

Atakayemuingilia mke wake kabla ya uhalalisho wa ibada wa mwanzo basi huyo imeharibika Hijja yake na inamlazimu kuikamilisha na atairudia mwaka mwingine.

Na inamlazimu kichinjo.

CHENYE FIDIA YA UDHIO

Mambo mengine yaliyobakia. Fidia yake atachagua baina ya kufanya moja katika matatu haya:-

- Kufunga siku tatu
- Kulisha maskini sita kila mmoja wao pishe ($^1/_2$kg)
- Kuchinja mbuzi na kuigawa kwa maskini wa Makkah.

MAJINA YA SIKU ZA HIJJA

1. **TARWIYAH:** hii ni siku ya nane ya mwezi wa Dhul Hijja. Walikuwa masahaba wakibeba maji kupeleka uwanja wa Mina.
2. **ARAFA:** hii ni siku ya kisimamo. Na inakuwa siku ya tisa ya mwezi wa Dhul Hijja.
3. **EID NA NAHR:** hii ni siku ya Eid kubwa. Ni siku ya kumi ya mwezi wa Dhul Hijja
4. **QARR:** siku ya kumi na moja ya mwezi wa Dhul Hijja (siku ya kwanza ya Tashriiq)
5. **FARRI YA KWANZA:** siku ya kumi na mbili ya mwezi wa Dhul Hijja. Siku hii wanarahusiwa kikundi cha kwanza wenye haraka kuondoka.
6. **FARRI YA PILI:** siku ya kumi na tatu ya mwezi wa Dhul Hijja. Siku hii waliobaki wanarahusiwa kuondoka; ni siku ya mwisho katika ibada za Hijja.

SEHEMU MUHIMU ZA KUOMBEA DUA KATIKA IBADA YA HIJJA

ARAFA	MUZDALIFA	RAMYU	TWAWAAF	SA^YI
Katika uwanja wa Arafa, siku ya Arafa, baada ya jua kupinda hadi magharibi.	Siku ya Arafa baada ya alfajiri hadi kupambazuka.	Baada ya kurusha mawe (ndogo na za kati)		Katika mbio za Swafa na Marwa na sehemu baina yao.

SIFA YA HIJJA NA UMRAH

Amesema Sheikh Muhammed bin Swalih Uthaimin, Allah amrehemu:

Akifika mtu kwenye miiqaat basi aoge na ajifukize manukato na marashi mwilini na kichwani. Kisha ahirimie (avalie mavazi ya ihraam na anuwie anachokikusudia katika Hijja au umrah). Kisha aende Makkah kwa talbiyah. Akifika msikiti mtukufu wa Makkah aanze twawaaf kwa kuizunguka Kaabah mara saba. Na afahmu kuwa msikiti wote ni sehemu anaweza kufanyia twawaaf, lakini akiweza kufanyia karibu na Kaabah ni bora zaidi kama haitoleta maudhi au msongamano. Akimaliza twawaaf, atasali rakaa mbili nyuma ya masimamo ya nabii Ibrahim (*maqaam Ibrahiim*) kwa ukaribu au mbali; la muhimu ni kuwa masimamo yawe baina yake na Kaabah. Kisha baada ya hapo, ataenda kwenye Sa^yi aanze na mlima wa Swafa akielekea Marwa; mara saba. (Swafa hadi Marwa ni mara moja na kutoka Marwa kuja Swafa ni nyingine). Akishamaliza apunguze

nywele zake za kichwani kwa usawa na haifai kupunguza baadhi ya pande na kuziacha zingine.
Ikifika siku ya nane ya Dhul Hijja, aoge, ajifukize na ahirimie kwaajili ya Hijja sehemu alipo. Kisha aelekee Mina asali huko sala ya Dhuhur, Asr, Maghrib, Isha na Fajr (kwa kupunguza sala za rakaa nne ziwe mbili).
Ikichomoza jua siku ya Arafa, wataondoka kwa unyenyekevu kuelekea uwanja wa Arafa huku wakizidisha utajo na talbiyah. Watajumuisha sala ya Dhuhur na Asr kwa muda wa Dhuhur pamoja na kuzifupisha. Kisha watatokomea kwenye kumuomba Allah na kujikurubisha Kwake na ajitahidi mtu awe kwenye hali ya twahara na aelekee Qiblah kama ilivyo kwenye sheria. Na awe makini sana aizingatie mipaka ya uwanja wa Arafa na alama zake kwa sababu wingi wa mahujaji wanadhani wamesimama uwanjani Arafa kumbe wako nje ya uwanja na wakaikosa Hijja. Kwa sababu anasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Hijja ni arafa*". Na uwanjani Arafa kote kunaruhusiwa kusimama isipokuwa ndani ya bonde.
Jua likizama kiuhakika, aondoke kuelekea Muzdalifa kwa utulivu na unyenyekevu kama ilivyoamrishwa. Wakifika huko Muzdalifa, watasali Maghrib na Isha kisha watapumzika hadi AlFajr na haruhusiwi mtu yeyote kutoka kabla ya AlFajr isipokuwa wenye udhaifu au majukumu ya huduma.
Akishasali Fajr, ataelekea Qiblah kwa utajo na dua hadi kupambazuke vyema kisha ataondoka kuenda Mina. Atakusanya mawe madogo saba aelekee Jamara Kubwa, iliyoko mwisho karibu na Makkah, arushe mawe yale kwa Takbir kila akirusha kimoja. Ahakikishe mawe yote yametumbukia kwenye ukanda ule wa nguzo la Jamara.
Akimaliza, atachinja kwa kuzingatia masharti ya uchinjaji na inaruhusiwa amwakilishe mtu kumtekelezea shughuli ile ya uchinjaji. Kisha atanyoa nywele zote za kichwani kwa usawa baada ya kuchinja na haifai kunyoa baadhi ya sehemu tu. Na mwanamke ananyoa nywele kidogo tu kadri ya kichwa cha kidole cha gumba. Na akitimiza hayo basi atakuwa amefikia uhalalisho wa mwanzo. Basi hapo anaweza akavaa mavazi ya kawaida, kukata kucha, kujifukiza marashi isipokuwa tu haruhusiwi kufanya tendo la ndoa. Kisha ataelekea msikitini kabla ya sala ya Dhuhur afanye twawaaf na sa^yi, kisha atarudi Mina. Kwa kutimiza twawaaf hiyo na sa^yi atakuwa ameingia uhalalisho wa pili ambapo sasa amehurusiwa kila kitu hata kufanya tendo la ndoa na mkewe.
Enyi watu! Hakika ya mambo anayoyafanya mtu siku ya Eid katika ibada ya Hijja ni mambo manne kuu: kuchinja kisha kunyoa kisha twawaaf na sa^yi. Na huu ndio utaratibu bora lakini akitanguliza yeyote katika mambo hayo mbele ya nyingine haina tatizo. Na lau akichelewesha kuchinja hadi siku ya kumi na tatu ya Dhul Hijja hakuna tatizo pia.
Kisha kwa siku atakazokuwa Mina atarusha mawe ishirini na moja kila siku kwa kila jamara mawe saba. Na anaruhusiwa kuondoka baada ya kurusha mawe siku ya 12.
Na akitaka kuondoka Makkah, aende afanye twawaaf ya kuaga isipokuwa tu kwa mwanamke mwenye hedhi na damu ya uzazi.

MASUALI KUHUSU HIJJA

1. Hijja ni lazima kwa mwenye sifa hizi:
   1……
   2……
   3……
   4……
2. Mwanamke ana ziada ya sharti moja ambalo ni …….
3. Nguzo za Hijja ni ngapi?

○ 2

○ 3

○ 4

4. Ihraam katika nguzo za Hijja inamaanisha ……
5. Twawaaf ni nini? ……..
6. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alifanya Hijja ngapi? …….
7. Watu wa Madinah wanahirimia Yalamlam. ……. (sahihi / sio sahihi)
8. Mwezi maalum wa Umrah ni Ramadhani. …….(sahihi / sio sahihi)
9. Ni wajibu mtu kutekeleza Hijja mara ngapi katika umri wake?

○ Kila mwaka

○ Mara tatu

○ Mara moja

○ Kila mwezi

10. Watu wa Makkah wanahirimia wapi? ……
11. Mwanamke anavalia mavazi ya ihraam meupe. …… (sahihi / sio sahihi)
12. Je. inafaa mwanamke kuvaa nguo lililoshonwa lenye kutenganisha viungo?
13. Haifai kufunga mkanda/mshipi kwa mwanamume. …….(sahihi / sio sahihi)
14. Hijja inaanza siku ya …… na kuisha siku ya ……..
15. Kusimama katika uwanja wa Arafa ni

○ Nguzo

○ Sharti

○ Wajib

16. Je ni lazima mtu kuupanda mlima wa Arafa? ……..
17. Ni lazima qaarin kuchinja. ……. (sahihi / sio sahihi)
18. Je Hijja ya mtoto inakubaliwa? ……..
19. Je Hijja ya mwanamke bila mahram wake inakubalika?
20. Kukopa deni ili kuenda Hijja inakubalika?

SOMO LA KUMI NA TANO

KUSIFIKA KWA TABIA NJEMA

Kila Muislamu ni wajibu asifike kwa tabia njema za kidini. Miongoni mwa tabia njema ni: kuwa mkweli, kutunza amana, kuzuia matamanio, kuwa na haya, ushujaa, ukarimu, utekelezaji ahadi, kujiepusha na alichoharamisha Allah, ujirani mwema, kusaidia wenye haja kadri ya uwezo na mengineo katika tabia njema zilizofunzwa kwenye Kur'ani na Sunnah.

UFAFANUZI MFUPI WA BAADHI YA TABIA HIZI

- **UKWELI:** awe mkweli na Allah katika maneno yake, vitendo vyake na itikadi yake. Pia awe mkweli na waja katika kuamiliana nao. Kinyume chake ni uongo.
- **AMANA:** hii ni faradhi kubwa na jukumu kubwa alilojitwika mwanadamu. Kinyume chake ni khiana.
- **KUJIZUIA MATAMANIO:** kujizuia kuangukia katika makatazo.
- **HAYA:** ni jambo linalompelekea mtu kufanya nzuri na kuachana na mabaya.
- **UJIRANI MWEMA:** na katika ujirani mwema ni kuhifadhi macho na kutoangalia na kutochunguza siri na madhaifu ya jirani.
- **KUSAIDIA WENYE HAJA:** amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*atakaye muondoshea ndugu yake uzito miongoni mwa uzito wa duniani basi Allah atamuondolea uzito wa siku ya Kiyama……na atakayesitiri aibu ya Muislamu basi Allah atasitiri aibu yake siku ya Kiyama*" (Ameipokea Muslim)

SOMO LA KUMI NA SITA

KUISHI KWA ADABU ZA KIISLAMU

Miongoni mwa adabu za Kiislamu ni: kutoa salamu, bashasha, kula kwa mkono wa kulia, kunywa kwa mkono wa kulia, kutaja jina la Allah mwanzo wa kila jambo, kumshukuru Allah baada ya kumaliza jambo, kumhimidi Allah baada ya kupiga chafya, kumuombea mpiga chafya akishukuru, kumzuru mgonjwa, kufuata jeneza kwaajili ya sala na mazishi, adabu za kisheria wakati wa kuingia nyumbani na kutoka, nwakati wa safari, ukiwa na wazazi na familia na ukoo, majirani, waliokuzidi umri na wadogo zako, kumpongeza aliyeruzukiwa mtoto, kumtakia baraka aliyefunga ndoa, kumliwaza aliyefiwa na adabu zingine katika mavazi.

UFAFANUZI MFUPI WA BAADHI YA ADABU HIZI

- **SALAMU:** kumtolea salamu anayemjua na asiyemjua na kujibu salamu akisalimiwa.
- **KULA NA KUNYWA KWA KULIA:** ni wajibu kula na kunywa kutumia mkono wa kulia na vilevile kukabidhi au kupokea kitu. Na ale kilicho karibu naye wala asiwe na tamaa wala pupa.
- **JINA LA ALLAH KWA KILA JAMBO:** alitaje jina la Allah kabla ya kuanza jambo lolote ili liwe na baraka na kheri ndani yake.
- **KUMSHUKURU ALLAH BAADAKE:** arudishe shukrani kwa Allah akishamaliza jambo lile ili Allah apate kumzidishia.
- **AKIPIGA CHAFYA:** aseme *Alhamdu Lillah*
- **KUMUOMBEA MPIGA CHAFYA:** mpiga chafya akisema *Alhamdu Lillah* basi yeye amwambie *Yarhamuka Allah* (Allah akurehemu)
- **KUMZURU MGONJWA:** azidishe ziara yake kwa mgonjwa kwa nyakati zinazofaa. Wala asiketi sana akamuudhi na wala asimkatishe tamaa na rehema za Allah.
- **KUFUATA JENEZA:** inaruhusiwa kwa wanaume na sio ruhusa kwa mwanamke.
- **KUINGIA NA KUTOKA MSIKITINI:** autangulize mguu wake wa kulia na aseme: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillah. Allahumma iftah lii abwaaba rahamtika*
  (***Kwa jina la Allah. Rehema na amani zimwendee mjaWake na Mtume Wake. Mola wangu nifungulie milango ya rehema Yako.***)
  Na akitoka autangulize kushoto na aseme: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillah. Allahumma inniy as-aluka min fadhlika.*
  (***Kwa jina la Allah. Rehema na amani zimwendee mjaWake na Mtume Wake. Mola wangu nakuomba unipe katika fadhila Zako***)
- **KUTOKA NYUMBANI:** atangulize mguu wa kulia wakati wa kuingia na wakati wa kutoka na asome nyiradi za kuingia na zile za kutoka nyumbani.

SOMO LA KUMI NA SABA

KUJITAHADHARISHA NA SHIRKI NA AINA ZA MAASI

Kuhadhari na kujitahadhirisha kutokana na shirki na aina za maasi:

Miongoni mwake **MADHAMBI SABA KUBWA** ambayo ni: shirki, uchawi, kuua nafsi bila haki, kula riba, kula mali ya yatima, kutoroka uwanja wa jihad na kuwasingizia zinaa wanawake waumini waliojihifadhi.

Na miongoni mwa madhambi pia ni: kuwaasi wazazi wawili, kukata undugu, ushahidi wa uongo, kiapo cha uongo, kumuudhi jirani, kuwadhulumu watu katika damu, mali na heshima zao, ulevi, kucheza kamari, kusengenya, kufitinisha watu na mengine aliyoyakataza Allah na Mtume Wake.

UFAFANUZI MFUPI WA BAADHI YA YALIYOTAJWA

- **SHIRKI:** inakusanya shirki kubwa na shirki ndogo.
- **UCHAWI:** atakayefanya uchawi au akaridhia uchawi basi amekufuru. Na inaharamishwa kuwaendea wachawi au kuwazuru ili kushuhudia mambo yao au kutizama vipindi vyao, kusoma jarida lao au kujihusisha kwenye miradi yao. Na haifai kutengua uchawi kwa kutumia uchawi bali uchawi hutenguliwa kwa ruqya ya kisheria na mafunzo yaliyopokelewa.
- **UUWAJI WA NAFSI BILA HAKI:** haifai kuuwa nafsi ya Muislamu wala kafiri. Inaruhusiwa kuuwa nafsi kwa sababu tatu: akiua nafsi, akiritadi au akizini hali ya kuwa ameoa/ameolewa.
- **KULA MALI YA YATIMA:** yatima ni yule aliyempoteza (kufa) babake yake kabla ya kubaleghe.
- **KUTOROKA UWANJA WA JIHAD:** jeshi walioko vitani.
- **KUWASINGIZIA ZINAA WAUMINI:** waliojihifadhi.
- **KIAPO CHA UONGO:** vilevile kuapa kwa asiyekuwa Allah au kaburi.
- **KAMARI:** kila aina ya kamari ambayo ina chumo lililokatazwa kisheria.
- **KUSENGENYA:** ni kumtaja ndugu yako kwa lile asilolipenda
- **KUFITINISHA WATU:** kuhamisha maneno baina ya watu kwa nia ya kusababisha ugomvi baina yao.

HUKUMU YA MASHINDANO

YALIYOHARAMISHWA

Kamari kwa aina zake zote za kitambo na za kisasa.

INARUHUSIWA KWA MBADALA NA BILA MBADALA

Kama mashindano ya mbio za farasi na ngamia

INARUHUSIWA BILA MBADALA NA HAIRUHUSIWI KWA MBADALA

Michezo yote kando na zilizotajwa

SOMO LA KUMI NA NANE

MAANDALIZI YA MAITI, SALA YAKE NA MAZISHI

Maandalizi ya maiti ni kwa mambo yafuatayo:-

KWANZA : inafaa kumkaririsha maiti (talqiin) ya shahada kwa kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*wakaririsheni maiti wenu laa ilaaha illa Allah*" maana ya maiti katika hii ni yule mtu yupo kwenye kitanda cha mauti/ yamemfika wakati wa kuaga dunia.

PILI : ikisha kuwa uhakika kuwa amekufa, basi afungwe macho yake.

TATU : ni jambo la lazima kuoshwa maiti wa Kiislamu isipokuwa tu yule aliyekufa katika uwanja wa jihad; huyu haoshwi wala hasaliwi na atazikwa katika mavazi yake aliokufa nayo. Dalili ya hili ni kuwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, hakuwaosha waliokufa kwenye vita vya Uhud wala hakuwasalia.

NNE : SIFA YA KUMUOSHA MAITI: asitiriwe uchi wake, kisha anyanyuliwe kidogo ili kulikamua tumbo lake kwa utaratibu. Kisha muoshaji ataweka funda la maji mkononi ili amchambishe maiti. Kisha atatawadhishwa kama Wudhuu wa sala. Kisha atakoshwa kichwa chake na ndevu zake kwa maji na kafuuri au chochote kile katika vitu vyenye harufu nzuri. Kisha ataoshwa ubavu wake wa kulia kisha wa kushoto. Kisha ataoshwa hivyo pande zote mbili kwa mara tatu; katika kila muosho, ataupitiza mkono wake tumboni taratibu ili kuhakikisha hakuna uchafu utokao tumboni. Uchafu ukitoka atausafisha na ukizidi kutoka basi atamziba tundu zile kwa pamba au udongo au njia ya kisasa kisha atamtawadhisha tena. Na isipotosheleza kumuosha mara tatu basi muoshaji atazidisha kadri ya haja. Kisha atamkausha maji mwilini kutumia ngua au kitambaa kisha atamnyunyizia marashi mwilini hasa chini ya kwapa, baina ya mapaja na kwenye viungo vya sijda. Kisha sanda zake zitafukizwa kwa udi au ubani. Ikiwa masharubu yake au kucha zake ni ndefu basi zitakatwa. Na zikiachwa pia hamna tatizo. Wala asinyolewe nywele za kichwani wala za sehemu za siri wala asitahiriwe.

TANO : KUMKAFINI MAITI: iliyo bora ni kumkafini maiti wa kiume kwa sanda tatu (billa kanzu wala kilemba) kama alivyokafiniwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake; kila sanda inaingizwa ndani ya nyingine. Na ikiwa ni maiti ya kike basi atakafiniwa kwa sanda tano: dera, shungi, mtandio na shuka mbili.

Inatosheleza kumkafini mtoto kwa sanda moja hadi tatu.

Na pia inatosheleza (wajib) maiti yeyote kuvishwa sanda moja ikitosha kuusitiri mwili mzima.

Ikiwa maiti mwanamume alikufa katika ibada ya hijja basi ataoshwa kwa maji na kafuuri na atakafiniwa kwa mavazi yake ya ihraam au mavazi mengine bila kufunikwa kichwa wala uso wala kufukizwa marashi kwa sababu atafufuliwa siku ya Kiyama hali ya kuwa anatoa utajo.

Lakini ikiwa ni maiti mwnamke aliyekufa katika ibada ya Hijja, basi huyu atakafiniwa kama maiti wengine wa Kiislamu bila kufukiziwa marashi wala kufunikwa usoni kwa nikabu wala kuvishwa glavu lakini atafungwa kwa mavazi aliyokuwa amevaa kama ilivyotangulia.

SITA **:** wenye haki zaidi katika kumuosha maiti ni: aliohusiwa na maiti kisha babake kisha babu yake kisha wa karibu katika wanaume hadi mwisho ikiwa maiti ni mwanamume. Ikiwa maiti ni mwanamke, basi wenye haki zaidi katika kumuosha ni: aliohusiwa na maiti kisha mamake kisha bibi yake kisha wa karibu hadi mwisho katika wanawake.

Ni ruhusa baina ya wana ndoa wawili kuoshana akifa mmoja wao kama vile Abubakar, Allah awe radhi naye, alivyooshwa na mkewe na kama vile Ali, alivyomuosha mkewe Fatuma, Allah awe radhi nao.

SABA **:** sifa ya sala ya jeneza: inakuwa na Takbir nne: Baada ya Takbir ya kwanza atasoma suratul Fatihah; na akisoma baadake surah nyingine fupi pia haina tatizo. Kisha baada ya Takbir ya pili atamsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. kisha baada ya Takbir ya tatu atamuombea maiti dua akisema: *Allahumma ighfir lihayyinaa wa mayyitinaa, wa shaahidinaa wa ghaaibinaa, wa swaghiirinaa wa kabiirinaa, wa dhakarinaawa unthaanaa. Allahumma man ahyaitahu minhu fa-ahyihi alal Islaam. Wa man tawaffaitahu minnaa fatawaffahu alal iimaan. Allahumma ighfir lahu wa-r-hamhu wa aafihi wa\fu anhu wa akrim nuzulahu, wa wassi' mudkhalahu, wa-ghsilhu bilmaai wa thalji wal barad. Wa naqqihi minal khatwaayaa kamaa yunaqqaa th-thaubul abyadh mina ddanas. Wa abdillhu daaran khairan min daarihi, wa ahlan khairan min ahlihi, wa adkhilhul jannah wa a-idh-hu min adhaabil qabri wa adhaabi nnaar. Wa-f-sah lahu fii qabrihi wa nawwir lahu fiihi. Allahuma laa tahrimnaa ajrahu wa laa tudhwillunaa ba'dahu*. Kisha ataleta Takbir ya nne atatoa salamu moja upande wakulia. Katika Sunnah ni imam asimame upande wa kichwa cha maiti ikiwa maiti ni wa kiume na katikati ya mwili wa maiti akiwa wa kike.

NANE : Sifa ya kuzika: katika sharia inafaa kuchimba kaburi fiti sita na ndani kuchimbwe mwanandani (*lahd*) ikielekea Qiblah. Maiti alazwe kwenye mwanandani kwa ubavu wake wa kulia pamoja na kulegeza kanda zilizoshikilia sanda bila ya kutolewa. Wala haipaswi maiti kufunuliwa uso awe mwanamke awe mwanamume. Kisha ataegezewa udogo wa matope au tofali la kushikilia mwili usipinde au chochote kile au mbao kisha kumwaga mchanga. Inapendekezwa kusema wakati wa kumuingiza maiti kaburini: *Bismillahi wa alaa millati rasuulillah.* Kaburi lifukiwe na linyanyuliwe kadri shibiri moja na liwekwe alama kuonyesha kaburi na kunyunyiziwa maji ikiwezekana.

TISA : inaruhusiwa kwa yule ambaye hakuwahi sala ya jeneza, atamsalia baada ya kuzikwa kama alivyofanya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. (lakini iwe ndani ya mwezi mmoja baada ya mazishi)

KUMI : haifai familia ya maiti kuandaa chakula cha hitma isipokuwa kwa sababu ni kinyume na mafunzo ya dini. Bali ni wajibu wa ndugu zao na majirani kuwaandalia familia.

KUMI NA MOJA : haifai mwanamke kukaa hidda ya kuomboleza karibu wake zaidi ya siku tatu isipokuwa tu mumewe ambaye ataketi miezi mine na siku kumi. Isipokuwa kama mumewe alikufa akiwa mjamzito baasi hidda ya (kukaa ndani bila ya kujipamba) hadi ajifungue.

Ama mwanamume, hana kuketi hidda kabisa.

KUMI NA MBILI : inaruhusiwa wanaume kuzuru makaburi kwa lengo la kuwaombea wafu, kuwatakia rehema na kujikumbusha na akhera kama alivyosema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Zuruni makaburi, hakika kuzuru huko kutawakumbusha akhera.*" Na alikuwa akiwafunza masahaba zake wakizuru makaburi waseme: *Assalamu aleikum ahla diyaar minal mu'miniina wal muslimiin. Wa innaa in shaa Allah bikum laahiquun. Nas-alu Allaha lanaa wa lakumul aafiyah. Yarhamu Allahu almustaqdimiina wal musta'khiriin.*

Wala hawaruhusiwi wanawake kuzuru makaburi kwa kaui ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, "*Wamelaaniwa wanawake wenye kuzuru makaburi.*" Na kwa sababu pia wanawake ni wepesi wa kufitiniwa na wepesi wa subira. Na vivyo hivyo hawapaswi kufuata jeneza hadi makaburini kwa katazo la Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.

Na ni ruhusa kusaliwa maiti msikitini au kwenye muswala kwa wa kike na kiume.

Kwa haya machache, Allah atuwafikishe katika kila kheri na atusamehe kwa kila kosa.

AINA ZA ZIARA MAKABURINI

ZIARA YA KISHIRKI	ZIARA YA KIZUSHI	ZIARA YA KISHERIA
Ziara kwa nia ya kumuomba au kumuabudu au kujikurubisha kwa maiti kwa kutaka msaada wake.	Ziara kwa nia ya kumuomba Allah kwenye makaburi.	Ziara kwa nia ya kujikumbusha akhera. Wala haifai kufunga safari kwa sababu kuenda kuzuru makaburi. Na anapozuru makaburi basi awaombee wafu na awatakie rehema na asifanye jambo linaloenda kinyume na sharia.

MASUALI KWA YALIYOTANGULIA

1. Kuhifadhi nidhamu na adabu za kidini ni katika tabia za Muislamu……. (sahihi / sio sahihi)
2. Dini yangu inaniamrisha kufanya urafiki na waovu. …….. (sahihi / sio sahihi)
3. Uislamu unatufunza kuwa wema katika kuamiliana na watu. (sahihi / sio sahihi)
4. Je. Inaruhusiwa kufanya urafiki na mtu mwenye kuwaudhi watu?
5. Akinishtumu mtu inafaa nimshtumu pia. …….. (sahihi / sio sahihi)
6. Uislamu unatufunza kuwasaidia wenye haja na wenye madhaifa……. (sahihi / sio sahihi)
7. Katika haki za Muislamu juu ya Muislamu mwenzake ni kumzuru akiwa mgonjwa? …….
8. Kuchunguza siri za majirani ni katika mafunzo ya dini yetu…… (sahihi / sio sahihi)
9. Ni mtu yupi anayependwa na Allah zaidi?
10. Dua ya kutoka nyumbani ni ipi? ……..
11. Dua kwa mpiga chafya ni gani? ……..
12. Nyiradi anazozihifadhi Muislamu zinamkurubisha kwa Allaha. …… (sahihi / sio sahihi)
13. Dalili za kuonyesha unampenda ndugu yako Muislamu ni? ……
14. Katika upungufu wa imani: kumhusudu ndugu yako Muislamu?
    ……
15. Aina za mapenzi ni ……
16. Je. Ni haramu mtu kutumia kilevi? ……
17. Inachukiza kupumulia chakula au kinywaji…… (sahihi / sio sahihi)
18. Inaruhusiwa kuramba vidole baada ya kula…….. (sahihi / sio sahihi)
19. Sifa ya mavazi ya Kiislamu ni …….
20. Ni nani mwenye haki sana kumuosha maiti? ……
21. Kulipa deni za maiti ni

- ○ Lazima
- ○ Inapendekezwa
- ○ Inaruhusiwa

22. Hukumu ya kumzika maiti ni

- ○ Inapendekezwa
- ○ Lazima
- ○ Faradhi ya kutosheleza ikifanywa na baadhi ya watu

23. Hukumu ya kumlakinisha maiti shahada ni

- ○ Lazima
- ○ Sunnah
- ○ Haramu

24. Kumuosha maiti ni …….
25. Maiti anafaa kuvuliwa sanda akiwekwa kaburini? ……
26. Haifai wanandoa wawili kumuosha mwenziwe akifa…….. (sahihi / sio sahihi)
27. Atakayepitwa na sala ya jenenza …….
28. Kupiga mayowe msibani ni ……
29. Maiti anaelekezwa Qiblah ndani ya mwanandani……. (sahihi / sio sahihi)

SHERHE YA KITABU

AL-USULU – THALATHA NA DALILI ZAKE

(MISINGI MITATU YA IMANI)

BISMILLAH RAHMAN RAHIM

Kwa hakika kila sifa njema ni milki yake **Allah**. Nasi tunamsifu na tunamuomba msaada na tunamtaka msamaha, tunajilinda kwa **Allah** na shari zote zitokanazo na nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu.

Yeyote ambaye ameongolewa na **Allah** basi hakuna yeyote atakae mpoteza na yule aliyempoteza hakuna wa kumuongoa.

Ninashahadia ya kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa ila ni **Allah** pekee asiye na mshirika Na nashuhudia ya kuwa **Muhammad** swalalahu walaih wasalam ni mja wa **Allah** na mtume wake.

Ama ba'ada

YALIYOMO.

AL-USULU – THALATHA NA DALILI ZAKE.

NO.	MAUDHUI	UKURASA
1	UTANGULIZI	
2	MAMBO MANNE YA MSINGI	
3	MAMBO MATATU YA MSINGI	
4	UMUHIMU WA KUSOMA TAUHID	
5	AL-USULU – THALATHA	
6	HITIMISHO	
7	MUHTASARI YA SHERHE YA KITABU	
8	MAZOEZI YA AL-USULU THALATHA NA DALILI ZAKE	

UTANGULIZI:



SABABU YA KUKICHAGUA KITABU HIKI KUWA CHA MWANZO KATIKA KUJIFUNZA (TAUHID)

- Ni kushughulika waja wema waliotangulia na wanachuoni wetu katika ahlul sunna waljamaa kukifundisha kitabu hichi kilichobarikiwa kutokana na yale yaliyomo ndani yake katika manufaa na faida kubwa ambazo zimekifanya kitabu hiki kuwa ni msingi atakaoutumia mwanafunzi na atajenga juu yake paa lake zima la elimu ya kisheria, basi kwa hali hiyo na sisi tunawafuata waja wema waliotangulia na tunapita kwenye nyendo zao katika kufuata mfumo huu (wa kuanza na kitabu hiki kujifunza).
- Na kama ilivyo pia kwa watu wote hawatajitosheleza na elimu hii ya (Tauhid) kabla ya kukisoma kitabu hiki na maudhui zote zilizo ndani yake zinazoeleka misingi ambayo ni lazima kila muumini aiamini kwa imani ya kweli isiyo na chembe ya shaka yoyote.

UBORA NA UPEKEE WA KITABU HIKI ALICHOKIANDIKA MTUNZI WAKE
(Allah amrehemu)

Wepesi wa lafdhi zake na uwazi wa ibara zake	Anataja masaili mbalimbali yakiambatanishwa na dalili zake	Anakusanya masaili anayopanga na kuyawekea idadi kisha ndio anaanza kuyasherehesha	Kukithirisha sana dua kwa kila anayesoma na kusikiliza utunzi wa vitabu vyake

KUITAMBUA MISINGI MITATU YA IMANI.

Kwa ufupi misingi mitatu ni yale maswali matatu atayoulizwa mtu kaburini.

1. ***Nani Mola wako?***
2. ***Ipi dini yako?***
3. ***Yupi Mtume wako?***

Ni nusra ipi tutakayoipata ikiwa tutaisoma hii misingi?

Bila shaka yoyote utakapoisoma hii misingi mitatu, kisha ukaifanyia kazi na ukailingania kwa wengine, ikiwa umefanya subra katika kusoma, kutenda na kulingania biidhinillahi utayajibu maswali haya kaburini

YALIYOMO KWENYE KITABU HIKI CHA MISINGI MITATU:

Kitabu hiki kimegawanywa katika sehemu kuu tano nazo ni:-

1. MAMBO MANNE YA MSINGI KATIKA SURATUL-ASRI
2. MAMBO MATATU YA MSINGI KWENYE VIGAWO VYA TAUHID
3. UMUHIMU WA KUJIFUNZA ELIMU YA TAUHID
4. MISINGI MITATU YA IMANI (MASWALI YA KABURINI)
5. HITIMISHO

1. MAMBO MANNE YA MSINGI

1. Kutafuta elimu
2. Kuifanyia kazi elimu
3. Kulingania elimu hiyo
1. Kuwa na subira kwa maudhi yote wakati wa kulingania

2. MAMBO MATATU YA MSINGI

2. Tauhid Rububiya na Tauhid Asmai wa sifati
3. Tauhid Uluhiya (Tauhid ya ibada)
4. Kujitenga mbali na shirki na wenye kufanya shirki (kwa kutumia ulimi, moyo na viungo)

3. MUHIMU KUJIFUNZA TAUHID

Hili ni jawabu la swali hili: Kwanini tunajifunza Tauhid?

4. MISINGI MITATU

Kwa ufupi misingi mitatu ni maswali matatu ya kaburini

- Ni nani Mola wako
- Ni ipi dini yako
- Nani Mtume wako

5. HITIMISHO

Ni kuanzia kauli ya mtunzi wa kitabu Allah amrehemu

"WATU WATAKAPOKUFA WATAFUFULIWA TU" mpaka mwisho wa kitabu hiki.

JAMBO LA KWANZA

MAMBO MANNE YA MSINGI:

Bismillah Rahman Rahim.

Tambua ewe Muislamu **Allah** akurehemu inakupasa kujifunza mambo manne ya msingi:

1. Kutafuta elimu nako ni kujifunza kumjua **Allah,** na Mtume wake ***(swalla llahu alayhi wasallam)*** na kuijua dini ya Uislamu kwa dalili.
2. Kuifanyia kazi elimu (baada ya kusoma)

HIZI NDIZO SABABU ZA MTUNZI KUANZA KWA BISMILLAH

1. Ni kwaajili ya kukifuatisha kitabu cha Allah (Qur'an) na kuwaiga Mitume (rehema na amani ziwe juu yao)
2. Kuwaiga waja wema na wanachuoni waliopita ambao ilikuwa ni ada yao kuanza na Bismillah katika utunzi wa vitabu vyao
3. Pia ni katika mlango wa kutabaruku kwa jina tukufu la Allah aliyetukuka.

Kama tulivyoonesha kwenye utangulizi ya kwamba ilikuwa ni ada ya Sheikh Mtunzi wa kitabu kuanza kwa kuwaombea dua wanafunzi na kuwaombea kwa Allah awarehemu na kwa ibara ifuatayo ni ushahidi tosha juu ya hilo.

Huruma ya wanachuoni wa Ahlu Sunna waljamaa ipo kwa wanafunzi wao, nayo ni kwa sababu dini ya Uislamu imejengwa katika misingi ya rahma.

ELIMU NI NINI?

Elimu ni kuitambua haki kupitia dalili zake, na kinyume chake ni ujinga (kutoitambua haki kwa dalili)

Pamesemwa kwenye ubainifu wa mahusiano kati ya elimu na matendo. "Elimu huyasemeza matendo ikiwa yatakubali elimu itakaa (kwa mtu huyo) na ikiwa matendo yatagoma kuifata elimu basi elimu huondoka kwa ajili hiyo hakuna faida yoyote ya elimu isiyo na matendo, pale mwanafunzi anapojifunza inampasa aifanyie kazi elimu yake na kama hakufanya hivyo anakuwa sawa sawa na mayahudi wanayo elimu lakini hawaifanyii kazi. Amesema Allah "Wale tuliowapa kitabu wanayajua haya kama wanavyowajua watoto wao 2:147" Na watu wa mwanzo kabisa watakao chomwa moto ni wa aina tatu, miongoni mwao ni mjuzi aliyojifunza elimu lakini hakuifanyia kazi, Amesema mshairi "Na kila mjuzi ambaye hakufanyia kazi elimu yake, Ataadhibiwa kwanza kabla ya washirikina."

3. Kuilingania hiyo elimu. (Haki)

KULINGANIA KUNA SHARTI NA KANUNI NI LAZIMA UZIFUATE NA ZA MUHIMU KABISA NI HIZI ZIFUATAZO:

1. Iwe huko kulingania ni kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah
2. Kulingania huko kuwe kumejengwa katika misingi ya elimu ya kisheria
3. Da'wa iwe kwa hekima na subira
4. Kutimie kuchunga hali zote za wanao linganiwa

DALILI YA SHARTI HIZI NI KAULI YAKE ALLAH (Subhanahu wataala)

Sema hii ndio njia yangu ninayolingania kwa **Allah** kwa ujuzi mimi na wanaonifuata, Na ametakasika **Allah** wala mimi si katika washirikina. 12: 109

SEMA HII NDIO NJIA YANGU …… Kinachokusudiwa hapa ni sharia aliyokuja nayo Mtume swalalahu walaih wasalam

NINALINGANIA KWA **ALLAH**…….. Mwenye kulingania hasa kwa **Allah** ni Yule mwenye Ikhlasi ambayo lengo lake ni kuwafikisha watu kwa **Allah.**

KWA UJUZI…… (BASIRA) ni elimu na basira ya hapa inakusanya

Elimu ya sharia | **Hali ya mlinganiwa** | **Njia yenye kufikia lengo**

Bila shaka Mtunzi (Sheikh) Allah amrehemu anasema:

Utakaposima kisha ukaifanyia kazi elimu inakupasa upite kwenye njia ambayo aliyoipita Mtume ***swalla llahu alayhi wasallama*** na masahaba pamoja na waja wema waliotangulia, kwa sababu Allah amesema:-

"Sema hii ndio njia yangu ninayoilingania kwa **Allah**, kwa (kutumia) ujuzi mimi pamoja na wanaonifuata ……. Kwa mujibu wa aya hii ni lazima kufanya da'wah

4. Kuvumilia maudhi katika mchakato wote wa kiutendaji.

Na dalili ya hoja hii ni kauli yake **Allah.**

"Naapa kwa zama

(1) Hakika binadamu bila shaka yumo katika hasara.
(2) Isipokuwa tu wale walioamini na wakatenda mema na wakausiana kwa haki na wakausiana kusubiri

1. Mwandishi (Sheikh) Allah amrehemu baada ya kuizungumzia da'awah na subira utadhani anakuambia haya: Hakika Yule ambaye anapita njia hii yatampata mambo mengi tu kama yalivyowapata mitume – Alayhimu-salammu kwa hali hii ni lazima mtu awe na subira.

SUBIRA.

Na kisheria subira ni kuifunga nafsi iweze kutelekeza maamrisho au kuacha makatazo

Kwa lugha ya kiarabu subira ni kifungo

IMAMU IBNUL QAYYIM (ALLAH AMREHEMU) AMEIGAWA SUBIRA KATIKA VIGAWANYO VITATU.

1. Kufanya subira katika kumtii Allah ili kuitekeleza twaa (utiifu) ipasavyo
2. Kufanya subira kutokumuasi Allah ili kujiepusha na madhambi
3. Kufanya subira juu ya qadari za Allah zinazoleta majonzi.

2. BAADA YA MWANDISHI KUTAJA MAMBO MANNE YA MSINGI AKATAJA DALILI ZAKE KUTOKA NDANI YA QUR'AN NAYO NI SURATUL-ASRI NA MARA ZOTE MWANDISHI AMEKUWA AKITAJA MASAILI MBALIMBALI AKIAMBATANISHA NA DALILI ZAKE. UNAJUA SABABU?

1. Ili amlee mwanafunzi kufuata mambo kwa dalili si kwa taqlidi (kibubusa)
2. Ili mwanafunzi awe na hoja madhubuti atakazozitumia kumpinga kila anayeenda kinyume na dalili.
3. Ili mwanfunzi awe na uwezo wa kuzitohoa hukumu kutoka kwenye dalili zake juu ya misingi maalum.

Amesema Imamu Shafii (Allah amrehemu) "Lau Allah asingeteremsha hoja yoyote kwa waja wake isipokuwa sura hii (suratul Asri) ingeliwatosheleza."

Na amesema Imamu Bukhari (Allah amrehemu. *"Huu ni mlango wa kujifunza elimu kabla ya kusema na kutenda, na dalili juu ya hilo ni kauli yake Allah! Basi tambua ya kwamba hapana anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah na omba msamaha kwa dhambi zako na za waumini wanaume na waumini wanawake"*

Allah amrehemu Imamu Shafii makusudio yake ni kwamba Sura hii tu peke yake inatosha kusimamisha hoja kwa viumbe ili wajifunze watende walinganie na wafanye subira.

Ikiwa sura hii moja tu inajenga hoja hizo je kwa sura zingine zilizo bakia kwenye Qur'an hali ikoje? Basi Qur'an yote ni hoja.

Amiri Muuminina kwenye fani ya hadithi ameweka mlango kwenye kitabu chake SAHIHUL-BUKHAR. Akasema:

Huu ni mlango wa elimu kabla ya kusema na kutenda na akaitaja dalili ….. Hivyo kwanza kabisa ni wajibu kusoma kabla ya kusema na kutenda. Haifai mtu yeyote kutenda jambo bila ya ujuzi, na ikiwa mtu huyo atatenda bila ujuzi juu ya jambo hilo huyo atakuwa sawa sawa na wakristo.

JAMBO LA PILI

MAMBO MATATU YA MSINGI (KATIKA UISLAMU)

Tambua ewe mwanafunzi "Allah akurehemu" ni kwamba inampasa kila muislamu wa kike na wa kiume kujifunza mambo haya matatu na kuyafanyia kazi hapa katika mambo

Mwandishi ameanza kwenye hii sehemu ya kitabu hiki kwa kumuombea dua.

Amemuombea dua mwanafunzi kwenye kitabu hiki katika sehemu tatu.

Mwanzoni alipoanza kuelezea mambo manne ya msingi kisha matatu ya msingi, na sehemu ya tatu ni katika Tauhid iliyonyooka"

UTANGULIZI KABLA YA KUSHEREHESHA MAMBO MATATU:

TAUHID

Tauhid kwa mujibu wa lugha ya kiarabu ni neno lenye maana ya kukifanya kitu kuwa kimoja (Kukipwekesha).

Tauhid kisheria: Ni kumpwekesha Allah katika ibada zote zinazomuhusu yeye tu katika Rububiyya, Uluhiyya na majina na sifa zake.

TAUHID INAGAWANYIKA VIGAWANYO VITATU

AL-RUBUBIYYAH:

Nako ni kumpwekesha Allah kwenye matendo yake, kama vile kuhuisha, kufisha, kuruzuku, kuumba, kuendesha ulimwengu n.k

AL-ULUHIYYA:

Huku ni kumpwekesha Allah kwenye ibada zote tunazozitenda.

AL-ASMAI WAS-SIFATI:

Huko ni kumpwekesha Allah kwenye majina na sifa zake alizojisifia kwenye Qur'an au kwenye ulimi wa Mtume wake. Bila kubadilisha maana zake au kuzigeuza au kuzijengea taswira au mifano na viumbe

JAMBO LA KWANZA LA MSINGI:

Bila shaka Allah ndiye aliyetuumba na akaturuzuku wala hakutuacha bure bali alitutumia mtume kwa atakaye mtii mtume huyo ataingia peponi na atakae muasi ataingia motoni. Na dalili yake ni kauli ya Allah (Hakika sisi tumemtuma kwenu mtume aliyeshahidi juu yenu kama tulivyomtuma mtume kwa Firauni lakini Firauni alimuasi mtume huyo basi tukamshika mshiko wa mateso (AL-MUZAMIR) (16:17)

MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE YANA MIPAKA HUCHUNGWA MAANA ZAKE KWA MUJIBU YALIVYOKUJA KWENYE QUR'AN NA SUNNA.

- Nako ni kuthibitisha majina na sifa ambazo Allah ameithibitishia nafsi yake au alimthibitishia mtume wake.
- Kukanusha majina na sifa ambazo Allah amezikanusha juu yake au amemkanushia mtume wake ***swalla llahu alayhi wasallama*** kama vile kusahau, kusinzia, kuchoka n.k. Inapasa kuamini haya bila ya kubadilisha maana ya majina na sifa zake, au kuzigeuza au kuzijengea taswira na kuzifanyia mifano kwenye viumbe.

UFUPISHO WA MAMBO MATATU YA MSINGI

JAMBO LA KWANZA.

Ni kumpwekesha Allah kwenye matendo yake na majina na sifa zake tukufu

JAMBO LA PILI.

Kumpwekesha Allah kwenye Ibada.

JAMBO LA TATU.

Ni kujitenga mbali kabisa na kila shirki pamoja na washirikina.

Katika jambo la kwanza mwandishi Allah amrehemu amethibitisha ndani yake kumpwekesha Allah katika matendo yake na pia katika majina na sifa zake. Ya kuwa Allah pekee ndio Muumba mtoaji wa riziki na hakutuacha bure bali alitutumia Mtume ili kutufundisha maamrisho na makatazo

LENGO KUU LA ALLAH SUBHANAHU WATAALA KUTUMA MITUME (AMANI ZIWE JUU YAO)

Kuwasimamishia hoja viumbe wake. Allah subhanahu wataala amesema: “Sisi hatuadhibu mpaka tumpeleke mtume.” 17:16

Kuwarehemu viumbe wake. “Nasi hatukukutuma ila uwe ni reheme kwa walimwengu wote”. 21:108.

JAMBO KUU LA PILI NDANI YAKE KUNA KUTHIBITISHA HAKI YA KUABUDIWA KWA ALLAH MTUKUFU.

2. Hakika Allah haridhii kushirikishwa na yeyote kwenye ibada zake, si kwa malaika wala mtume yeyote.

Na dalili ju ya hilo Allah amesema:

Na hakika misikiti ni ya Allah, Basi msimuabudu yeyote pamoja na Allah (72:19)

Amesema mwandishi Allah amrehemu. Hakika Allah haridhii kushirikishwa pamoja naye yeyote, si mtume, walii, jinni, malaika, mja mwema au mwingine yeyote hata aweje!

KATIKA NENO MASAJIDI KUNA KAULI TATU AMBAZO INAFAA

1 Misikiti iliyojengwa kwa lengo la kuabudiwa Allah peke yake ndani ya misikiti hiyo

2 (Masajidi) Linachukua maana ya viungo vyote vya kusujudia.

3 ARDHI: Amesema mtume swalalahu walaih wasalam na Ardhi imefanywa kwangu kuwa ni msikiti na sehemu ya kujitaharishia

JAMBO KUU LA TATU.

Hakika yeyote atakae mtii mtume ***swalla llahu alayhi wasallama*** na akampwekesha Allah subhanahu wataala Haifai kabisa kwa mtu huyo kuwafanya kuwa marafiki wale wote wenye kumpiga vita Allah na mtume wake hata kama atakuwa ni ndugu yake wa karibu mno.

Dalili yake Allah anasema: "Huwakuti watu walio muamini Allah na siku ya mwisho wanawapenda wanao mpinga Allah na mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao au jamaa zao.

Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa roho itokayo kwake: Na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito kati yake humo watakaa milele, Allah awe radhi nao na wao wawe radhi naye.

Hao ndio Hizbullah kundi la Allah. Hakika kundi la Allah ndilo lenye kufanikiwa. (58:22)

KWENYE JAMBO KUU LA TATU MWANDISHI AMEBAINISHA WAJIBU WA KUJITENGA MBALI NA SHIRKI NA WASHIRIKINA.



1. KWA MOYO:

Ni kuwachukia makafiri na sikukuu zao na sherehe zao na hasa zinazoambatana na mambo ya shirki na bidaa mbalimbali walizo nazo.

2. KWA ULIMI:

Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu (43:26)

Sema: Enyi makafiri (1) Siabudu mnacho kiabudu (2) Wala nyinyi hamuabudu ninaye muabudu (3) Wala sitaabudu mnacho abudu (4) Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu (5) Nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu (6) (109:1-6)

3. KWA VIUNGO:

Ni kutoshirikiana nao kwenye sherehe zao au kucheza nao au kuvaa kama wao, au kufuata itikadi yeyote waliyonayo.

JAMBO LA TATU

UMUHIMU WA KUJIFUNZA TAUHID

Tambua ewe mwanafunzi! Allah akuongoze: Hakika Tauhid iliyonyooka ni mila ya Nabii Ibrahim.

Nako ni kumuabudu Allah pekee na kumtakasia dini yake, na kwa ajili hiyo ndio Allah amewaamrisha watu wote na amewaumba kwa ajili hiyo tu. Kama alivyosema:

Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. (51:57)

Na maana ya waniabudu hapa wanipwekesha (kwenye ibada zangu).

Na amri kuu aliyoiamrisha Allah ni Tauhid. Nako ni kumpwekesha Allah kwenye ibada. Na katazo kuu alilolikataza ni shirki nako ni kumchanganyia Mungu mwingine katika kumuabudu Allah.

TAUHID ILIYONYOOKA

Kilugha imetoholewa katika neno hanafi lenye maana ya kuegemea upande.

Ama kisheria:

Hiyo ni mila iliyoacha upande wa shirki na imeelekea upande wa Ikhlasi, Tauhid na Imani

Nyenyekevu kwa Allah mwongofu) (16:120)

Kwa maana amemwelekea Allah na ameipa mgongo shirki.

Muongofu ni Yule anaeifuata Tauhid muda wote na anajitenga mbali na shirki

Hapa mwandishi ameweka wazi sababu kwanini tujifunze Tawhid. Na tumeishataja umuhimu wa kujifunza hapo nyuma

UTAMBULISHO WA TAUHID KAMA TULIVYOUTAJA KWENYE UTANGULIZI

Tauhid kilugha inatokana na asili ya neno (wahhada) pale mtu anapokifanya kitu kinakuwa pweke.

Tauhid kisheria ni kumpwekesha Allah na vyote vinavyo muhusu kwenye kila Tauhid Rububiyya, Uluhiyya na Tauhid ya majina na sifa zake tukufu

Amesema mtunzi wa kitabu na maana ya neno "waniabudu" ni wanipwekesha. Na maana hii ndio kauli ya Ibn Abbasi Allah amridhie pale aliposema: Hakika kila neno Ibada ndani ya Qur'an lina maana ya Tawhid (upwekeshaji). Katika aya hii "Na mwabuduni Mola wenu Mlezi" maana yake ni Mpwekesheni Mola wenu……. Na maana ya aya hii: Enyi watu muabuduni Mola wenu Mlezi…. (Mpwekesheni).

JAMBO LA NNE

MISINGI MITATU (YA IMANI):

Utakapoambiwa! Ni ipi misingi mitatu ambayo ni lazima kwa kila mtu aitambue?

Basi wewe sema: Ni kumjua Allah, Dini yake na Mtume wake Muhammad ***(swalla llahu alayhi wasallam)***

Mtunzi Allah amrehemu ameanza kwa kuitaja misingi mitatu ambayo ndio maswali matatu ya kaburini.

Na akaamsha umakini wa msomaji au atakae sikia swali hilo na kisha akalijibu swali hilo mwenyewe

Pale utapoambiwa: Ni nani Mola wako mlezi? Basi useme: Allah ndio Mola wangu mlezi ambaye ndio aliyeniumba akanilea na kuwalea watu wote (viumbe wote) kwa neema zake, na yeye tu ndio ninae muabudu sina ninaye muabudu zaidi yake. Na dalili juu ya hilo ni kauli yake Allah subhanahu wataala Sifa zote njema zinamstahiki. Allah Mola mlezi wa viumbe wote. Na ukimtoa Allah subhanahu wataala vilivyosalia vyote ni viumbe vyake na mimi ni miongoni mwa viumbe hao.

Kwa hapa mtunzi anaweka bayana msingi wa kwanza, akabainisha ya kuwa Mola mlezi anayestahiki kuabudiwa ni Allah pekee na akaitaja dalili yake ni kauli ya Allah subhanahu wataala Sifa zote njema zinamstahiki Allah Mola mlezi wa viumbe wote"

Ne "Rabbu" maana yake ni muabudiwa. Na aya hii imebeba maana zote tatu za aina za Tauhid.

AL-HAMDU:

Ndani yake kuna ithibati za Tauhid ya majina na sifa (za Allah).

LILLAHI:

Ndani yake kuna ithibati ya Tauhid ya Ibada (Uluhiyya)

RABBI:

Ndani yake kuna ithibati ya Tauhid ya utendaji wa Allah subhanahu wataala

Ukimtoa Allah subhanahu wataala vyote vilivyosalia ni viumbe, na mimi nikiwa ni kiumbe basi ni lazima itoe shukrani za dhati kwa Muumba mwenye kuneemesha na mwenye hisani subhanahu wataala

Ikiwa utaambiwa: Kwa dalili zipi umeweza kumjua Mola wako mlezi?

Basi wewe utasema: Nimemjua Mola wangu kupitia ishara zake na viumbe vyake, na miongoni mwa ishara zake ni usiku na Mchana, Jua na Mwezi na miongoni mwa viumbe vyake ni Mbingu saba na Ardhi saba na viumbe vyote vilivyomo ndani yake na viumbe vyote vilivyomo kati ya Mbingu na Ardhi.

DALILI ZAKE NI KAULI YAKE ALLAH

"Na katika ishara zake ni usiku na mchana na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Allah aliye viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu yeye tu. (41: 37).

NA KAULI YAKE ALLAH SUBHANAHU WATAALA

Hakika Mola mlezi wenu ni Allah aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akatawala juu ya kiti cha enzi. Huufunika usiku upesiupesi. Na jua, na mwezi,

Mwandishi ameanza kutaja mkusanyiko wa ishara za maumbile na viumbe ambavyo vinafahamisha uwepo wa Allah, na ndizo zinazothibitisha ya kuwa, hakuna Mola mlezi muabudiwa yeyote anayestahiki kuabudiwa isipokuwa ni Allah, na akaleta dalili juu ya haya kutoka ndani ya Qur'ani kama zilivyotajwa kwenye matini ya kitabu.

Kila kiumbe kilichopo ni alama tosha ya kuwepo Allah subhanahu wataala

Lakini Imam ametofautisha kati ya ishara na kiumbe, kwa sababu ishara inabadilika kama vile mchana na usiku.

Na chochote kinachobadilika kinakuwa ni dalili yenye nguvu kushinda kila ambacho hakibadiliki.

Katika aya hii ya 21 iliyopo kwenye suratul-Baqarah, wamesema baadhi ya wanachuoni: Hakika aya hii ndani yake ndio kuna wito wa kwanza ndani ya Qur'an (Enyi watu).

Na nyota zinazotumika kwa amri yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Allah, Mola mlezi wa viumbe vyote. (7:54) 1

NA MAANA YA RABBU NI MWABUDIWA, NA DALILI YAKE NI:-

Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliyekuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu ili mpate kuokoka (21)

(Allah) ambaye amekufanyiaeni hii ardhi kuwa tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu: Basi msifanyie Allah washirika na hali nyinyi mnajua (22)

Ibn Kathir Allah amrehemu amesema: Yule aliye viumba vitu vyote hivi huyo ndio anayestahiki kuabudiwa.

Na aina za ibada ambazo Allah subhanahu wataala ameziamrisha ni kama vile Uislamu, Imani na Ihsani, na miongoni mwa ibada ni kuomba, khofu, kutaraji,

Na ndani ya aya hiyo ndiyo kuna kitendo cha kwanza cha kuamrisha ndani ya Qur'an (Abuduni) Pwekesheni.

Na ndani yake ndio kuna katazo la kwanza ndani ya Qura'n, (Basi msimfanyie Allah washirika na hali nyinyi mnajua). Hilo ni katazo la shirki.

3- Yule aliye pekee kwenye Tauhid ya matendo ndio anayepaswa kupwekeshwa kwenye Tawhid ya ibada.

Mtunzi ameifatisha kauli ya Ibn Kathiri kwa kutaja idadi ya ibada za moyoni na za kiwiliwili pamoja na kuweka dalili kutoka kwenye Qur'an ya kila amali kwa mpangilio ufuatayo:-

MAOMBI HUGAWIKA KAMA IFUATAVYO:-

DUA YA IBADA.

Hiyo ni kila ombi linalofanywa kimatendo kama kuswali, kufunga, kuhiji,

DUA YA HAJA.

Hilo ni kila ombi linalo ombwa kwa maneno tu. Kama kusema: nisamehe, nirehemu

Kumtegemea, kumpenda, kuwa na khofu, kunyenyekea, kuogopa, kurejea, kuomba msaada, kuomba ulinzi, kuomba uokovu, kuchinja, kuweka nadhiri, na mengineyo miongoni mwa aina mbalimbali za ibada alizoziamrisha Allah. Ibada zote hizo zinamstahiki Allah peke yake na dalili yake ni kauli yake Allah subhanahu wataala

(Na hakika misikiti yote ni yake Allah basi msimuabudu yeyote pamoja na Allah)

Yeyote atakaye ipeleka ibada yoyote katika hizo kwa asiye kuwa Allah subhanahu wataala basi atakuwa ni mushiriki kafiri, na dalili juu ya hilo kauli yake Allah:

(Na anayemuomba pamoja na Allah Mungu mwingine hana ushahidi wa hili, basi bila shaka hisabu yake iko kwa Mola wake mlezi. Kwa hakika makafiri hawatafanikiwa. (23:117).

Kuyapeleka maombi hayo ya kimatendo kwa asiyekuwa Allah subhanahu wataala hiyo ni shirki kubwa

Hukumu ya maombi ya maneno ndani yake kuna ufafanuzi, nayo inagawanyika vigawanyo viwili kama ifuatavyo:-

DUA YA HAJA (MAHITAJI) INAGAWANYIKA SEHEMU KUU MBILI

kwenye mambo ambayo hakuna mwenye uwezo nayo isipokuwa Allah subhanahu wataala pekee kuyapeleka maombi hayo kwa mwingine. Hiyo ni shirki kubwa.

Kwenye mambo ambayo yamo ndani ya uwezo wa binadamu itafaa ila kwa kufuata masharti yafuatayo:

MASHARTI YA MAOMBI YA HAJA

1- Yule anayeombwa ni lazima awe hai, kufuatana na sharti hili linamtoa maiti haitofaa kumuomba.

2- Yule anayeombwa awepo, (Mbele ya muombaji) Kwa sharti hili linamtoa asiyekuwepo, aliyembali na muombaji

Na imekuja katika hadithi

“Dua ndio ubongo wa kila ibada”

Na dalili ni kauli ya Allah subhanahu wataala

Na Mola wenu mlezi amesema niombeni nitakuitikieni, kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu mimi wataingia Jahannamu wadhalilike. (40:60)

3- Yule mwenye kuombwa ni lazima awe na uwezo wa kulitenda ombi hilo. Kwa sharti hili linamtoa kila asiye na uwezo wa kulifanya ombi hilo

4- Muombaji aitakidi ya kuwa Yule muombwaji yeye ni sababu tu katika kutenda siyo ndio mwezeshaji kwa dhati yake.

Ama muombaji akiitakidi ya kuwa huyu anayeombwa ana uendeshaji wa siri (Uliofichikana) wa huu ulimwengu, tena ana uwezo wa kuleta manufaa na kuondoa madhara (mabalaa). Hii itakuwa ni shirki kubwa.

NB: Sisi tunajifunza hukumu ya matendo tu, ama hukumu ya mtendaji inahitajia kumsimamishia hoja (dalili) na kusiwepo pia shubha.

Na wanachuoni wao ndio wanaostahiki kutoa hukumu ya mtendaji kuwa yeye ni muumini (kwa kutenda jambo Fulani) au ni kafiri.

WAMEGAWANYIKA WATU KWENYE KUITAKIDI KWENYE SABABU KATIKA VIGAWANYO VITATU.

Kigawanyo cha kwanza.

Wanaitakidi, na wanajaalia yale aliyoyajaalia **Allah Subhanahu Wataala** kuwa ni sababu sababu. Na hii ndio sahihi

Kigawanyo cha pili.

Wanaitakidi na wanajaalia yote ambayo hakuyajaalia **Allah Subhanahu Wataala** kuwa ni sababu sababu. Na hii ni shirki ndogo

Kigawanyo cha tatu.

Wanaitakidi ya kwamba hakika sababu yenyewe kwa dhati yake ina athiri na kwa kupitia hiyo sababu inaleta manufaa na inaondoasha madhara. Basi hii ndio shirki kubwa.

Sababu za kisheria	Sababu za hisia
Ni kama vile kufanya Rukiya ya kisheria hakika amejaalia **Allah Subhanahu Wataala** Ruqya ya kisheria kuwa ni sababu ya kuondoa	Ni kama vile kutumia dawa kwa hakika amejaalia **Allah** dawa kuwa ni sababu ya kujitibu

Hadithi: (dua ni ubongo wa ibada) Hadithi hii ni dhaifu na ilio sahihi ni kauli ya Mtume ***swalla llahu alayhi wasallama*** (Dua ndio ibada)

Vipi dua iwe ni ibada?

Aya ndio inayojulisha hivyo: (Na Mola wenu mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni, kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.) Amesema **Allah Subhanahu Wataala** (kuniabudu mimi) kwa hiyo hii ni Dalili ya kwamba dua ni ibada.

(1) Khofu: Nayo ni athari inayopatikana kwa kuchelea jambo ambalo ndani yake kuna maangamizi, au kuna madhara, au kuna maudhi. Na Allah Subhanahu Wataala amekataza kuwakhofia viongozi wa masheitani. Na akaamrisha kumkhofia yeye

Na dalili ya khofu ni kauli yake Allah Subhanahu Wataala (Basi msiwaogope bali niogopeni mimi mkiwa nyinyi ni waumini)(1)

Na dalili ya kutaraji ni kauli yake Allah Subhana Wataala (Mwenye kuraraji kukutana na mola wake mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya mola wake mlezi.) (2)

KHOFU ZIPO AINA TATU

Khofu ya Ibada na kuadhinisha, na ya siri: Nayo ni kumkhofia mwenye kuabudu yule anayeuabudu, ndani yake kuna kujidhalilisha na kunyenyekea, na kumtukuza muabudiwa. Khofu ya namna hii ni wajibu kwa Allah, na kuielekeza kwa mwingine asiekua Allah ni shirki kubwa.

Khofu ya kimaumbile. Nayo ni kama vile mwanadamu anapo muogopa simba, moto, adui au mnyama anaeshambulia…. Khofu ya namna hii ni halali.

Khofu iliyoharamishwa. Ni kama vile kukata tamaa katika rehma za Allah. Au kumtii kiumbe katika kumuasi muumba.

(2) Kutarajia.

Kutarajia ni kutamani ya mwanadamu kwa jambo lililokua karibu kupatikana. Na mda mwingine huwa linakua mbali kupatikana lakini hulishusha kama vile lipo karibu

kupatikana. Matarajio ambayo ndani yake kuna kujidhalilisha na kunyenyekea hayatatakiwi kuwepo kwa mtu isipokua kwa ajili ya Allah Subhanahu Wataala.

Na kuyaelekeza matarajio ya namna hiyo kwa asiekua Allah Subhanahu Wataala jambo hilo ni shirki kubwa.

Hivyo matarajio yenye kushukuriwa na kupendwa yanakuwa kwa Yule atakae mtii Allah. Na akatarajia thawabu, au akatubia kwa maasi yake, na akataraji kukubaliwa toba yake.

Ama kutarajia bila kufanya matendo mema huko ni kujidanganya pia ni matarajio yasio kubalika na kupendeka.

DALILI YA KUMTEGEMEA ALLAH

Ni kauli yake Anasema: (Na mtegemeeni Allah ikiwa nyinyi ni waumini)

Na kauli yake (Anaemtegemea Allah yeye humtosha) (1)

Dalili ya Raghba na Rahba na Khushui ni kauli yake mtukufu (Hakika wao walikuwa wepesi wakutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea) (2)

UTAMBULISHO WA TAWAKKULI

Tawakkuli kilungha ni kukitegemea kitu.

Tawakkuli kisheria ni kumtegemea Allah kiukweli na kumuamini yeye na kuchukua sababu za kisheria.

Hapana budi katika Tawakkuli yapatikane mambo matatu

- Ukweli katika kumtegemea Allah
- Kuamini kwamba Allah Subhanahu Wataala ni mwenye kutekeleza yote alioahidi
- Kufanya sababu za kisheria.

(2) Raghba: Ni kupenda kukifikia kitu chenye kupendwa. Rahba: ni khofu yenye kusababisha kukikimbia kinacho khofiwa. Kwahiyo Rahba ni khofu yenye kukutana na matendo mema.

Khushui: ni kunyenyekea utukufu wa Allah, kwa namna ya mtu kujisalimisha kwa Allah katika aliohukumu kiulimwengu na kisheria. Yeyote ambae ana muendea Allah Subhana Wataala, hapana budi awe na khofu pamoja na matarajio. Vyote viwe sawa, usizidi upande wowote katika hivyo. Ukizidi upande mmoja wapo ataangamia. Hivyo lazima iwe khofu na matarajio kama vile mbawa mbili za ndege.

1) **KHASHYAH :** Ni khofu iliyojengeka kutokana na elimu aliyokuanayo mtu. Kwakumtukuza Yule anaemukhofia. Na kwa ukamilifu wa nguvu zake.
2) **INAABABAH:** Ni kumrejea Allah mtukufu kwa kumtii na kujiepusha na maasi. Allah anasema: (Na rejeeni kwa Mola wenu mlezi, na silimuni kwake) kwa maana salimisha jambo lako kwa Allah Subhana Wataala, kwani wewe ni mtumwa wake, na mtumwa hapana budi ajisalimishe kwa Bwana wake, na bwana mwenyewe ndie Allah. Kama alivyosema mtume rehma na amani ziwe juu yake. (Bwana ni Allah).
3) **ISTIANAH:** Ni kuomba msaada. Allah anasema(wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada) katika aya hii kimetangulizwa kitu ambacho haki yake kichelewe. Hii inajulisha (Hasri,) kwa maana hakuna tunae muabudu wala kumuomba msaada isipokua ni wewe tu.
4) **ISTIADHAH:** Ni kuomba ulinzi na kinga kwa Allah kutokana na yenye kuchukiza.
5) **ISIGHAATHAH :** Ni kuomba kuokolewa kutokana na matatizo na maangamizi. Kuomba msaada na kutaka ulinzi, na kutaka kuombewa hivi vyote unaruhusiwa, kumuomba kiumbe katika vile alivyoweza kukusaidia kwa masharti manne: Huyo kiumbe awe hai, awepo hapo mahala awe ana uwezo wa kufanya hicho anachoombwa, awe ni sababu
6) **Kuchinja:** Ni kuitoa roho, kwa kumwaga damu kwa namna maalum.

1) **Dalili ya kumkhofu Allah ni kauli yake** Allah mtukufu: (Basi msiwaogope wao lakini niogopeni mimi)
2) **Dalili ya kumrejea Allah ni kauli yake** (Na rejeeni kwa Mola wenu mlezi na silimuni kwake)
3) **Dalili ya kuomba msaada ni kauli yake Allah.** (Wewe tu tunakuabudu na wewe tu tunakuomba msaada) Na katika Hadithi (Utakapotaka msaada basi muombe msaada Allah)
4) **Dalili ya kuomba ulinzi ni kauli yake Allah** (Sema najikinga kwa Mola mlezi wa mapambazuko) (Sema: Najikinga kwa Mola mlezi wa Wanadamu)
5) **Dalili ya kuomba kuokolewa ni kauli yake Allah:** (Mlipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu mlezi, naye akakujibuni)
6) **Dalili ya kuchinja ni kauli ya Allah.** (Sema: hakika sala yangu na Ibada zangu na uhai wangu ni kwaajili ya Allah Mola mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika) Na katika Hadithi (Allah amelaani mwenye kuchinja si kwa ajili ya Allah)

KUCHINJA KUMEGAWANYIKA SEHEMU TATU

- Kuchinja kwa ajili ya Allah. Kama vile wanyama wa zawadi, na waudh-hiya – na sadaka mbalimbali
- Kuchinja sio kwa ajili ya Allah. Kwa kupenda na kutukuzu. Kama vile kumchinjia jinni. Na watu wa makaburini. Na hii ni shirki kubwa
- Kuchinja kuliko halalishwa. Kama vile mbuzi wa nyama na kumkirimu mgeni na kwa ajili ya biashara

Dalili ya nadhiri ni kauli yake Allah mtukufu.
(Wanatimiza ahadi (Nadhiri) na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana)

UTAMBULISHO WA NADHIRI

- **Kilugha:** ni kuahidi na kujilazimisha
- **Kisheria:** ni mtu kuilazimisha nafsi yake kitu ambacho sio wajibu

❖ **Tanbihi:** Kuna ziada ya ufafanuzi katika masuala ya kuchinja itakuja ziada hiyo katika kitabu cha Tauhidi kwa idhini ya **Allah.**

❖ **Tanbihi:** Nadhiri ina vigawanyo na masharti na kafara utakuja ufafanuzi wake katika kitabu cha Tauhidi kwa idhini ya **Allah.**

AINA ZA NADHIRI

- **Kuweka nadhiri kwa ajili ya Allah**
- **Kuweka nadhiri sio kwa ajili ya Allah**

❖ Mtunzi wa kitabu hiki amezitaja hizi ibada sio kwa malengo ya kuzidhibiti. Bali ni kwa njia ya kupiga mifano tu. Kwani kuna ibada nyingi tu lakini hazikutajwa hapa.
Ushahidi ni kwamba yeyote atakae elekeza au kuzitumia Ibada hizi au zingine sio kwa ajili ya Allah basi atakuwa amefanya shirki.

1. Ameingia mtunzi katika kuelezea msingi wa pili nao ni kuitambua mja dini yake na akaanza kuutambulisha Uislamu Akasema:

Uislamu ni kujisalimisha kwa **Allah** kwa kumpwekesha na kumnyenyekea kwa kumtii na kujiepusha na shirki na washirikina

Huu ndio utambulisho wa uislamu ni kusalimisha mambo yako kwa **Allah** Subhanahu Wataala kwa sababu wewe ni mtumwa, na mtumwa ni lazima ajisalimishe kwa bwana wake. Na bwana ni **Allah,** kama alivyo sema mtume ***swalla llahu alayhi wasallama***.



2. Nguzo za uislamu ni tano ya kwanza ni;
   Shahaada

Msingi wa pili.

Kuitambua dini ya uislamu kwa dalili. Uislamu ni kujisalimisha kwa **Allah,** kwa kumpwekesha na kumnyenyekea na kujiepusha na shirki na washirikina.

Uislamu una daraja tatu.

1. *Uislamu*
2. *Imaani*
3. *Ihsani*

Na kila daraja ina nguzo zake .

Daraja ya kwanza ni Uislamu.

Nguzo zake ni tano

1. Kushuhudia kwamba hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa ni **Allah** tu.
2. Na kushuhudia kwamba Muhammad ni mtume wa **Allah**
3. Kusimamisha swala
4. Kutoa zaka
5. Kufunga Ramadhani na kuhiji nyumba ya **Allah** tukufu.

Dalili ya shahada ni kauli yake Allah mtukufu: (Allah na malaika, na wenye elimu wameshuhudia kuwa hakika hapana Mungu ila yeye ndiye mwenye kusimamisha uadilifu: Hapana Mungu ila yeye mwenye nguvu na hekima)

Maana yake ni kwamba:

Hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah (laailaaha) inakanusha vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah. (illa Allah) inathibitisha ibada kwa Allah pekee hana mshirika katika ibada zake kama ilivyo pia hana mshirika katika ufalme wake. Na tafsir inayo weka wazi maneno haya ni kauli yake Allah (Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu. Isipokuwa Yule aliyeniumba, kwani yeye ataniongoza. Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee)

Ametaja mtunzi Allah amrehemu dalili ya shahada. Na akabainisha maana yake ambayo ni: Hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.



Kukanusha ni kusema: (Hapana anaestahiki kuabudiwa)

Kuthibitisha ni kusema: (Isipokuwa Allah)

Mfumo wa maneno namna hii huleta husisho na thibitisho. Kwa maana ya kuhusisha na kuthibitisha ibada kwa Allah pekee, na kukanusha kwa mwengine. Ndio akasema mtunzi Allah amrehemu katika tafsiri ya maneno ya Allah akifafanua hilo: (Na pale Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi najitenga mbali na hayo mnayo yaabudu. Isipokuwa Yule aliye niumba, kwani yeye ataniongoza.

- Lau atasema msemaji:
  Maana ya (Shahadatu anlaa ilaaha illa allahu) Hapana muabudiwa isipokuwa Allah?
  Tutamwambia, haya maneno ni batili. Kwani kwa maneno hayo yana sahihisha kila kinachoabudiwa kinyume na Allah. Lakini pale anaposema na kuongeza neno (kwa haki) akasema (Hapana Mola muabudiwa kwa haki isipokuwa Allah) hii itakuwa ni dalili kwamba yeye ana pinga vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah. Na ni kwamba Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.

Na kauli yake Alla anasema:

Sema: Enyi watu wa kitabu njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi, ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allah, wala tusimshirikishe na chochote, wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa waola walezi badala ya Allah. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.(1)

- Lau atasema msemaji:
  Maana ya (laa ilaaha illa allah) ni hapana Mola mlezi wa haki isipokuwa Allah?
  Tutamwambia: haya maneno ni sahihi. Lakini sio tafsiri ya (Laa ilaaha illa allah). Hii ni Tauhid Rububiyya (matendo ya Allah) kwani Tauhid hii waliikubali makafiri ambao alipelekwa kwao mtume Muhammadi, ***swalla llahu alayhi wasallama***. Na haikuwaingiza katika uislamu.
  (1)(Sema: Enyi watu wa kitabu! Njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na nyinyi) Aya hii ndani yake kuna ushahidi wa kubatilisha ukaribu baina ya dini.

Na dalili ya kushuhudia ya kwamba Muhammadi ni mtume wa Allah, ni kauli yake Allah anasema: (Hakika amekwisha kujieni mtume kutokana na nyinyi wenyewe, yanamuhuzunisha yanayo kutaabisheni. Ana kuhangaikieni sana. Kwa waumini ni mpole na mwenye huruma)(1)

Maana ya kushudia kwamba Muhammadi ni mtume wa Allah: Ni kumtii katika aliloamrisha, na kumkubali katika aliloeleza. Na kujiepusha na yale alio kataza na kukemea. Na asiabudiwe Allah isipokuwa kwa namna aliofundisha yeye (2)

(1) Ameitaja mtunzi aya hii Allah amrehemu, ikiwa ni dalili katika kushuhudia kwamba Muhammadi Swalla allahu alayhi wasallam ni mtume wa Allah. Pia Allah ametia mkazo katika hiyo aya ya kushuhudia kwa vitu vitatu (kiapo kilicho kadiriwa,) (Laam) na (Qad).

(2) Amebainisha mtunzi Allah amrehemu maana ya kushuhudia ya kwamba Muhammadi ni mtume wa Allah na hakika ina muwajibikia kila muislamu kuthibitisha hii shahada, kumtii mtume swalla allahu alayhi wasallam. Katika yote alioamrisha. Na kumkubali katika alioeleza, na kujiepusha na yote aliokataza na kuyakemea, na asiabudiwe Allah isipokuwa kwa namna aliofundisha na kubainisha. Rehma na amani zimfikie.

Hujulisha shahada ya kuwa Muhammadi ni mtume wa Allah. (ya kwamba yeye ni mja wa Allah asiabudiwe, pia ni mtume asipingwe) hii ikimaanisha kwamba:

- Tumtii katika kila alichoamrisha. Rehma na amani zimfikie. Kwani yeye ni mfikishaji kutoka kwa Allah
- Tumkubali katika alichoeleza, Rehma na amani zimfikie, kwani yeye ni mkweli mwenye kukubaliwa. Rehma na amani zimfikie.
- Tujiepushe na alichokataza na kukemea, kwa kukiweka alichokataza mtume Rehma na amani zimfikie katika upande mwingine na wewe uwe upande mwingine
- Tusimuabudi Allah isipokuwa kwa maelezo au mafundisho aliokuja nayo mtume Rehma na amani zimfikie. Katika maelezo haya ndani yake kuna kuwa rudi wazushi katika dini

(1) Nguzo ya pili ni swala:

Nayo ni kumuabudu Allah, kwa vitendo na maneno maalumu. Huanzwa kwa Takbira na huisha kwa salamu. Na ndio jengo au nguzo ya dini. Na ilifaradhishwa kutoka kwa Allah moja kwa moja kwa mtume wake rehma na amani zimfikie, pale alipo pandishwa mbinguni rehma na amani zimfikie.

Nguzo ya tatu ni zaka.

Kilugha ni: kukua na kutwaharisha. Zaka zipo aina mbili: zaka ya mwili na zaka ya mali.

(2) Nguzo ya nne ni kufunga.

Kilugha ni kujizuwia kisheria

(1) Dalili ya swala na zaka ni kauli ya Allah mtukufu: *(Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allah. Kwa kumtakasia dini, wawe waongofu, na washike sala, na watoe zaka. Ni hiyo ndiyo Dini madhubuti)*

(2) Na dalili ya swaumu, funga, ni kauli yake Allah: *(Enyi mlio amini mmeandikiwa saumu, kama walivyo andikiwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu)*

(3) Dalili ya Hija ni kauli ya Allah: *(Na kwa ajili ya Allah imewajibika watu wahiji kwenye nyumba hiyo kwa Yule awezae njia ya kwendea. Na atakae kanusha basi Allah si mhitaji kwa walimwengu.)*

Ni kumuabudu Allah kwa kujizuwia na vyenye kufunguza, pamoja na kunuwia tokea kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuzama kwa jua. Na funga ni katika aina bora za ibada, kwa kukusanya kwake aina tatu za subira. Na kutokana na ukubwa wa hadhi yake. Hakika Allah subhanahu wataala amenasibisha malipo ya funga kwake yeye mwenyewe.

(***3) Nguzo ya tano ni Hija.***

Hija kilugha ni kukusudia na kisheria ni kumuabudu Allah, kwa kutekeleza ibada kwa mujibu wa mafundisho yaliyo kuja katika sunna za mtume rehma na amani zimfikie. Kuhiji ni lazima kwa kila muislamu katika umri wake ni mara moja.

Daraja ya pili ni Imani:

Na Imani ipo zaidi ya matawi sabini na tisa, imani ya juu zaidi ni kusema *(Laa ilaaha illa allah)* na ya chini yake ni kuondoa uchafu njiani. Na kuwa na haya ni sehemu katika imani. Na nguzo zake ni sita:

1. Kumuamini Allah
2. Kuamini malaika wake
3. Kuamini vitabu vyake
4. Kuamini mitume wake
5. Kuamini siku ya mwisho
6. Kuamini Qadari yake. (mipango)

Dalili ya hizi nguzo sita za Imani ni kauli yake Allah. (Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anayemuamini Allah na siku ya mwisho, na malaika na kitabu na manabii)

Dalili ya kuamini Qadari kauli yake Allah mtukufu (kwa hakika sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo (Qadari)

Daraja ya pili ni Imani

Imani kilugha ni kukiri na kisheria ni kukiri kwa ulimi, na kuitakidi kwa moyo na ulimi na kuitakidi kwa moyo na kutenda kwa viungo na moyo inazidi kwa kutii na inapungua kwa kufanya maasi.

Kwa hiyo imani kisheria lazima ikusanye hayo mabo matano. Likikosekana moja katika hayo mambo matano, hutoka katika utambulisho wa maana ya imani kwa Ahlusunna waljamaa.

Ni ipi dalili ya haya mambo matano?

Amesema mtume Swalla allhu alayhi wasallama (Ya juu yake katika imani ni kusema: (Laa ilaaha Ila allah) hii ndio dalili ya (Qauli) kusema, (Na ya chini yake ni kuondoa uchafu njiani) hii dalili ya (kutenda kwa viungo) Na (kuwa na haya ni sehemu katika imani.)

Hii ni dalili katika (Amalul-qalbi) matendo ya moyoni. Na kauli yake Allah anasema: (Ni nani miongoni mwenu sura hii imemzidishia imani?) hii aya ni dalili kwamba imani huwa inazidi na ikiwa inazidi basi bila shaka inaweza pia kupungua.

Na yamekuja maelezo yalio wazi kabisa katika hadithi ya mtume rehma na amani zimfikie, akielezea kuhusu kupungua kwa dini (sijapata kuona wapungufu wa akili na dini….) akizungumzia mapungufu ya wanawake.

NGUZO ZA IMANI NI SITA

- Kumuamini Allah
- Kuamini Malaika
- Kuamini vitabu
- Kuamini mitume
- Kuamini siku ya mwisho
- Kuamini Qadari kheri yake na shari yake

Nguzo ya kwanza ni kumuamini Allah na inalazimu mambo manne.

- Kuamini kuwepo **kwa Allah Subhanahu Wataala** na inakuwa kwa mambo manne
- Kuamini Tauhidi ya matendo ya Allah
- Kuamini Tauhidi ya ibada
- Kuamini Tauhidi ya majina ya Allah na sifa zake.

KWA KUTUMIA AKILI.

Akili haiwezi kufikiria kuwepo kiumbe bila ya muumba wake.

Allah amesema: (Au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote au ni wao ndio waumbaji?)

KWA KUHISI

Unakuwa katika shida na matatizo. Unanyoosha mikono yako kuelekeza mbinguni, na kusema: Ewe Mola wangu mlezi. Ukimuomba utakuta tatizo linaondoka kwa idhini ya Allah

KIMAUMBILE.

Mtume rehma na amani zimfikie, anasema (kila mtoto huzaliwa katika ufahamu wa muumba wake hivyo wazazi wake ndio humtia katika uyahudi au unaswara au umajusi)

KWA SHERIA.

Ametaja Ibnul-Qayyim Allah amrehemu, kwamba, hakuna aya yeyote katika Qur'an isipokuwa ndani yake kuna dalili juu ya Tawhidi.

NGUZO YA PILI NI KUAMINI MALAIKA

Malaika ni ulimwengu ulio fichika. Na Allah amewaumba kwa nuru. Wanamtii Allah wala hawamuasi, wana roho (Roho takatifu) na wana miili. (Sifa zote njema ni za Allah, muumba mbingu na ardhi, aliyewafanya malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili mbili, na tatu tatu na nene nne. Huzidisha katika kuumba apendavyo) pia wana akili na mioyo. (Hata itapoondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: mola wetu mlezi kasema nini?) Tuna waamini wao na alichotujulisha Allah kutokana na majina yao. Kama vile: jibril, na Mikail, na Israfil. Pia tunaamini sifa zao (hawamuasi Allah kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa) pia tunaamini kazi zao, mfano (wenye kubeba Arshi ya Allah) na tunaamini maelezo ambayo yamekuja kuwaelezea wao kwa ujumla na mmoja mmoja.

NGUZO YA TATU NI KUAMINI VITABU

Inatupasa kuamini kwamba hivyo vitabu ni maneno ya Allah kiuhakika na sio majazi. Na pia yameteremshwa na hayakuumbwa. Na Allah amemteremshia kila mtume kitabu. Na tuna viamini, na vile ambayo ametueleza Allah majina yake na habari zake na hukumu zake, kiujumla na kimoja kimoja, ambavyo havijafutwa. Na tunaamini kwamba Qur'an imefuta vitabu vyote vilivyo tangulia kabla yake, ambavyo ni Tawrat, Injil, Zabur, Suhufi za Ibrahim na Mussa Rehma na amini ziwafikie.

NGUZO YA NNE NI KUAMINI MITUME

Inatupasa kuamini kwamba wao ni viumbe, hawana sifa za kiuungu kwa chochote. Na wao ni waja wa Allah hawaabudiwa. Allah amewapa utume, na akawapa wahyi, na akawatia nguvu kwa alama mbalimbali, na wao wametekeleza amana waliopewa, wameunasihi umma na wakafikisha ujumbe, na wakapambana kwa ajili ya Allah ukweli wa mapambano. Tunawaamini na wale aliotujulisha Allah majina yao na sifa zao, na habari zao kwa ujumla na mmoja mmoja. Nabii wa kwanza ni Adam amani zimfikie, na mtume wa kwanza ni Nuhu amani zimfikie.

Na nabii na mtume wa mwisho ni Muhammahi rehma na amani zimfikie, na sharia zote zilizotangulia zimefutwa na sharia za Muhammadi rehama na amani zimfikie. Na mitume wenye maazimio na subira ni watano. Wametajwa kwenye sura mbili Shuura na Ahzab (1- Muhammadi rehma na amani zimfikie) (2- Nuhu amani zimfikie) (3- Ibrahim amani zimfikie) (4- Mussa amani zimfikie) (5- Issa amani zimfikie)

NGUZO YA TANO: NI KUAMINI SIKU YA MWISHO

Hii inajumlisha kuamini yote aliyoyaeleza mtume rehma na amani ziwe juu yake. Katika yale yatakayotokea baada ya kifo. Mfano Adhabu za kaburini, kupulizwa baragumu na kusimama kufufuka kutoka katika makaburi yao, na mizani ya kupima matendo ya watu na madaftari ya matendo ya watu, na siratwa na birka ya mtume ambayo waja wema watakunywa, na kuombewa na mtume, na pepo na moto na waumini watamuona mola wao mlezi siku ya kiyama wakiwa peponi, na mengineyo katika mambo ya ghaibu.

NGUZO YA SITA: NI KUAMINI QADARI, KHERI YAKE NA SHARI YAKE

Inapasa ijumuishe nguzo hii kuamini mambo manne.

ELIMU

Kuamini ya kwamba Allah subhaanahu wataala anafahamu kila kitu kwa ujumla na kwa uchambuzi wake.

KUANDIKA.

Kuamini ya kwamba Allah ameandika makadirio ya kila kitu mpaka kitakapo simama kiyama.

MATAKWA.

Kuamini kwamba alichokitaka Allah, basi kimekuwa na kile ambacho hakutaka kiwe hakikuwa na mja ana matakwa lakini matakwa yake yapo chini ya matakwa ya Allah subhanahu wataala.

KUUMBA.

Kuamini kwa mja yeyote ni kiumbe, yeye na matendo yake pia viumbe wote waliobakia. Dalili (Allah ni mwenye kuumba kila kitu). Allah ndiye amewaumba nyie na matendo yenu.

Na hizi daraja nne zilizotajwa hapo juu amezikusanya mtunzi wa kitabu.

(1) Elimu
(2) Maandishi ya Mola wetu
(3) Matakwa yake.
(4) Na kuumba kwake ambako ni kukipatisha kitu na kukitengeneza.

DARAJA LA TATU NI IHSANI:

Na nguzo yake ni moja tu ambayo ni (Kumuabudu Allah Kama vile unamuona ikiwa humuoni yeye anakuona)

Na ushahidi ni maneno ya Allah mtukufu: (Hakika ya Allah yupamoja na wenye kumcha na watendao mema.) Na kauli yake Allah: (Na mtegemee mtukufu mwenye nguvu mwenye kurehemu. Ambaye amekuona unapo simama. Na mageuko yako kati ya wanao sujudu. Hakika yeye ndio mwenye kusikia, mwenye kujua) Na kauli ya Allah: (Na huwi katika jambo lolote wala husomi sehemu yoyote katika Qur'an wala hamtendi kitendo chochote ila sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo)

DARAJA YA TATU NI IHSANI.

Nayo ni daraja ya juu katika dini, nayo ni nguzo moja na huingia ndani yake daraja mbili.

Ibada ya kuonekana.

Ambayo ni ibada ya kupenda na kutamani na kuwa na shauku na yalio mbele ya Allah. Mfano; Ibada za mitume na manabii amani ziwafikie. Na inawezekana kwa wengine kufikia katika daraja hii.

Ibada ya kumchunga Allah.

Na hii ni ibada ya kumkhofia Allah, na kukimbia maasi kwa ajili ya Allah.

Na hatoki nje ya daraja hii muislamu yeyote.

UFAFANUZI: Hii haina maana kwamba mtu mwenye daraja hii ana mapenzi ya Allah tu na hana khofu ya Allah subhaanahu wataala lakini kwenye daraja hii kuna msukumo mkubwa ambao unamsukuma mja katika kufanya ibada. Ambao ni kumpenda Allah subhaanahu wataala Na miongoni mwayo ni kauli ya mtume rehma na amani zimfikie(Kwanini nisiwe mja mwenye kushukuru ?)

DALILI YA HADITHI:

Hadithi ya Jibril iliyo maarufu kutoka kwa Umar radhi za Allah ziwe juu yake amesema:-

Baina za nyakati tulipokuwa mbele ya mtume rehma na amani zimfikie juu yake, siku moja alijitokeza kwetu mtu mmoja mwenye nguo zilizokuwa nyeupe sana, mwenye nywele nyeusi sana, hazionekani kwake athari za kusafiri wala hamtambui yeyote kati yetu mpaka akakaa mbele ya Mtume rehma na amani ziwe juu yake, akayaegemeza magoti kwenye magoti ya mtume rehma na amani ziwe juu yake, na akaweka viganja vyake kwenye mapaja yake na akasema:- Ewe Muhammadi nielezee kuhusu uislamu, akasema mtume rehma na amani ziwe juu yake, (Uislamu ni kushuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hakika ya Muhammadi ni mtume wa Allah na kusimamisha swala na kutoa zaka na kufunga ramadhani, na kuhiji nyumba ya Allah ukiweza njia ya kuiendea nyumba hiyo).

Akasema (Yule mtu) umesema kweli, Akasema tena;

Nieleze kuhusu Ihsani, Akasema mtume(Ni kumuabudu Allah kana kwamba unamuona ikiwa humuoni yeye anakuona) Akasema (Yule mtu) Nieleze kuhusu kiyama; Akasema (Mtume) Hakuwa mwenye kuulizwa hicho kiama anatambua zaidi kuliko muulizwaji. Akasema (Yule mtu) Nieleze alama zake, Akasema (Mtume) Ni mjakazi kumzaa bwana wake, na kuwaona watembea peku, waenda uchi, maskini wachunga mbuzi, wakishindana katika majengo

Akasema Umar, Akaondoka Yule mtu, tukakaa muda mrefu kidogo Akasema (Mtume) (Ewe Umar unamfahamu Yule muulizaji?) Nikasema, Allah na mtume wake ndio wanafaham/wajuzi. Akasema (Mtume) (Yule ni Jibril alikujieni akufundisheni mambo ya dini yenu)

Hadithi hii ni dalili ya nguzo za uislamu na imani na Ihsani kwa kauli ya Mtume rehma na amani zimfikie, (Hakuwa muulizwaji ni mjuzi zaidi kuliko mwenye kuuliza) Maneno hayo ni dalili ya kwamba hafahamu wakati wa kusimama kiyama isipokuwa Allah.

KAULI YAKE MTUME REHMA NA AMANI ZIMFIKIE: (MJAKAZI KUMZAA BWANA WAKE MAANA YAKE NI:-

3. Kukithiri kuwaasi wazazi

2. Kukithiri kwa watumwa

1. Kubadilika hali

Mfalme atamuoa mjakazi atakuja kumzalia kijana, atakuwa huyu kijana ni mfalme baada ya kifo cha baba yake naatakuja kuwa bwana wa mama yake

(Na utawaona watembea peku, waenda uchi, maskini) maana yake ni Mafakiri. (Wachunga mbuzi wanashindana katika majengo) maana yake ni Hali za watu zitabadilika atabadilika huyu fakiri kuwa tajiri mbaya.

FAIDA ZINAZOPATIKANA KUTOKANA NA HADITHI YA JIBRIL AMANI ZIWE JUU YAKE.

1. Mwanafunzi ana haki sita(6) juu yake kuzitekeleza:-
   Haki ya nafsi yake, Haki ya walimu wake, Haki za mahala anaposomea, Haki za wenzie, Haki za kitabu chake, Haki ya elimu aliyojifunza.

HAKI YA NAFSI YAKE: Elimu ni ibada (awe na ikhlasi na awe mwenye kufuata) kuwa salafi wa sawa sawa. (salafi ni mfuasi wa wema waliopita) Amukhofie Allah na amchunge, kwa unyenyekevu na kuacha majivuno, kukinai na kuipa nyongo dunia, kujipamba na elimu nzuri kuwa na tabia njema, kudumu katika sifa za uanaume, kuzihama starehe, kupuuza vikao vya upuuzi, kujipamba na upole kuthibiti na kuthibitisha kuwa na hima, kuwa na shauku katika kutafuta, kusafiri, kuifunga elimu, kuhifadhi, uchungaji, kuyapitia aliyoyahifadhi, kujielimisha kwa kuitafuta hukumu kwenye misingi, kujitegemeza kwa Allah, uaminifu wa kielimu. Ukweli.(Kinga au ngao ya mwanafunzi ni kusema sifahamu), kuhifadhi rasilimali(muda), kuipumzisha nafsi, kujielimisha katika elimu mbalimbali, usomaji wa kusahihisha na kudhibiti, kuacha makala zilizo ndefu zaidi, kuuliza vizuri kisha kusikiliza na kufahamu pia kuyafanyia kazi, kufanya majadiliano bila ubishani, kuidurusu elimu, Awe kati ya Qur'an, Sunna na elimu zake, kukamilisha ala za kila fani, matendo, kutokupenda madaraka, na kuacha umaarufu na dunia, kuidhania vibaya nafsi, na uwadhanie vizuri watu, kusafisha elimu (kutetea haki, awe mwenye kuamrisha mema, mwenye kukataza mabaya, mwenye kupima kati ya maslahi na madhara, mwenye kuieneza elimu na kupenda manufaa, kutoa cheo, na kuwaombea mema waislamu katika mambo ya haki na mema) Utukufu, kuhifadhi elimu, kujivutia maslahi sio kudhihaki, kuacha ujuaji na kimbelembele kabla ya kustahiki kwako. Msimamo wako wakutokua na shaka kwa mwenye elimu na kutotofautiana na maulamaa,, hakuna utaifa wala makundi unaoweza kuleta chuki na mapenzi baina ya watu.

- **HAKI YA SHEIKH WAKE:**

  Watu kwenye mlango huu wamegawika pande mbili, pia na ya kati na kati. Tutakuja kufahamu kwamba shirki ya kwanza kupatikana katika ardhi ni kwa sababu ya kuchupa mipaka katika haki za watu wema. Hivyo hapana budi tuwe ni wakati na kati katika kuwapenda watu wema si kuchupa mipaka kwao, wala kupoteza haki zao.

- **HAKI YA MAHALA ANAPOSOMEA.**
- **HAKI YA MWENZIE:** Amesema Allah mtukufu (Nyinyi mmekuwa Umma bora uliotolewa kwa watu) Na amesema mtume rehma na amani zimfikie: (Hawi na imani mmoja wenu, mpaka ampendelee ndugu yake inachopenda nafsi yake)
- **HAKI YA KITABU:** Ni kukihifadhi kitabu, kwani Allah subhaanahu wataala ametuneemesha hivi vitabu, hapana budi tuvihifadhi na kuvitunza.
- **HAKI YA ELIMU:** Ni kuithibiti elimu na kuikagua daima, kwa kuirejea mara kwa mara, na kuifanyia kazi, kisha baada ya hapo alinganie kwenye elimu hiyo, kwani hii ni neema na hapana budi kuishukurru hii neema.

2. Miongoni mwa adabu za kuuliza ni kutanguliza swali ambalo hutarajiwa kuwa na manufaa na faida.
3. Ni wajibu kwa mwanafunzi kudumu katika hali nzuri na ya usafi.
4. Baada ya kufa mtume rehma na amani zimfikie, hairuhusiwi kusema (Allah na mtume wake wanajua zaidi) na huruhusiwi kusema (Allah ndie anajua)

Kifungu hiki kimekusanya dondoo kutoka kwa Mtume
Na zikafungamanisha kuanzia jina lake , nasaba yake , umri wake na chochote alichokifanya katika kazi ya kulingania kwake

Hatuna budi kujua kutoka kwa Mtume mambo muhimu na miongoni ni :-

UMRI WAKE.

Anao umri wa miaka sitini na mitatu (63) miongoni mwa hiyo miaka arobaini (40) kabla ya kpewa utume , na miaka ishirini na mitatu baada ya kupewa utume

JINA LAKE NA NASABA YAKE.

Yeye ni Muhammad mtoto wa Abdallah , na Abdallah ni mtoto wa Abdil-mutwalib, na Abdil-mutwalib ni mtoto wa Hashim , na Hashim katokana na kabila la makuraishi lililotokana na waarabu katika kiazazi cha Ismail mtoto wa Ibrahimu kipenzi cha Allah (amani ziwe juu yake)

MSINGI WA TATU :

KUMJUA MTUME WENU MUHAMMAD.

Yeye ni Muhammad mtoto wa Abdallah , na Abdallah ni mtoto wa Abdil-mutwalib, na Abdil-mutwalib ni mtoto wa Hashim , na Hashim katokana kabila la makuraishi lililotokana na waarabu katika kiazazi cha Ismail mtoto wa Ibrahimu kipenzi cha Allah (amani ziwe juu yake)

Anao umri wa miaka sitini na mitatu (63) miongoni mwa hiyo miaka arobaini (40) kabla ya kupewa utume , na miaka ishirini na mitatu baada ya kupewa utume.

Alipewaunabii kwa kuteremshiwa suratul (ALAQ)

Na alipewa utume kwa kutershiwa suratul (MUDDATHIR)

Umegawanyika muda wa utume wake katika sehemu :-

MUDA ALIOISHI MAKKA
Alidumu kwa muda wa miaka mitatu

MUDA ALIOISHI MADINA
Alidumu kwa muda wa miaka kumi

Je yeye ni Nabii au Mtume?
Yeye ni Nabii na Mtume Alipewe unabii kwa tamko la (SOMA) na kupewa utume kwa tamko (Ewe mweye kujigubika)

DONDOO ZINAZOHUSU MWENENDO WA MTUME

Allah alimtuma Mtume kuwaonya watu na shirki , na kulingania katika Tauhid

dalili ni kauli ya Allah mtukufu : ((Ewe uliejigubika) (simama na uonye) . (na mola wako mlezi mtukuze) . (na nguo zako zisafishe) (na yaliyo machafu yahame) (wala usitoe kwa kutarajia kuzidishiwa .

maana ya (simama uonye) uonye kutokana shirki na ulinganie kwenye Tauhid.

(na mola wako umtukuze) mtukuze kwa Tauhid (kumpwekesha).

(na nguo zako zisafishe) safisha matendo yako kutokana ushirikina .

(na yaliyo machafu yahame) masanamu .

Na kahama kwake ni kuyaacha na kujiweka mbali nayo na watu wake .

Ilichukuwa kazi hii ya kulingania kwa mtume miaka kumi , na baada ya miaka hiyo kumi alipandishwa mbinguni , na akafaradhishiwa swala tano , na aliswali akiwa Makka muda wa miaka mitatu , na baada yake aliamrishwa kuhama kwenda madina .

Ulikua ulinganizi katika muda aliokuwa Makka umejikita katika Tauhid , na ulingazi ulikuwa ni kuupuuza ushirikina na kujitakasa na na ibada kwa ajili ya Allah peke yake , na uliendelea ulinganizi huu kwa muda wa miaka mitatu .kisha akapewa amri bwana mtume kuhama kwenda MADINA , vile vile aliendelea na kazi ya da'awa hali ya kusimamisha Tauhid kwa kuongeza kile kilicho teremshwa katika sheria zilizobaki katika dini miongoni mwa Ibada mbali mbali na matendeano pamoja n a mambo ya kimaisha .

Ispokuwa Hakika mwenye kuona katika mwenendo wake Mtume katika kulingania hakika ulinganizi wa Tauhid unabaki kuwa ni wenye kulazimiana nae mpaka pale Allah alipomfisha , na jambo hili ni majibu ya wazi katika kuwarudi kwa kila mwenye kuwapa nyongo watu katka kujifundisha tawheed na kudai ya kuwa tawheed haihitajii mtu kujifundisha ispokuwa kwa dakika zenye kuhesabika .

Kauli yake رَحِمَهُ اللّٰهُ (alipandishwa mbinguni) tunapata faida ya :-

1- Hakika alichokisema Mtume miongoni mwa mambo yasiyoonekana , sisi tunasema : tunaamini , tunasadikisha na tumejisalimisha .
2- Umihimu wa swala tano zilizo faradhishwa ,kwa nanmna ya kuwa Allah mtukufu alizifaradhisha mbinguni.

Hijra: Ni kuhama kutoka mji wa shirki kwenda mji wa uislamu. Na hijra imekuwa ni faradhi juu ya huu umma. Kutoka mji wa shirki kwenda mji wa kiislamu kuhamia huku kutabakia hadi kitakapo simama kiama. Amesema Allah subhanahu wataala "Hakika malaika atawaambia wale ambao wamewafisha nao wamejidhulumu nafsi zao: Mlikua vipi? Watasema: Tulikuwa tunaonewa. Watawaambia: Kwani ardhi ya Allah haikuwa na wasaa wa kuhamia humo? Basi hao makazi yao ni jahanam, nao ni marejeo mabaya kabisa, isipokuwa wale waliokuwa wanyonge miongoni mwa wanaume na wanawakena watoto wasio na uwezo wala hila na kuongoza njia ya kuhama.

Basi hao Allah akawasamehe na Allah ni mwingi wa kusamehe na mwinyi wa maghfira. Na kauli yake Allah mtukufu "Enyi waja wangu mlio amini hakika ardhi yangu ina wasaa basi mniabudu mimi peke yangu" amesema Imaam Al-Bagh'awi Allah amrehem: "Sababu ya kuteremka ayah ii ni kwa waislam wa Makkah ambao hawakuhama. Allah aliwaita kwa jina la (Iman)

Na dalili ya hijra kutoka katika sunnah ni kauli ya mtume swalalahu walayhi wasalam "Hakutakoma kuhama vingineyo mpaka iishe toba na haitaikoma toba mpaka lichomoze jua upande wa magharibi"

Kauli ya Mtume swalalahu walayhi wasalam (Hakuna kuhama baada ya ufunguzi wa mji wa Makka (Yaani kutoka Makka kwenda Madina na katika hili kunaisha kutoka kwa mtume swalla llahu alayhi wasallama Hakika mji wa Makka haiwezekani tena ukawa mji wa kikafiri.

KUNAGAWANYIKA KUHAMA KATIKA SEHEMU KUU TATU.

- Kuhama kwenda kuliendea lile ambalo ameliwajib isha Mwenyezi Mungu.

  Miongoni ni kufanya Amal, na muda wa kufanya a'mal na sehemu ya kufanya a'mal
- Kuhama kutoka Makka kwenda Madina kuhama huku hakupo kumekoma baada ya ufunguzi wa mji wa Makka
- Kuhama kutoka katika mji wa kikafiri kwenda mji wa kiislamu hukumu yake ni wajib

Neno a'mal

Kila jambo alililoliharamisha Allah subhanahu wataala na jambo kubwa alililoliharamisha ni shirki.

A'amil: Ni makafiri na wanafiki na wengineo.

Zamaan: Ni kuhama kwa muda ambao wanakusanyika makafiri.

Makaan: Sehemu: Ni kuhama sehemu ambayo wanakusanyika sehemu hiyo makafiri.

Inakoma tawbah kwa moja ya mambo mawili.

1. Ni kuchomoza jua kutoka magharibi
2. Kufikwa na umauti. Amesema Allah subhanahu wataala

" *Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yatakapomfikia mmoja wao umauti, kisha hapo akasema. Hakika mimi sasa nimetubia, wala wale wanaokufa na hali yao ni makafiri hao tumewaandikia adhabu chungu"*

Kauli ya mtume ***(swalla llahu alayhi wasallam)*** " Hamna Hijra baada kuukomboa mji Makka" yaani kutoka Makka kuhamia Madina , ni ishara kwamba mji wa Makka haiwezekani tena kurudi kwa mji wa kikafiri .

Baada ya kuweka makazi mji wa madina akapewa sheria zilizobakia katika uislamu mfano : Zaka, Swaum, na Hija, Jihadi na Adhana , kuamrisha mema na kukataza maovu na mengineyo miongoni mwa sheria za kiislamu .

Kazi hii aliifanya kwa muda wa miaka kumi na baada ya miaka hiyo alifishwa (Rehma na amani ziwe juu yake)

Na hii dini yake ipo , na katika dini hii , hakuna kheri yoyote ila ameifundisha na wala shari yeyote ila ameitahadharisha.

Na kheri ambayo ameifundisha kuitekeleza ni Tawheed na mambo yote anayoyapenda Allah na kuridhia .

Ama shari aliyoitahadharisha ni Shirki na mambo yote anyoyachukia Allah na kuyakataa.

1- Anasema shikh **IBN- UTHAIMIN** Rehma za Allah ziwe juu yake:-

Zaka ilifaradhishwa mwanzo katika mji wa Makka lakini hikupangiwa viwango vyake wala kukdriwa uwajibu wake .

Na katika mji wa madina ndiko kulipangwa viwango vyake na kukadirwa uwajibu wake .

2- Alifishwa Mtume (Rehma za Allah ziwe juu yake) katika mwaka wa kumi baada ya kuhama , na alizikwa katika chumba cha mkewe bibi Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake)

3- Hakuna kheri yoyote ila ameifundisha katika umma na wala shari yeyote ila ameitahadharisha.

Hatuna budi kuthibitisha kuwa hakika ametekeleza amana , amefikisha utume , amenasihi umma , amepigania jihadi dini ya Alla ukweli wa kupigania, na akatuacha katika mwanga usiku wake kama mchana wake hakuna atakaepotea ila atakuwa mwenye kuangamia.

MAMBO YALIYO HARAMISHWA

Shirki kubwa

hii inamtoa mja katika mila ya uislamu

Shirki ndogo

hii haimtoi mja katika mila ya uislamu

Dhambi kubwa

ni kila aina ya dhambi iliyo andikiwa adhabu maalum

Dhambi ndogo

ni kila jambo lililoharamishwa na halijaandikiwa adhabu maalum

Allah alimtuma mtume wake kwa watu wote na akalazimisha twaa yake kwa viumbe wa aina mbili nao ni majini na watu.Nadalili ni kauli yake Allah mtukufu(Sema waambie watu hakika mimi ni mtume wa Allah kwenu nyinyi wote) 1.

Na Allah akaikamilisha yake kupitia Mtumewake Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu: (Leo nimewakamilishia dini yenu na nimezitimiza neema zangu juu yenu na nimeridhia kwenu ya kwamba uislamu ndio dini)

Na dalili inayoelezea juu ya kufa kwake mtume ni kauli ya Allah mtukufu:

(Hakika wewe utakufa na wao watakufa kisha bila shaka siku ya qiyama mtalumbana mbele ya mola wenu)

Alitumwa mtume Muhammad swalalahu walaihi wasalam kwa watu wote na zikafutwa sheria zote zilizo kuwepo kabla yake .

basi mayahudi na manasara(makafiri)kuanzia zama za mtume swalalahu walaihi wasalam na katika zama zetu hizi leo pindi itakapowafikia da'awa na wasiingie katika dini basi hao watakua ni makafiri hata kama wakiwa na sifa kama za wale aliekua nao nabii Mussa na nabii Issa amani za Allah ziwe juu yao.

Na miongoni mwadalili ya hayo ni

1.kauli ya allah alie tukuka(Sema:enyi watu wa kitabu! Njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na nyinyi:ya kwamba tusimuabudu yeyote isipokuwa Allah na wala tusimshirikishe na chochote ,

2.kauli ya Allah mtukufu(piganeni na wale wasio muabudu Allah na siku ya mwisho wala hawaharamishi aliyo haramisha Allah na mtume wake ,wala hawashiki dini ya haki miongoni mwa waliopewa kitabu.

3.kauli yake mtume swalalahu walaihi wasalam (Naapa kwa Yule nafsi yangu ipo mikononi kwake hato sikia kutoka kwangu myahudi yeyote wala mnasara yeyote(mkristo)kisha asiniamni isipokua atakua mtu huyo ni miongoni ya watu wa motoni).

JAMBO LA TANO - HITIMISHO

1- Watu wote wataonja mauti bila shaka na ni wenye kufufuliwa siku nzito hiyo nayo ni siku ya qiyama na ni wenye kuhesabiwa na kulipwa kulingana na amali yake mja.
2- mwenye kupinga kufufuliwa na kuhesabiwa ni kafiri kwa sababu mtu huyo amepiga nguzo miongoni mwa nguzo za imani.
3- Nuhu amani za Allah ziwe juu yake ni mtume wa kwanza na dalili ni kauli yake Allah mtukufu(Hakika sisis tumekuletea wahy kama tulivyo mpelekea Nuhu na manabii waliokuja baada yake).

Ama nabii wa kwanza ni nabii Adam na dalili nikauli yake Allah mtukufu(Hakika mtume swalalahu walaihi wasalam aliulizwa kutokana na Adam je yeye ni nabii?akasema:ni nabii mwenye kusemeshwa na Allah).

Na mwisho wa manabii ni nabii Muhammad swalalahu walayhi wasalam na dalili ni kauli yak e Allah mtukufu (Muhammad si baba wa yeyote katika waume zenu bali ni mtume wa Allah na wa mwisho katika manabii)

Basi kila mwenye kudai unabii au utume baada ya mtume Muhammad swalalahu walayhi wasalam basi mtu huyo atakua ni muongo na ni kafiri ,na kila mwenye kumsadikisha mtu huyo mwenye kudai unabii basi na yeye atakua ni kafiri mfano wake.

Na watu pindi watakapo kufa watafufuluwa na dalili ni kauli yake mtukufu(Kutokana na ardhi tumekuumbeni na humohumo tutakurudisheni,nakutokea humo tutakutoeni mara nyingine)

Na kauli yake Allah mtukufu(Na Allah ame kuotesheni katika ardhi kama mmea.kisha atakurudisheni humo na atakutueni tena)

Baada ya kufufuka mtahesabiwa na mtalipwa kwa matendo yenu .

Na dalil ni kauli yake Allah mtukufu(Ni vya Allah vyote vya mbinguni na aridhini ili awalipe walio tenda ubaya kwa walio yatenda,na walio tenda mema awalipe mema)

Na mwenye kupinga kufufuka ni kafiri dalili ni kauli yake Allah mtukufu(waliokufuru wanadai kwamba hawato fufuliwa,sema :kwani?naapa kwa mola wangu mlezi!hapana shaka mtafufuliwa kasha hapana shaka mtaambiwa mlioyatenda.na hayo ni mepesi kwa Allah)

Na aliwatuma Allah mitume wake wote kutoa bishara njema kwa watu wao na kuwahofisha na moto,na dalili nii kauli yake Allah mtukufu(mitume hao ni wabashiri na waonyaji)

Mtume wa kwanza kwa hao mitume ni Nuhu amani za Allah ziwe juu yake na wa mwisho ni mtume Muhammad swalalahu walaihi wasalam na ni wa mwisho kwa manabii.

Na dalili inayo onyesha kwamba mtume wakwanza ni Nuhuamani ziwe juu yake ,kauli ya Allah mtukufu(Hakika sisi tumekuletea wahy wewe kama tulivo wapelekea wahy Nuhu na manabii wengine waliokua baada yake)

Allah amewaamrisha waja wake wote kumpinga shetani na kumuamini Allah,amesema mwanachuoni IBNUL-QAYYIMU Allah amrehemu;(ushetani :ni kitendo cha mja kuvuka mipaka katika kuabudu au kufata au kutiiwa)

Na katika kila umma Allah amepeleka mtume kuanzia mtume Nuhu subhanahu wataalampaka mtume Muhammad swalalahu walaihi wasalam na kazi yao ilikua ni kuamrisha waja kumuabudu Allah pekee na kuwakataza juu ya kumuabudu shetani.Na dalili ni kauli yake Allah mtukufu (Hakika tumempeleka mitume katika umma zote kwamba wamuabudu Allah na wajiepushe na shetani)

Na mashetani ni wengi sana na viongozi wao ni watano(5):Ibilisi alie laaniwa na Allah,(2)ni yule anae abudiwa na waja hali ya kuwa yupo radhi(3)na Yule mwekuwaita watu katika ibada yake binafsi(4)na Yule mwenye kudai kujua elimu ya ghaibu(mambo yasio onekana) (5) na Yule anae hukumu tofauti na alivyo teremsha Allah mtukufu.Na dalili ni kauli yake Allah (Hakuna kulazimishana katika dini kwani uongofu umesha pambanuka na upotofu.basi anaemkataa shetani na kumumini Allah bila shaka amekamata kishiko kisicho vunjika)

Na hii maana ya kwamba Hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah.

katika hadithi(Msingi mkubwa katika uislamu na nguzo zake ni swala na kilele cha juu ni jihadi katika njia ya Allah

Allah alituma mitume na manabii kuwabashiria watu pepo na kuwahofisha na moto na wote hao kazi yao ilikua juu ya kumpwekesha Allah subhanahu wataala na kupambana na shetani na ushirikina kwa namna zote na dalili ni kauli yake Allah mtukufu (Na kwa hakika kwa kila umma tumewatumia mtume kwamba muabuduni Allah na muogopeni shetani).Na kwa hakika kila umma tuliutumia mtume wake:maana yake kila watu (wamuabudu Allah) na (wampwekeshe) na (wajiepushe na shetani)—maana yake mfanyeni shetani katika upande na nyinyi muwe katika upande mwengine.Na hii itakua ni njia ya juu katika kumkemea shetani na kumuweka mbali na wao nahilo jambo ni lakujihakikishia usafi kutokana na shirki na watu wake ,na ameamrisha Allah kwa waja wake wote kumpinga shetani na kumuamini Allah na hapana shaka ndani yake ,Allah anasema(Atakae mpinga shetani na kumuamini Allah).

Na ushetani:ni mja kuvuka mipaka katika kuabudu(kama kuabudu mawe na miti) au kufuata (kama kuwafata wanachuoni waovu) au kuwatii (kama viongozi walio nje nay a twaa ya Allah.

Na mashetani ni wengi sana na viongozi wao ni

watano(5) na kiongozi wa juu kabisa ni Iblisi Allah amemlaani na miongoni mwa mlango wa kutolea habari na atakae abudiwa na akiwa radhi na yeyote Yule atakae lingania watu katika ibada yake binafsi na Yule mwenye kudai kujua elimu ya ghaibu(mambo ya sio onekana) na atakae hukumu kinyume na alivyo teremsha Allah.

KUKUFURU KWA KUFANYA JAMBO ASILOTEREMSHA ALLAH

KUFURU KUBWA

Mwenye kuitakidi ya kwamba hukumu ya mtu ni sawa na hukumu ya Allah au au zaidi yake .

KUFURU NDOGO

Mwenye kuitakidi ya kwamba hukumu bila kufuata aliyoteremsha Allah ni batili , lakini anahukumu kwa matamanio au kuapenda uongozi au au kwa sababu nyingine yeyote .

IMAMU IBNUL- QAYYIM AMEIGAWA JIHADI KATIKA SEHEMU

JIHADI YA NAFSI.

Inakuwa kwa kutafuta elimu ,kuifanyia kazi katika njia sahihi katika njia ya allh .na kusubiri

JIHADI YA SHETANI.

Inakuwa kwa kuacha yenye kutatiza (shirki na uzushi)

Na katika yenye kutatiza kuna makubwa na madogo

JIHADI YA MAKAFIRI NA WANAFIKI

Inakuwa kwa kuudhibiti moyo , ulimi , mali na nafsi .

JIHADI YA VIONGOZI WA DHULMA , WAZUSHI NA WAPINGAJI

Inakuwa kwa kutumia mkono , ulimi na moyo .

MWISHO

Ni wajibu kwa kila mwenye akili kuzingatia huu msingi ,na kuuchunga kwa uangalifu maalum sana , kwa kuwa imekusanya misingi mikuu anayoihitaji kila mwanadamu kaburini kwake

Kwa haya yote ALLAH ni mjuzi zaidi , rehema na amani zimuendee mtume Muhammad

MISNGI MITATU (NAYO KWA MUKHTASARI MASWALI YA KABURINI) , DALILI ZAKE , KWA NINI TUNASOMA TAWHEED ? KWA NINI TUNASOMA MISINGI MITATU ?

MAS'ALA MANNE NA DALILI ZAKE(SURATUL-ASR)

ELIMU

Kumjua Allah , na kumjua mtume wake na kuijua dini ya kiislamu kwa dalili .

(kwa maana ya : **MISINGI MITATU**)

KUIFANYIA KAZI ELIMU

" Inaita elimu kwa kuifanyia kazi , basi ikiwa mtu ataitikia itakuwa kheri kweke na kama si hivyo inaondoka."

" Namweye elimu kwa elimu yake aspoifanyia kazi Atakuwa ni mweye kuadhibiwa kabla ya wenye kuabudu masanamu

KULINGANIA WATU KWA HIYO ELIMU

MASHARTI YA KULINGANIA: Utakaso . Elimu ya kisheria . Kujua hali ya mwenye kulinganiwa , Hekima . Subra

Jambo la kwanza kulinganiwa ni Tauhid , na hii ndio kazi waliofanya Manabii na Mitume .
Na nafasi iliyokuwa ya juu kabisa katika kulingania ni Tauhid na kupinga shirki

KUWA NA SUBIRA JUU YA MAUDHI NDANI YAKE.

Kusubiri katika kumtii Allah kama (kuswali) na kujizuia kutokana maasi kama (riba)
Na juu ya yote aliyoyakadiria Allah yenye kuumiza kama (ufakiri)

Maana yake : kusubiri katika kutafuta elimu kasha katika kuifanyia kazi na kasha kuilingania .

MAS'ALA MATATU

Tauhid ya malezi (kumpwekesha Allah katika malezi hapana budi kupwekesha vilevile katika uungu wake)

Na kumpwekesha katika majina na sifa zake

Kusubiri katika kumtii Allah kama (kuswali) na kujizuia kutokana maasi kama (riba)
Na juu ya yote aliyoyakadiria Allah yenye kuumiza kama(ufakiri)

Tauhid ya uungu (utakaso) , na hakika Alla haridhii kushirikishwa pamoja nae yeyote katika ibada yake , si Malaika alie karibu wala Nabii mwenye kutumwa .

Kujisafisha na kujiweka mbali na shirki na watu wake : kwa moyo (kuchukia) na ulimi

" HAKIKA MIMI NIKO MBALI NA VILE MNAVYOVIABUDU"

MISNGI MITATU (NAYO KWA MUKHTASARI MASWALI YA KABURINI) , DALILI ZAKE , KWA NINI TUNASOMA TAUHID ?	SABAU ZA KUSOMA TAUHID	**Al-HANAFIYA-**Ni mila iliyo kuwa mbali na shirki iliyo jengwa katika misingi ya Tauhid iliyotakasika.
		MAANA YA TAUHID KILUGHA:Neno hili limetokana na kitendo ;alipwekesha,anapwekesha,kupwekesha,kupwekesha kitu ni kufanya kitu kuwa ni kimoja . **MAANA YA TAUHID KILUGHA:**Ni kumfanya Allah kuwa ni mmoja katika
		AINA ZA TAUHID.1-Tawheed ya malezi;Ni kumpwekesha Allah kwa vitendo vyake ,kuumba,ufalme na uendeshaji.2- Tauhid ya uungu;Ni kumpwekesha Allah katika ibada na katika vitendo vya waja.Tawheed ya sifa ;Ni kumpwekesha Alllah kwa majina aliojiita yeye mwenyewe katika kitabu chake au kwa maneno ya mtume wake swalalahu walayhi wasalam na hayo kwa kuthibiti yale alioyathibitisha na kuyakanusha aliye ya kanusha bila kuzidisha au kupunguza na bila ya kufananisha.
		Maana ya shirki ; Ni kulingania kwa asiyekua Allah alietukuka,nah ii ni dhambi kubwa aridhini
	MISINGI MATATU	**KUMJUA ALIYE TUKUKA ;** Mola mlezi ni Yule mwenye kuabudiwa,Aina za ibada,Hukumu kwa mwenye kufanya chochote katikaaina za ibada kwa asiye kuwa Allah pamoja na dalili zake
		KUJUA DINI YA KIISLAM KWA DALILI; Kujua uislam,misingi ya dini ,nguzo za uislam,kujua shahada ,nguzo za imani ,sehemu ya imani,dalili za misingi ya imani dalili za kiama.
		KUMJUA MTUME WAKE;Kuzaliwa kwake umri wake ,unabii wake ,utume wake,mji wake hekma ya kupewa kwake utume,muda aliolingania tawheed,safari ya ISRAA,na MIRAJI,wap na lini ilifundishwa swal,kuhama na lini na ipi hikma yake ,wakati gani sheria zilizo bakia zilianza kufanya kazi,muda wa kulingania ,na kufariki kwake,mambo alio kuja nayo katika dini kuenea kwa utume wake kwa viumbe wa aina mbili kukamilika kwa dini na kwa kutumia neema.

MISNGI MITATU (NAYO KWA MUKHTASARI MASWALI YA KABURINI) , DALILI ZAKE , KWA NINI TUNASOMA TAUHID? KWA NINI TUNASOMA MISINGI MITATU ?	MWISHO	Kufufuka baada ya kufa na kuhesabiwa kwa matendo,ukafiri kwa mwenye kupinga kufufuka ,wadhifu wa mitume na kulingana kwao,wa kwanza kwa mitume na wa mwisho wao,nguzo za Tauhid;ukafiri wa shetani na kumuamini Allah,kumjua shetani,viongozi wa mashetani,sifa ya ukafiri wa shetani maana ya neno(Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah uislamu ndio iniini ya dini.msingi wa			
		AINA ZA JIHADI	**JIHADI YA NAFSI**	Hii jihadi inakua kama ilivyo elezwa katika suratul-Asri(Ni elimu,kuifanyia kazi hiyo elimu,na kulingania elimu,pia na kuwa na subira)	
			JIHADI YA SHETANI	**MATAMANIO YA NAF SI**	Madhambi makubwa (Ni kila dhambi ilivopangiwa adhabu yake maalum)
					Madhambi madogo(Ni kila lililo haramishwa likawa halikupangiwa adhab maalumadhabu yake maalum)
				MAMBO YENYE KUTAMANISHA	Shirki kubwa (Ni ile yenye kumtoa mtu katika mila ya uislamu. Shirki ndogo
					Uzushi
			JIHADI YA MAKAFIRI NA WANAFIKI	Jihadi hii inakuwa kwa moyo, kwa ulimi, kwa viungo na kwa mali	
			JIHADI YA VIONGOZI WA DHULMA , WAZUSHI NA WAPINGAJ	Jihadi hii inakuwa kwa moyo, kwa ulimi na kwa viungo .	

TWAGHUTI	Ni kuvuka mipaka yake mja katika kuabudu kama vile (kuabudu mawe na miti) au mwenye kufuatwa (kama vile kuwafuata wanachuoni waovu) au mwenye kutiiwa (kama vile kuwatii viongozi walio nje na twaa ya Allah. Mashetani niwengi ,na viongozi wao wapo aina tano 1. Iblisi alie laaniwa na Allah.(na shekh hapa tambua hakika si vinginevyo amemlaani kwa kumwambia) 2.Mwenye kuabudiwa na akawa radhi 3. mwenye kudai kujua mambo ya sio onekana.4.mwenye kulingania watu katika ibada yake ,5mwenye kuhukumu kinyume na alivyo teremsha Allah .

ALLAH NI MJUZI ZAIDI

Rehma na amani ziwe juu yake mtume Muhammad syeye na ahli zake na Maswahaba wake.

MTIHANI WA MISINGI MITATU NA DALLI ZAKE.

*CHAGUA JIBU KUTOKA NDANI YA YALE YAMO KWENYE MABANO

1. misingi mitatu ni kwa muhtasari maswali ya kaburi(ndiyo-hapana)

2.mtunzi wa hiki kitabu MISINGI MITATU amemlinga n mwenye kukisoma hiki kitabu katika (sehemu mbili –sehem tatu)

3-vimesifika vitabu vya mtunzi kitabu hiki kwa(sentensi nyepesi-kwa ujumla na ufafanuzi-kwa dalili kutoka katika Qur-an na sunna)

- kumuombea mwanafunzi- kujibu shubha za kisasa h – uwingi wa sherhe katika vitabu hivyo - kuleta maswali muhimu na majibu yake - Allah kuvijaalia vitabu kuwa ni vyenye kukubalika – yote yaliyotangulia .

4-inawezekana kugawa mpangilio wa asili ya kitabu hiki cha misingi mitatu katika vipengele (5, 6)

5-Kusoma Tawheed (ni faradhi itoshelezayo-faradhi ya lazima)

Dalili ya misingi mine(suratil-asr(surai-iklas)

6-Mwenye kujifunza kasha asiyafanyie kazi aliyojifunza mfano wa (manasara- mayahudi-wote wliotangulia)

7-Subra(inatosha kusimisha hoja-inatosheleza sura zilizobakia)

8-Maana ya kauli ya imam Shafi katika suratul asri ya kwamba hiyo sura(inatosha kusimamiaha hoja inatoshelezasura zilizobakia)

9-Mwenye kuamini aina moja ya tawheed bila ya kuamini aina zilizo bakia hawezi kuwa na imani ya Tawheed(sahihi-kosa)

10-mwenye kujitakasa na shirki na jamii yake kunakuwa kujitakasa huko ni kwa (moyo,ulimi na viungo-kujitakasa na matendo na mwenye kutenda-vyote)

11-Maana ya neno (misikiti)katika jina lake Allah (Na hakika misikiti ni ya Allah) maana yake(misikiti iliyojengwa –viungo vya kusujudia-Ardhi ammbayo husujudiwa juu yake –majibu yote sawa)

12-Mwenendo wa wema waliotangulia ni (dalili kasha ndio itikadi-ni itikadi kasha ndo dalili)

13-Mwenye kupotea miongoni mwa wanachuoni wetu basi huko ni kufanana(mayahudi-manasara)

14-Mwenye kupotea miongoni mwa waaumini wetu basi huko ni kufanana na (mayahudi-manasara)

15-mambo matatu ndio misingi ya misingi Mitatu(sahihi-kosa)

16-Inagawanyika dua kwenye (dua ya ibada,na dua ya maombi na uhalisia wa mtu,na dua ya hali ya kusoma)

17inagawanyika dua ya mambo kwenye(sehem-sehem nne)

18- Wamegawanyika watu katika kuitikadi sababukwenye(vigawanyo viwili na katika –shirki kubwa na ndogo na inavyofaa)

19-kuna sahihi kujiokoa kwa kutumia viumbe(bila sharti kwa kile anocho kiweza kwa masharti manne)

20-Maana ya neno (Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokua Allah ni(Muweza juu ya kuumba –Hakuna wa kuabudiwa isipokua Allah –yote yalio tangulia ni majibu)

21-kujikurubisha na dini nyingine (inajuzu-kukubwa-ukafiri)

22-Dalili zenye kuonesha uwepo Allah kwa ujumla dalili hizo ni (Nyingi-Nne)

23-Je malaika wana mioyo(ndio-hapana)

24-Uhusiano wa Tauhid na imani ni kwamba imani ni jambolililo kusanya vitu vyote,na Tauhid ni sehem katik iman(sahihi-kosa)

25-Nguzo za imani (5,6,8)

26-Washirikina wanasehemu katika kumuabudu Allah(sahihi-kosa)

27-Maana ya neno (misikiti)katika jina lake Allah (Na hakika misikiti ni ya Allah) maana yake(misikiti iliyojengwa –viungo vya kusujudia-Ardhi ammbayo husujudiwa juu yake –majibu yote sawa)

14-Mwenendo wa wema waliotangulia ni (dalili kasha ndio itikadi-ni itikadi kasha ndo dalili)

15-Mwenye kupotea miongoni mwa wanachuoni wetu basi huko ni kufanana(mayahudi-manasara)

16-Mwenye kupotea miongoni mwa waaumini wetu basi huko ni kufanana na (mayahudi-manasara)

17-mambo matatu ndio misingi ya misingi Mitatu(sahihi-kosa)

18-Inagawanyika dua kwenye (dua ya ibada,na dua ya maombi na uhalisia wa mtu,na dua ya hali ya kusoma)

1-.inagawanyika dua ya mambo kwenye(sehem-sehemnne)

2-.Wamegawanyika watu katika kuitikadi sababukwenye(vigawanyo viwili na katika –shirki kubwa na ndogo na inavyofaa)

21-kuna sahihi kujiokoa kwa kutumia viumbe(bila sharti kwa kile anocho kiweza kwa masharti manne)

22-Maana ya neno (Hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokua Allah ni(Muweza juu ya kuumba –Hakuna wa kuabudiwa isipokua Allah –yote yalio tangulia ni majibu)

23-kujikurubisha na dini nyingine (inajuzu-kukubwa-ukafiri)

24-Dalili zenye kuonesha uwepo Allah kwa ujumla dalili hizo ni (Nyingi-Nne)

25-Je malaika wana mioyo(ndio-hapana)

26-Uhusiano wa Tauhid na imani ni kwamba imani ni jambolililo kusanya vitu vyote,na Tauhid ni sehem katik iman(sahihi-kosa)

27-Nguzo za imani (5,6,8)

28-Washirikina wanasehemu katika kumuabudu Allah(sahihi-kosa)

29-Mwenye kuabudiwa kinyume na anavyo abudiwa Allah na akaridhia huyo (ni shetani –siyo shetani)

30- Mwenye kumpwekesha Allah kwa kuuendesha ulimwengu huuna kuteremsha mvua hiyo tawheed (uungu-mlezi na majina masfi)

31-Miongoni mwa yanayo pingwa na misingi ya Tawheed ni(shirki –ndogo-na uzushi)

32-Miongoni mwa yalio wajibishwa ni pamoja na kuwatendea wema wazazi wawili(sahih-kosa)

34-Miiraji ni safari ya mtume kutokea makkah kwenda nyumba takatifu pale palestina(sahihi-kosa)

35-Alitumwa mtume Muhammad swalalahu walayhi wasalam kwa (watu wake maalumu-viumbe wa aina mbalimbali)

36-Nabii Muhammad swalalahu walayhi wasalam alikufa (manabii hawafi)

37-Mwenye kupinga kufufuliwa amekufuru kwa ukafiri(mkubwa-mdogo)

38-Dini ya manabii ni moja (kila nabii alikua na dini yake)

39-kuha (kulikoma baada ya ufunguzi wa mji wa makkah-bado kuendelea mpaka siku ya qiama)

40-hijra(kuhama kutoka mji kutoka mji wa ukafiri kwenda mji wa kiislam –kuachana nay ale aliyo ya haramisha Allah

41-Dini ya kiislamu imekamilika isipokua yale yaliopo ni miongoni mwa ndoto za waja wema(sahihi-kosa)

42-Kfanya ibada isiyo ya Allah ni shirki (kubwa-ndogo)

43-Hapana budi katika kutofautisha baina ya hukumu ya kitendo na hukumu ya mtendaji(sahihi-kosa)

44-Nabii wa kwanza ni(Nuhu(s.a)-Adam(s.a)

45-Nabii wetu swalalahu walayhi wasalam ni(nabii-mtume)

CHAGUA KUTOKA ORODHA YA MANENO YALIYO SAHIHI NA ORODHA YA PILI

ORODHA YA KWANZA	NAMBA	NAMBA	ORODHA SEHEMU YA PILI
Tawheed kilugha		1	Kauli ya Ah-mad:(utakapo muona kafiri amefumba macho kwa kuogopa kumuona adui wa Allah.
Tawheed kisheria		2	Inafungamana imani hii kwa kile linalo kuwa baada ya mauti.
Tawheed ya uungu		3	Ni kutamka kwa ulimi na kuamini kwa moyona kuto leglega kwa vitendo na nguzo(imani)inayo ongezeka kwa twaa na ina pungua kwa maasi. Ni uislamu na imani na ihsani.
Tawheed ya malezi		4	
Tawheed ya majina na sifa		5	Kwa ajili ya Allah na asiyekuwa Allah.
Hanifinya mlingano na kwanza na ni amri katika qur an		6 7	Wajibu na inajuzi na haramu. Ni kisheria na kihisio.
Shirki		8 9	Maswali ya kaburini. Ni elimu na amali na ulinganizi na subra. Ni kujitakasa na kufata.
Kutegemea		10	Ni uaminifu wa kuegemea kwa Allah pamoja na ujasiri wake na kuchukua sababu.
Sharti za kukubaliwa ibada		11	Ni khofu iliyojengwa juu ya elimu na kwa ukubwa wa Yule anaemuogopa na ukamilifu wa mamlaka yake.
Masaail manne kwa muhtasari		12	Ni mfano na uasawa.
Masaail matatu kwa muhtasari		13	Katika suuratul-baqara.
Misingi mitatu kwa muhtasari		14	Ni mila iliyo mbali na shirki iliyojegwa katik ikhlasi na Tauheed.
Sababu zina gawanyika kwenye		15	Ni kumpwekesha Allah kwa vile alivyojiita na kujisafisha katika kitabu chake na kwa maneno ya mtume wake swalla llahu alayhi wasallama na hayo ni mwenyewe na kukanisha yale aliyoyakanusha yeye mwenyewe bila ya kubadilisha wala kuzidishs na bila ya kufananisha .
Nadhiri imegawanyika kwenye		16	Ni kumpwekesha Allah katika ibada
Kunagawanyika kuchinja kwenye		17	
Kinagawanyika khofu		18	Kumpwekesha Allah katika kuumba,kumiliki na kuendesha

kwenye		19	
Uslamu		20	Ni kumpwekesha Allah kwa yale ambayo yana muhusu.
Misingi ya dini		21	Ni asili ya kitendo(alifanya kitu kuwa kimoja)
Imani			Ni kuchomoza jua upande wa magharibi au kufikiwa na umauti.
Kuamini siku ya mwisho kuna fungamana		22	Yale ambayo anavuka mja mipaka yake katika kuabudu au kufata au kutii.
Miongoni mwa Kujiweka mbali na shirki		23	Ni Tawhed ya majina na sifa au Tawheed ya uungu na kujiweka mbali na shirki.
Muda wa kukoma toba		24	Ni kujisimamisha na Allah na kufuata kwa kutii na kujiepusha na shirki na watu wake.
Shetani		25	Kile kinacho abudiwa kinyume na Allah juu ya picha.

KUNAGAWANYIKA KUCHINJA KWENYE		17	NI KUMPWEKESHA ALLAH KWA IBADA
INAGAWANYIKA KHOFU KWENEYE		18	NI KUMPWEKESHA ALLAH KWA KUUMBA NA UFALME NA KUENDESHA .
UISLAMU		19	NI KUMPWEKESHA ALLAH KWA YANAYOMHUSU .
MISINGI YA DINI		20	ASILI YA KITENDO ALIPWEKESHA KITU . NI KUKIFANYA KITU KUWA KIMOJA .
IMANI		21	NI KUCHOMOZA JUA KUTOKA MAGHRIBI AU KUFIKWA MAUTI .
KUAMINI SIKU YA MWISHO KUNAFUNGAMANA		22	NI KUVUKA MTU MIPAKA YAKE KWA KUABUDU AU KUFATA KUTII .
KATIKA KUJIEPUSHA NA SHIRKI		23	TAWHEED YA MALEZI NA MAJINA NA SIFA NA TAWHEED YA UUNGU NA KUJIEPUSHA NA SHIRKI NA WATU .
WAKATI WA KUKOMA TOBA		24	NI KUJISALIMISHA KWA ALLAH NA KUFATA KWAKE KWA KUTII NA KUJIEPUSHA NA SHIRKI NA WATU .
SHETANI		20	NI KLE KINACHOABUDIWA KWA PICHA

AL-QAWAAIDUL-AR-BAA

(KANUNI NNE)

BISMILLAH RAHMANI RAHIM

Kwa hakika kila sifa njema ni milki yake Allah. Tunamsifu na tunamuomba msaada. Na tunamtaka msamaha, tunajilinda kwa Allah na shari zote zitokanzo na nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu. Yeyote ambaye ameongolewa na Allah basi hakuna yeyote atakae mpoteza, na Yule aliyempoteza hakuna wa kumuongoa.

Ninashuhudia ya kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa ila ni Allah pekee asiye na mshirika. Na namshuhudia ya kwamba Muhammadi rehma na amani ziwe juu yake ni mja wa Allah na mtume wake. Ama ba'ada

Al-qaiwaidul-Ar-baa ndio matini ya pili ambayo imesomeshwa katika mfululizo wa matini za mtafuta Elimu. (mwanafunzi) umepatikana umuhimu wa kushughulikia matini hii kutokana na sababu nyingi sana. Miongooni mwazo ni:

- Kutunasihi wanachuoni wetu juu ya kuifundisha
  - Ndani yake kuna kujibu shubha za washirikina wa zama zetu
- Kuwaiga wanachuoni wema waiopita
  - Kwakuwa ni mukhtasari wa kitabu (kashfu shubhati)

Tutaianza hii matini kabla ya kitabu (kashfu shubhati,) ili isinase katika nafsi ya mwanafunzi shubha yeyote ile.

YALIYOMO KWENYE AL-QAWAAIDUL-AR-BAA

Imegawanywa hii matini katika sehemu tatu ambazo ni;

1. Utangulizi (Anuani ya mafanikio)
2. Umuhimu wa kuisoma Tawhid
3. kanuni

JAMBO LA KWANZA: UTANGULIZI

(ANUANI YA MAFANIKIO)

BISMILLAH RAHMAN RAHIM.

(1) Namuomba Allah mkarimu Mola mlezi wa Ar-sh tukufu akupende Duniani na Akhera
(2) Na akufanye kuwa ni mbarikiwa popote uwapo(3)

1. Sababu ya mtunzi kuanza matini yake kwa (Bismillah)

1. Kukiiga kitabu cha Allah na mitume na manabii, amani ya Allah iwafikie
2. Kwa kuwaiga walio kabla yake, katika wanachuoni wema ambao ilikua kawaida yao kuanza vitabu vyao kwa (Bismillah)
3. Ni katika mlango wa kutafuta Baraka kwa jina la Allah mtukufu.

Amesema Shaikhul Islami bin Taimiyya Allah amrehemu: (Atakae kuwa ni muumini mchamungu, atakuwa kipenzi cha Allah) dalili yake ni maneno ya Allah mtukufu: (Jueni kuwa vipenzi vya Allah hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika (62) Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu)

BARAKA: Maana yake ni kukua na kuzidi

TABARRUKU: Maana yake ni kuomba kukua na kuzidia. (kuomba Baraka)

MUBARAKU: Maana yake ni Yule ambaye hupatikana manufaa kupitia yeye popote awapo. (alie barikiwa)

Na akujaalie miongoni mwa wale wanapo pewa humshukuru Allah (1)

KUOMBA BARAKA KUMEGAWANYIKA KATIKA SEHEMU MBILI

Kuomba Baraka kisheria

Kuomba Baraka kuliko katazwa. Huo ni uombaji ambao haikuthibiti chochote kisheria, wala kihisia na hiyo ni katika aina za shirki ndogo.

Ama kisheria. Mfano; kuswali ndani ya masjidil-haram (Makka) au masjidi Nnabawiy. Msikiti wa mtume (Madina)

Ama kihisia: Elimu au dua na vinginevyo mtu hutakwa Baraka kwa elimu alionayo na kwa kule kulingania kwake kwenye kheri, kwa hiyo hii inakua ni Baraka kwa sababu sisi tunapata kheri nyingi kutoka kwake. Mfano vitabu vya shaikhul- islam na wengine katika wanachuoni ambao Allah ametia Baraka na kheri katika vitabu vyao, na umma ukanufaika navyo.

(1) Neema yeyote ni majaribio, pia ni mtihani. Dalili za hilo ni nyingi sana miongoni mwazo Allah anasema: (Na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri,) (Basi alipokiona kimewekwa mbele yake (kiti cha ufalme) akasema: Haya ni katika fadhila zake Mola wangu mlezi, ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru
Na mwenye kushukuru, kwa hakika anashukuru kwa manufaa ya nafsi yake, na anaye kufuru, kwa hakika Mola wangu mlezi ni mkwasi na karimu). (Ama mtu anapojaribiwa na Mola wake mlezi, akamkarimu na kumneemesha, husema: Mola wangu mlezi umenikirimu!) Na katika Hadithi (Hakika watatu katika wana wa Israili, Allah alitaka kuwajaribu…….)

NEEMA NI ZENYE KUSHIKAMANA NA TAUHID YA MALEZI YA ALLAH. (RUBUBIYYA) NA TAUHID YA IBADA (ULUUHIYYA) NAKUZISHUKURU KWAKE KUMEGAWIKA VIGAWANYO VIWILI.

Kushikamana na Allah kabla ya kupata neema

Na aina hii inamtaka mja aamini imani isiyo na shaka ya kwamba mwenye kutoa neema ni Allah swalalahu walayhi wasalam hivyo ushikamane moyo wake kwa asiekuwa Allah wala asitafute kheri kwa yeyote isipokuwa kwa Allah tu. Kama vile pepo hutafutwa kwa Allah swalalahu walayhi wasalam kwani yeye ndiye mmiliki wake, pia hata riziki haiwezekani kutafutwa isipokuwa kwa Allah tu. Allah anasema (Na mtegemee aliye hai ambaye hafi) hakika hao mnaowaabudu badala ya Allah hawakulimikini riziki yoyote.

Takeni riziki kwa Allah, yaani kutoka kwa Allah tu, na si kwa mwingine, na mumuabudu yeye na mumshukuru yeye.

Kushukuru baada ya kupata neema inakuwa kwa;

MOYO

Kwakuwa na imani ya kweli na kumuamini, na kujisalimisha kuliko timia ya kwamba anaeetoa riziki na kuneemesha ni Allah subhanahu wataala hakika kila neema aliyokuwa nayo mja inatoka kwa Allah subhanahu wataala

ULIMI

Hilo ni kwakuzungumza neema za Allah na kwa kusifu na kumshukuru juu ya hizo neema kwa kauli yake Allah mtukufu (Na neema za Mola wako mlezi zisimulie)

VIUNGO

Na hilo ni kwa kuzitumia neema kwa namna ambayo Allah subhanahu wataala ataturidhia, pia kwa kuongeza kufanya matendo mema kwa lengo la kujiweka karibu na Allah subhanahu wataala na kujiepusha na maasi. Kwa kutekeleza amri zake Allah.

1. **HAKIKA SUBIRA NI WAJIBU KWA MAKUBALIANO YA UMMAA HUU.**

NA PINDI AKIPEWA MTIHANI ANAKUWA NA SUBIRA (1)

WATU WANAPOPATA MATATIZO KATIKA HII DUNIA HUGAWANYIKA SEHEMU KUU NNE NAZO NI

- MWENYE KUCHUKIA
- MWENYE KUSUBIRI
- MWENYE KURIDHIA
- MWENYE KUSHUKURU

1. **KUCHUKIA.** Ni jambo la haramu na ni katika madhambi makubwa na huwa kwa;

- **MOYO**
- **ULIMI**
- **VIUNGO**

- **KUCHUKIA KWA MOYO**. Amesema Imaam Ibnul-qayyim Al-jauziyya. Katika maana ya maelezo yake, "hakika baadhi ya watu hawathubutu kuseema maneno haya kwa ulimi wao lakini nafsi yake ambayo ipo katika mwili wake hushuhudia hilo. Kwa kumdhania Mola wake mlezi dhana mbaya Husema kwa moyo wake, Mola wangu mlezi dhana mbaya Husema kwa moyo wake, mola wangu mlezi amenizuwilia. Kuna anaesema sana na anaesema kidogo. Kwa hiyo ichunguze nafsi yako, je wewe umesalimika na hii dhana? Ukiwa umeokoka nayo basi umeokoka katika jambo kubwa sana."
- **KUCHUKIA KWA ULIMI.** Inakuwa kwa kupiga kelele, na kunung'unika na kupiga mayowe, na kulaani na kutukana.
- **KUCHUKIA KWA VIUNGO.** Inakua kwa kupiga mashavu na kuchana nguo, na kunyofoa nywele.

2. **SUBIRA.** Hukumu yake ni wajibu kwa makubaliano ya umma huu ni wajibu kuwa na subira katika moyo wake na ulimi wake na viungo vyake.
   Amesema Imaam Ahmad (Limekuja neon SUBIRA katika Qur'an karibu sehemu tisini kuwa na subira ni wajibu kwa makubaliano ya umma huu. Subira ni nusu ya iman, Kwani imani ipo nusu mbili. 1. Nusu ni kusubiri 2. Nusu ni kushukuru) Rejea kitabu (MADARIJUASSALIKINA) CHA Ibn-qayyim.
3. **KURIDHIA;** Hukumu yake ni mustahabu (Ni jambo lenye kupendwa) na hilo lina daraja ya juu kuliko subira.
4. **KUSHUKURU;** Hukumu yake ni mustahabu. (Ni jambo lenye kupendwa) na ndio daraja bora na kamilifu yake.

JAMBO LA PILI: KANUNI NNE

BISMILLAH RAHMAN RAHIM

Fahamu ewe Muislamu, Allah akuongoe kwenye twaa yake, Hakika uongofu wa kweli ni kufuata mila ya Nabii Ibraim (Amani ziwe juu yake) Nako ni kumuabudu Allah pekee hali ya kumtakasia dini yake, kwa sababu Allah ndio amewaamrisha watu wote (waifuate hiyo tauhid) na amewaumba kwa ajili yake. Kama alivyosema Allah:

"Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu mimi" (1)

Ikiwa umetambua kuwa dhumuni kuu la Allah kukuumba wewe ni kwa ajili ya kumuabudu yeye tu, Basi tambua pia kuwa ibada haitoitwa ni ibada ila iwe na tauhid ndani yake, kama ilivyo swala haiwezi kuitwa swala ila iwe na twahara, Basi shirki ikiingia kwenye ibada yoyoyte huiharibu kabisa ibada hiyo, kama vile hadathi inapoingia kwenye twahara (huiharibu)

(1) Mwandishi Allah amrehemu anabainisha sababu za sisi kujifunza Tauhid.

(2) Makafiri ambao mtume swalallah alayih wasalama alitumwa kwao walikuwa wakiikiri Tauhid rububiyya pamoja na hivyo mtume swalla llahu alayih wasallama aliwapiga vita. Ugomvi uliokuwa kati yao na mtume swalla llahu alayihi wasallama ilikuwa ni Tauhid ya ibada, Basi kwa kila atakaye elekeza ibada yoyote kwa asiye kuwa Allah huyo atakuwa ni mshirikina kafiri.

Ikiwa umefahamu kwamba shirki inapochanganyika na ibada huiharibu, na huporomosha thawabu za amali hiyo na mwenye kutenda hilo atakuwa mtu wa motoni milele hapo utakuwa umefahamu kuwa lililo hapo wajibu kwako ni kujua Tauhid tu ili Allah subhanahu wataala akunasue kwenye huo mtego wa shirki, ambayo Allah ameisemea ndani ya Qur'an 4:48:

"Hakika Allah hasamehi kushirikishwa, na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye, Na anaye mshirikisha Allah basi hakika amezua dhambi kubwa sana"(1)

Na hilo la kujiepusha na shirki litafanikiwa kwa kuzijua kanuni nne ambazo Allah kazitaja ndani ya kitabu chake.

KANUNI YA KWANZA.

Ni kufahamu kwamba, makafiri mabao mtume subhanahu wataala alipigana nao walikuwa wakithibitisha kuwa Allah aliye tukuka ndiye muumbaji na ndiye mpangaji wa mambo yote, lakini imani hiyo haikuwafanya wao kuingia kwenye Uislamu. Dalili ya hilo ni kauli yake Allah subhanahu wataala

Sema: Ni nani anaye kuruzuku ni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Au ni nani anaye miliki kusikia na kuona? Na ni nani amtoaye hai kutoka maiti? Na akamtoa maiti kutoka aliye hai? Na nani anaye yapangilia mambo yote? Watasema: Allah. Basi sema: Je Hamumchi? (10:31) (2)

KANUNI YA PILI:

Makafiri husema: sisi hatuwaombi (hao) na kuwaelekea isipokuwa ni kwa ajili ya kufuta kurba na shafaa kutoka kwao.

Dalili ya kutafuta kurba ni kauli yake Allah subhanahu wataala

"Na wale wanaowafanya wenginewe kuwa walinzi wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Allah – Hakika Allah atahukumu baina yao katika wanayokhitalifiana. Hakika Allah hamwongoi aliyemuongo kafiri (39:3) (1)

DALILI YA KUTAFUTA SHAFAA.

Nao badala ya Allah wanabudu wasio wadhuru wala kuwanufaisha na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Allah! Sema: Je! Mnamwambia Allah asiyoyajua ya katika mbingu wala katika ardhi? Subhannahu wa Taa'la! Ametakasika na ametukuka na hao wanao mshirikisha naye. 10:18

SHAFAA (UOMBEZI) UKO WA NAMNA MBILI:

1- Uombezi unaokubalika
2- Uombezi usio kubalika. *2

*(1) Makafiri na washirikina hujenga hoja ya kuwa wao hawaiombi na kuielekea Miungu yao ya batili isipokuwa ni kwa ajili ya kuruba na uombezi kutoka kwao kwa hakika walistahiki kwa hali hiyo mtume swalalahu walayhi wasalam awakufurishe na kuwapiga vita.

***(2) SHAFAA:** Kilugha ni kukusanya na kukifanya kitu kimoja kuwa viwili.

SHAFAA: Kisheria ni kumuweka kati kiumbe mwingine kwa lengo la kuleta manufaa au kuondoa madhara.

VIGAWANYO VYA SHAFAA

SHAFAA INAYOKUBALIKA.

Hiyo ni ile inayoombwa kutoka kwa Allah. na sharti zake ni kama ifuatavyo:

1- Ruhusa ya Allah kwa uombezi huo.
2- Ridhaa ya Allah kwa aneombea.
3- Ridhaa ya Allah kwa anae ombewa.

KWENYE MAMBO YALIYO KWENYE UWEZO WA KUIMBE.

Shafaa itafaa kwa sharti nne zifuatazo:

1- Muombezi awepo
2- Awe hai
3- Awe na uwezo juu ya jambo hilo
4- Awe ni sababu tu (Asiitakidiiwe ndio muwezeshaji)

SHAFAA ISIYOKUBALIKA:

Shafaa hii iliyokanushwa na Qur'an ni ile ambayo huombwa kwa asiye kuwa Allah katika mambo ambayo hakuna mwenye uwezo nayo ila ni Allah pekee. Hukumu ya shafaa hii ni shirki kubwa atakayeifanya.

Shafaa inayomuhusu mtume pekee wala hakuna anaye shirikiana nae katika hilo

- SHAFAA KUU
- Shafaa kwa amini yake ABU TWALIBU apunguziwe adhabu
- Uombezi wake mtume ili milango ya peponi ifunguliwe

Shafaa ya pamoja ya mitume, malaika, waja wema na watoto wadogo.

- Kwenye kuinua daraja za waumini
- Kwa Yule aliyestahiki kuingia motoni asiingie motoni
- Kwa Yule aliyeingia motoni katika waislamu atolewe humo

UOMBEZI USIOKUBALIKA:

Ni ule utakao kuwa unaombwa kutoka kwa asiye kuwa Allah subhanahu wataala kwenye mambo ambayo hakuna awezaye ila yeye tu. Na dalili yake ni kauli ya Allah subhanahu wataala;

"Enyi mlio amini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika siku ambayo hapatakuwapo na biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhalimu. (2:254)

UOMBEZI UNAOKUBALIKA:

Huu ni ule ambao unaombwa kutoka kwa Allah, Lakini muombaji awe amekimiriwa huo uombezi na anayeombewa awe ni Yule Allah aliyemridhia kwa kauli na matendo baada ya kutoa ruhusa. Kama alivyosema Allah subhanahu wataala

"Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila idhini yake? (2:255).

KANUNI TA TATU: (1)

Hakika Mtume swalla llahu alayhi wasallama alikuja kwa watu waliokuwa wametofautiana katika ibada zao, miongoni mwao wamo waliokuwa wakiwaabudu malaika, Wengine wakiwaabudu mitume na watu wema, wengine wakiabudu miti na mawe, na wengine wakiabudu Jua na mwezi. Mtume swalla llahu alayhi wasallama hakuwatenganisha bali alipigana nao wate.

Ushahidi juu ya hilo ni kauli yake Allah subhanahu wataala

"Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na dini yote iwe kwa ajili ya Allah……(8:39)

DALILI YA KUABUDU JUA NA MWEZI NI KAULI YAKE ALLAH SUBHANAHU WATAALA:

Na katika ishara ake ni usiku na mchana, na jua na mwezi: Basi msilisujudie jua wala mwezi bali msujudieni Allah aliye viumba ikiwa nyinyi mnamuabudu yeye tu. (41:37)

*(1) Kanuni hii dalili ya wazi kabisa katika kuwapinga wale wote wanaosema kuwa shirki inakuwa tu kwa wale wanaoabudu masanamu zikaja dalili zote za kisheria kuhusiana na kuabudu masanamu na miungu mingine yote ya batili iliyokuwa ikiabudiwa kipindi hicho.

Wala mtume ***swalla llahu alayhi wasallama*** hakubagua kabisa kati ya miungu hiyo bali alihesabu miungu yote ni katika mataghuti, akapigana na wote wenye kuiabudu bila kumuacha hata mmoja ili dini yote iwe ni ya Allah subhanahu wataala isiyokuwa na hata chembe moja ya shirki.

NA DALILI YA KUABUDU MALAIKA NI AYA IFUATAYO:

Wala hatakuamrisheni kuwafanya malaika na manabii kuwa ni miungu……(3:80)

NA DALILI YA KUABUDU MITUME NI KAULI YAKE ALLAH SUBHANAHU WATAALA

"Na pale Allah atakaposema: Ewe Isa bin Maryam! Ati wew uliwaambia watu: nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Allah? (Na Isa) atasema: Subhanaka, wewe umetakasika! Hainifai mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila shaka umekwisha yajua; Wewe unayajua yaliyomo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyomo ndani ya nafsi yako. Hakika wewe ndiye mjuzi mkubwa wa yaliyofichikana. (5:116).

NA DALILI YA KUABUDU WAJA WEMA NI AYA HII?

Hao wanao waomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kwendea kwa Mola wao mlezi Hata miongoni mwao walio karibu mno – na wanataraji rehema zake na wanaikhofu adhabu yake. Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi yafaa kutahadhari nayo (17:57)

NA DALILI YA KUABUDU MITI NA MAWE INAPATIKANA KATIKA AYA IFUATAYO:

Je! Mmemuona Lata na Uzza? (19) Na Manaat, mwingine wa tatu? (20) (53:19-20)

Na hadithi iliyoelezwa na sahaba ABU WAQID AL-LAYTH (Radhiyallah an'hu) amesema:-

'Tulitoka tukiwa na mtume swalla llahu alayhi wasallama kuelekea katika vita vya Hunaini (Baada ya Fatih – Makka)

Hali ya kuwa sisi ni wageni katika Uislamu, na washirikina zama hizo walikuwa wana mti wa mkunazi wakikaa itikafu kwenye mti huo na wakitundika silaha zao juu yake (kwa ajili ya kutabaruku) Mti huo uliitwa dhatu an-wati, tulipo upitia mkunazi nasi tukasema: Ewe mjumbe wa Allah! Nasi tuwekee mti wa kutundikia silaha zetu zibarikiwe kama wale washirikina wanavyofanya……

KANUNI YA NNE:

Hakika washirikina wa zama zetu (za sasa) wana shirki kubwa zaidi kuliko wale wa mwanzo, kwa sababu washirikina wa mwanzo walifanya shirki kipindi cha raha na wakijitakasa kipindi cha shida. Lakini washirikina wa zama zetu shirki yao ni ya wakati wote kwenye raha na shida (huendelea na shirki zao)

Dalili ya hilo ni kauli ya Allah:

"Na wanapopanda katika marikebu humuomba Allah kwa kumsifia utiifu. Lakini anapo wavua wakafika nchi kavu mara wanamshirikisha (1) (29:67)

WALLAHU – A'ALAMU

(ALLAH NDIO MJUZI ZAIDI)

Rehema na Amani zimwendee Mtume wetu Muhammad yeye na jamaa zake na sahaba zake wote.

*Kwenye kanuni hii ya nne mwandishi "Allah amrehemu" ameweka wazi upeo wa hatari ya msimamo wa washirikina wa hizi zama zetu, wao ni washirikina wakubwa mno kuliko hata wale washirikina wa mwanzo, kwa sababu washirikina wa hizi zama tulizo nazo humshirikisha Allah subhanahu wataala katika shida na raha, ama washirikina wa mwanzo wao walimshirikisha Allah subhanahu wataala katika kipindi cha raha tu, na kipindi cha dhiki na tabu waliukiri upweke wa Allah subhanahu wataala wakamtakasia ibada.

Ikiwa washirikina ambao Mtume *swalla llahu alayhi wasallama* alipelekwa kwao, shirki yao ni ndogo ukilinganisha na zama hizi, lakini Allah subhanahu wataala aliwapinga na kuwakufurisha, Je hali itakuwaje kwa wale ambao shirki zao ni kwa wakati wote, kwenye shida na raha? Basi hao ndio wanastahiki zaidi kuwa makafiri (kuliko wale wa mwanzo).

KANUNI NNE NAYO NI UFUPISHO (KASHF-SHUBHAT)		
UTANGULIZI NA NDANI KUNA ANWANI YA MAFANIKIO		
ANWANI YA WEMA		
PINDI AKIPENDA HUSHUKURU		
NEEMA NI MTIHANI ALLAH AMESEMA (NA TUNAKUJARIBUNI KWA MTIHANI WA KHERI NA SHARI)		
KUSHUKURU NEEMA	YENYE KUFUNGAMANA NA TAUHID YA MALEZI	Kutafuta pepo hakuwi isipokuwa ni kutoka kwa Allah kwa sababu yeye aliyetukuka ndiye ambae anaimiliki, na hivyo hivyo Riziki haitafutwi ila kutoka kwa Allah. Basi hatuna budi kufungamana kwa Allah, na sio kwa Mwingine.
	YENYE KUFUNGAMANA NA TAUHID YA IBADA	**Kushukuru kwa moyo wake**: kwa kujua na kukiri kuwa, hakika kila jambo lenye neema basi jambo hilo limetoka kwa Allah na sio kwa mwingine
		Kushukuru kwa kusema kwake. *(Haya ni katika fadhila zake mola wangu mlezi ili anijaribu nitashukuru au nitakufuru)*
		Kushukuru kwa viungo vyake: Ni kuitumia neema katika kumshukuru mwenye kuneemesha, na kila neema kwa kiwango chake, kwa hiyo kushukuru neema ya mali ni kuitoa katika Twaa ya Allah, na kushukuru neema ya elimu ni kuitoa kwa mwenye kuiomba, ima kwa kusema kiuhalisia au kimakala.
	HALI YA WATU WAKATI WA MATATIZO	**Hasira:** Hukumu yake ni kubwa bali inampeleka mtu kwenye shirki ndogo, na nakuwa na hasira kwa moyo, kuzungumza na kutekeleza
		Subira: Hukumu ya subira ni wajibu kwa makubaliano ya umma, husubiri mtu kwa moyo wake, ulimi wake, na viungo vyake na subira mfano wa jina lake imejipamba kutokana na utamu (asali).

	RADHI: Hukumu yake ni yenye kupendeza (inastahiki) na kukamilika radhi zake kwa Mola wake ajue kwamba kila lile lililo mpata basi limetoka kwa Allah na kila lile alilokadiria Allah kwa mja wake
	KUSHUKURU: Ni jambo lililokuwa juu zaidi ya misingi nalo ni jambo lenye kupendeka zaidi na linakuwa jambo hilo kwa waja wa Allah wenye kushukuru
PINDI ANAPOFANYA DHAMBI HUOMBA MSAMAHA.	
KWANINI TUNAJIFUNZA TAUHID NA HATARI YA SHIRKI?	HANIFIA: Mila ya Ibrahimu, Hakika Allah amekuumba wewe kwa ajili ya ibada yake (kumuabudu) Ibada yoyote haiwezi kuitwa ni ibada mpaka ibada hiyo iwe pamoja na Tawhid. Na pindi shirki ikichanganyikana na ibada huiharibu na kuporomosha amali za mja, na kumfanya mja huyo kuwa ni miongoni mwa watakaoishi motoni milele. Na ni mambo yaliyo muhimu zaidi juu yako kuyajua.
MSINGI WA KWANZA: Hakika makafiri waliompinga mtume swalalahu walayhi wasalam walikuwa wanakiri Tauhid ya malezi, lakini walikuwa hawakiri Tauhid ya uungu. Jambo hili la kukiri halikuweza kuwafanya wawe waislamu.	
MSINGI WA PILI: Hakika Makafiri walikuwa wanaabudu masanamu kwa ajili ya maombi na kujikurubisha.	
MSINGI WA TATU: Hakika mtume aliwakuta watu wametofautiana katika ibada zake, na hakutofautisha kati ya shirki na shirki.	
MSINGI WA NNE: Hakika washirikina wa zama hizi, shirki zao ni kubwa kuliko shirki za watu waliotangulia.	

MTIHANI WA KANUNI NNE.

JINA: _____ KIWANGO CHA KUHIFADHI KITABU CHA TAWHID _____

JE UMEHIFADHI MISINGI MINNE: _____

KAZI	DALILI KUTOKA KATIKA QUR'AN AU HADITHI.
NEEMA YA MTIHANI	
KUKIRI MAKAFIRI TAUHID YA MALEZI	
KUTAFUTA UKARIBU	
MAOMBEZI YALIYOKATALIWA	
DALILI YA JUA NA MWEZI	
DALILI ZA MALAIKA	
DALILI ZA MANABII	
DALILI ZA WEMA	
DALILI ZA MAWE NA MITI	
HAKIKA WASHIRIKINA WAKATI WA MATATIZO WANAMUAMINI NA KUMTAKA ALLAH WAKATI WA RAHA WANAMSHIRIKISHA.	
DALILI ZA SHIRKI	

ANDIKA KILE UNACHOKIJUA KWA YAFUATAYO:-

KWANINI TUNAJIFUNZA TAUHID	**1- 2- 3- 4-**
5- 6- 7- 8- 9-	
KWANINI TUNAJIFUNZA MISINGI -4	**1- 2-**
-3 4-	
INAGAWANYIKA MISINGI 4 KWENYE	**1- 2- 3-**
MISINGI YA MUKHTASARI KWA KITABU	
KWANINI TUNAJIFUNZA KITABU (KASHFU SHUB-HAAT)	
ANWANI YA MAFANIKIO	**1- 2- 3-**
"HANIFIA" NI	
FAIDA YA KUSOMA MISINGI	
VIPENZI WA ALLAH NI:-	**AMESEMA SHEIKH WA UISLAMU**
NA DALILI JUU YA HAYO	**NA KWA AJILI GANI?**
KUNAKUWA KUSHUKURU NEEMA PAMOJA NA MFANO	
	1-
2-	
3-	

Vipi kunakuwa kufungamana kwa mja ?	
Hali za watu wakati wa matatizo pamoja na hukmu	
Shafaa kwa kilugha	**Shafaa kwa kisheria**
Inagawanyika Shafaa kwenye :	
Masharti ya Shafaa iliothibiti	
Na inagawanyika kwenye : 1- **na**	**Na inagawanyika kwenye :** **na**
2- **na**	**Na inagawanyika kwenye :** **na**
Msingi wa kwanza	
Msingi wa pili	
Msingi wa tatu	
Msingi wa nne	
Hukmu ya matendo pindi yatakapochangayika na na shirki	**Na Dalili**

	YALIYOMO:	UKURASA
1.	**UTANGULIZI**	***3***
2.	**JAMBO LA KWANZA** MAMBO MANNE YA MSINGI	***10***
3.	**JAMBO LA PILI** MAMBO MATATU YA MSINGI	***16***
4.	**JAMBO LA TATU** UMUHIMU WA KUJIFUNZA TAUHID	***20***
5.	**JAMBO LA NNE** MISINGI MITATU	***21***
6.	**JAMBO LA TANO** HITIMISHO	***50***
7.	KINAAMBATANA NA(MUHTASARI WA SHERHE YA MATINI KATIKA SURA YA JEDWALI)	***53***
8.	MTIHANI WA MISINGI MITATU NA DALILI ZAKE	***57***

	YALIYOMO	UKURASA
1.	**UTANGULIZI** (NA NDANI YAKE KUNA ANWANI YA MAFANIKIO)	66
2.	**JAMBO LA KWANZA** KANUNI YA KWANZA	71
3.	**JAMBO LA PILI** KANUNI YA PILI	71
4.	**JAMBO LA TATU** KANUNI YA TATU	73
5.	**JAMBO LA NNE** KANUNI YA NNE	75
6.	**JAMBO LA TANO** KINAAMBATANA NA(MUHTASARI WA SHERHE YA MATINI KATIKA SURA YA JEDWALI)	76
7.	**JAMBO LA SITA** MTIHANI WA KANUNI NNE	78
8.	**JAMBO LA SABA** YALIYOMO	81

مترجم الى اللغة السواحلية

Kimetafsiriwa kwa lugha ya kiswahili

SHERHE YA KITABU TTAWHIID

شرح كتاب التوحيد

JINA LA MTUNZI
DR:HAYTHAM SARHAAN

HAIFAI KUUZA

SHERHE YA KITABU TTAWHIID • شرح كتاب التوحيد

VIGAWANYO NA MISINGI (KANUNI) ZA KITABU CHA “ALQAULUL-MUFID”(MANENOYENYE FAIDA)

Kwa kalamu yamahitaji msamaha wa Mola wake

HAYTHAM MUHAMMAD SAR-HAAN

Mwalimu mstaafu katika maahad ya Haram kwenye msikiti wa mtume na msimamizi wa tovuti ya:- (kitengo cha)

http://attasseel–alelmi.com

Allah amsamehe yeye na wazazi wake na atakae saidia kukitoa kitabu hiki.

CHAPA YA KWANZA.

Haki zote zimehifadhiwa.

Isipokuwa atakaetaka kukichapa au kukifanyia tarjama ili akisambaze bure baada ya kukirejea mtunzi

Wasiliana kwa:

Islamtorrent@gmail.com

KWA JINA LA MWENYEZIMUNGU MWINGI WA REHMA MWENYE KUREHEMU

Hakika shukrani/sifa njema anastahiki Mwenyezimungu, tunamtukuza na kumtaka msaada na kumtaka msamaha. Na tunajikinga kwa Mwenyezimungu kutokana na shari za nafsi zetu na kutokana na maoni ya matendo yetu. Atakae muongoza mwenyezimungu hakuna wa kumpoteza, na atakaempoteza hakuna wa kumuongoza. Na nashuhudia kuwa hakuna Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezimungu mmoja peke yake hana mshirika. Na namshuhudia kuwa Muhammadi ni mtume wake.

MISINGI INAYPTAKIKANA KUIJUA KABLA YA KUSOMA (KUJIFUNZA) KITABUHIKI.

[1] Ni juu ya mwenye kutafuta elimu, kuhifadhi matini kabla ya kujifunza (hifadhi kuwa kila mwenye kuhifadhi ni Imamu (kiongozi)
[2] Kujua kujua kila mtazamo wa kutoa dalili ya kila aya. Na sababu ya kuletwa kwake katika mlango husika.
[3] Kujua munasaba wa kila mlango wa kitabu cha Tawhid, na sababu ya kuletwa ndani yake, ili afungamanishe na kitabu hiki.
[4] Tuna weka mkazo juu ya sherhe moja tu. Na nguzo kwetu ni kitabu cha“kauli yenye faida” cha shekhe Ibn Utheymin Mwenyezimungu Amrehem. Tutakapo imaliza tuna chukua sherhe nyingine. Ili yasichanganyike maalumati (ufahamu)

KWANINI TUNASOMA HIKI KITABU?

[1] Kwa sababu wanachuoni walezi wametunasihi kuhusu hiki kitabu.
[2] Kwa sababu ni katika kitabu kizuri zaidi kilichotungwa katika mlango huu.
[3] Kwa sababu mtunzi Mwenyezimungu Amrehemu, ameleta vizuri ubatili wa hoja za mwenye kukhalifu/kupinga/kwenda kinyume na akarejesha shubuha kwa dalili.
[4] Kwa sababu Mwenyezimungu amemwekea kukubalika katika ardhi.
[5] Nasaha za wanachuoni katika kuhifadhi na kukifahamu
[6] Uzuri wa mipangilio ya milango yake na utaratibu
[7] Wana wachuoni kutilia umuhimu katika kukifundisha na wingi wa sherhe katika kitabu hicho
[8] Kwa sababu kitabu kimesheheni dalili kutoka katika Qur’ani na sunnah
[9] Wepesi wa Ibara zake
[10] Ushuhuda wa wanachuoni kwa mtunzi wa kitabu katika kubobea kwake kwenye elimu na usalama wa itikadi yake.
[11] Kwa sababu kitabu kimetilia umuhimu mkubwa kwenye Tawhid ya Ibada, kwa sababu ya makosa makubwa yaliyoingia kwenye Tawhid hiyo pamoja na kutaja kumpwekesha Mwenyezimungu katika matendo yake, majina, na sifa zake.
[12] Kwa sababu mtunzi Mwenyezimungu amrehemu, amefuata (pita) ndani yake njia ya wema waliotangulia. Haja taja chochote katika maneno yake. Kama alivyofanya Imamu **Bukhari** katika sahihi yake.

MUKH-TASARI WA MILANGO YA KITABU CHA TAWHID (MLANGO WA

Kabla ya kuanza kusoma kitabu chochote, Inatakiwa kusoma utangulizi na yaliyomo. Ili kujua madhumuni ya kitabu na njia ya utunzi na kukitambua kitabu kiukamilifu. Na kwa kufuata mfumo huo inatupasa kukigawanya kitabu chetu hiki vigawanyo kumi (10)

SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI (MILANGO 5)

MLANGO WA I

Ni kwa lipi wanatilia umuhimu mlango huu. Nao ni mlango wa kubainisha uwajibu wa Tauhid.

Sheikh ameuleta mlango huu ili kubainisha kwamba Tauhid (kumpwekesha Mwenyezimungu) ni ya kwanza na ni wajibu mkuu zaidi ya nyajibu zote na kwa sababu hio tauhid ndio daa'wa ya manabii Rehema na Amani ziwe juu yao.

MLANGO WA II

Mlango unaobainisha ubora wa Tauhid (kumpwekesha Mwenyezimungu) Na yale madhambi inayoyafuta.

- Ameleta mlango huu kwa ajili ya kutia shauku na kubainisha ya kwamba kutaja ubora wa kitu, sio dalili ya kutokuwa kweke ni wajibu. Na kwa sababu kuna wanao wakurupusha (watu) na kuwatia nyongo ya kusoma Tawhid na kuifundisha.

MLANGO WA III

Mlango unaobainisha kuwa mwenye kuihakiki tauhid anaingia peponi bila ya hesabu.

- Ameletamlango huu kwa ajili ya kuitakasa tauhid kutokana na shirki na bid-a (uzushi) na maasi. Ikawa ni mnasaba sheikh alete Mlango huu baada ya milango miwili yenye kubainisha uwajibu wa Tauhid na Fadhila zake

MLANGO WA IV

Mlango wenye kubainisha khofu ya shirki (kuogopa shirki)

- Ameleta mlango huu kwa kuwa Mwenye kutaka kuihakiki Tauhid, ni wajibu aiogope shirki juu ya nafsi yake na juu ya wengine, na kwa hakika anaweza akadhani kwamba yeye ameihakikisha Tauhid hali yakuwa hajaihakiki, na kila mlango ameuleta baada ya Mlango huu, nao ni kuhakiki Tauhid. Kwa mfano Mlango wa khofu ya shirki ni katika kuhakiki Tauhid. (kuithibitisha)

MLANGO WA V

Mlango wenye kubainisha kulingania, katika kushuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah.

- Umekuja mlango huu. Na Allah ndio mjuzi zaidi kwa sababu mbili:-

1. Kwa sababu atakaetaka kuihakikisha tauhid, hana budi ailinganie kama alivyofanya Mtume (S.A.W) Na maswahaba zake.
2. Na ni kwa sababu ya kuradi(kurejesha) kauli ya mwenye kusema kwamba jambo la kwanza lenye kulinganiwa ni swala.

SEHEMU YA PILI.

2. TAFSIR YA TAUHID (MILANGOTISA)

(MLANGO WA 6)

Mlango wa kutafsir maana ya Tawhid na kushuhudia hapana mola apasae kuabudiwa isipokuwa Allah.

- Baada ya sheikh kututajia uwajibu wa Tawhid na kutupa shauku ya kuijua (Tawhid) na uwajibu wa kuihakiki. Na kuwa na hofu na shirki pia kuilingania hiyo Tawhid imekuwa nimnasaba. kututafsiria uhakika wa Tawuhid (kumpwekesha Allah) kwa kuanza na mlango huu mpaka mlango wa mwisho wa kitabu hiki.

(MLANGO WA 7)

Mlango huu unaeleza ni katika shirki: kuvaa bangili na uzi na mfano wake kwa ajili ya kuondosha mabalaa au kinga ya mabalaa.

- Na hii ndio tafsiri ya Tawhid inathibiti kwa kufahamu kinyume chake (ambayo ni shirki)

(MLANGO WA 8)

Mlango uliokuja kuzungumzia (kubainisha) Ruqya na hirizi.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutafsiri maana ya ruqya na hirizi za kishirikina ambazo zinakwenda kinyume na Tawhid.

(MLANGO WA 9)

Mlango uliokuja kubainisha anaye taka Baraka kwenye miti au mawe na mfano wake

- Sheikh ameleta mlango huu kutafsiri (kubainisha) kutaka Baraka iliyokatazwa inayopingana na Tawhid

(MLANGO WA 10)

Mlango uliokuja kubainisha kuchinja kinyume na Allah (Sub'hana wataala)

- Sheikh ametaka kututafsiria (kutubainishia) kitendo cha kuchinja kinyume na Allah (Sub'hanawataala)kwa mapenzi na kutukuza ni kwenda kinyume na Tawhid.

(MLANGO WA 11)

Mlango uliokuja kubainisha katazo la kuchinja kwa ajili ya Allah katika sehemu inayochinjwa kinyume cha Allah (Sub'hana wataala)

- Ametaka kutubainishia (tafsiri) yale wanayofanya baadhi ya watu wajinga kwenye kujifananisha na kushirikiana na washirikina kwenye (sherehe) zao na sehemu za ibada zao hayo ni miongoni mwa mambo yaliyokinyume kabisa na Tawhid.

(MLANGO WA 12)

Mlango huu unabainisha kuwa shirki kutia nadhiri kwa asiyekuwa Allah(Sub'hana wataala) ambayo inapingana na Tawhid.

- Ametaka kutubainishia (kututafsiria) kuwa nadhiri iliyokatazwa ni ile ambayo inapingana na Tauhid

(MLANGO WA 13)

Mlango uliokuja kubainisha kuwa ni katika shirki kutaka kujikinga kinyume na Allah (Sub'hana wataala)

- Sheikh ametaka kutubainishia (tafsiria) kujikinga kinyume na Mwenyezimungu kunakuwa kwa yale mambo asio kuwa na uwezo nayo kiumbe isipokuwa Allah (Sub'hana wataala)na na hilo ndilo hupingana na Tauhid.

(MLANGO WA 14)

Mlango uliokuja kubainisha ni shirki kutaka uwokozi kinyume na allah (Sub'hana wataala)

- Sheikh ametaka kutubainishia matendo ya shirki nayo ni kutaka uwokozi na maombi kwa asiyekuwa Allah kwenye mambo ambayo hakuna awezaye isipokuwa Allah(Sub'hana wataala)na hayo ndio mambo ambayo yanapingana na Tawhid.

SEHEMU YA TATU.

3. KUBATILISHA IBADA ZINAZO FANYIKA

(MLANGO WA 15)

Huu ni mlango wenye kubainisha maana ya kauli ya Allah

"Ati wanawafanya viumbe kuwa ni washirika wa mwenyezimungu nao hawaumbi bali wao ndio wanaumbwa?"(Surat Al'Araaf 191)

- Sheikh ameleta mlango huu ili kukanusha kuabudiwa yeyote kinyume na Allah, sawa sawa awe nabii au sanamu au tofauti na hivyo.

(MLANGO WA 16)

Mlango wenye kubainisha maana ya kauli ya Allah(Sub'hana wataala)

(....hata itakapo ondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: Mola wenu mlezi kasema? Watasema yaliyo kweli nay eye ndiye aliye juu mkubwa)

- Ameleta aya hii ili kukataza au kupinga ibada kwa malaika watakatifu.

(MLANGO WA 17)

Mlango wenye kubainisha maombezi.

- Ameleta mlango huu kutubainishia ubatili wa yale yanayofungamana na makafiri katika miungu yao nako ni kule kuiomba miumgu hiyo.

(MLANGO WA 18)

1. **Mlango wenye kubainisha maana ya kauli ya Allah**(Sub'hana wataala)

(Kwa hakika wewe humwongoi umpendae, lakini Mwenyezimungu humwongoa amtakae nay eye ndiye anawajua zaid waongokao)

Ameleta mlango huu kutubainishia ubatili wa uongofu wa tawfeeq kutoka kwa yeyote isipokuwa Allah pekee

SEHEMU YA NNE.

4. SABABU ZA KUKUFURU KWA WANADAMU

Sheikh baada ya kututafsiria maana ya Tawhid na kubatilisha ibada zote kwa asiyekuwa Allah imekuwa ni muafaka kututajia sababu za kuingia kweye ukafiri ili tujiepushe nao.

(MLANGO WA 19)

Mlango huu umekuja kutubainishia sababu za kukufuru wanadamu na kuacha dini yao ni kule kuchupa mipaka katika kuwatukuza waja wema ambao ndio

- Sababu ya hatari zaidi ya kutumbukia wanadamu kwenye ukafiri, nayo ndio shirki ya kwanza kuzuka (kutokea) katika ardhi.

(MLANGO WA 20)

Mlango huu umekuja kubainisha makemeo kwa Yule ambaye anamuabudu Allah(Sub'hana wataala) akiwa mbele ya kaburi la mtu mwema, je utakuwa na mazito atakapo muabudu mtu mwema moja kwa moja?

- Katika sababu ya kuingia kwenye shirki ni kuchonga masanamu kutengeneza picha na kuyafanya makaburi kuwamisikiti (sehemu za ibada)

(MLANGO WA 21)

Mlango umekuja kubainisha kuwa kuchupa mipaka katika makaburi ya watu huyageuza makaburi hayo kuwa masanamu yanayo ubudiwa kinyume na Mwenyezimungu.

- Miongoni mwa sababu za ukafiri ni kuchupa mipaka katika makaburi ya watu wema.

(MLANGO WA 22)

Mlango huu umekuja kubainisha ulinzi wa mtume muhammada(swalallahu aleyhi wasalam) upande wa Tauhid na kuziba njia zote zinazopelekea katika shirki

- Mtume Mohammad (swalallahu aleyhi wasalam) Amesema: njia zote zinazopelekea katika shirki kwenye itikadi na vitendo, na utakuja mlango unaobainisha kuzuia kwake mtume Muhammad (swalallahu aleyhi wasalam)kauli zote zinazopelekea katika shirki.

SEHEMU YA TANO

KUVUNJA HOJA KWA WANAOSEMA SHIRKI HAITATOKEA KATIKA UMMA HUU AU KWENYE BARA ARABU (MLANGO 1.)

MLANGO WA 23

2. **Huu ni mlango unaozungumzia baadhi ya umma huu wanaabudu masanamu.**

SEHEMU YA SITA

5. MATENDO YA KISHEITWANI (MLANGO 7.)

MLANGO WA 24

Mlango unaozungumzia uchawi.

- Sheikh ameleta mlango huu kwa kuwa uchawi hauwezi kutokea isipokuwa kwa njia ya kumkufuru Allah, na huo uchawi ndio njia kuu zaidi ya kuwalingania watu katika kukufuru. (ukafiri)

MLANGO WA 25

Mlango unaobainisha kitu katika aina za uchawi

- Sheikh ameleta mlango huu kutuelimisha ya kuwa uchawi upo aina nyingi lazima tujiepushe na aina zote.

MLANGO WA 26

Mlango unaobainisha kuhani N.K.

- Sheikh ameleta mlango huu kutubainishia hao makuhani na kutuwekea wazi hukumu ya kuwaendea na namna ya kuwaendea.

MLANGO WA 27

Mlango unaozungumzia nushurati (kisomo).

- Sheikh ameleta mlango huu ili kuondoa mkanganyiko katika kutaja kisomo kilichokatazwa na kile kilichoruhusiwa.

MLANGO WA 28

Mlango unaozungumzia kutabiri mkosi

- Sheikh ameleta mlango huu ili kukanusha yale yaliokuwepo zama za ujinga katika kutazamia mikosi (kuoneana shonga)

MLANGO WA 29

Mlango unaozungumzia, kuangalia nyota ya mtu

- Sheikh ameleta mlango huu ili kubatilisha elimu ya nyota inayodaiwa kuleta athari kwenye maisha yenye kuathiri kwa wenye kujidai

MLANGO WA 29

Mlango unaozungumzia kupata mvua kupitia nyota

- Sheikh ameleta mlango huu ili kubatilisha kufungamana na sababu za kishirikina.

SEHEMU YA SABA

6. MATENDO YA NYOYO (MLANGO 9.)

(MLANGO WA 31)

Mlango huu unaelezea kauli ya Mwenyezimungu: *"Na katika watu wapo wanaochukua waungu wasio kuwa Mwenyezimungu"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili Tawhid (kumpwekesha Allah) kwa atakae penda sana viumbe kama anavyompenda Allah au zaidi.

(MLANGO WA 32)

Mlango kauli ya Mwenyezimungu: *"Hakika huyo ni shetani anawatia khofu marafiki zake"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kukataa Tawhid kwa atakae ogopa sana viumbe kama atakae muogopa Allah au zaidi.

(MLANGO WA 33)

Mlango kauli ya Mwenyezimungu: *"Na mtegemeeni Mwenyezimungu ikiwa nyinyi ni waumini"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kukanushaTawhid kwa atakae mtegemea kinyume na Allah.

(MLANGO WA 34)

3. **Mlango kauli ya Mwenyezimungu:** *"je, Wamejiaminisha na mipango ya Mwenyezimungu?"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kila mwenye Tawhid akusanye katika kwenda kwake kwa Allah kati ya hofu na matumaini.

(MLANGO WA 35)

Mlango huu unaeleza nikatika kumuamini Allah kusubiri katika khadari zake.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kuweka wazi hali ya kila mwenye Tawhid wakati wa mitihani.

(MLANGO WA 36)

Mlango unaozungumzia Riya (kujionyesha)

Sheikh ameleta mlango huu ili kubainisha hatari y aria kwa kila mwenye Tawhid, na hiyo ria ndio dhambi inayo ogopewa mno kuwakumba waja wema.

(MLANGO WA 37)

Mlango ni katika shirki mtu kukusudia kwa amali zake kuipata dunia (shirki ndogo)

- Sheikh ameleta mlango huu ili kuweka wazi kuwa atakae taka dunia kwa kufanya matendo ya akhera ameingia kwenye ushirikina na tafasiri ya haya ni mtu kuridhia na kuchukia kwa ajili ya dunia.

(MLANGO WA 38)

Mlango atakae watii wanachuoni na viongozi katika kuharamisha aliyo halalisha Allah na kuhalalisha aliyoyaharamisha kuwa miungu.*(ni ushirikina katika kutii)*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kuweka wazi kuwa mambo yanayo punguza Tawhid ni kuhukumiana kwa sheria isiyokuwa ya Allah

(MLANGO WA 39)

Mlango kauli ya Mwenyezimungu: ***"Wanataka wakahukumiwe kwa njia ya upotofu"***

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumsadia kila mwenye Tawhid katika kufahamu maana ya, kukufuru twaghuti na tafsiri ya kuamini imani ya kweli na ya uwongo.

SEHEMU YA NANE

7. KUMPWEKESHA ALLAH (TAWHID) MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE

(MLANGO WA 40)

40. Mlango unaozungumzia mwenye kupinga chochote katika majina ya Allah(S.W)

SEHEMU YA TISA

2. MATENDO YA KISHEITWANI (MLANGO 29.)

(MLANGO WA 41)

Mlango unaozungumzia kauli ya Allah(Sub'hana wataala)**.** *"Wanazijua neema za Mwenyezimungu kisha wanazikanusha"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia uwajibu wa mpwekeshaji katika upande wa neema.

(MLANGO WA 42)

Mlango unaozungumzia kauli ya Allah(Sub'hana wataala) *"Basi msimfanyizie Mwenyezimungu washirika na hali nyinyi mnajua"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia hali ya mwenye kumpwekesha katika kuapa kwa jina la Allah(Sub'hana wataala)si kinyume chake nautofauti wa "Na" na "Kisha"

(MLANGO WA 43)

Mlango unaozungumzia Yule asiyetosheka na kiapo cha Allah(Sub'hana wataala)

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia hali ya ukubwa wa Allah(Sub'hana wataala)kwenye moyo wa mwenye kumpwekesha katika kuapia kwake kwa jina la Allah.

(MLANGO WA 44)

Mlango unaozungumzia akitaka Allah(S.W) na wewe.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia na kumtahadharisha kila mwenye kupwekesha kujaalia ushirika katika matakwa.

(MLANGO WA 45)

Mlango unaozungumzia mwenye kutukana zama atakuwa amemuudhi Allah(Sub'hana wataala)

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha mwenye kupwekesha akatukana kitu katika zama akawa kwa sababu ya huko kutukana amemtukana Allah ambaye ndio ameziamrisha zama hio na kuzisalitisha.

(MLANGO WA 46)

Mlango unaozungumzia mtu kujuta hakimu wa mahakimu na mfano wake.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha kila mwenye kupwekesha kunako kuchupa mipaka katika yale yanayo muhusu ulezi (Rububiyah) wa Allah.

(MLANGO WA 47)

41. Mlango unaozungumzia kuheshimu majina ya Allah(Sub'hana wataala) **na kubadilisha jina kwa ajili hiyo**

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia haki ya kila mpwekeshaji kuwa na adabu kwa Allah(Sub'hana wataala)na majina yake, sifa zake, dini yake na mitume wake.

(MLANGO WA 48)

Mlango unaozungumzia mwenye kufanya masikhara kwenye kitu ambacho kina utajo wa Allah, au kwenye qur'an au kwa mtume (swalallahu aleyhi wasalam)

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia kukosekana kabisa Tawhid kwa mwenye kufanya masikhara na namna ya kuamiliana naye na ulazima wa kuhifadhi ulimi.

(MLANGO WA 49)

Mlango unaozungumzia kauli ya Allah(Sub'hana wataala) *"Na pindi tukimwonjesha rehema itokayo kwetu baada ya kumgusa dhara bila ya shaka husema haya nayastahiki mimi"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutambulisha kila wajibu kwa mwenye kumpwekesha Allah kabla ya kupatikana neema au baada ya kupatikana neema.

(MLANGO WA 50)

Mlango unaozungumzia kauli ya Allah(Sub'hana wataala) **)** *"Basi anapowapa mwana mwema wanamfanyia washirikina Mwenyezimungu katika kilekile alicho wapa"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia hali ya mwenye kupwekesha wakati wa kupatikana neema na kuharamisha kila jina linaloonyesha utumwa kwa asiyekuwa Allah(Sub'hana wataala)

(MLANGO WA 51)

Mlango unaozungumzia kauli ya Allah(Sub'hana wataala) *"Na Mwenyezimungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo"*

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha mwenye kupwekesha kuchupa mipaka katika majina ya Allah(Sub'hana wataala)na sifa zake

(MLANGO WA 52)

Mlango unaobainisha. Haisemwi amani iwe juu ya Allah(Sub'hana wataala) **.**

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha mwenye kupwekesha kutamka matamko yanayopingana na adabu kwa Allah(Sub'hana wataala)

(MLANGO WA 53)

Mlango unaozungumzia kauli. Ewe Mola wangu nisamehe ukitaka.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha mwenye kupwekesha kwa sharti la matakwa ya Allah(Sub'hana wataala)katika dua zake na kutaka kujua uwezo wa Allah

(MLANGO WA 54)

Mlango unaobainisha. Mtu asiseme huyu ni mja wangu wangu.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kubainishia mwenye kupwekesha uzuri wa kutumia matamshi mazuri

(MLANGO WA 55)

Mlango unaobainisha. Aombaye kwa jina la Allah(Sub'hana wataala) asikataliwe ombi lake

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia hali ya mwenye kupwekesha akiombwa jina la Allah basi akubali ombi hilo kwa ajili ya kumtukuza Allah

(MLANGO WA 56)

Mlango unaobainisha haiombi kwa dhati katika dhati za Allah isipokuwa pepo.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia hali ya mwenye kupwekesha katika kumtukuza Allah(Sub'hana wataala) na kuwa na adabu juu ya Allah(Sub'hana wataala)

(MLANGO WA 57)

Mlango unaobainisha. Yaliyokuja katika laiti.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia adabu ya mwenye kupwekesha kwa kutumia maneno mazuri na kuipinga sheria ya Allah na qadari zake.

(MLANGO WA 58)

Mlango unaokataza kutukana upepo.

- Sheikh ameleta mlango huu ili uwe mwongozo kwa kila mpwekeshaji kwa kufuata maneno yenye manufaa pindi atakapoona kinachomchukiza.

(MLANGO WA 59)

Mlango unaobainisha kauli ya Allah(Sub'hana wataala) **"Wakamdhania Mwenyezimungu dhana isiyo kuwa ya haki dhana ya kijinga**

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha kili mwewnye kupwekesha kuwa na dhana mbaya kwa Allah kama ilivyo dhana ya jahiliya.

(MLANGO WA 60)

Mlango unaobainisha kwa wenye kupinga Qadari

- Sheikh ameleta mlango huu ili kutubainishia hali ya imani ya mpwekeshaji katika kuamini hukumu (kadha) za Allah na qadari zake.

(MLANGO WA 61)

Mlango unaoelezea yale yaliokuja katika wapiga picha.

- Sheikh ameleta mlango huu ili ambainishie mpwekeshaji juu ya uhatari wa kuchupa mipaka katika upande wa matendo ya uumbaji wake Allah.

(MLANGO WA 62)

Mlango unaobainisha yale yaliokuja katika kukithirisha wingi wa kuapa.

- Sheikh ameleta mlango huu, ili amuusie mwenye Tauhid (mpwekeshaji Mungu) kunako kuhifadhi viapo. Na pia kumtukuza Mwenyezimungu wakati wa kuamiliana na watu.

(MLANGO WA 63)

Mlango unaobainisha yaliokuja katika dhima(haki) ya Allah.

- Amekuja na mlango huu, ili mpwekeshaji atukuze haki ya Allah na haki ya Mtume wake (S.A.W) katika hali ya furaha na katika hali ya madhara (tabu)

(MLANGO WA 64)

Mlango unaobainisha yaliokuja katika kumuapiza Allah.

- Amekuja na mlango huu, ili ampe tahadhari Yule mwenye kumpwekesha Allah kunako kuchupa mipaka juu ya upande wa matendo ya Allah kwa kufunga mlango wa huruma (rehema) ya Allah kwa waja wake.

(MLANGO WA 65)

Mlango unaobainisha kuwa, haitakiwi kumfanya Allah kuwa muombezi juu ya viumbe vyake.

- Sheikh ameleta mlango huu ili kumtahadharisha mwenye kumpwekesha Allah kutokana na kujalia nafasi ya viumbe kuwa juu kuliko muumbaji

(MLANGO WA 66)

Mlango unaobainisha yaliokuja katika himaya ya mtume (S.A.W) kulinda Tauhid na kuzuia njia za shirki.

- Amekuja na mlango huu, ili kumuepusha mwenye kumpwekesha Allah kujitenga na kila kauli inayopelekea kuwa shirki.

SEHEMU YA 10

10. MWISHO (MLANGO MMOJA)

Mlango unaobainisha maana ya kauli ya Allah. (Na hawa kumkadiria Allah kwa haki ya kadari yake…..)

- Ameleta mlango huu, ili ambainishie Yule mpwekeshaji kwamba washirikina ambao hawakumpwekesha Allah, hawa kumkadiria Allah kwa haki ya kadri yake. Tahadhari ewe mwenye kumpwekesha Allah kutokana na njia yao (washirikina)

SEHEMU YA KWANZA

1. UTANGULIZI (MILANGO 5) KITABU CHA TAUHID

KWA NINI HAKUTAJA UTANGULIZI KWA KITABU HIKI?

(1) Utangulizi huo umefutika kwenye baadhi ya nakala, zikapatikana katika baadhi ya nakala, bismillah na Alhamdulillah na kumsalia mtume(S.A.W)

(2) Ametosheka na Tarjama kwa sababu hio tarjama ndio anuani (juu ya maudhi ya kitabu. Ambacho ni kitabu.

(3)kumuiga Imamu Bukhari rehema za Allah ziwe juu yake, pale ambapo hakuweka utangulizi katika kitabu chake na akataka awafungamanishe watu kwa qur'an na sunnah

(4) Milango mitano ya mwanzo katika kitabu. Milango hio ndio inachukua nafasi ya utangulizi

2. MAANA YA TAWHID

Kisheria: Ni kumpwekesha Mwenyezimungu kwa yale yanayomuhusu peke yake katika uungu wake na pia ibada zake na majina na sifa zake

Kilugha: Imetokana na kupwekesha jambo/kitu,pindi atakapo lifanya jambo hilo kuwa moja

(1) TAWHID YA RUBUBIYA. NI KUMPWEKESHA

Mwenyezimungu mtukufu, katika uumbaji na ufalme na kuendesha mambo.

Au kumpwekesha Mwenyezimungu mtukufu kwa anayo yafanya yeye mwenyewe (vitendo vyake)

(2) TAWHID YA IBADA

Ni kumpwekesha Mwenyezimungu mtukufu, kwa ibada zake au kwa matendo ya waja (wake)

(3) TAWHID YA MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE.

Ni kumpwekesha Mwenyezimungu kwa majina aliyo jiita yeye mwenyewe na sifa zake katika kitabu chake, Au kupitia ulimi wa mtume(S.A.W). na hivyo ni kwa kuthibitisha mwenyewe na kukataa alio yakataaa mwenyewe, bila kubadili maana na bila kufananisha sifa za Allah na viumbe.

Matendo hayakubaliwi isipokuwa kwa kumpwekesha Mwenyezimungu. Na tumeumbwa ili kumpwekesha. Na pepo hatoingia isipokuwa Yule mwenye kumpwekesha. Na kumpwekesha Allah ndio wito wa Manabii amani iwe juu yao. Na kuihakiki ndio kinga ya kuingia katika shirki. Nayo ndio sababu ya kukithirisha mema.

IBADA INATUMIKA KATIKA MAANA MBILI (VITU VIWILI)

1: Mfanya ibada, kuabudu maana yake kujidhalilisha kwa kufuata maamrisho ya Allah na kuacha makatazo yake kwa kupenda na kutukuza

2: Ibada ni jina ambalo limekusanya kila anacho kipenda Allah (S.W) na kukiridhia katika kauli na matendo ya dhahiri na yaliyojificha (amesema Ibn Taaymiyyah rehema za Allah ziwe juu yake.

MLANGO WA UWAJIBU WA TAWHID

Hakuweka mlango mtunzi wa kitabu rehema za Mwenyezimungu ziwe juu yake katika mlango huu ili wafungamane watu na kitabu (qur'an) na sunna (hadithi za mtume) pamoja na dalili ambazo amezitaja, zinajulisha uwajibu wa Tauhid. Inawezekana tukaiita mlango wa uwaibu wa Tawhid.

DALILI YA KWANZA

Amesema Allah (Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu mimi) Surat dhaariyaat (56)

(waniabudu) maana ya wampwekeshe au wajidhalilishe kwangu kwa kunitii kwa kufanya maamrisho yangu na kuacha makatazo.
Kila ibada katika qur'an maana yake ni Tauhid nayo ni kauli ya Ibn Abbas. Na maana ya ayat. Sikuwaumba majini na wanadamu isipokuwa kwa ajili ya ibada.

DALILI YA PILI.

Amesema Allah "Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia mtume kwamba. Muabuduni Mwenyezimungu na muepukeni sheitwani ……" Suratul Nahli.

- **Aya hii imetiliwa mkazo na vitilia mikazo vitatu;**1. Kiapo kilicho kadiriwa 2. Laamu 3. Qad
- Katika aya kuna kuafikiana mitume wote rehema na amani ziwe juu yao juu ya da'wa kulingania katika Tauhid. Na hakika Allah(S.W) aliwatuma kwa ajili hiyo.

LINATUMIKA NENO "UMMA" KATIKA QUR'AN KWA MAANA.

taifa	Kama ilivyo katika aya hiyo iliyotangulia
Kiongozi	Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema mnyenyekevu kwa Mwenyezimungu mwongofu wala hakuwa miongoni mwa washirika
Mila (Desturi)	Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wameshika dini makhuasi basi na sisi tunaongoza nyayo zao
Zama (Muda)	Hapo akasema yale aliye okoka katika wale wawili akakumbuka baada ya muda.

(Na muepukeni sheitwani) maana yake: Jiepusheni nae muwe upande mwingine nay eye upande mwingine

- Na hakika jumla ya yaliokusanya katika maana yake ni kile alichosema (taja) Ibn qayyim rehema za Allah ziwe juu yake kuwa. Ni mtu kutenda jambo ambalo linachupa mipaka ya Allah kutoka kwa Yule anaye mfuata au kumuabudu au kumtii lakini na Yule aliyefuatwa au akaabudiwa awe radhi.
  1. Mwenye kufuatwa – mfano kuhani na wachawi na wanazuoni waovu
  2. Mwenye kuabudiwa – mfano masanamu
  3. Mwenye kuabudiwa – mfano viongozi wenye kutoka nje ya twaa (utii) wa Mwenyezimungu
- **Ushahidi wa aya hii kwa Tawhid:** Ni kuwa masanamu ni katika matwaghuti ambao huabudiwa kinyume na Allah(subhanah wataala)
- **Tawhid haitimii isipokuwa kwa kutimia nguzo mbili nazo ni:**1) Kukanusha 2) Kuthibitisha
  Hivyo kukataa basi bila sababu ni kupinga bila sababu na kuthibitisha bila sababu haizuii kupatikana shirki mfano wa hilo (zaidi amesimama) inajulisha kuthibitisha kisimamo cha zaid lakini haijalishi kuwa kasimama peke yake. Na (hakusimama zaidi) inajalisha kukataa kusimama kwa zaidi, ama (hakusimama isipokuwa zaidi) Hiyo inaonesha upweke wake katika kusimama kwa sababu imekusanya kuthibitisha na kukanusha.

HEKMA YA KUTUMWA MITUME

1. Kusimamisha hoja: Mitume hao ni wabashiri na waonyaji ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezimungu baada ya kuletwa mitume.
2. Rehema (Nasi hatukutuma ila uwe reehema kwa walimwengu wote
3. kubainisha njia yenye kumfikisha mtu kwa Mwenyezimungu.

DALILI YA TATU:

Kauli ya Allah (S.W): "*Na Mola wako mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila yeye tu*" na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata Ah! Wala usimkemee na sema nao kwa msemo wa hishima.

Msimwabudu yeyote ila yeye tu: Hii ndio Tauhid iliyokusanya kukataa na kukubali

HUKUMU YA ALLAH IMEGAWANYIKA KATIKA AINA MBILI(2)

1. HUKUMU YA KISHERIA.

- Haipatikani ila katika jambo ambalo analipenda Allah(subhanah wataala)
- Inajuza kutokea kwake na kutotokea. *"Na Mola wako mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila yeye tu"* inakuwa maana ya hukumu hapa ni kuweka sheria au kuusia.

2.HUKUMU YA ULIMWENGU.

- Inapatikana katika jambo analolipenda Allah(subhanah wataala) au asilolipenda

- Lazima itokee *"na tukawahukumia wana wa Israili katika kitabu kwamba, Hakika nyinyi mtafanya fisadi katika nchi"* na ufisadi hajaweka Allah na pia hapendi.

NI VIPI ANAHUKUMU ALLAH(SUBHANAH WATAALA) YALE ASIYOYAPENDA?

Jambo lenye kupendwa kwa ajili ya kitu kingine huenda likawa ni lenye kuchukiwa kwa dhati yake lakini hupendwa jambo hilo kwa ajili ya hekima na maslahi yaliyomo ndani yake hapo ndio huwa jambo hilo liapendeka kwa upande mmoja na kuchukuwa kwa upande mwingine mfano wa hilo ni ufisadi katika ardhi ulio andikwa kwa bani Israil kwa dhidi yake ni chukizo kwa Allah kwa sababu Allah hapendi.

Mfano huo:*Ufisadi katika nchi kwa wana wa Israili katika uhalisia wa jambo lenye kumchukiza Allah(S.W) hapendi ufisadi wafanya fisadi. Lakini hekima ambayo inafungamana yenye kupendwa na Allah(S.W) katika namna nyingine kwa namna hiyo inapatikana ukame, maradhi, ufakiri.*

Ufisadi na mafisadi lakini kwa sababu ya hekima iliyomo ndani yake unakuwa unapendwa mbele ya Allah kwa upande mmoja (wa mitihani) mfano wa hivyo pia ni ukame maradhi na ufakiri

Mwenye kupendwa imegawanyika sehemu mbili (2)

Mwenye kupendwa kwa ajili ya jambo lingine: kama dawa hupendwa kwa sababu inaponyesha

Mwenye kupendwa kwa dhati yake naye ni Allah(S.W)

IMEGAWANYIKA IBADA AINA TATU

IBADA MAALUMU KWA WATU MAALUMU.

Nayo ni ibada ya mitume . (Nayo ni ibada iliyo kamili zaidi)

Amesema Allah(S.W): Ametukuka aliyeteremsha furqani kwa mja wake, kwa sababu hiyo hakuna yeyote atakaye weza kushindana na mtume kwenye ibada hii

IBADA MAALUMU:
Ibada ya Twaa zote, Amesema Allah(S.W) (Na waja wa Arrahman mwingi wa rehema ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha) ***na hii ina kusanya kila chenye kumuabudu Allah kwa sheria zake***

IBADA YA VIUMBE VYOTE: nayo ni ibada za uumbaji. Ibada ya kulazimishwa nayo kila kiumbe

Amesoma Allah(S.W): *"Hakuna aliye mbinguni, miongoni mwa binadamu na majini isipokuwa atamjia Mola wake siku ya kiyama akiwa ni mja mdhalilifu mnyenyekevu mwenye kukubali kuwa mja wake kwake"*na anaingia pia kafiri.

DALILI YA NNE (4)

KAULI YA ALLAH(S.W) *(Muabuduni Mola wenu na msimshirikishe na kitu chochote)*

Kitu chochote: Ni tamko linalokusanya kila kitu si nabii wala malaika wala walii. Hata jambo lolote katika mambo ya dunia. Wala msiijalie dunia inaushirika pamoja na **Allah**

DALILI YA TANO NA YA SITA.

Kauli ya Allah(S.W) (Sema: njooni nikusomeeni aliyo kuharamishieni. Mola wenu mlezi nayo ni kuwa, msimshirikishe yeye na chochote) Amesema IBN Masoud, radhi za Allah ziwe juu yake ambaye anataka kuchukua wasia wa mtume(S.A.W) ambao ameacha muhuri wake. Basi asome kauli ya Allah(S.W) Sema: "Njooni nikusomeeni vile alivyo kuharamishieniMola wenu mlezi"

Hadi kauli ya Allah *"Na kwa hakika hii ndio njia yangu iliyo nyooka, basi ifuateni.*

Njia inaegemezwa kwa:

1.Allah(S.W) kwa sababu ndio inatupeleka kwake na ndiyo ambaye ameiweka kwa waja wake*"Na kwa hakika hii ndio njia yangu"*
2. Kwa waendaji wake: kwababu ndio ambao wanaipita na njia yenye kuokoa ni moja tu haizidi na zilizobakia zote nizenye kufarakana.*" njia ulio waneemesha.*

AYA HIZI ZIMEKUSANYA HII AYA WASIA KUMI(10)

AYA YA PILI NYASIA NNE(4)

6. Tusikurubie mali za mayatima - ni Yule aliyefiwa na baba bado hajabalegha, isipokuwa tutumie kwa wema.
7. Tuwe waadilifu tunaposema.
8. Tutimize kilo na mizani tunapopima.
9. Tutimize ahadi za Allah(S.W)

AYA YA KWANZA. (NYASIA 5)

1. Kumpwekesha Allah
2. Kufanya wema kwa wazazi wawili
3. Tusiuwe watoto wetu
4. Tusikurubie maasai
5. Tusiuwe waliozuiliwa kuuwawa ila kwa haki

AYA YA TATU (WASIA MOJA)

"*Na kwa hakika hii njia yangu katika hadithi hakika mtume(S.A.W) alichora mstari uliyonyooka*" Akasema; *"Hii ndio njia ya Allah(S.W*)" kisha akachora mistari pembeni kulia na kushoto. Akasema hizi ni njia ambazo kila njia kuna shetani anawaita kwenye njia hizi, kisha akasoma aya hii.

BAADHI YA FAIDA MUHIMU

"Sisi tunakurukuzuni nyinyi na wao" imeanza riziki wazazi wawili kwa sababu ufakiri unapatikana kwao katika surat israa *"Sisi tunawaruzuku wao na nyinyi, imeanza riziki kwa watoto kabla riziki ya wazazi kati yao wazazi wamejitosha lakini wanaogopa ufakiri*

Nafsi ambayo ameharamisha Allah(S.W) (Waliozuiliza)kuuwawa

1. Muislamu.
2. Dhimiyu kafiri anayeishi kwa mkataba kwenye dola ya kiislamu
3. Muahada (baina yetu na wao kuna mkataba wa amani)
4. Mustaamini (ambao tunawapa amana za kuishi kati yetu)

Kufikia ujana ambao ndio kuna taklifu ya sheria.

1. Kutimiza miaka kumi na tano
2. Kudhihiri kwa nywele sehemu za siri
3. Au kwa kutokwa na manii na inazidi kwa mwanamke kwa kuingia kwa hedhi

"Isipokuwa kwa haki"

1. Aliyeuwa auwawe
2. Mzinifu aliyeolewa au kuoa
3. Aliyeritadi na kuacha jamaa ya kiislamu

WASIA: Maana yake ni ahadi na haiwezi kuwa ahadi ni wasia isipokuwa iwe katika jambo muhimu.

KWANINI AMESEMA IBN MASOOUD RADHI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE KATIKA HII AYA. WASIA WA MTUME (S.A.W) ILIHALI MTUME(S.A.W) HAKUHUSIA?

1. kwasababu ameona aya zimekusanya dini yote nazo ni aya tukufu zenye maana pana sana

2. kwasababu ni wasia wa Allah (S.W) "Hayo amekuusieni" na mtume (S.A.W) ni mjumbe kutoka kwa Allah(S.A)

DALILI YA SABA(7)

Kutoka kwa muadhi ibn Jabali radhi za Allah ziwe juu yake; Amesema: nilikuwa nyuma ya mtume (S.A.W) juu ya punda. Akaniambia mimi, Ewe Muadhi unajua haki ya Allah kwa waja wake? Na waja wana haki gani juu ya Allah? Nikasema: Allah na mtume wake wanajua. Akasema: haki ya Alla kwa waja wake ni kumuabudu Allah na asishirikishwe na kitu chochote. Na haki za waja kwa Allah: asimwadhibu asiyemshirikisha na kitu chochote. Nikasema: ewe mjumbe wa Allah, hivi nisiwape bishara watu? Akasema: Hapana usiwape bishara watabweteka. Imepokelewa na bukhari muslim.

- "Unajua" swali lenye kutoa shauku: na liwe lenye kukita kwa nguvu kwenye moyo, na hii uzuri wa kuelimisha wa msikilizaji na utaratibu huu ndio ufundishaji ulio bora
- "Haki ya waja juu ya Allah"wapo hawakumuajibishia chochote Allah, bali Allah amewajibisha kwa nafsi yake na fadhila zake
- "Nitoe bishara" Bishara nayo ni habari yenye kufurahisha. Wakati mwingine inatumika habari yenye madhara.
- Usiwape bishara: yaani usiwape habari
- Na katika hadithi hii kuna ubora na fadhila za Tauhid, na hiyo Tawhid inazuia adhabu ya Allah(S.W).
- Ndani yake hakika Allah hamuadhibu ambaye hamshirikishi na chochote maasi yanasamehewa kwa kuhakiki Tauhid. Amekataa mtume (S.A.W) kuwapa habari wasije wakategemea hii bishara pasina ya kuhakiki mukhutadhwa wake, kwasababu kuhakiki Tauhid inalazimu kujiepusha na maasi kwa sababu ya maasi yanatokana na matamanio na hii ni aina ya shirki.

HAPA KUNA MAS -ALA.

Haya masaili hayapo katika kitabu cha Tauhid ameweka mtunzi kama sherhe ya kitabu, na mtunzi ndio bora kwa mwenye kusherehesha kwa sababu anajua lengo. Inatulazimu kutilia umuhimu kwenye masaili hayo

JAMBO LA MOJA: Hekima katika kuumba majini na watu. *(ni kumpwekesha Allah wala sio kustarehe kwa kula na kuoa tu)*

JAMBO LA PILI: hakika Ibada ndio Tauhid kwa sababu ndani yake kuna ugonvi kati ya mtume(S.A.W) na makuraishi. *(Basi kila ibada ambayo haijengeki juu ya Tauhid basi hiyo ni batili)*

JAMBO LA TATU: Hakika asiye iendea Tauhid, huyo hajamuabudu Allah. Na ndani yake kuna maana ya kauli ya Allah *(Wala nyinyi si wenye kuabudu nunaye muabudu)*

JAMBO LA NNE: Hekima katika kutuma mitume *(Ni kumuabudu Allah pekee yake na kujiepusha na kujiepusha na kumuabudu twaghiti (kinyume cha Allah)*

JAMBO LA TANO: Hakika ujumbe huu wa Tawhid umeenea kila ummah (Kundi/Taifa)

JAMBO LA SITA: Hakika dini ya mitume ni moja (Asili ya dini ni moja, na sheria za kiibada na matendo zina tofautiana kutokana na tofauti za umma sehemu pamoja na zama.

JAMBO LA SABA: Mas-ala makubwa, Hakika kumuabudu Allah haipatikani isipokuwa kwa kuwakufuru matwaghuti. Pia ndani yake kuna maana ya kauli ya Allah(S.W) (Basi unaemkataa shetani (Twaghuti.aya) amelifanya jambo hili kuwa kubwa kwa sababu watu wengi hawajui (wajinga) wala haifai kutumika shirki au kukufuru au laana kwa mwenye kufanya chochote katika hayo, kwa sababu hukumu ya hayo katika jambo hili, na lingine linakuwa na sababu na linakuwa na vizuizi.

JAMBO LA NANE: Hakika Twaghuti ni jina lililokusanya kila chenye kuabudiwa kinyume na Allah na kikiwa kimeridhia kuabudiwa.

JAMBO LA TISA: Ukubwa na utukufu wa aya tatu za hukumu katika surat An-aami kwa wema waliotangulia, na ndani yake kuna mambo kumi. Jambo la kwanza ni kataza kunako shirki.

JAMBO LA KUMI: Aya za Muhkamu (ambazo ziko wazi kimaana) katika surat Israili na ndani yake kuna mas-ala kumi na nane ameyaanza Allah kwa kauli yake Allah (Usimfanye Mungu mwingine pamoja na Mwenyezimungu usije ukawa wa kulaumiwa ulie tupika (Mwenye kukosa wa kukunusuru) na akahitimisha kwa kauli yake (Wala usimuwekee pamoja na Mwenyezimungu mungu mwingine, usije ukatupwa katika Jahannam hali ya kuwa mwenye kulaumiwa mwenye kufukuzwa (huku na huku). Na akatuzindua Allah(S.W) juu ya ukubwa wa mas-ala haya kwa kauli yake (hayo ndio katika aliyokufungulia (wahai) katika hikima zake.

JAMBO LA KUMI NA MOJA: Aya ya surat nisai ambayo inaitwa Aya ya haki kumi ameianza Allah kwa kauli yake *(Mumuabudu Mwenyezimungu wala msimshirikishe na chochote)*(*Haki kubwa zaidi ni Haki ya Allah(S.W))*

JAMBO LA KUMI NA MBILI: Tan-bih juu ya wasia wa mtume (S.A.W) wakati wa kufa kwake (Na lakini hakumuusia moja kwa moja isipokuwa aliashiria kuwa tukishikamana na kitabu cha Allah (Qur'an) hatutopotea milele)

JAMBO LA KUMI NA TATU: Kujua Haki ya Allah juu yetu. (kwa kumuabudu yeye na wala tusimshirikishe na chochote)

JAMBO LA KUMI NA NNE: Kujua haki ya waja juu yake Allah. Pindi watakapo tekeleza haki yake Allah (haki ya ihsani)

JAMBO LA KUMI NA TANO: Hakika mambo haya hawayajui wengi katika maswahaba (na hio ni kwasababu Muwadhi ameyaeleza ili kujitoa katika dhambi ya kuficha elimu wakati wa kufa kwake baada ya kufariki maswahaba wengi. Na alikuwa mtume (S.A.W) anahofia wasije wakabweteka. Na wala hakutaka mtume kuficha moja kwa moja kwasababu lau angetaka hivo asingemuelezea jambo hilo Muwadhi wala mwingine yeyote)

JAMBO LA KUMI NA SITA: Kufaa kuficha elimu kwa ajili ya kulinda mas-lahi (hukumu ya jambo hili si muda wote)

JAMBO LA KUMI NA SABA: Inapendeza kumpa biashara njema muislam kwa mambo yenye kumfurahisha (Na hii ni katika faida nzuri zaidi)

JAMBO LA KUMI NA NANE: Khofu ya kubweteka kutokana na ukubwa wa rehema za Allah (na kadhalika kutokukata tama na rehema za Allah)

JAMBO LA KUMI NA TISA: Kauli ya mwenye kuulizwa kwa jambo asilokuwa na elimu nalo. “Mjuzi zaidi ni Mwenyezimungu na mtume wake” (Inasemwa hivo katika uhai (maisha) ya mtume (S.A.W) na katika mambo ya kisheria ambayo ameyafundisha mtume (S.A.W)

JAMBO LA ISHIRINI: Inafaa kuwahusisha baadhi ya watu kwa elimu kuliko wengine.

JAMBO LA ISHIRINI NA MOJA: Kujishusha kwake mtume (S.A.W) kwa kupanda punda mmoja na mtu mwingine nyuma yake.

JAMBO LA ISHIRINI NA MBILI: Kufaa kukaa nyuma ya mtu akiwa juu ya kipando (mnyama) (kwa sharti asimpe tabu/shida mnyama)

JAMBO LA ISHIRINI NA TATU: Ukubwa na utukufu wa mambo haya.

JAMBO LA ISHIRINI NA NNE: Fadhila na ubora wa Muwadhi Ibn Jabali.

(2) MLANGO FADHILA ZA TAWHID NA YENYE KUFUTA MADHAMBI

Ameleta mlango huu ili kuingiza shauku ndani ya nafsi tofauti na mambo anayo yaingiza shetani kwenye nafsi. Wala haitulazimishi kuthibitisha ubora wa kitu kwa muonekano mwingine. Ulazima bali ubora ni matokea yenye athari kama sala ya jamaa

DALILI YA KWANZA:

Kauli ya Allah(S.W) "Wale ambao wameamini na hawakuchanganya imani yao na dhulma – hao ndio watakao pata amani na wao ndio walioongoka"*Al-Anaam (82)*

- Hawakuvaa, hawakuchanganya (na dhulma) dhulma hapa inakabiliana na imani nayo ni shirki.
- Walioongoka (1) hapa duniani. Katika sheria ya Alah kwa elimu na matendo (2) Amma Akhera ni peponi.
- Na katika fadhila za Tauhid kuishi na amani hapa duniani na Akhera.

DALILI YA PILI:

Kutoka kwa ubbada Ibn Swamiti Amesema: Amesema mtume (S.A.W) mwenye kushuhudia hapana Mola apasae kuabudiwa isipokuwa Allah pekee yake hana mshirika, na Muhammad ni mja wa Allah na mjumbe wake na Issa ni mja wa Allah na ni mtume wake, na neno aliompa Mariamu na malaika wake, pepo ni haki. Moto ni haki Allah atamwingiza peponi kwa amali yoyote atakayo kuwa nayo.

Wamtoa Bukhari na muslimu

DALILI YA TATU:

Hadithi ya Itbani(hakika Allah ameharamisha moto kwa mwenye kusema laaila hailallah) hapana Mola apasae kuabudiwa isipokuwa allah, anaetaka kutafuta radhi za Allah.

- **Shahada:** Kutamka kwa ulimi. Kuitakidi moyoni na kutekeleza kwa haki ila kwa viungo.
- **LA ILA HAILALLAH:** Hapana anastahiki kuabudiwa Allah tu.
- **WAHADUHU:** Kutia mkazo kwa kuthibitisha "hana mshirika" LAA SHARIKA LAHU" kutia mkazo wa kukataa kila yanayo pingana.

- **HAKIKA MUHAMMAD:** Ibn Abdillah ibn Mutwalib Kharishy Hamishiy, nabii wa mwisho
- **MJA WAKE:** Maana (1) hana ushirika pamoja na Allah (S.W) (2) Mfanya ibada zaidi.
- **MJUMBE WAKE:** Maana aliyotumwa kwa yale anayopokea na wala si mwenye kuzua uongo kwa Allah. Na inatenguka uhakika wa hii shahada kwa (1) Amefanya maasi (2) kudai katika dini ambayo hayapo katika dini.
- Maasi maana yake kwa ujumla inawezekana tukayazingatia kuwa miongoni mwa shirki na kwa maana ya maalumu maasi yamegawanyika katika sehemu kuu 4 (1) Shirki kubwa (2) Shirki ndogo (3) Maasi makubwa (4) Maasi madogo.
- **ISSA MJA WA ALLAH:**Ni kuwapinga wanaswara. Na Mjumbe wake. kuwapingamayahudi tunaamini ujumbe wake haitulazimishi kumfata ikiwa, sheria yake inatofautiana (kupigana) na sheria yetu na sheria iliyo kabla yetu sisi ina hali zifuatazo;
  1. Ikiwa imepingana na sheria yetu, tutafanyia kazi sheria yetu.
  2. Ikiwa imeafikiana na sheria yetu, sisi tutafata sheria yetu.
  3. Ikiwa yenye kunyamaziwa na sheria yetu, basi itakuwa ni sheria yetu
- Wamegawanyika watu kuhusu utume wa Issa rehema na amani ziwe juu yake aina mbili(2) aina ya kati kwa kati.

  KUNA WALIO MKATAA KABISA?
  1. Nao ni mayahudi mayahudi ulipomkadhibisha na kumponda katika zama zake na wakaupinga unabii wake na wakamuhukumu kuuwawa.
  2. Kuna walio chupa mipaka zaidi:kama manaswara walisema hakika Issa ni mtoto wa Allah,na ni watatu katika utatu na wakamfanya ndio mungu wao
  3. Kuna walio kuwa Kati kwa kati:Wakasema tunashuhudia hakika yeye ni mja wake na mtume wake na mama yake ni mkweli tena ni bikra amehifadhi utupu wake hakika mfano wa Issa kwa Allah ni kama mfano wa adamu. Aliumbwa kwa udongo kisha Allah akasema kuwa na akawa.
- **NENO LAKE:** Kwa sababu aliumbwa kwa neno na sio Issa ni neno la Allah kwakuwa maneno ni sifa ya Mwenyezimungu.
- Na ni roho kutoka kwake:yeye Issa ni kiumbe katika viumbe vya Allah Imeegemezwa kwake Allah kwa ajili ya kutukuza na kumpa heshima.
- Anamwingiza Allah peponi:Kuingia peponi kuna aina mbili (2)
  1. Kuingia kikamilifu bila kutanguliwa na adhabu kwa mwenye kutimiza matendo
  2. Kuigia nusu kutanguliwa na adhabu kwa mwenye kupunguza matendo
- Amesema: hapana Mola aabudiwe isipokuwa Allah: sharti kutakasa nia kwa dalili “anatafuta radhi za Allah (S.W)
- Hii hadithi ni pingamizi kwa makundi mawili
  1. **MURIJIA:** Wale ambao wanatosheka na kusema hapana Mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Pasina kufanya matendo wala kutakasa nia zao
  2. **KHAWARJI:** Wale ambao wanasema hakika mwenye kutenda madhambi makubwa ni kafiri atakaa milele motoni.

VIUMBE AMBAVYO ALAH AMEVIEGEMEZA KWENYE NAFSI YAKE

Kuegemeza sifa zisizo egemezwa kwenye thati ya kiumbe *"kwa vile nilivyoumba kwa mikono yangu"* na hii ni sehemu ya kuegemeza sifa kwa chenye kusifiwa.

Kuegemeza dhata ya kitu chochote kinachosimamia chenyewe na viungo vinavyoungana na dhati ya kitu hicho vyote hivyo ni viumbe (Ngamia wa Allah) na hii ni katika mlango wa kuegemezwa viumbe kwa muumbaji basi kila dhati inayojisimamia yenyewe ambayo haiungani na dhati ya Allah itakuwa ni kiumbe tu.

UEGEMEZI UMEGAWANYIKA SEHEMU KUU MBILI

uegemeziwa ujumla(Hakika ardhi yangu ni pana)

Uegemezi wa kutukuza (ni roho iliyo toka kwake) yaani Issa bin Maryamu

SOMO LA NNE NA LA TANO:

4. Kutoka kwa Abu Saidi Alkhudriyy Radhi za Mwenyezimungu ziwe juu yake, kutoka kwa Mtume Muhammad (S.A.W) amesoma: *"Amesema Mussa (A.S) ewe Mola wangu nifundishe kitu ambacho nitakuwa nakutaja kwa hicho na nakukuomba kwa hicho." sema, Ewe Mussa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake. Akasema kila waja wako wanasema Hivyo. Akasema Ewe Mussa laiti kama mbingu saba na viumbe wake (isipokuwa mimi) na Ardhi saba katika kipimo na Lai llaha illa Allah katika kipimo kingine, ingezidiwa uzito mbingu na ardhi na vyote vilivyomo"*

Hadithi imepokelewa na Ibn Hibbaan na Hakimu.

5. Na kutoka kwa Timidhiyy – kutoka kwa Anas amesoma nilimsikia Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema. *"Amesema Mwenyezimungu mtukufu. Ewe mwanadamu hakika ya wewe ukunijia kwa ukubwa wa ardhi iliyojaa madhambi kisha ukakutana na mimi haukunishirikisha na chochote nitakujia na msamaha ulio sawa sawa na ardhi hiyo"*

"LAA ILAAHA ILLA LLAH" Ibara hii ni dhikri imefungamana na dua kwani kila anaetaja anataka radhi za Allah, nayo ni ufunguo wa pepo lakini atakae kuja na ufunguo ambao hauna meno hawezi kufungua mlango na masharti yake ya Laillaha illa llahu ni meno yake.

Na msamaha ulio sawa sawa na ardhi hiyo: Ubora wa Tawhid ni mkubwa mno inafuta madhambi makubwa pindi anapokutama mja na Allah nae akiwa hajamshirikisha Allah na chochote na msamaha ni kuyastiri madhambi na kuyasamehe kabisa.

MAS-ALA YANAYO AMBATANA NA MLANGO HUU:

Jambo lakwanza:- Upana wa fadhila za Allah

Jambo lapili:- uwingi wa thawabu za Tawhid kwa Allah

Jambo latatu:- Allah kufuta madhambi pale itakapo kuwepo hiyo Tawhid

Jambo lanne:- Tafsiri ya aya katika surat Al-an-am (wale walio amini na hawakuchanganya imani zao na dhulma) (shirki)

Jambo latano:-Yazingatie mambo matano ambayo yako katika hadithi ya Ubbaada

Jambo lasita:- Hakika wewe ukijaalia baina ya hadithi hii ya Ubbaida na hadithi ya Itbaan na ile iliyoko baada yake inabainika kwako, maana ya kauli ya **(Lla ilaha illa llah**) na inabainika kwako makosa ya wale walio ghurulika (kwani hakika hapana budi kwa mja kukusudia kwa kalmia hiyo radhi za Allah na ikiwa Hivyo basi hapana budi afanye matendo yaliyo mema)

Jambo lasaba:- Kuzinduka katika sharti ambayo iko katika hadithi ya Itbaan (Wala haitoshi kwa kauli tu.)

Jambo la nane: Ikiwa Manabii wote wa nahitajika kutanabahishwa fadhila za (Laa ilaha illa allah) (kwa wasio kuwa manabii ni awlaa zaidi.)

Jambo latisa:- kuzindua kuhusu uzito wa Laillaha illa llah kwenye mizani inavizidi viumbe vyote pamoja na kuwa watu wengi hulisema neno hilo mizani zao zitakuwa nyepesi kwa sababu ya kuhesabu moja ya sharti zake au kuwepo kizuizi chenye kuzuia kusihi neno hilo.

Jambo lakumi:- Kuwepo dalili ya kuwa ardhi saba ni kama mbingu (Zinafanana katika idadi)

Jambo la kumi na moja:- kuwepokuwa katika mbingu na wakazi na wakazi wenyewe ni malaika wa Allah

Jambo la kumi na mbili:- Kuthibitisha sifa za Allah kinyume na madhehebu ya ashiariyya (na myatillah, kupitia dalili hizo nyuma zinathibitisha uwepo wa uso kwa Allah)

Jambo la kumi na tatu:- Hakika ukijua hadithi ya Anas, utafahamu kauli ya mtume katika hadithi ya Itbaan "Hakika Allah ameuharamisha moto kwa atakaesema, Laa illaha illa allah akitaka kwa hilo radhi za Allah "Hakika kuiacha shirki sio kutamka kwa ulimi tu"

Jambo la kumi na nne:- Kuzingatia kuwa Issa na Muhammad ni waja wa Allah na ni mitume wa Allah

Jambo la kumi na tano:- Maarifa juu ya kuhusishwa Issa kwa kuumbwa kwake ni kauli (neno) la Allah (Nae ni kiumbe asiyekuwa na baba)

Jambo la kumi na sita:- Maarifa juu ya kuwa Issa ni roho kutoka kwake Allah (ni katika jumla ya roho za viumbe)

Jambo la kumi na saba:- Maarifa juu ya ubora (fadhila) za imani kuhusu kuwepo pepo na moto (nayo ni sababu ya kuingia peponi)

Jambo la kumi na nane:- Maarifa juu ya kauli yake mtume: (Ataingia peponi kwa amali yeyote atakayo kuwa nayo)

Jambo la kumi na tisa:- Maarifa juu ya mizani ina sehemu mbili

Jambo laishirini:- Maarifa juu ya kutajwa uso (nayo ni sifa miongoni mwa sifa za Allah)

MLANGO UNAOBAINISHA MWENYE KUIHAKIKI TAUHID ANAINGIA PEPONI BILA YA HESABU,

Ameleta mlango huu ili tuihakikishe Tauhid ambayo imewajibishwa juu yetu na tukawa na shauku nayo. Na kuihakikisha hio Tauhid ni kuitakasa kutokana na shirki na uzushi na maasi na jambo hilo hufanywa kwa elimu na itikadi na kwa unyenyekevu.

Na kuihakiki Tauhid kwa mtunzi Allah amrehemu, inakuwa kwa kusoma mlango kwa upambanuzi, na kwa ujumla inakuwa kwa:-

1] Kumuiga (kumfuata) Mtume wa Allah Ibrahimu juu yake iwe amani.
2] Kuwaiga (Kuwafuata) Vipenzi watukufu yaani Maswahaba
3] Kubaki katika Tauhid hata kama utakuwa mmoja (peke yako)
4] Kumtegemea Alla na kuacha tiba za ruqya kujitibu kwa moto na kutazamia kupitia ndege.

DALILI YA KWANZA

Kauli ya Mwenyezimungu mtukufu: (Hakika Ibrahimu alikuwa Imamu mfano mwema, mnyenyekevu kwa ALLAH, mwongofu wala hakuwa mwa washirikina)

Kwenye aya hii ALLAH anamsifu Ibrahimu Amani iwe juu yake, Ikawajibishwa juu yetu kumpenda na kumuiga (kumfuata), tunapaswa pia kumsifu kwa kadri ya tutakavyo muiga (mfuata). Na hii ni kwa sababu ameihakiki Tauhid kwa mambo sita yaliyo tajwa katika aya….

1. Imamu: Kiongozi mwema wa kuigwa, katika matendo yake na kazi zake na jitihada yake pamoja na kumtegemea Mwenyezimungu.
2. Mnyenyekevu: Mtiifu daima mwenye kuendelea na utiifu kwa kila hali, hivyo basi yeye ni mtiifu, mwenye msimamo mwenye kudumu na hali hiyo.
3. Kwa ajili ya Mwenyezimungu: Jambo hilo linajulisha utakasifu (kumkusudia Mwenyezimungu katika ibada)
4. Muongofu: Mwenye kumuelekea Mwenyezimungu, mwenye kuachana na shirki na mwenye kujiepusha na kila linalopinga utiifu kwa Mwenyezimungu.
5. Hakuwa miongoni mwa washirikina: Kujiondoa (kujitenga) katika ushirikina na watu wake (kwa moyo na ulimi na viungo)
6. Mwenye kushukuru neema zake: Kwa sababu neema ni mtihani inahitajika kushukuru.

FAIDA:

1. Baba yake na Ibrahimu Amani iwe juu yake anaitwa Azari alikufa katika ukafiri (ilipombainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezimungu alijiepusha nae)
2. Wazazi wake na nabii Nuhu amani iwe juu yake, wote walikuwa ni waumini (Mola wangu nisamehe na wazazi wangu)
3. Amesema imamu Ahmad: Mambo matatu hayana asili (Isnad). Vita vidogo, vita vitaumbwa na tafsiri zake, mara nyingi hutajwa mambo hayo bila Isnad, hakuna mtu anayejua chochote kuhusu umma zilizopita isipokuwa kwa njia ya wahyi ambayo ni maneno ya Allah na sunna za mtume wake.

DALILI YA PILI

Amesema Allah mtukufu **(Na wale ambao mola wao mlezi hawamshirikishi)**

- (Hawamshirikishi) shirki kwa maana yake kwa upana, kuihakiki Tauhid haiwi isipokuwa kwa kujitenga na shirki kwa maana yake kwa upana, na lakini maana hii sio kwamba hayata tokea maasi kwao, kwasababu kila mwanadamu ni mkosefu, na wala yeye hajakingwa (maasumi) na maasi, lakini wanapofanya maasi basi wao wanatubia na wala hawaendelei na kufanya maasi.

DALILI YA TATU.

Kutoka kwa Huswayn Ibn Abdulrahman: amesema kuwa, Nilikuwa kwa Said Ibn Jubayri akasema: Nani katika nyinyi aliona nyota ambayo iliodondoka usiku wa jana? Nikasema: Mimi, kisha nikasema: Ama mimi sikuwa katika swala, lakini niligongwa (na mdudu mwenye sumu). Akasema ukafanya nini baada ya kugongwa? Nikasema: mlifanya tiba (kinga) ya kisomo Akasema jambo gani lilipelekea kufanya hivyo? Nikasema: ni hadithi alitusimulia Shaabiyu. Akasema: aliwasimulia nini? Nikasema: alitusimulia kutoka kwa Burayda Ibn Huswaybi, kwa hakika yeye alisema (Hakuna ruq-ya (kutaka kinga/tiba) isipokuwa kutokana na kijicho au kuumwa na mdudu mwenye sumu) Akasema: Hakika atakuwa amefanya (vizuri zaidi ambaye amekemea mwenye jambo alilosema, lakini alituhadithia Ibn Abbas (Radhi ya Allah ziwaendee) kutoka kwa mtume (s.a.w) hakika yeye alisema (Imedhihirishwa kwangu nyumati nikaona Nabii akiwa na kundi la watu, Na nabii mwingine akiwa na mtu mmoja na mwingine wawili. Punde (gafla) pakanyanyuliwa kwangu kundi kubwa la watu nikadhani kuwa hao ni umma wangu. Nikaambiwa huyu ni nabii Musa na watu wake, Nikatazama tena ghafla kundi kubwa zaidi nikaambiwa huu ni umma wako, wakiwa pamoja na watu elfu sabini wanaingia peponi bila ya hesabu wala adhabu) kisha akasimama na kuingia ndani kwake, wakawa watu wanazungumza kuhusu hao watu. Wakasema baadhi yao: Huenda hao ni maswahaba wa mtume (s.a.w) na wakasema baadhi yao: Huenda hao ni wale waliozaliwa katika uislamu wala hawakumshirika Allah kwa chochote wakataja vitu vingi. Kisha akawatokea mtume (s.a.w) wakamuelezea akasema (Watu hao ni wale ambao hawatafuti kinga (tiba) na wala hawategemei kinyume na Allah na wala hawafungamanishi mambo yao na mikosi na ni wenye kumtegemea mola wao) akasimama Ukasha Ibn Mihswin akasema “ ewe mjumbe wa Allah niombee kwa Allah anijaalie kuwa miongoni mwao” akasema mjumbe wa Allah (wewe ni miongoni mwao) kisha akasimama mtu mwingine akasema, muombe Allah anijaalie niwe miongoni mwao, akasema mtume (Amekwisha kutangulia Ukasha)

- (Iliyodondoka): Iliyo anguka (Nilijikinga): Nilitafuta kujikinga (kijicho): jicho la mwenye kuhusudu.

* Kwa ushahidi gani umekupelekea kufanya hivyo? Kwenye swali hili kuna kujuzu kuomba dalili lakini kwa njia ya adabu.
* Hakuna ruhusa ya kusoma ruqya ila kwa kupantwa na kijicho au kung'atwa na mdudu mwenye sumu. Maana ya ibara hii hakuna tiba wala dawa yenye kunufaisha zaidi kwenye tiba ya husuda au kung'atwa na wadudu wenye sumu kuliko kisomo cha ruqya, pamoja na kuwa imethibiti tiba ya ruqya kwenye magonjwa mengine.
* Huma ni kila mng'ato mwa kila mdudu mwenye sumu, lakinihumma ni ugonjwa unaosababisha kupanda kwa joto lamwili.
* Ar-rabtu – Ni kikundi cha watu wanaoanzia watatu mpaka tisa.
* Hawafanyi rqya, maana yake hawaombi kwa yeyote asomee kisomo kwa sababu zifuatazo:
  1. Nguvu kubwa ya kumtegmea Allah [2.] Nguvu za nafsi zao kutotaka kujidhalilisha kwa asiyekuwa Allah. [3] N tija inayo patikana kwa kufanya hivyo nako ni kle kujiambatisha kwa asiye Allah.
* **VIGAWANYO VYA WATU KATIKA KUTAKA VISOMO VYA RUQYA.**

1- Mtu kumtafuta atakayesomea ruqya: Huyu atakuwa amepitwa na ule ukamilifu (anatoka kwenye ibada ya watu 70,000 watakaoingia peponi bila hesabu)

2- Asije mzuia Yule atakayetaka kumsomea: Huyu hawezi kutoka kwenye ule ukamilifu kwa sababu hakumtafuta wala kumuomba msomaji.

3- Mtu kumzuia anayemsomea, kufanya hivi ni kwenda kinyume na sunna, kwa sababu mtume hakumzuia Aisha pale alipokuwa anamsomea.

* - Wale ambao hawatafuti tiba ya kuuguza kwa moto katoka kwa watu wengine.
* - Wale ambao hawafanyi shonga, kufanya shonga (nuksi) ni kutazamia niksi kwenye kitu kinachoonekana, au kusikiwa au kujulikana sehemu kilipo au nyakati, na hukumu ya kufanya hivi ni shirki ndogo.

  Ruqya yoyote isiyohusiana na aina tatu zilizotajwa hapo juu haimzuii mtu kuingia peponi bila kutanguliwa na hesabu au adhabu kwa sababu ya daily zilizokuja zikiamrisha kufanya tiba na zikisifia baadhi ya dawa kama asali na Hubbat sauda.

AINA ZA UMMA

1- UMMATUL-DA'WAH

Umma huu unawakusanya wote waliomkubali Allah na mtume wake na wale ambao bado hawajamkubali (ambao ni makafiri)

2- UMMATUL-IJABAH.

Umma huu ni wale ambao wamemkubali Allah na mtume wake (Nao ni waislamu)

MASAILI YANAYOHUSIANA NA SOMO LILILOTANGULIA.

1- Utambuzi wa kujua daraja za watu katika Tawhid.
2- Nini maana ya kuihakiki Tawhid? Maana yake ni kutakasa Tawhid hiyo wa shirki bidaa (uzushi) na maasi yote.
3- Sifa za Allah kwa Nabii Ibrahim kuwa hakuwa katika washirikina
4- Sifa za Allah kwa vipenzi vyake vitukufu kwa kusalimika na shirki
5- Kuacha kufanya ruqya na tiba ya kutumia moto ni kuthibitisha Tawhid
6- Kukusaya mambo yote hayo (ya kuacha hizo tiba) huo ndio ukamilfu katika kumtegemea Allah
7- Ukubwa wa elimu ya maswahaba walipofahamu kuwa hawataweza kupata daraja hilo (kuingia peponi bila hesabu) isipokuwa kwa kutenda matendo mema yaliyotakasika.
8- Kupupia kwa maswahaba kwenye mambo ya kheri.
9- Ubora wa umma huu umethibiti kwenye wingi wao na matendo yao
10- Ubora wa wafuasi wa Nabii Mussa
11- Kudhihirishwa nyimati kwa mtume kuna sababu [1] kumliwaza [2] kuonyesha ubora wa mtume na utukufu wake
12- Kila umma utafufuliwa peke yake ukiwa na mtume wao
13- Ni watu wachache sana waliowafuata mitume.
14- Mtume yeyote ambaye hakuaminiwa hatuna mtu mmoja atafufuliwa peke yake.
15- Faida ya elimu hii (ya Tawhid) ni kutodanganyika na wigi wa watu (ambao hawakuamini) Tutaangamia pamoja nao na kutojitenga na wale wachache (kwa sababu ya imani zao) huwenda wachache wakaja kuwa bora kuliko wale wengi.
16- Kuruhusiwa kisomo cha ruqya ya kisheria kutokana na tiba ya kijicho au sumu ya mdudu na magonjwa mengineyo
17- Kuzama kielimu kwa salafi salahe (said bin Jubair pale aliposema: Amefanya vyema Yule atakaekomea kwenye kile tu alichosikia, lakini kuna hili na hili …… imefahamika kutokana na maelezo hayo kuwa ila hadithi ya pili (ya Ibn Abbas)
18- Kujitenga mbali kwa salafi kunako kumsifia mtu kwa sifa asizokuwa nazo
19- Mtume kumwambia ukasha: Wema utakuwa (miongoni mwao) hiyo ni alama katika alama za utume.
20- Ubora wa swahaba Ukasha (kwa kuwa miongoni mwa watakaoingia peponi bila bila ya kutanguliwa na hesabu wala adhabu.
21- Kutumika kwa msamiati wa mafumbo ima itakuwa aliyekuwa akiomba kuingia eponi ni mnafiki au mtume aliogopea kufungua mlango wa maombi (baada ya Ukosha) wakaomba daraja hilo hata wale wasio stahiki kulipata.
22- Tabia njema ya mtume.

KWANINI MTUNZI AMELETA MLANGO HUU BAADA YA KUHAKIKI TAUHID?

Kwasababu mwanadamu anaona kuwa tayari amehakiki Tauhid na hali ya kuwa hajahakiki asidanganye nafsi yake

Kwasababu kila mlango baada ya kuhakiki Tawhid utakuwa ni miongoni mwa, na miongoni mwa kuhakiki Tawid ni kuiogopa shirki na kuilingania Tawhid yenyewe.

DALILI YA KWANZA NA YA PILI.

1] Kauli ya Allah (s.w) "hakika Allah asamehidhambi ya kushirikishwa na husamehe dhambi iliyo duni ya hiyo kwa amtakaye".

2] Kauli ya Allah (s.w) "Na aniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu. *(surat: Ibrahim(35)*

VIPI TUTAIOGOPA SHIRKI?

Kujiepusha na shirki na washirikina na kuwa mbali nao ili asiwe miongoni mwao

Dua na kutaka msaada kwa Allah (s.w)

Kisoma shirki na kuijua sababu zake na vinavopelekea kwenye shirki na huko ndio kujiepusha na shirki

Kusoma Tauhid na kuifanyia kazi na kulingania na kuwa na subira.

- Shirki Allah haisamehi milele, akifa mtu na shirki kwa sababu hiyo shirki ni kosa la jinai(kosa) katika haki ya Allah(s.w) nayo ni Tauhid atakae kufa na shirki kubwa atakuwa na makazi ya milele motoni Na atakae kufa juu ya shirki ndogo huyo ataadhibiwa kwa kiwango cha shirki yake kisha ataingia peponi wala hatokaa motoni milele kwa kuwa yeye ni katika waislamu
- Na uniepushe) Nijaalie pembeni na ujalie ibada za masanamu katika upande mwingine mpaka nijiweke mbali nayo.
- Niweke upande wa mbali na uwaweke waabudu masanamu upande mwingine wa mbali ili ibada hiyo iwe mbali name.

- Masanamu) sanamu ni kila kilichotengenezwa kwa sura ya mwanaadamu na kinaabudiwa kinyume na Allah(s.w) Ama mzimu ni kile kinachoabudiwa kinyume na Allah kwa namna yeyote ile. Kwa hiyo mizimu maana pana zaidi kuliko masanamu.
- Ibrahim (a.s.w) anaogopa katika nasfi yake ni Khalili Rahmani ua Immam wa hunafaa wewe unazani nini kuhusu sisi? Usijiaminishe na shirki na wala usijiaminishe na unafiki hajiamrishi na unafiki ila atakuwa ni mnafiki

DALILI YA TATU HADI YA TANO.

3] KATIKA HADITHI: "Jambo mnaloliogopea zaidi kwenu ni shirki ndogo".Wakamuulizakuhusu shirki ndogo? Akasema: "Kijionyesha"

4] Kutoka kwa Ibn Masuud Allah amuwie radhi. Hakika mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake Amesema: "Atakae kufa na akawa anamjaalia Allah mshirika, ataingia moyoni" Amepokea Bukhari.

5] Na muslim kutoka kwa Jaabiri Allah amuwie radhi. Hakika mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake Amesema: "Atakae kutana na Allah (s.w) hali ya kuwa hamshirikishi na kitu chochote ataingia peponi na atakae kutana na Allah hali yakuwa anamshirikisha na kitu chochote ataingia motoni"

- Kujionyesha (Ria) ni mtu kumuabudu Allah ili watu wamuone au wamsikie na kumsifu kwa vile unafanya ibada na si kwamba anafanya ibada kwa ajili ya watu hiyo itakuwa shirki kubwa. Ama Yule atakae fanya ibada kwa lengo la watu wamuige jambo hilo si katika ria bali huku ni katika kulingania kwa Allah na tiba y aria inakuwa kwa kufanya yafuatayo:-
  1] Kusoma Tawhid kwa sababu atakapoisoma Tawhid atamtukuza Allah tu wala hatomjali yeyote katika kuitekeleza dini ya Allah.
  2] DUA.
  3] PUPA katika kufanya mtu matendo mema kwa siri kati ya mja na mola wake
  4] Kutokuacha kufanya matendo kwa hoja ya kuingia kwenye (Ria)
  5] Kufanya matendo mengi mema ambayo yanatukumbusha Akhera kama vile kufanya ziara makaburini kwa masharti yake.

KWANINI ALIONGOPA MTUME (S.A.W) JUU YA UMMA WAKE KUTOKANA NA RIA SANA KULIKO KUONGOPA JUU YA MASIHI DAJALI.

Kwasababu ya fitini ya mashihi Dajali ni mda maalum (mwishoni muna zama) Ama Ria inapatikana kila muda

Kwa sababu fitni ya mashihi Dajali ipo wazi.

Ama fitini ya Ria imejificha.



- (NIDDA) maana yake ni mwenza au mshirika.
- Kuingia motoni: hii ni adhabu atakae mjalia Allah washirika.
- Kitu: Inakusanya kila shirki hata kama akimshirikisha Allah pamoja na kiumbe kitukufu zaidi ataingia tu motoni.
- Atakae kutana na Mwenyezimungu hali ya kuwa amemshirikisha na kitu chochote ataingia motoni. Ikiwa amemshirikisha shirki ndogo hakika haimlazimu yeye kukaa milele motoni, na ikiwa amemshirikisha shirki kubwa hakika itamlazimu akae motoni milele
- Shirki ni jambo gumu sana, si jepesi lakini anaweka wepesi Mwenyezimungu kumtakasa kila mja wake na kwa hali hiyo amjalie Allah mbele ya macho yake akusudie kufanya matendo kupata radhi za Allah si kupata sifa za watu au bughudha zao kusifiwa na watu kwenye ibada hizo. Hakika ya watu hawakupi faida milele (hawatakunufaisha milele)
- Na hivyo hivyo pia ni muhimu kabisa kwa mtu yeyote asifurahishwe na kuona watu wameikubali kauli yake kwa sababu inatoka kwake, bali imfurahishe kuona watu wameikubali kauli yake kwa kuwa ipo kwenye haki na kinyume chake pia. Ikhlasi ni jambo gumu sana. Ispokuwa mwanadamu atakapokuwa amemwelekea Mwenyezimungu mwelekea wa kweli ulio salama katika njia iliyonyooka hakika ya Allah anamsaidia na anamfanyia wepesi.

DUA IMEGAWANYIKA AINA MBILI

DUA YA MAOMBI

- Ama ambayo anaweza kiumbe (viumbe) kwa namna hii ni sahihi lakini kwa mambo manne, awe anaeombwa , awe hai, au yupo au anauwezo na iwe ni kwa sababu
- Ama ambayo hawezi kiumbe isipokuwa Allah, kwa namna hii kinyume na Allah atakuwa amefanya ushirikina mkubwa kama mtu kutafuta motto au kuomba mvua kinyume na Allah

DUA YA IBADA: Kama kusali au kuhitaji au kufunga kinyume na Allah huu ni ukafiri Ukafiri mkubwa

TOFAUTI KAZI YA SHIRKI KUBWA NA NDOGO

SHIRKI NDOGO

- Haimtoi mtu katika mila ya kiislamu
- Inamporomoshea tendo maalumu
- Hatokaa motoni milele na milele
- Si halali kumwaga damu yake au mali yake
- Inakuja dalili kwamba ni jambo dogo
- Na aitakidi hakika ambaye hatomjalia Allah sababu basi ni sababu
- Kila ambalo linapelekea shirki kubwa basi ni shirki ndogo
- Kila kilichoelezwa na sheria moja kwa moja ni shirki au kufuru wala haikufahamika basi asili ni ndogo

SHIRKI KUBWA

- Inamtoa mtu katika ila ya uislamu
- Inaporomosha matendo yako yote
- Mtu huyu atakaa milele na milele motoni
- Ni halali kumwaga damu yake na kula mali yake kwa kiongozi (raisi)
- Inakuja dalili kwamba ni ni jambo kubwa
- Na aitakidi kufanya kinyume na Allah jambo lolote lililofichikana katika ulimwengu na katika mkono wake kuna manufaa na kutoa madhara

MAMBO YANAYO AMBATANA NA MLANGO HUU WA AINA ZA SHIRKI:

MAS-ALA.

1. Kuogopa shirki
2. Hakika ya kujionyesha (Riya) ni shirki
3. Ni katika shirki ndogo (Riya ndogo)
4. Ria inawaogopesha watu wema, kwa sababu inaweza kuingia katika moyo wa mwanadamu bila ya kuhisi chochote na kudhihiri katika nafsi yake, hakika ya nafsi nyingi zinapenda kusifiwa kwa kufanya ibada.
5. Kukaribia peponi na motoni.
6. Kukusanya kati ya ukaribu wa pepo na moto kwenye hadithi moja.
7. Ambaye atakae kutana na Allah hali ya kuwa anamshirikisha na kitu chochote ataingia motoni hata kama anayefanya ibada kushinda watu wengine (ikiwa ni kubwa hatoingia peponi ikiwa ni ndogo ataadhibiwa kutokana na dhambi yake kisha ataingia peponi
8. Dua kubwa (tukufu) aliyoomba Ibrahim yeye na watoto wake ni kuwekewa kizuwizi cha kuabudu masanamu.
9. Kuzingatia Ibrahim hali ya watu wengi kwenye dua yake, kwa kauli yake: Ewe mola wangu masanamu wamesababisha kuwaepusha watu wengi na njia ya ukweli.
10. Kuwepo tafsiri ya (hapana Mola aabudiwe isipokuwa Allah, kama alivo taja Bukhari,
11. Fadhila ambaye atakaesalimika na shirki ataingia peponi

[5] MLANGO WA KULINGANIA KATIKA JAMBO LA KUSHUHUDIA YA KWAMBA HAPANA MOLA APASAE KUABUDIWA KWA HAKI ILLA ALLAH

KWANINI AMELETA MTUNZI MLANGO HUU?

1. Pindi alipotaja Tawhid mwanadamu kwa nafsi yake ametaja da-awa ya mwingine kwa sababu haitimii imani isipokuwa amelinginia kwenye Tauhid si budi pamoja na Tauhid katika kulingania kwayo isipokuwa itakuwa pungufu.
2. Kurejesha kwa mwenye kusema hakika jambo la kwanza kuanza nalo ni sala si Tauhid

DALILI YA KWANZA:

Kauli ya Allah (s.w) " sema: Hii njia yangu ninalingania kwa Mwenyezimungu kwa kujua mimi na wanao nifuata.

- (Njia yangu): Njia inakusanya aliyokuja nayo Nabii (rehema na amani ziwe juu yake kutoka kwa Allah katika ibada na kulingania kwa ajili ya Allah.
- Kwa Mwenyezimungu": Da-awatu ina aina mbili;- [1] Mlinganiaji wa Allah [2] Mlinganiaji kwa wengine.
- Kwa kujua";Inakusanya [1] Elimu ya kisheria, [2] Elimu ya hali ya walinganiwa [3] Hekima
- Masharti ya kulingania kwa ajili ya Allah: [1] Ikhilasi [2] Elimu ya kisheria [3] Hekima [4] Kujua hali ya walinganiwa [5] Subra.

DALILI YA PILI

Kutoka kwa Ibn Abasi Allah awaridhie: Hakika mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake pindi alipomtuma Muadhi kwenda Yaman alimwambia "hakika unaenda kwa watu wa kitabu (mayahudi/manaswara) liwe jambo lako la mwanzo uwalinganie shahada (أن لا إله إلا الله)(hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokwa Allah (s.w) Na katika mapokezi mengine: Wampwekeshe Allah (s.w) wakiitikia hili na kutii, wafundishe/wafahamishe kuwa allah (s.w) amewafaradhishia sala tano kila siku usiku na mchana, wakitii. Wafahamishe kuwa Allah (s.w) amewafaradhishia kutoa sadaka zinachukuliwa kwa matajiri na zinapelekwa kwa mafukara. Wakitii hili. Ole wako na kula malizao na uongope duwa aliyedhulimiwa hakika duwa ya aliyedhulumia hakuna pazia kati yake na Allah (s.w) *Amepokea Bukhar na Muslim.*

• MAFUNZO YANAYOPATIKANA KWENYE HADITHI HII YA MUADHI:

1. Ni katika sheria kutuma walinganiaji kwa ajili ya Allah na kuwaelimisha
2. Mtume kumpeleka mtu mmoja kulingana na tunayojufunza ndani yake kukubaliwa kwa taarifa ya mtu mmoja hata ikiwa katika mas-ala ya itikadi
3. Mtume hakushartisha masiku maalum ya kulingana, bali mlinganaji atakaa kwa anaewalingania kwa mujibu wa mahitaji yao.
4. Jinsi ya kuwalingania wote wanaoenda kinyume na njia iliyo nyepesi zaidi ni kuwalingania kwanza kwenye Tawhid si kuweka nao mjadala.
5. Haitoshi kulingania kwenye uislamu tu bali aawaeleza yote yaliyo wajibu kwao mpaka watosheke na kuyafanyia kazi, lakini atafundisha kwa kufuata utaratibu uliomo kwenye hadithi ya muadhi bin Jabali.

DALILI YA TATU.

Kutoka kwa Sahli Ibn Saadi Allah amuwie radhi, Hakika mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake alisema siku ya khaybara: “nitampa pendera kesho mtu ambaye anampenda Allah na mtume wake na anapendwa na Allah na mtume wake, atafungua Allah kwa mikono yake” wakalala watu wakiwa wanafikiria usiku huo wakiwaza ni nani atakae pewa. Walipoamka kesho yake aliyoisema mjumbe wa Allah wote wakawa wanategemea apewe akasema: “yuko wapi Ally Ibn Abitwalibu?” wakasema: anashitakia macho yake. Akatuma watu waende wakaja nae, akamtea macho yake na kumuombea dua, akaona kama vile hakuwa na tatizo, akampa pendera. Akasema: “nenda na ujumbe huu hadi kwenye uwanja wao, Kisha walinganie kwenye uislam. Wafahamisheni yale yalio lazima kwao katika dini ya Mwenyezimungu. Naapa kwa Allah akiimuongoza Allah mtu kwa kupitia mtu na akamuongoza mtu mmoja ni bora kwako kuliko ngamia mwekundu”.

- Ndani ya hadithi hii kunakuthibitisha sifa ya kupenda (mahaba) kwa Allah na kwa Allah hupenda na kupendwa lakini mapenzi yake si kama mapenzi tuliyoyazoea..
- Kuthibiti ubora kwa mtu mmoja hailazimu kuthibiti ubora wake kwa watu wote, kama mtume alivyomwambia Abu Ubaidah yeye ni amiu wa umma huu, kauli hii haimaanishi kuwa yeye ndio mbora zaidi kuliko mswahaba wote, na hivyo hivyo hata kwa Muadhi bin Jabali..
- Humuri nighani” ningamia mwekundu amemtaja anapendwa sana na waarabu

MAMBO YENYE KUVUNJA DESTURI YAPO AINA NNE:
Ni mambo yote yaliyokuja kinyume na utaratibu ambao wameuzoea watu

2. KARAMA: inakuwa kwa mawalii wa rahman nao ni wale ambao wamekusanya imani na taquwa mfano wa Karama ni yaliotokea kwa watu wa pangoni

1. AYA: inakuwa kwa manabii na haisemwi ni miujiza kwa sababu hii imethibiti kwenye qur'an na muujiza baadhi ya watu hushindwa na inakuwa si kwa manabii na haiwezekani kwa yeyote adai aya baada ya kufa kwa mtume (s.a.w)

4. FEDHEHA: Kila aliye muongopea Allah alimfedhehesha hapa duniani kabla ya Akhera na mfano wa fedheha ni ile iliomtokea musayilama Alkadhabi alipompuliza mgonjwa machoni akawa kipofu.

3. MUUJIZA AU FITINA: inakuwa kwa mawalii wa kishetani tunaujua kihali ya mtu mwenyewe, si kwa kuangalia imani na taqwa

Ni mambo yote yatakayotokea kwa masihi Dajjal.

MAASAILI:
MOJA: Hakika kulingania dini ya Allah ndio njia ya kila mtu aliyemfuata mtume wa Allah (Njia ya mtume na wafuasi wao)
PILI: Tanbihi juu ya ikhlasi kwa sababu watu wengi hata kama wanalingania kwenye haki basi atalingania kwenye maslahi ya nafsi yake.
TATU: Hakika elimu ni katika faradhi na kufanya"Da'awa ni faradhi. Kwa ajili hiyo elimu inakuwa ni faradhi zaidi miongoni mwa dalili za ubora wa Tawhid ni kumtakasa Allah na kila upungufu
NNE: Miongoni mwa dalili za ubora waTawhid ni kumtakasa Allah na kila upungufu.
TANO; Katika ubaya wa shirki ni kumfanya Allah kuwa mpungufu, na hali ya kuwa kila mwenye Tawhid humtakasa Allah na kila upungufu.
SITA: Na umuhimu zaidi wa Da'awa ya Tawhid ni kumpwekesha muislamu kuwa karibu na wasirikina ili asije akawa miongoni mwao hata kama hakufanya shirki.
SABA: Kujifunza Tawhid ndio wajibu wa kwanza
NANE: Tawhid ndio huanzwa kufundishwa kabla ya ibada yeyote hata swala
TISA: Maana ya ("kumpwekesha Allah) ndio maana: ya Shahada alla lah ila Lala (hapana mola apasae kuabudiwa isipokuwa Allah.

KUMI: Hakika mwanadamu anaweza akawa miongoni mwa watu wa vilabu na ikawa havijui vitabu hivyo au anavijua lakini havifanyii kazi.

KUMI NA MOJA: Tanbii juu ya kutoa mafunzo kidogo kidogo.

KUMI NA MBILI: Kuanza na muhimu jambo Zaidi kisha linalofuatia katika umuhimu

KUMI NA TATU:kuanza kufundisha Tawhid kwanza kisha sala, kisha zaka

KUMI NA NNE: mjuzi (mwalimu) mfunulie mwanafunzi kila jambo lenye utata kwa kumfundisha vyema na kumuondolea ujinga.

KUMI NA TANO: Makatazo juu ya kuchukua mali.

KUMI NA SITA: Kuogopa dua ya mdhulumiwa.

KUMI NA SABA: Dua ya mwenye kudhulumiwa haina kizuizi

KUMI NA NANE: Katika dalili za Tawhid ni yale yaliyojiri kwa mtume na maswahaba kupata matatizo, njaa na maradhi "imechukuliwa katika kisa cha Khaybara

KUMI NA TISA: Kauli yake (Nitampa bendera) hiyo ni alama katika alama za utume

ISHIRINI:kutemea kwenye jicho la Ali ibn Abitwalibu ni alama ya utume pia

ISHIRINI NA MOJA: Fadhila za Ally radhi za Allah zimwendee na kupewa bendera kwa Ali ni katika matkufu yake

ISHIRINI NA MBILI: Fadhila za maswahaba katika pupa ya usiku ule na kushughulishwa na bishara ya fath "kufungua)

ISHIRINI NA TATU: Kuamini Qadari katika kuipata yule aliyoipigia mbio na kuikosa yule aliyeipigia mbio

ISHIRINI NA NNE: Inapatikana adabu kwenye kauli ya mtume alipomwambia Ali "nenda polepole", akimuamrisha aende kwa upole wala asifanye haraka

ISHIRINI NA TANO: Kulingania katika uislamu kabla ya vita

ISHIRINI NA SITA:Ni katika sharia kuwalingania watu kabla ya kuanza vita na mapambano

ISHIRINI NA SABA: Kulingania kihekima kwa kauli ya mtume kwa Muadhi "Wape habari yaliyo lazima kwao" kwa sababu huenda wakaufuata uislamu au wasiufate ni lazima kwenda nao taratibu ili wasije wakarudi kwenye ukafiri.

ISHIRINI NA NANE: Kujua haki ya Allah ndani ya uislamu

ISHIRINI NA TISA: Malipo makubwa yeyote ambaye ataongoka hata mtu mmoja kupitia ulinganizi wake na huko kuongea ni bora kwako kuliko kupata kila kitu kinachoonekana ni bora hapa duniani

THALATHINI: Kuapia fatwaa kwa sababu haifai kuapia fatwaa isipokuwa kimaslahi au faida.

MTIHANI SEHEMU YA KWANZA. (5 MLANGO)

SWALI LA KWANZA: TAJA MWANZO MILANGO MITANO YA MWANZO YA KITABU CHA TAUHID NA KINACHOENDANA NA KILA MLANGO WA KITABU.

ANWANI YA MLANGO.SABABU YA MTUNZI KUULETA MLANGO HUO.

1. ……
2. …… ……
3. …… ……
4. …… ……
5. …… ……

SWALI LA PILI: KAMILISHA IBARA ZINAZOKUJA

1. Tunajifunza kitabu cha Tauhid sababu ni 1. …… 2. ……
   3. …… 4. …… 5. ……
2. Hakutaja mtunzi utangulizi wa kitabu kwa sababu: 1. ……
   2. …… 3. ……
3. Inawezekana tukagawa kitabu cha Tauhid kwenye: 1. ……
   2. ……..…….. 3. …….. 4.……
   5. …….. 6. …….. 7. ……..……..……..
   8. …….. 9. …… 10. ……
4. Tunapinga kile aliyesema hakika ya kitabu cha Tawhid kuna Tawhid ya ibada tu, kwa kutumia mlango wa ……... mlango ……. Na mlango wa …….. na mlango wa …….
5. Ibada zimegawanyika sehemu 1. Ibada ……. Nayo ni …… dalili ni …… 2, ibada …… nayo ni ……. Dalili ni ……. 3 ibada ……. Nayo ni …… dalili ni ……
6. Nafsi alizoharamisha Allah kuuwawa ni nne nazo ni ……, ……, ……, ……..
7. Imesemwa na Ibn Masood radhi ziwe juu yake aya ya wasia wa mtume (s.a.w) kwa sababu ni …….
8. Amatu katika qur'an lina maana ya …… au …….. au …… au ……
9. Kuhakiki Tauhid ni …… na …… wa ……. Wa ……..
10. Huu umma ni mwingi Zaidi kuliko umma zilizopita katika …… wa ……
11. Kudhibiti kwa ubora wa mtu mmoja haulazimishi kuthibiti ubora wake kwa watu wote ……
12. "Hakuna riba ya Ruqya isipokuwa kwenye maradhi ya kijicho, maana yake ni ……
13. Yamekuja makatazo kutafuta Ruqya na kujichanja bila kwenda kwa dokta kwasababu …….
14. "Hasamehe kushirikishwa" maana yake …….. "lakini yeye husamehe yasiyokuwa hayo" maana yake……

15. “na ni roho iliyotoka kwake” maana yake…… “na neno lake” maana yake……
16. aliyojiegemeza Allah katika nafsi yake yanagawanyika kwenye 1. Kujiegemeza …….. nayo ni mlango wa kujiegemeza ……. 2. Kujiegemeza …… nayo ni mlango wa kujiegemeza ……..
17. “Amesema: “Amekutangulia Ukasha” hadi …… au ……
18. “na hawakuchanganya” yaani ……. “na dhulma” yaani ……
19. Tunaogopa kutokana na shiriki kwa sababu 1. …….……. 2. ……..…… 3. ……..…… 4. ……..
20. “Anataka fadhila za Allah” yaani …….. na kuthibiti sifa …….
21. Masharti ya da’awa 1. …….……. 2. ……..…… 3. …… 4. …….. 5. ……..
22. Mambo yenye kuvunja desturi ni 1, ……..na inakuwa kwa …….. na kwa 2. ……. Na inakuwa kwa …….. 3. ……. Na inakuwa kwa …….. 4. …….. na inakuwa kwa ……
23. Amesoma mtunzi: “ kuacha Rukhiya na tiba ya mila ni katika kuhakiki Tawhid hakutaja tatwayuri kwa sababu tatwayuri …….

SWALI LA TATU:JAZA UWAZI KWENYE JEDWALI LA AINA ZA RIA:



SWALI LA NNE: Weka alama ya (v) kwenye kisanduku cha jawabu sahihi

1. Mtunzi wa kitabu cha Tauhid: ☐ Ibn uthaimini ☐ Muhammed Abduwahab Tamimu.
2. Nasaha za wanachuoni: ni ☐ kuhifadhi matini kabla ya somo ☐ hamna faida ya kuhifadhi la muhimu ni kufahamu tu
3. "Wale tuliowapa kitabu wakakisoma kama ipasavyo kusoma" anapata faida mwanafunzi hatoacha elimu hadi atambue ☐ ndio ☐ hapana.
4. Wanachuoni wamekuchunguza kitabu cha Tawhid hawakukuta hadithi yeyote dhaifu na katazo: ☐ ndio ☐ hapana
5. Wanachuoni ,wote hata elimu zao ziwe kubwa kiasi gani haiwalindi wao: ndio ☐ hapana ☐
6. Katika vitabu vya shekh Muhammad AbdulWahab: ☐ kuweka wazi Shubuha ☐ masiala ya ujinga ☐ ufupisho wa sira ☐ misingi ya imani ☐ yote yalio tangulia
7. Milango ya kitabu Tauhid ☐ ango 67 ☐ ango76 ☐ ango 10
8. Utakapopata kitabu usikiingize katika maktaba yako isipokuwa baada ya kupitia au kusoma utangulizi wake na yaliyomo na maudhui yake. ☐ Ndio ☐ Hapana
9. Inawezekana kugawa Tawhid cha kitabu katika ☐ aina 11 ☐ aina 9 ☐ aina10
10. vitabu vyenye manufaa Zaidi ni vile vilivyotungwa kwa mfumo wa kutaja dalili na kufahamisha sababu za hukumu kama kitabu cha Tawhid. ☐ Ndio ☐ Hapana
11. Elimu ni kukusanya masaili kuyagawa kuyachambua na kuyawekea vigawanyo. ☐ Ndio Hapana ☐
12. Lazima kuthibiti taarifu za wanachuoni na vigawanyo vyao. Ndio ☐ Hapana ☐
13. Sehemu ya kwanza katika kitabu Tauhid ni. ☐ Utangulizi ☐ Maana ya Tauhid ☐ Ulazima wa Tauhid
14. Amefanya mtunzi rehema za Allah amemuigaAlbukhary katika utangulizi na hitimisho. ☐ Ndio ☐ Hapana
15. Hakuweka mtunzi mlango wa kwanza tunaweza tukauita: mlango wa utangulizi. ☐ Ndio ☐ Hapana
16. Imekusanya sehemu ya kwanza katika kitabu juu ya: ☐ milango5 ☐ milango 6 ☐ milango 7
17. Tauhid imegawanyika katika: ☐ ulezi na uungu na majina na sifa ☐ maarifa na kukiri na kutaka na kukusudia ☐ yote yaliyotangulia hayana utofauti
18. Mwenye kuamini moja na kuacha zingine katika aina ya Tauhid hatokuwa ni mwenye kumpwekesha Allah. ☐ Ndio ☐ Hapana
19. Kuigawanya Tawhid katika vigawanyo ni kwa uzushi kukosa dalili. ☐ Ndio ☐ Hapana
20. mahusiano kati ya Tawhid na Imani, Imani ina maana pana na Tawhid ni sehemu ya Imani hiyo. ☐ Ndio ☐ Hapana
21. Shahada LLA ILLA HAILLA LLAH ina: ☐ mbili nguzo ☐ nane nguzo ☐ saba nguzo
22. Kumpwekesha Allah katika kuuendesha ulimwengu na kuteremsha mvua niTawhid ya. ☐ Ulezi ☐ ibada ☐ majina na sifa
23. Ambayo yanapingana na asili ya Tauhid ni ☐ shirki kubwa ☐ shirki ndogo ☐ uzushi
24. Wajibu ulio mkubwa zaidi ni kuwafanya wema wazazi wawili. ☐ Ndio ☐ hapana
25. madhambi makubwa yaliyo haramishwa ni zinaa na kuuwa nafsi iliyoharamishwa ☐ ndio ☐ hapana
26. Ibada hutafsiriwa kwenye: ☐ jambo mojam ☐ bo mawili

27. Ibada ni (jina linalo kusanya kila:-) hii ni kauli ya: ☐ Ibn Qayyim ☐ Ibn Taymiyah
28. Thwawabu (ni kinyume :-) ☐ takufu wala kufananisha ☐ takufu wala kushabiisha ☐ hakuna utofauti
29. Kila aya iliyopo kwenye qur'an imefungamana na Tauhid: ☐ ndio ☐ hapana
30. Lengo la kuumbwa majini na wanadamu ni sawa na lengo la kuumbwa wanyama ☐ ndio ☐ hapana
31. (Nami sikuwauumba majini na watu) tatizokwenye aya hiyo mara nyingi linakuwa katika : ☐ uelewa ☐ utendaji
32. Majini yamekalfishwa: ☐ imani ☐ni na sheria
33. Neno umma hutafsiriwa: ☐ imamu ☐ mila ☐ zama ☐ taifa ☐ yote yaliotangulia ni sawa
34. (hakika kwa kila umma tuliutumia mtume) kuamia zama za: ☐damu ☐hu) hadi zama za Issa ☐ Muhammad) na hekima ya kutumwa kwao ni; ☐a na hoja ☐hma kubainisha njia ya kwenda kwa Allah yo☐
35. Masanamu ni katika matwaghuti ambayo yanaabudiwa kinyume na Allah: ☐ ndiyo ☐ hapana
36. yale yanayofuatwa katika matwaghut ni mfano wa viongozi waliotoka nje ya twaa ya Allah Allah ☐ ndiyo ☐ hapana
37. Atakae abudiwa kinyume na Allah na hajaridhia hayo atakuwa ni: ☐ twaghut ☐ si twaghut
38. Aya ya pili katika kitabu cha Tauhid inatujulisha juu ya kuafikiana mitume katika kulingania Tauhid: ☐ ndio ☐ hapana
39. Kauli ya mtunzi (aya au ayat) maana yake ni: (kukamilisha aya au ayat): ☐ ndio ☐ hapana
40. Kadhwaa na hukumu na matakwa yamegawanyika katika sheriya na maumbile; ☐ ndiyo ☐ hapana
41. Katika kadhwaa (z☐maumbileza kishe☐) zipo zinazokuwa nizenye kupendeza kwa Allah kwa upande mmoja na zenye kuchukiza kwa upande mwingine.
42. Na tunawahukumu wana wa Israel katika kitabu kwamba; "Hakika nyinyi mtafanya fisadi katika nchi) ☐ hukumu ya hapa ni yakis☐a kim☐nbile
43. Kila mnyama anamsabih Mwenyezimungu isipokuwa mjusi; ☐ ndio ☐ hapana
44. Ibada imegawanyika katika sehemu: ☐2 ☐ 3 .ndege wanapofanya tasbihi ni ibada ya ☐ lazima ☐ utii
45. Washirikina wana sehemu katika ibada ya Mwenyezimungu ☐ ndiyo ☐ hapana
46. Ibada haiwi ila kwa ulimi na viungo ☐ ndiyo ☐ hapana
47. Msimshirikishe na chochote) inakusanya kila kitu: si Nabii, malaika, wala walii wala jambo katika mambo ya dunia. ☐ ndiyo ☐ hapana
48. Bishara ni habari yenye kudhihirisha haikusanyi habari yenye kudhuru (madhara) ☐o ☐ hapana
49. Nafsi ambayo Allah ameiharamisha ni kuuwawa nafsi ya muislamu. dhimmiyu ☐hadi ☐ mustaaminu ☐ yote ni sawa
50. Je mtume alihusia. ☐ kweli ☐ si kweli
51. Kauli ya Ibn Masood (wosia) kwa sababu: ☐ imekusanya dini yote ☐ wasia wa Allah ☐ yote ni sawa

52. Haki za waja juu ya Allah hiutwa: ☐ haki ya lazima ☐ haki ya fadhila (ihsani)
53. "Allah na mtume wanajua": unasema ☐ katika maisha ya mtume ☐ wakati wote
54. Amekataza mtume (s.a.w) Muadh asiwabashirishie isije: ☐ wakashindana ☐ wakabweteka yote ni sawa, Je, Muadhi alimkhalifu mtume (s.aw) katika katazo hili? ☐ kweli ☐ si kweli. Kwasababu inaharamishwa kuficha elimu kwa kila hali: ☐ ndio ☐ hapana
55. Je hukumu hii ni maalum kwa Muadh radhi ziwe peke yake: ☐ kweli ☐ si kweli
56. Inalazimu ubora wa kitu kisiwe ni wajibu: ☐ ndiyo ☐ hapana
57. "Na anapotajwa Mwenyezimungu peke yake nyoyo za wasio iamini Akhera huchafuka. Na wanapotajwa wengine asiye kuwa yeye basi wao hufurahi" aya hii imeendana pamoja na mlango: ☐ ☐ ☐
58. Mambo ambayo aliyojiegemeza Allah katika nafsi yake zimegawanyika sehemu: ☐ mbili tatu ☐
59. Dhulma kubwa ni dhulma ya mwanadamu,kumdhulumu mwenye kuamua kuchukua mali yake au kuvunja heshima yake cheo: ☐ ndiyo ☐ hapana
60. Matukio ya mwenye kukutana na Allah hali ya kuwa ana dhambi si za shirki ni ☐ Adhabu dini ya matakwa ☐
61. (LAA ILA HAILLAH) ni dhikiri na sio dua: ☐ ndiyo ☐ hapana
62. hapatikani mtu mwenye kusema (Laaila haillah) lakini hana thamani yoyote kwa Allah ndio ☐ hapana ☐
63. Shahada ya Hakika Muhammad ni mja wa Allah na mjumbe wake, inapingan☐? kufanya maasi ☐ kuleta bidaa ☐ ni sawa
64. Kauli: (Issa ni mja wa Allah) ni majibu kwa mayahudi (mtume wa Allah) ni majibu kwa manaswara: ☐ ndio ☐ hapana
65. (Na ni roho iliyotoka kwake) utegemezaji huu ni wa:dh☐ au☐afi
66. Kauli yake: Amemwingiza Allah peponi: ☐ amemwingiza moja kwa moja ☐ amemwingiza sifa ☐ yote
67. Kuhakiki Tawhid ,nikujitakasa na: ☐shirki ☐bidaa ☐maasi ☐yote ni sawa
68. (Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema: ☐ qudra ☐ imamu ☐ mwalimu wa kheri yote ni sawa
69. Hakuna Rukya katika maradhi ya mwili na nyoyo isipokuwa kijicho na sumu ya mdudu na homa: ☐ ndio ☐ hapana
70. Hadithi (wala hawataki ruqya) Amezidisha Muslim (wala hawafanyi rukya hii ziada ni: ☐ sahihi ☐ dhaifu
71. Shirki kubwa inahalalisha damu ya kafiri na mali asipokuwa dhimiyu au muahidi: ☐ ndio hapana ☐
72. Utofauti kati ya msoma ruqya na mwenye kuomba ruqya hakika mwenye kuomba kusoma ruqya. Ama ruqya anaweza kumuelekea asiyekuwa Allah kwa moyo wake ama msoma ruqya yeye ni muhsin: ☐ ndiyo ☐ hapana
73. kumlinganisha asiyekuwa Allah pamoja na Allah: ☐ kubwa ☐ ndogo
74. Kilichotengeneza kwa shirki ya sura huitwa: ☐ sanamu ☐ sanamu la mbao ☐ yote
75. Mali nzuri ni: ☐ ya juu ☐ ya kati ☐ ya chini
76. Elimu na matendo, anakamilika mja na nafsi yake kwa da'awa na suburi inakamilisha mwingine: ☐ ndiyo ☐ hapana

77. Ameogopa mtume (s.a.w) juu ya umma wake kwa dajali Zaidi kuliko kuogopa juu yaria (kujionyesha, kwa sababu ria ni katika shirki ndgo: ☐ ndiyo ☐ hapana
78. Mja pindi atakapokua mkweli katka itikadi, hapana budi awe ni mwenye kulingania itikadi hiyo: ☐ ndiyo ☐ hapana
79. Muono: ☐ elimu ya kisheria ☐ hekima ☐ kujua hali ya walinganiwa ☐ yote
80. Idadi ya masharti ya daa'wa ni: ☐ tano ☐ nne ☐ tatu
81. Eleza tofauti kati ya shirki kubwa na shirki ndogo

SHIRKI NDOGO	**SHIRKI KUBWA**
……	……
……	……
……	……
……	……
……	……

SWALI LATANO:WEKA KATIKA FUNGU (A) YANAYONASIBIANA NA FUNGU (B)

AB	
1. Huma (sumu)	Kujidhalilisha kwa Allah kwa kufanya maamrisho yake na kujiepusha na makatazo kwa kupenda na kutukuza.
2. Uungu	iyo ngamia mwekundu ametajwa kwasababu anapendwa zaidi na waarabu.
3. Ibada	Kuhisi mkosi kwa jambo lenye kuonekana au kusikiwa au kujulikana sehemu yake au muda wake.
4. Twaghuti	Mwenye kufananishwa na kulinganishwa na Allah.
5. Ria	Kitakacho abudiwa kikiwa katika sura ya mwanadamu au kiumbe kingine.
6. Kutazamia mkosi kwa ndege	Atakae abudiwa kinyume na Allah kwa sura.
7. Ni doa (mshirika)	Mja ilikuvuka mipaka kwa mola wake mwenye kufuatwa, kuabudiwa, au kutiiwa.
8. Sanamu	Anamuabudu Allah aonekane au asikie watu wakimsifia.
9. Tawhid	Ni kumpwekesha Allah kwa kuumba na katika ufalme na kuendesha ulimwengu.
10. Ibada	Ni kumpwekesha Allah kwa ibada au kumpwekesha Allah kwa matendo ya ibada.
11. Khawariji	Ni jina linakusanya kila anachopenda Allah na akaridhia iwe ni maneno au matendo.
12. Mzimu	Ni wale wanaosema hakika mwenye madhambi makubwa ni kafiri anakaa milele motoni.
13. Tawhid ya uumbaji	Kumpwekesha Allah kwa yote yanayo muhusu mwenyewe ulezi na uungu na majina na sifa zake.
14. Ngamia mwekundu	Ni mwenye kuelekea kwa Allah anapinga shirki anajiepusha kwa kila jambo linalomkhalifu Allah
15. Mwongofu	Ni mng'ato wa kila mdudu mwenye sumu.

Mbili: Tafasiri ya Tauhid (9 milango)

[6] mlango tafasiri Tauhid na shahada ya laa ila haila llah

Baada ya ktangulia maelezo mengi kuhusu hii Tawhid, utadhani kuna ameinua shingo yake kutazama kujua bayana, sasa ni ipi hii Tawhid ambayo imewekewa milango yote hii? (wajibu wake, ubora wake, tahkiki yake kuogopa shirki na kulingania hiyo Tawhid. Swali hilo litajibiwa kwa huu mlango ufuatayo nao ni mlango wa ufafanuzi wa Tawhid ambao utaendelea mpaka mwisho wa kitabu hiki

DALILI YA KWANZA

Kauli ya Allah "Hao ambao wanao waomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kwenda kwa mola wao mlezi – ni yupi miongoni mwao atakuwa karibu mno (na mola wake)

Hawa wanao waomba" wao wenyewe wanatafuta njia ya kwenda kwa mola wao mlezina yupi miongoni mwao atakuwa karibu nae? Vipi mnawaomba hali ya kuwa na wao ni wenye kuhitajia tena hawana chochote (cha kuwasaisia)

Hii ndio shirki kwenye dua (maombi)

DALILI YA PILI

Kauli yake Allah: "na pale Ibrahim alipomwambia baba yake na kaumu yake; "Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu (26) isipo kuwa Yule aliye niumba" aya

- "Isipokuwa Yule aliyeniumba": Ibrahim amekusanya kati ya kukanusha miungu yote na kuthibitisha ibada pekee kwa aliyemuumba wala hakusema Nimejitenga mbali na mnavyoviabudu isipokuwa Allah kwa faida mbili.
  1. Kubainisha sababu za kumpwekesha Allah (s.w)katika ibada, kwa sababu ikiwa Allah yu pekee katika uumbaji, basi ni wajibu kupwekeshwa katika ibada.
  2. Kubainisha ubatili wa ibada za masanamu, kwa sababu masanamu hayo hayakukuumbeni ili nyinyi mpate kuyaabudu
- Tauhid haipatikani kwenye kumuabudu Allah subhanahu pamoja na miungu mingine bali lazima kumtakasa yeye tu katika ibada zake utakufa katika baadhi ya miji yay a kiislamu kuna wanao swali, kufunga na kutoa zakalakini pamoja na ibada hiyo, wanasujudia makaburi.

DALILI YA TATU NA NNE

3. kauli yake Allah (wamewafanya mapadri wao na makuhani kuwa ni miungu yao badala ya Allah)
4. kauli yake (Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasiokuwa Allah wanawapenda kama wanavyompenda Allah.

(Ahbarahum)wanazuoni wao na husemwa bahari kwa wingi wa elimu zao (ruhbannahum) wafanya ibada (Arbaaba) miungu nao ni wanachuoniwanao watu katika kumuasi Allah akawaabudupia wale wafanya ibada miongoni mwao (watawa) kufanya hivyo ni shirkikatika utii wanawapenda miungu yao mapenzi yalio sawa sawa na kumpenda Allah.

VIGAWANYO VYA MAHABA

MAHABA YA KIMAUMBILE.
(jaaizi) kwa sharti asiya tangulizemapenzi haya Zaidi kuliko kumpenda Allah. Kama mtu kumpenda mke na mtoto na watoto kuliko anavyompenda Allah

KUPENDAKWA AJILI YA ALLAH.
Ni (Wajibu) kifungo cha Imani kilicho madhubuti kabisa ni kupenda kwa ajili ya Allah

KUPENDA YA KITU KINGINEPAMOJA NA ALLAH.
Ni (shirki kubwa) inakanusha mapenzi ya kiumpenda Allah kuwa sawa na mapenzi yoyote asiyekuwa Allah au zaidi

Na yanagawanyika mapenzi kwa ajili ya Allah kwenye mapenzi ya amali, mtendaji wake na mfanyakazi au muda (zama) au sehemuu) pamoja na nyakati na sehemu.

DALILI YA TANO.

Na katika sahihi ya Bukhari kutoka kwa Mtume (s.a.w) hakika yeye amesema (Atakae sema LAA ILLAHA ILA LLAH na akakufuru kwa yale yanayoabudiwa kinyume na Allah inaharamishwa mali yake na damu yake na hesabu yake kwa Allah azza wajalla.

Na sherhe ya tafsiri hii: ipo kwenye milango inayofuata.

(AKAKUFURU KILE KINACHOABUDIWA) Haina budi kukufuru chochote kinachoabudiwa kinyume na Allah bali akufuru vilevile (kupinga) kila kufuru,na atakaetoa shahada na akaona kuwa manaswara na mayahudi wa zama za leo ni dini sahihi basi hakika yeye si muislamu. Na vile vile atakayeona dini nyinginezo ni kifikra tu anachagua kila anacho taka kwenye dini hizo basi huyo si muislamu

MAS-ALA YANAYOFUNGAMANA NA TAWHID

kuna masaaili yale ya muhimu zaidi. Tafsiri ya Tawhid tafsiri ya shahada na baina yake kuna mambo yalio wazi: (hakuna budi kuyapinga na kuyathibitisha)

- Aya ya Israa inabainisha raddi juu ya washirikina ambao wanaomba watu wema. Ndani yake kuna ubainisho wa kufanya hivyo ni katika shirki kubwa (shirki ya du'aa)
- Ayatul Baraa: Inabainisha kuwa ahlul kitabu walifanya makuhani wao na wamonaki wao ni miungu kinyume na Allah. Na ikabainisha kuwa hakika wao hawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu Mungu mmoja pamoja na kwamba tafsiri yake haina matatizo ndani yake. Kuwatiii wanazuoni na kuwaabudu katika ma'aswiya si kuwaomba (shirki twaa)
- Kauli ya Khalili Alayh ssalaam kwa makafiri: (Hakika mimi ninajitenga mbali na mnayo yaabudu)(Isipokuwa Yule aliye niumba) akawatoa wenye kuabudiwa isipokuwa Allah. Na akataja Subhaana katika huko kujitenga na hayo mapenzi ndio: Tafsiri ya shahada an laa ilaaha illa llah. Kisha akasema (Na akalifanya kuwa hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee)
- Ayatul Baqarah ikiwaelezea makafiri ambao amewazungumzia Allah: (Wala hawatakuwa wenye kutoka motoni) akataja kuwa wao wanawapenda miungu yao kama wanavyo mpenda Allah akajulisha kuwa wao wanampenda Allah mapenzi makubwa lakini hayakuwaingiza katika uislamu. Vipi wale wanaowapenda miungu wengine zaidi kuliko kumpenda Allah? Na je vipi kwa wale wanaowapenda miungu yao pekee na hawampendi Allah? (Shirki ya mahabba (mapenzi). Imegawanyika sehemu nne:-
  1. Kumpenda Allah zaidi kuliko kitu kingine, na hiyo ndiyo Tawhid
  2. Kumpenda asiyekuwa Allah kama anavyompenda Allah. Nayo ni shirki
  3. Kumpenda zaidi asiyekuwa Allah kuliko Allah. Na hii ni shirki kubwa kuliko iliyo tangulia
  4. Kumpenda asiyekuwa Allah na kutokuwa katika moyo wake hata chembe ya mahaba kwa Allah (hii ndio shirki kubwa zaidi)
- Kauli yake Swalla llahu alayhi wassalama (Atakae sema**LAA ILAHA ILLA LLAH** na akakufuru kwa yale anayoyaabudu kinyume na Allah ni haramu mali yake na damu yake kumwagwa na hisabu yake ni kwa Allah) Na hii ni dalili kubwa yenye kubainisha maana ya **(LAA ILAAHA ILLA LLAH)** Hakika mtume hakujaalia kutamka shahada iwe ni kinga ya kumwaga damu na mali, hata kufahamu maana yake na matamshi yake. na kukiri juu ya hilo. Hata ikiwa hamuombi yeyote isipokuwa Allah peke yake asiye na mshirika. haiwezi iharamisha mali yake na damu yake mpaka aegemeze juu ya hayo kukanusha ibada ya vyote vinavyoabudiwa kinyume na Allah ikiwa atakuwa na mashaka katika kukanusha miungu au akasita haiwezi kuwa haramu mali yake wala damu yake

  Ni utukufu na ukubwa ulioje wa haya masiala! Na uwazi wake na hoja zake kubwa zenye kumshinda na kumnyamazisha mpinzani!

7–HUU NI MLANGO UNAOFAFANUA SHIRKI YA KUVAA CHENI (BANGILI) NA UZI NA MFANO WAKE KWAJILI YA KUONDOSHA BALAA AU KUJIKINGA NA BALAA

(Katika shirki) Baadhi ya shirki na miongoni mwa hiyo ni shirki kubwa au ndogo na hivyo nako ni kuvaa bangili ili kuondoa balaa lililoshuka au kujikinga na balaa kabla ya kushuka

JE KUVAA (BANGILI) NA UZI NA MFANO WAKE NI SHIRKI NDOGO AU KUBWA?

SHIRKI NDOGO
Aitakidi kuwa bangili n.k ni sababu ya kuondoa madhara au kuleta madhara hali ya kuwa Allah hakuijalia kuwa ni sababu ya kimaumbile (dawa) au kisheria

SHIRKI KUBWA
Atakapo itakidi kuwa bangili n.k inaathari yenyewe na inaleta manufaa au kuondosha madhara

MGAWANYIKO WA WATU KATIKA KUITIKADI SABABU UPO KATIKA AINA TATU

SHIRKI KUBWA
Aitakidi kuwa dawa inaathari yenyewe kwa dhati yake na inaleta manufaa na kuondosha madhara

ITIKADI SAHIHI
Aitikadi na kuvifanya ni sababu vile alivyoijalia Allah kuwa ni sababu na sababu ima itakuwa ni ya kiada (kama dawa) au kisheria kama (ruqya)

SHIRKI NDOGO
Aitakidi na kuvifanya sababu vile ambavyo Allah hakuvifanya kuwa sababu ili kama kufunga kichwa cha ng'ombe dume kwa kujikinga na vijicho hali ya kuwa hiyo sio sababu katika kuondoa madhara aukuleta manufaa.

WAMEGAWANYIKA WATU KATIKA KUCHUKUA SABABUKATIKA MAKUNDI MAWILI NA KATI KWA KATI

KUNDI LINALO AMINI KATI NA KATI KWENYE KWASABABU
Kundi hili linathibitisha sababu ya ada na kisheria tu si kinyume na hizo nalo ni Ahlu sunna waljamaa

KUNDI LENYE KUCHUPA MIPAKA KWENYE SABABU SABABU
Linathibiti isiyo kuwa sababu kuwa sababu kama vile kundi la masufi

KUNDI LINALOKUPINGA KUFANYA SABABU
Wale wanao pinga hekima ya Allah kama vile kundi la Jabriyah na Ashiariyah.

HUKUMU YA HALI ZINAZOMUHUSU MTU ANAYEFUNGA UZI NA MFANO WAKE

Huyu hufundishwa	Awe ni jaahili (mjinga) wa hukumu zake
Hii ni shirki ndogo	Aitakidi kuwa zina sababu na Allah mtukufu hakujaalia huo uzi n.k kuna sababu
Hii ni shirki kubwa	Aitakidi kuwa zina athari kwa dhati yake na zitaleta manufaa na kuondosha madhara
Hii ni katika madhambi katika madhambi makubwa	Asiwe na itikadi yeyote lakini anavaa kama mapambo kama ilivyo katika hali za vijana kwa sasa – Allah atuongoze woote – Basi kila atakae ona bangili hizi kwa vyana huenda akadhani kuwa inajuzu, na wakati huo atakuwa amefungua mlango wa shari kwa watu na kuna kujifananisha na wanawake na washirikina. (kwenye uvaaji wa hizo bangili)

DALILI YA KWANZA

Kauli yake Allah mtukufu (Sema: Je! Mnawaonaje wale mnao waomba badala ya Mwenyezimungu akitaka kunidhuru wao wanaweza kumondoa madhara yake?)

Haya masanamu hayamnufaishi mwenye nayo si kuleta manufaa wala kwa kuondosha madhara hayo masanamu si sababu ya hivyo.Na huunganishwa kila kisichokuwa na sababu za kisheria au za qadari (maumbile) basi huzingatiwa kuvifanya sababu ni shirki kwa Allah mtukufu (sema Mwenyezimungu ananitosha) kuna maelekezo ya kutosheka na kumtegemea Allah si kutegemea sababu zilizo dhaifu kabisa.

DALALI YA PILI.

Kutoka kwa Imrani Ibn Huswayni: Hakika nabii swalla lahu alayhi wassalama alimuona mtu mmoja katika mkono wake ana bangili ya shaba akasema (kitu gani hiki? Akasema nimevaa kujikinga na homa (ugonjwa) akasema (Ivue hakika haikuondoshei chochote isipokuwa inakuzidishia unyonge (ugonjwa) hakika laiti ungelikufa na hicho ulichovaa basi usingefaulu kamwe *(imepokelewa na Ahmad kwa sanadi isiyo na shaka)*

DALILI YA TATU

Kutoka kwa Uqbah Ibn Amir wa (mwenye kuninginiza (kujifunga) shingoni hirizi basi Allah hatomtimizia jambo lake. Na atakae funga chaza vile vile hatamtimizia Allah jambo lake, na katika riwaya (atakae funga hirizi basi amefanya shirki)

(Atakae funga hirizi) funga na akafungamana nayo katika mopyo wake na sababu hiyo akasema (funga) wala hakusema (kufichika) (Basi asimtimizie Allah jambo lake) ima hii ni dua juu yake au khaba ya changanya chochote
(mwenye kutundika chaza) vitu vitokavyo baharini
(Hata mtimizia Allah jambo lake) hata muacha Allah katika dua: utulivu hivyo imetendewa kinyume cha makusudio yake.
(Atakuwa amemshirikisha) shirki kubwa atakapo itakidi kuwa hirizi inaathari kwa dhati yake kinyume na amri ya Allah na kinyume cha hapo itakuwa shirki ndogo.

DALILI YA TATU

Na kutoka kwa Ibn Hatim kutoka kwa Hudhaif: Hakika yeye alimuona mtu mmoja katika mkono wake kuna uzi wa kuzuia homa akaukata. Kisha akasoma kauli yake Allah (wala hawakuamini wengi wao kwa Allah isipokuwa walikuwa ni washirikina)

- **(Homa) maana yake:** kwa sababu ya homa kwa kutaka kuipoza au kupona
- (Akataka) kuondosha munkari kwa mkono na (kutumia nguvu) ndani yake kuna nguvu ya salafi katika kuondosha munkari (maovu)
- **Hukumu ya kutundika:** hirizi kutundika kote (kwa aina yeyote ni haramu iwe cheni, bangili, uzi, chaza, hirizi na macho ya mbwa mwitu kwato ndala za zamani, na mshipi na kiganja na jicho na kichwa cha ng'ombe dawa na sanam la simba au baadhi ya miti na kitambaa na vinginevyo.

MAS-ALA YANAYO FUNGAMANA NA HIRIZI

Jambo la kwanza: makemeo makubwa katika kuvaa bangili na na uzi na mfano wake kwa lengo la kujikinga

Jambo la pili: Hakika yule swahaba lau angelikufa na hiyo mkononi mwake asingelifaulu. Ndani yake kuna ushahidi wa maneno ya maswahaba kuwa shirki ndogo ni katika madhambi makubwa (kwa sababu shirki haisamehewi hata kama ikiwa ndogo kinyume na madhambi makubwa)

Jambo la tatu: Hakika Yule sahaba hakupewa udhuru wa ujinga (kutojua)(Hakupewa udhuru baada ya kubainishwa na mtume, na ujinga uko aina mbili;

1. **Ujinga usiopewa udhuru:** Nao ni ule ujinga unaotokana na uzembe au kupuuza pamoja na kuwepo muqtadha wa kusoma hakika huo ujinga haupewi udhuru sawa iwe kwenye kutojua ukafiri au maaswiya
2. **Ujinga unaopewa udhuru:** Nao ni ule ujinga ulio kinyume na ujinga wa kwanza maana yake mtu hakupuuzia wala kurembea na wala hayakupatikana mazingira ya kuelimishwa kwa kutopita kwenye akili yake kuwa jambo hili haramu basi mtu huyo hupewa udhuru ikiwa ni mwenye kunasibishwa na uislamu hautomdhuru na ikiwa ni mwenye kunasibishwa na kufru basi atakuwa kafiri hapa duniani na akhera jambo lake litakuwa kwa Allah.

Jambo la nne: Hakika hilo bangili (hirizi) halinufaishi chochote hapa duniani zaidi ya kumzidishia mtu madhara, kama alivyosema mtume " hilo halikuzidishii chochote isipokuwa ugonjwa tu.

Jambo la tano: Kuzuia kwa ukali kwa mwenye kufanya hivyo (kuvaa hirizi)

Jambo la sita: Kueleza wazi kuwa mwenye kutundika chochote (kwa ajili ya kinga) hutegemezwa kwenye kitu hicho

Jambo la saba: kueleza wazi kuwa mwenye kutunika hirizi huyo amefanya shirki

Jambo la nane: Hakika kuvaa uzi kwa kuondosha homa ni katika shirki

Jambo la tisa: Kusoma hudhaifa aya ni dalili kuwa hakika maswahaba hutolea dalili kwa aya ambazo zinazohusu shirki kubwa juu ya shirki ndogo kama alivyo taja Ibn Abbas katika ayatuh ya suratul- Baqara (kuhusiana na mapenzi)

Jambo la kumi: Hakika kutundika chaza kuilinda kutokana na kijicho ni katika shirki (ni katika hirizi za kishirikina)

Jambo la kumi na moja: Kumuapiza mwenye kutundika hirizi ni kuwa Allah hatamtimizia jambo lake na atakae tundika chaza maana yake Allah atamuacha na jambo lake. Hatutayatoa maelezo haya uwazi (mele za watu) bali tutamuambia mtu tuliemuona amevaa hirizi "Allah asikutimizie shida zako" Tumefanya hivyo kwa sababu tukimwambia mtu mbele za watu tena kwa kumtaja (kuwa umevaa hirizi) inaweza ikawa sababu ya kuchukia kabisa dini lakini tukimwambia (kwa siri) acha kuvaa hirizi au chaza na tukamsomea hadithi (zenye kukataza ataonyeka).

8} MLANGO ULIOKUJA KUELEZEA KUHUSU (RUQYA) TIBA ZISIZOKUA ZA KISHERIA NA HIRIZI.

Kwanini mtunzi amesema (mlango uliokuja kuelezea) na hajasema (na hajasema (ni katika shirki kujitibu kinyume na sheria) kama ilivyo katika mlango ulotangulia?

1. Kwa sababu (Ruqya) tiba imegawanyika katika vigawanyo viwili ya kisheria na isiyokua ya kisheria.
2. Na hirizi zote ni katika ushirikina isipokua ikiwa inatokana na qur'an basi hiyo ni haramu

Katika kitabu cha Swahili hadithi kutoka kwa Abuu Bashiri al-ansaariy ya kwamba yeye alikua pamoja na Mtume (s.a.w) katika moja ya safari zake, mtume (s.sw) akamwagiza mjumbe (ya kwamba isibakie katika shingo ya ngamia yoyote mkufu wa kamba - au fundo lolote ila likatwe).

(fa-arsala): akamtuma mjumbe ili kuchunguza hali zao, uchunguzaji unakubalika kisheria (qilaadatu) fundo, washirikina huitakidi ya kwamba inmkinga na kijicho kwa ngamia nah ii ni itikadi potofu.

DALILI YA PILI NA YA TATU.

2. Na kutoka kwa Ibn Masood (R.a) amesema; nimemsikia mtume (s.a.w) akisema (Hakika tiba isiyokuwa ya kisheria na hiziri na limbwata ni ushirikina) Imepokelewa na Ahmad na Abuu Doawnnd.
3. Na kutoka kwa Abdillah bin Ukaym kutoka kwa mtume (s.a.w) (atakae jifungamanisha au (kufungamanisha moyo wake na kitu huachwa au (huelekezwa katika kitu hicho) ameipokea hadithi hii Ahmad na Tirmidh.

- Hakika ruqya yaani iliyozoeleka kwao wao washirikina na inakusudiwa hapa ruqya ya kishirikina ambayo haijathibiti kisheria.
- Mtume amesma kwa atakae jifungamanisha na kitu atatelekezwa katika kitu hicho na hajasema (atakae fungamana), kwa sababu mtu huyu ameufungamanisha moyo wake na kitu hicho. Basi atakae jifungamainisha na Allah basi Allah akamtosha na atakaejifungamanisha kwa asiekua Allah atadhalilika.
- Mwanadamu hapaswi kuufungamanisha moyo wake na kuitegemea sababu, bali anapaswa aufungamanishe moyo wake kwa Allah na kumtegemea yeye, mfanyakazi ambae moyo wake ameufungamanisha na Yule aliemuajiri akielekeza kwake haja zake zote na akamsahau msababishaji wa kila kitu ambae ni Allah atakua ameingia katika aina miongoni mwa aina za shirki na akiitakidi ya kwamba aliemuajiri ni sababu tu na aliesababisha kila kitu ni Allah anakua hajapingana na (tawakul) kumtegemea Allah.

MASHARTI YA TIBA YA KISHERIA (RUQYA)

- Iwe inatokana na qur'an au sunna au aombe kupitia majina ya Allah na sifa zake
- Iwe ni kwa maneno yanayofahamika, na kusikika na kueleweka kwa lugha ya kiarabu.
- Aitakidi ya kwamba anayoyasoma nisabu tu za kisheria hazinufaishi ila kwa idhini ya Allah.

Likipungua sharti katika masharti haya basi (Ruqya) tiba hiyo inakua sio ya kisheria, Na hakuna tiba (Ruqya) isiyokua ya kiarabu, ila ikiwa katika hali ya dua basi inasihi kuomba dua kwa lugha isiyokua kiarabu kwa sharti asibadilishe majina ya Allah kwa sababu majina ya Allah ni taufiq (yamekuja kwa dalili maalum) (majina ya Allah yanasomwa kama yalivyo katika lugha zote).

Hirizi: Ni kitu kinachofungwa kwa watoto kuzuia na kijicho; lakini ikiwa kilichofungwa ni katika qur'an wameruhusu baadhi ya wema walotangulia, na baadhi yao hawajaruhusu hilo, na wamelifanya jambo hilo ni katika mambo yalokatazwa miongoni mwao ni Ibn Masood.

Na Ruqya:tiba ya kisheria ndio ile iitwayo Hirizi na ikaja dalili juu ya hli tofauti na ile ya ushirikina, kwa hakika ameiruhusu mtume (s.a.w) kujilinda kwayo kutokana na vijicho na homa.

Na limbwata: Ni kitu wanachokitengeneza na kudai kwamba kinamfanya mwanamke apendwe na mume wake na mume apendwe na mkewe

NI KATIKA LIMBWATA

PETE YA UCHUMBA

SHIRKI KUBWA

Akitakidi kuwa pete hiyo vinaathiri kwa dhati yake na kwamba vinaleta manufaa na kuzuia madhara

SHIRKI NDOGO

Akiitakidi kuwa pete hiyo (limbwata) ni sababu ya kubaki kwa mahusiano ya kindoa

NI HARAMU

Na hii ndio hali ya chini nay a mwisho kwa sababu ni katika ada ya manaswara kwani wao wanaitakidi kwa kuiweka kwake (limbwata) itikadi ya utatu na imetahadharishwa kwa wanaume kama ni pete hiyo ya dhahabu

DALILI YA NNE

Naamepokea imam Ahmad kutoka kwa ruwayfiu amesema :amesema kunambia mimi mtume (S.A.W) (Ewe ruwayfiu huwenda maisha yakawa marefu kwako basi uwaambie watu hakika mwenye kufunga ndevu zake au kuvaa fundo au akajisafisha kwa kutumia kinyesi cha wanyama au mifupa hakika ya Muhammad (S.A.W) yupo mbali na mtu huyo.

***(HAKIKA MWENYE KUFUNGA NDEVU ZAKE):**Ima iwe kwa mlango wa kujitukuza au ni katika mlango wa kumjulia ni sababu ya kumzuia na kijicho

***(KUVAA WATARA):**Alwatara ni kamba inayofungwa inachukuliwa kwa mbuzi na ina tumiwa kwa kuzuia kijicho.

***(AU AMESTANJI KWA KNYESI CHA MNYAMA):**Kuondosha athari itokayo katika njia mbili haja kubwa au ndogo kwa kinyesi cha wanyama

***(AW ADHMU):**Nacho ni chakula cha majini cha kinyesi chakula cha wanyama wa majini.

DALILI YA TANO NA YA SITA

5:Na kutoka kwa Said ibn Jubayri anasema (Mwenye kukataa hizi kujitoa kutoka kwa mwanadamu itakuwa kama kuacha huru mtumwa) amepokea wakiiy-i.

6:N hiyo kutoka kwa Ibrahim:(Walikua wanachukia hirizi kiujmla ya kwenye Qur-an na isiyo ya kwenye Qur-an

***(KAANA AADU RAQABATI):**Kwasababu yeye amemuacha huru kutoka katika utumwa wa kishetani ambao ndani yake kuna shirki na hili ni la juu miongoni mwa aliemuacha huru kutoka kwenye utumwa wa kibinadamu lakini anaishia kwa kile kilichokuwa kizuri.

KWANINI TUNAHUKUMIA KWA KUAHARAMISHWA HIRIZI ITOKANAYO NA QUR-AN

- Kuchukia baadhi ya waliopita kwa hilo na kuchukia kwa waliopita inamaanisha uharamu
- Kwa kuingia kwake chini ya kauli ya mtume(S.A.W)(Hakika ya rukia isiyo kisheria na hirizi na limbwata na shirki)
- Tunaweza kufungua mlango wa shari kwa sababu ya baadhi huenda wakadhania ya kwamba hirizi zote inajuzu mpaka isiyotokana na Qur-an
- Kwasababu ndani yake kuna kudhalilisha Qur-an nahuenda ikaingiizwa chooni au ikapatwa na najsi.

MAS-ALA MBALI MBALI

Ya kwanza :Tafsiri ya rukia isiyo ya kisheria na hirizi.

Ya pili : Tafsiri na maana ya limbwata.

Ya tatu : hakika ya vitu hivi vyote ni katika shirki pasipo kutoa hata moja.

Ya nne : Ya kwamba ruqia kwa maneno ya kweli ya kisheria kw aajili ya kujikinga kijicho na sumu za wanyama wanaouma sio katika shirki (Na vilevile inakusanya na vinginevyo kama vile uchawi).

Ya tano Ya kwamba hirizi ikiwa inatokana naQur-an:hapo wametofautiana wanazuoni je hiyo ni katika shirki au siyo?(Na kauli iliyo sahihi ni madhehebu ya ibn masuudi(Radhi za Allah ziwe juu yake)kuwa ni jambo lililokatazwa Kwa sababu ya asili yake ni kutokuwa ni sheria ku fanya).

Ya sita : Ya kwamba kuwafunga kamba wanyama kwa ajili ya kuwakinga kutokana na kijicho (ni miongoni mwa shirk).

Ya saba : Adhabu kali kwa Yule atakae funga hizo kamba .

Ya nane : Ubora na thawabu kwa Yule mwenye kukata hirizi kwa watu.

Ya tisa : Hakika ya maneno ya Ibrahim hayatofautiani na ikhtilafu zilizotangulia kwa sababu aliwakusudia wafuaisi wa Abdullah ibn masoud(Na sio makusudio yake ni wafuasi au maswahaba watu wa mtume(S.A.W)wala waliokuja baada ya maswahaba zake mtume(swallahu alayhi wassalama)kwa ujumla.

9.MLANGO UNAO ZUNGUMZIA KUTAFUTA BARAKA KWENYE MTI ,MAWE AU MFANO WA HIVYO

TABARUK: Ni kutafuta Baraka na katika hivyo

- Kutafuta Baraka kisheria
  - Katika jambo la kisheria kama vile swala katika msikiti mtukufu (makka)na kusoma Qur-an
  - Katika kila kinachoonekana kama vile kusoma vitabu vya ahli sunnah kama vile vitabu vya shekhe Al-islam
- Kutafuta Baraka kuliko zuiliwa Na uthibiti katika hilo ni kila ambacho hakijathibiti kisheria mfano kugusa chumba cha mtume na kupangusa , kwa lengo la kutafuta Baraka

DALILI YA KWANZA

Ni kauli ya Allah : " Je mmemuona Lata na Uzza *na Manata mwingine wa tatu ? "

Kutoka kwa abi waaqid Allaythiy:amesema tulitoka na mtume kuelekea Hunain na sisi tukiwa wageni kutoka katika ukafiri nawashirikina na walikua na mti wakitafuta Baraka katika mti huo na wakatundika silaha zao katika mti huo mti ule unaitwa (dhaata an waatwi)tukapit katika mti ule tukasema :Ewe mtume wa Allah na sisi tuwekee mti wa kutafutia Baraka kama wao walivyo na mti wa kutafutia Baraka.Akasema mtume wa Allah(Rehma na Amani ziwe juu yake) Allahu Akbar (Mwenyezi Mungu mkubwa) hakika ni jambo mmelisema naapa kwa Yule nafsi yangu ipo mikononi mwake ni kama walivyo sema banu israil kumwambia mussa(jaalia kwetu sisi mungu kama walivyo kuwa wao na Allah akasema : nyinyo ni watu wajinga Na mtafata mienendo ya walio kuwa kabla yenu .Imepokelewa na tirmidhi

***(Je mmemuona Lata na Uzza ?)** niambieni jambo la hayo masanamu mnayo ya tukuza na ipi hali ya hayo masanamu kwa kunasibiana na hili aya tukufu kama katika kisa cha miiraji hakika wao wanaitakidi ya kwamba hayo masanamu yanawanufaisha na yanawadhuru na kwa sababu hiyo wanayaendea na wanayaomba na wanachinja kwa ajili ya hayo masanamu na wanajikurubisha kwayo

*(Allaat)Inasomwa kwa kuwekea mkazo (te)alikuwa ni mtu mwema alikuwa akiandaa uji kwa mahujaji (kipndi cha hijja)

2.inasomwa kwa kukhafifisha:imenyambulisha katika majina ya Allah jina la hili sanamu na wakaliita Lata.

*(AL-UZA) linatokan na jina la Allah ambalo ni (AL-AZIZI)

*(Manatah):linatokan na jina la Allah (mannani)linatokana na kudhihirisha kutunuku

*(WAGENI):hawana muda mrefu kutoka kwwenye ukafiri wakasema hivyo kuweka udhuru kwa kutafuta kuuliza kwao.

*(WAKITUNDIKA)wakitundika silaha zao na mapanga yao kwa kutafuta Baraka.

*(MTI WA KUTUNDIKIA SILAHA): Kwa sababu huo mti zinatundikwa silaha kwa kutegemea bararaka zake

*(TUWEKEE MTI WA KUTUNDIKIA SILAHA KAMA WAO): jaalia kwetu sisi mti wa kutaka Baraka kama wao walivyo na mti wa kutafutia baraka:wamejua kuwa ibada .ni lazima kwao kupata idhini na kwa hilo walitaka idhini na kwa mitume(S.A.W)likawa jambo hilo zitokwao na wala hawa kuingia katika shiriki hiyo.

(Latar kabunna);Mtafata:Mtafanya kama walivyo fanya na mtasoma kama walivyo sema na kuna habari na uonyaji.

MAS-ALA MBALI MBALI

Ya kwanza:tafsisiri ya aya katika suratul nnajim(je mmemuona lata na uza)na manata ambaye ni mungu wenu wa tatu na wa mwisho)
Ya pili: Ni kujua picha au sura ya jambo ambalo walilolitafuta(kuwa ajili ya kuwakasirisha sio kuabudiwa)

Ya tatu: ya kwamba wao hawaja fanya jambo hili .

Yan nne:ya kwamba wao walikusudia kujikurubisha kwa Allah katika jambo hili ;kwa dhana zao ya kwamba anapenda jambo hilo

Ya tano:ya kwamba wao hawajui jambo hili;na wengine ni zaidi ya kutojua(hatudanganyiki na matengo ya watu)

Ya sita; na kwamba wao wana mema na wame ahidiwa kusamehewa jambo ambalo halipokuwa kwa wengine(usiwataje isipokua kwa kitu kizuri kwa sababu kuwatukana wanachuoni ni kumtukana Allah na dini yake na mtume wake na kuwatukana wao)

Ya saba;ya kwamba mtume muhammadi (s..a.w) hakuwapa udhuru isopokuwa alirudisha kwao kwa kauli yake(Allah Akbar hakika huu ni mwenendo mtafata miendendo ya walio kuwa kabla yanu)

Ya nane;jambo kubwa linalo kusudiwa ya kwamba yeye Mtume ame khabarisha ombi lao kuwa nikama ombi la bani lsraail pale walipo mwambia musa(jaalia kwetu sisi Mungu)(na katika jambo hilo kuna katazo la kujifananisha na washirikina katika matamko)

Ya tisa; Ni kwamba **(LAAILAHA ILLALLAH)**na pamoja na undani wa maana (ni shahada inakanusha kuabudiwa kila mungu kinyume na Allah na hivyo baraka haiji kinyume na Allah)

Ya kumi;ya kwamba yeye mtume ameapa katika fatuwa nay eye haapi isipokua katika maslahi (au kuondoa jambo baya)

Ya kumi na moja : yakwamba katika shirki kuna kubwa na ndogo;kwa hivyo wao hawakuritadi (kujitoa katika uislamu)

Ya kumi na mbili: kauli ya maswahaba (na sisi tungali wageni ndani ya uislamu)maana yake ni kwamba wasio kuwa hao wanalifahamu(kwa hivyo wanapewa udhuru kutokuja kwako kwa sababu ya ugeni wao katika uislam

Ya kumi na tatu: kutoa takbira wakati wa kustaajabu kinyume na walilo lichukia hilo

Ya kumi na nne: kuziba mianya (nazo ni njia zinazo mfikisha mtu katika jambo)na mianya ipo aina mbili mianya inayo mfikisha mtu sehemu inayo takiwa hii huzibwa bali inafunguliwa na ina tafutwa,mianya inayo pelekea mtu katika mambo mabaya .hii haizibwi na ndio makusudio ya mtunzi

Ya kumi na tano: katazo la kujifananisha na watu wa jaahilia(siyo uislam na uliyo kuwa kabla ya utume tu bali kwa kila asiyejua haki na akafanya matendo ya kijahili huyo ni miongoni mwa majahili

Ya kumi na sita: kukasilika unapo fundisha

Ya kumi na saba: kanuni ya ujumla kwa kauli yake(hakika hiyo ni suna)(na hii ni kwa ajili ya tahadhari)

Ya kumi na nane: ya kwamba hii ni alama miongoni mwa alama za mitume kwa sababu imekuwa kama ilivyosemwa

Ya kumi na tisa; kila alichokipa Allah sifa mbaya kwa manaswara na mayahudi kuna sifa mbaya kwet

Ya ishirin: Ya kwamba wao wamekiri kuwa ibada asili yake imegawanyika katika amri ikawa katika amri hiyo ni tanbihi kunako maswali ya kaburini Ama swali (nani mtume wako)ni katika kukhabarisha kunako khabari za ghaibu na ama swali(ni ipi dini yako)ni kutokana na neno lao bani israil(ewe mussa tufanyie waungu sisi kama wao walivyo na miungu)mpaka mwisho wa aya.

Ya ishirini na moja; Ya kwamba mwenendo wa walio pewa kitabu(Mayahudi na Manaswara) ni wenye kupondwa na kuchukiza kama mwenendo wa washirikina.

Ya ishirini na mbili; ya kwamba yeyote anaehama kutoka katika batiri aliyoizoea katika moyo wake huaminiwa ya kwamba moyo wake umesalimika na mabaki ya batiri aliyokua ameyazoea ;kwa kauli yake (sisi tungali wageni wa uislamu)(na hili likawa ni katika hekima kumuondoa mzinifu baada ya kumsimamishia viboko mia moja katika sehemu aliyo fanyia zinaa ili asiweze kurudia kitedo hicho.Na mwana damu anapaswa ajiweke mbali na sehemu za ukafiri,ushirikina,na uovu na pia ahlsunna ni kuchukua elimu kutoka kwa wanazuoni wao wachamungu na kwamba yeyote mwenye kurejea katika sunna na alikua katika upotevu hakichukuliwi kurejejea kwake wala kuwa ni hoja mpaka washuhudie wamtolee ushahidi wanachuoni) kuwa kutakasika kwake na kuondokana na upotevu aliokuwa nao .

10.MLANGO ULIOKUJA KUELEZEA KUCHINJA KWA ASIE KUWA ALLAH

Kwa nini mtunzi amesema (mlango uliokuja kuelezea) na hajasem;(ni katika shirki kubwa kuchinja kwa asiye kuwa Allah

1/Ametaja kumzoesha mwanafunzi kutoa hukumu ndani ya dalili na hiyo ni katika mbinu za kielimu za ufundishaji.

2/au kwa sababu kuchinja kwa asiye kuwa Allah kunagawanyika katika vigawanyo viwili navyo ni kuchinja kunakofaa na kuchinja kusikofaa na ni shirki kubwa

DALILI YA KWANZA NA YA PILI

1. 1/Kauli yake Allah (sema hakika swala yangu na ibada zangu zote nyingine na uzima wangu na kufa kwangu zote ni kwa Allah muumba wa walimwengu wote (162)hana mshirika yeye
2. Kauli yake; (Basi Sali kwa ajili mola wako)

*(SEMA) kuwaambia hao washirikina ukiwatangazia msimamo wako katika tawhid ya kweli

*(SWALAATI) matendo yangu ya kimwili na katika bora ya matendo ya kimwili ni swala sawa iwe ya faradhi au ya suna

*(WANUSUKII); vichinjwa vyangu ,matendo yangu ya kimali na miongoni mwa matendo bora ya kamwili ni kuchinja kwa ajili ya Allah .

*(KIFO NA UHAI WANGU); kufanya na kuwendesha mambo yangu nikiwa hai au nimekufa ni kwa Allah

*(MUISLAMU WA KWANZA)1/mim ni muislamu wa kwanza katika umma huu.2/mim ni mkamilifu katika uislamu miongoni mwa watu wote.

*(KUCHINJA) vifanye vichijwa vyako ni kwa ajila ya Allah kama zilivyo swala zako ni kwa ajili yake na kuchinja ni kwa ajili yake.

VIGAWANYO VYA KUCHINJA

- Kuchinja kwa ajili ya Allah,kama vile wanyama wanao chinjwa na hakika kuvielekeza kwa asiyekuwa Allah ni shirki kubwa
- Kuchinja kunako faa kama vile nyama ya mbuzi na biashara na kumkirimu mgeni
- Kuchinja kwa mapenzi na kutukuza kwa asiye kuwa Allah (Ni shiriki kubwa) kama vile kuchinja kwa ajili ya watu , makaburini na majini.

DALILI YA TATU

Kutoka kwa Aliy ibn Abii Twalib radhiyallahu anhu amesema;Alinihadithia mtume (s.a.w)kwa maneno manne(Amemlaani Allah yeyote atakae chinja kinyume na Allah)Allah amemlaa mwenye kuwalaani wazazi wake , Allah amemlaani mwenye kumuhifadhi mzushi Allah ame mlaana kila mwenye kubadilisha mipaka ya Ardhi)
Hadithi hii imepokelewa na Muslim.

*Laana)laana kutoka kwa Allah ni kufukuzwa mbali na rehema ya Allah.Inawezekena kwamba mtume(s.a.w)ana eleza kuwa Allah ame mlaaani mwenye kuchinja kinyume na Allah .Au ikawa anaomba dua (Ewe Allah mlaani kila mwenye kuchinja kinyume cha Allah)

DALILI YA NNE

Na kutoka kwa Twariq ibn Shihab hakika mtume (s.a.w)Amesema (Aliingia mtu pepeno kwa sababu ya nzi.Na akaingia mtu motoni kwa sababu ya nzi)wakasema maswahaba,Na ni vipi ewe mtume wa Allah?Akasema (walipita watu wawili katika qaumu ya watu ambao wana sanamu havuki yeyote sehemu hiyo mpaka atoe chochote kwa ajili ya masanamu .Wakasema kumwambia mmoja kati yao toa : akasema sina chochote cha kutoa .Wakamwambia toa japo kwa kuchinja nzi.Akachinja nzi wakamuacha akaendaa zake akaingia motoni wakasema kumwambia mwingine toa , akasema sina cha kutoa chochote zaidi ya kumtegemea Allah , basi wakamkata shingo yake akaingia peponi)Hadithi hii imepokelewa na imamu Ahmad

(Katika nzi) makusudio ya neno hilo katika hadithi ni kwa sababu ya nzi

MAS-ALA MBALI MBALI

1. Tafsiri ya kauli yake Allah(sema hakika sala yangu na ibada yangu)
2. Tafsiri ya kauli yake Allah (Sali kwa ajili ya mola wako na uchinje kwa ajili ya mola wako)
3. Kwanza kulaaniwa mwenye kuchinja kinyume na Allah (kwa sababu hio ni shirki na haki ya Allah mtukufu ndio haki kubwa kuliko zingine)
4. Laana kwa mwenye kuwalaani wazazi wake.Na katika laana ni kulaani mtu wazazi wa mtu na yeye akalaani wazazi wake (kwa sababu ndio sehemu ya mwenye kuleta moja kwa moja au aka walaani wazazi wake moja kwa moja.
5. Laana kwa mwenye kuzua.Nae ni mtu mwenyekuzua.nae ni mtu mwenye kuzua jambo ambalo lina wajibu wa haki ya Allah kasha akataka msaada kwa Yule atakaemuhifadhi kutokana na hilo jambo. na mwenye kuwanusuru ndiye mbaya zaid kuliko Yule mwenye kuwahami .

Kwa Yule anaemuelekea kwa hilo (na mwenye kumnusuru ndio zaid na mkubwa tofauti na mwenye kuhami na kuzusha kunakua katika aina mbili :-

- ;katika dini kama upotofu walio uzusha kundi la Jahamiya , Muutazilah , Raafidwa na wengineo.
- ;Katika mambo ya umma kama kufanya makosa ya jinai na mfano wale wanaosaidia wezi kuiba na vibaka wanao kaba njiani.

6/Kulaaniwa kwa Yule mwenye kubadili mipaka ya ardhi nayo ni mipaka inayo tenganisha kati ya mipaka yako na ya jirani yako katika ardhi ukaibadilisha kwa kutanguliza au kuchelewesha.

7/Tofauti kati ya kumlaani mtu maalum na watu wenye kufanya maasi kiujumla (ya kwanza imekatazwa , ya pili inajuzu. Ama kulaani mtu maalum haifai juu yako umlaani.Na asili ya hilo kutofaa kutamka laana)

8Hichi ni kisa kitakatifu nacho ni kisa cha inzi(ni juu ya kauli zenye ukweli ndani yake.)

9/Kuingia kwake motoni kwasababu ya Yule nzi ambae hakumsaidia isipo kuwa alifanya kujiokoa na shari zao (kwasababu ya kulazimishwa haikua ni udhuru wenye kukubalika katika umma zilizotangangulia .)

10/Kujua kiwango cha shiriki katika nyoyo za waumini vipi alisubiri kwa hilo juu ya kuuliwa juu ya kile walichotaka na hakukubaliana nao pamoja na kuwa walimtaka afanye matendo ya wazi (kuua nzi) ikiwa kuwfikiana nao na kutokuwa na subira na madhara kwa uislamu , basi ni lazima kuvumilia .

11/Hakika ya Yule alie ingia motoni ni muislamu kwasababu yeye laity angelikua kafiri(angesema(ameingia motoni kwa sababu ya nzi)Basi ikawa kule kujikurubisha kwake ni sababu ya kuingia motoni

12/Ndani yake kuna ushahidi juu ya hadithi sahihi;pepo ipo karib kati ya mmoja wenu zaidi ya mkanda wa ndala yake anayoivaa na moto pia vilevile (lengo la hii hdithi ni kuwafanya watu wapende , pia waogope)

13/Kutambua ya kwamba hakika ya matendo ya moyoni ndio yanayo kusudiwa mpaka kwa wenye kuabudu masanamu (Na dawa ya moyo ni Qur-an basi usishughulishe moyo wako na dunia)

JE NI BORA KWA MWANADAMU ATAKAPO LAZIMISHWA KATIKA UKAFIRI AFANYE SUBRA HATA AKIUWAWA AU AKUBALIANE KWA NJE NA AITAFSIRI NIA YAKE ?

1/Akubaliane kwa wazi na kujificha nahii haifai kwa sababu anakua ametoka katika uislamu .

2/Akubaliane kwa wazi na sio kwa kujificha lakini akusaidie kujiokoa kwa huko kulazimishwa hii inafaa.

3/Asikubali kwa wazi wala kujificha na kasha akauwawa na hii inafaa.Nayo ni katika subra huyu akiwa amekubaliana na na kule kulazimishwa inafungamana juu yake na madhara katika jamii na katika dini kiujumla basi akubali kwa wazi na sio kwenye moyo wake. .

(11) MLAANGO ULIO KUJA KUELEZEA HAIFAI KUCHINJA KWA AJILI YA ALLAH KATIKA SEHEMU PANAPO CHINJWA KWA ASIYEKUWA ALLAH

- Uhamaji huu wa mtunzi kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine ni katika uhamaji ulio bora ;kwani baada ya kuwa ametaja kuhusu kuchinja kwa asiye kuwa Allah.Amefanikisha kutaja kutojuzu kuchinga katika sehemu panapo chinjwa kwa asiye kuwa Allah kama vile anaetaka kuchinja kichinjo cha Iddy (UDHW-HIYA) kwa ajili ya Allah katika sehemu panapo chinjwa kwa ajili ya masanamu na hekima katika hilo ni hayo yafuatayo.
    - Ya kwamba kitendo hicho kinapelekea kujifananisha na makafiri
    - Ya kwamba inapelekea kupumbazika kwa muumin kitendo hicho na aka dhania ni kitendo cha ushirikina kinafaa
    - Ya kwamba washirikina watapewa nguvu katika matendo na hili jambo ni haramu na inatakiwa tuwachukie

DALILI YA KWANZA.

Kauli yake Allah (usisimame msikitini humo milele)

SABABU YA MTUNZI KULETA AYA HII

- Pindi ulipokuwa msikiti wa madhara ni katika msikiti uliojengwa kwa ajili ya kumuasi Allah na kuwapa maudhi waumini na kuwapa nguvu makafiri na mahala pa kuwangoja wale wanaompiga vita Allah na mtume wake na kuleta mfarakano baina ya waumini Allah akamkataza mtume kusimama ndani ya msikiti huo pamoja ya kwamba swala yake anayosali ni kwa ajili ya Allah, kwa hiyo ikajulisha ya kwamba anapo asiwa Allah ndani yake haipaswi kusimama sehemu hiyo hata baada ya maasi kuondoshwa ndani yake, swala ni ibada na kuchinja ni ibada.Na dalili inayo kalibiana na hiyo ni katazo la kuswali wakati wa kuzama jua na wakati wa kuchomoza jua kwa sababu hizo ni nyakati mbili za makafiri kulisujudia jua na hili ni kuzingatia mda na wakati na hadithi imeeleza kwa kuzingatia wakati

DALILI YA PILI

Hadithi kutoka kwa Thabiti ibn Dhwahak ,Amesema ;mtu mmoja aliweka nadhiria ya kuchinja ngamia akifika sehemu inayoitwa BUWAANAT . mtume (s.a.w)akauliza na kusema (Je katika sehemu hiyo kulikua na masanamu ya kuabudia kabla ya uislamu) wakajibu Hapana ,mtume akasema (Na je katika sehemu hiyo kulikua na Iddy miongoni mwa Iddy za washirikina) Wakajibu ,Hapana ,mtume(s.a.w)akasema (Tekeleza nadhiri yako au lipa nadhiri yako kwani hakika hakuna kutekeleza nadhiri katika kumuasi Allah wala katika kitu asicho kimiliki mwanadamu))Imepokelewa na Abu daaud

NADHIRI KILUGHA: NI AHADI YA KUJILAZIMISHA .

AMA KISHERIA : NI MTU ALIYEBALGHE AKIJILAZIMISHA KUFANYA JAMBO FULANI AMBALO SI WAJIBU KULIFANYA .

Kumuwekea nadhiri Allah

Nadhiri kwa asiue kuwa Allah (shirki kubwa kama vile kuapa kwa asiye kuwa Allah tu Haielekezwi(yaani haitolewi kafara na inatakiwa tauba kwa aliye nadhiria)

Nadhiri maalum mfano kunadhiria kufanya jambo maalum.

Nadhiri ya wote : huingia katika nadhiri hii kila muislamu . kwa hiyo yafaa muislamu kundhiria kufanya maamrisho na kuacha makatazo

Baada ya kutamka nadhiri inatakiwainatakiwa itekelezwe au kutoa kafar ya kiapo kafara

Kabla ya kutamka : hukumu yake ni haramu kwani mtume rehmana Amani ziwe juu yake amekataa , na kama ingelikuwa ni kheri basi Mtume nae angelinadhiria

Utifu;Ni wajibu kutekeleza na akiacha ni wajibu kwake kutoa kafara , mfano (alinadhiria kswali sunna)

Maasi;Ni haramu kutekeleza ,na wajibu kuivuja nadhiri hiyo na kutoa kafara mfano;(kunadhiria kufanya jambo la haramu kama vile kusengenya .)

(Jambo la halali);Atakhiyarishwa kati ya kutekeleza au kuacha au kuvunja nadhiri yake na kutoa kafara mfano (kunadhiria kuvaa nguo hii)

(kung'anga'nizwa na Ghadhabu) hukumu yake ni kama nadhiri ya halali na hukusuciwa kwa nadhiri hiyo maana ya kiapomfano (kunadhiria kuhama mji)

Chukizo : Ni karaha kuitekeleza na sunna kuivunja na kutoa kafara mfano (kugeuka geuka ndani ya swala)

(Isiyofungamana na chochote) ni ile ambayo muhusika hakutaja kitu chochote ndani yake . akatoa kafara (mfano,akasema naweka nadhiri kwa ajili ya Allah kasha akakaa kimyaastioe kitu alichonadhiria)

- Mtu akinadhiria kwa ajili ya Allah hakika itafungamana na kuswihi imma aitekeleze au aivunje na kutoa kafara juu yake .
- Ikiwa si kwa ajili ya Allah mtukufu haifungamani wala kukubalika) hatoitekeleza na wala kutoa kafara na inatakiwa kutubia (shirki kubwa)

MAS-ALA

Jambo la kwanza :Tafsiri ya kauli ya Allah " Usisimame kwenye msikiti huo kabisa "

Jambo la pili . Hakika maasi yanaweza kuathiri Ardhi na vile vile utiifu . " pindi ilipokuwa ardhi hii ni sehemu ya shirki akaharamishiwa mwanadamu kufanya vitendo vinavyo fanana na shirki ndani yake kwa sababu ya kujifananisha na washirikina "

Jambo la tatu . kurejesha maswala yenye kutatiza kwa kuleta yasiyo tatiza ili kundoa tatizo.

Jambo la nne : kuomba ufafanuzi kwa mtoa fat-wa , ikihitajika kufanya hivyo au (atoe ufafanuzi kwenye jawabu .)

Jambo la tano: kuhusisha sehemu maalum katika kufanya si vibaya kama hakuna viziwizi (lakini kama itahofiwa watu wataitakidi kwamba mahala hapo kuna utukufu fulani basi itakuwa haifai)

Jambo la sita :itazuiliwa ikiwa mahala hapo kuna sanamu au mzimu katika mizimu ya kijahiliya hata kama mizimu au masanamu hayo yaliondolewa mahala hapo

Jambo la saba : itaazuiliwa ikiwa hapo kuna sikukuu katika sikukuu zao , hata kama ziliondoshwa .

Jambo la nane : Ni kwamba haifai kutekeleza kilicho nadhiriwa mahala hapo , kwani hiyo ni nadhiri ya maasi .

Jambo la tisa : kutahadharishwa katika kujifananisha na makafiri kwenye sikukuu zao hata kama hutokusudia kujifananisha nao (ameleza sheikh l-islam Ibn Taimiya ya kwamba : ktika kupatikana mafanano hapasharti makusudio , lakini ikiwa pamekusudiwa basi madhambi yake ni makubwa zaidi .
Jambo la kumi : Haifai kunadhiria katika maasi (kwa maana hufungamana na nadhiri , lakini haitekelezwi)

Jambo la kumi na moja : Mwanaadamu haruhusiwi kunadhiria kitu asichokimiliki (kwa maana hatotekeleza) na asivyovimiki vipo aina mbili :- 1- kisheria kama lau atasema : naweka nadhiri kwa Allah nikimuacha huru mtumwa wa Fulani . nadhiri hii haii\sihi kwa sababu yeyey hamiliki mtumwa huyo .

2- kwa kukadiria kama lau atasema : " naweka nadhiri kwa Allah kuwa ntapaa kwa mikono yangu basi nadhiri hii haisihi , kwani yeye hamiliki kufanya hivyo .

KAFARA YA NADHIRI YA ALLAH KAMA KAFARA YA KIAPO .

- Kama mtu atakhiyarishwa kati ya kumuacha huru mtu mtumwa muislamu , au kulisha masikini kumi .
- Kama hakumpata atahamia katika kufunga siku tatu mfululizo .

(12) MLANGO MIONGONI MWASHIRIKI KUNADHIRIA KWA ASIYE KUWA ALLAH.

DALILI YA KWANZA NA YA PILI

- Kauli yako Allah ;wanaiekeza nadhiri.
- Kauli yake ;Na chochote mtakacho au nadhiri muwezavyo Alah anajua

Munasaba wa aya mbili katika mlango huu ya kwamba nadhiri ni miongini mwa sababu zinazo ingiza wema peponi nayo ni ibada ika hukumumiwa ya kwamba kuieuza kwa asiye Allah ni shiriki ni ibada vilevile kufungamanisha kitu kwa ajili ya Allah nakuhitajia malipo.

DALILI YA TATU

Na sahihi kujitoa kutoka Aisha Allah Amuwe radhi ,Hakika mtume rehma na amani ziwe juu yake ;Atakae nadharia kumtii Allah na Amtii na atakae nadhiri kumuasi basi asimuasi.

TOFAUTI KATI YA KUMTII ALLAH,KUMUASI ALLAH NA KUNADHRIA KWA ASIYE KUWA ALLAH

NADHIRI YA KUMTII ALLAH

Kama vile kuapa kwa jina la Allah.
Inatuka (inatekelezwa au kutolewa kafara inalazimu kuelekezwa

NADHIRI YA KUMUASI ALLAH

Kama vile kuapa kwa jina la Allah na imefungamana na kutekelez kafara na in haramusha kuelekeza

NADHIRI KWA ASIYE KUWA ALLAH

Kama vile kuapa kwa asiye kuwa Allah na haifungamanishwi na chochote ina paswa kutubiwa na ni shirki kubwa

MAS-ALA

- ✓ Ya kwanza;Ulazima wa kutoleta nadhiri (nadhirin ya kutii kama vie kumtii Allah)
- ✓ Ya pili;ikisha thiniti kuwa ni ibada kwa ajili ya Allah basi kuitekeleza kwa asiye kuwa Allah
- ✓ Ya tatu;ya kwamba nadhiri ya maasi haijuzu kuitekeleza na inatakiwakafara ya kiapo yaani kufunga siku tatu)

MAZINGATIO

- Nadhiri na kiapo hukumu zake zinakaribiana na kwa hivyo wamevikusanya ndani mlango wa viapo na nadhiri

(13) MLANGO UNAOZUNGUMZIA NI KATIKA SHIRKI KUTAKA KINGA KWA ASIE KUWA ALLAH. (KATIKA YALE ASIYOYAWEZA ISIPOKUWA ALLAH)

DALILI YA KWANZA.

Na kauli ya Allah mtukufu: (Na hakika kulikuwa na wanaume miongoni mwa wanadamu wakijikinga kwa wanaume miongoni mwa majini kwa hivyo wanawazidishia madhambi)

- (yauudhuuna) wanajikinga.
- (fazaaduuhum rahaqaa): uoga ndani ya nyoyo na madhambi na kujikinga kwa asiekua Allah hakumfidishi mwenye kujikinga, bali kunamzidishia upuuzi na madhambi, Nayo ni shirki kubwa, na kwa hilo akaadhibiwa kwa ubatilifu wa nia yake na makusudio.

DALILI YA PILI.

Hadithi kutoka kwa Khawla binti hakim (Allah amridhie) amesema: Nilimsikia mtume (s.a.w) akisema: (atakae fika sehemu kisha akasema: ninajikinga (auudhu) kwa maneno ya Allah timilifu kutokana na shari ya alivyoviumba), hakitomdhuru chochote mpaka aondoke katika sehemu hiyo.(kaipokea muslim.)

- **(Manzila):** Inajumuisha mafikio ya kudumu ya mkaazi au msafiri mfano katika jahazi na mpita njia.
- **(Auudhu):** Najilinda na kujikinga (Bikalimaati llahi) kwa maneno ya Allah ya kilimwengu na kisheria.
- **(YALIYOKAMILIKA):** [1] Ya ukweli katika khabari [2] Ya uadilifu katika hukmu.
- **(KUTOKANA NA SHARI ALIZOZIUMBA):** shari hainasibishwi kwake Allah, kwa sababu yeye ameiumba shari kwa hekima, vigawanyo vya viumbe:
  [1] vyenye kheri endelevu: kama pepo na mitume na malaika
  [2] vyenye shari endelevu: kama moto na ibilisi kwa kuzingatia kidhati yake, ama hekima ya kuumbwa kwavyo ni kheri.
  [3] vyenye shari na kheri pamoja: kama binadamu,majini, na wanyama.
- (HAKITOMDHURU CHOCHOTE): haya ni maelezo ambayo hayawezi kwenda kinyume na alieisema, kwa sababu ni maneno ya mkweli mwenye kusadikishwa, lakini ikiwa ni kinyume na hivyo, basi itakuwa kwa kupatikana kizuizi, sio kwa upungufu wa sababu au kukiukwa kwa maneno hayo, kwa mfano, kumsomea mgonjwa suratul-fatiha ni tiba na ponyo, lakini baadhi ya watu wanawasomea wagonjwa na hawaponi.

MAS-ALA. MBALI MBALI

Ya kwanza: Tafsiri ya aya katika suratul jinni (Na hakika walikuwa wanaume miongoni mwa wanadam wakijikinga kwa wanaume miongoni mwa majini kwa hivyo wakawazidishia dhambi).

Ya pili: kua kwake ni shirki kubwa (yaani kujikinga kwa asiyekuwa Allah kwa yale asiyoyaweza asie kua Allah)

Ya tatu: Kutoa ushahidi katika hilo kwa kutumia hadithi, kwa sababu wanazuoni wanatoa ushahidi kwa kutumia hadithi hii ya kwamba maneno ya Allah sio kiumbe yaani hayajaumbwa katika jambo kama hili, na kama yangekua ni kiumbe asingeelekeza mtume (s.a.w) kujikinga kupitia maneno hayo)

Ya nne: Fadhila na ubora wa dua hii pamoja na ufupi wake (Hakikudhuru chochote maadamu upo sehem hiyo).

Ya tano: ya kwamba kua kwa kitu kinaleta manufaa ya kidunia, kwa kuzuwia shari au kuleta manufaahaijulishi kuwa kitu hicho sio shirki kwani kupata manufaa hakubatilishi kuwepo shirki katika kitu hicho).

FAIDA NYINGINEZO.

Katika hadithi: ya kwamba sheria haibatilishi jambo katika mambo ya jaahiliyyah (Enzi kabla ya uislam) isipokua inaleta lililobora zaidi, miongoni mwa hayo kwamba katika jaahiliyah walikuwa wakijikinga kwa majini, sheria ikabadilisha kitendo hicho kwa kuleta maneno haya.

Na hii ndio njia salama na sahihi anayotakiwa aipitie mlinganiaji, ya kwamba anapowafungia watu mlango wa shari ni wajibu kwake kuwafungulia mlango wa kheri na jambo hili lina mifano mingi katika kitabu na sunna.

14: MLANGO NI KATIKA SHIRKI KUTAKA MSAADA KWA ASIYE KUWA ALLAH AU KUMUOMBA ASIYE KUWA ALLAH

1. Na kauli yake Allah mtukufu (Na wala usiwaabudu badala ya Mwenyezimungu wale ambao hawakufai wala hawakudhuru basi ukifanya utakuwa miongoni mwa madhalimu (106) Na kama Mwenyezimungu akikugusisha dhara basi hakuna yeyote awezaye kuliondoa isipokuwa Allah mwenyewe
2. Na kauli yake (tufuteni riziki kwa Mwenyezimungu na mumuabudu)
3. Na kauli yake (Na wapotofu wakubwa ni kina nani kuliko wale wanao waomba asiye kuwa Mwenyezimungu ambao hawata wajibu mpaka siku ya kiama) aya mbili.
4. Na kauli yake Allah (Au Ni nani Yule anaemjibu aliyekuwa na dhiki amuombapo na kuondoa dhiki yake)
5. Na amepokea Twabaraniy kwa sanadi yake ya kwamba alikuwapo katika zama za mtume (s.a.w) mnafiki ambae anawaudhi waumini.
   Wakasema baadhi yako: simameni na sisi tutake msaada kwa mtume (s.a.w) kwa huyu mnafiki akasema mtume (s.a.w) ya kwamba yeye hatakiwi kuomba msaada kwangu na hakika anaombwa msaada Allah mwenye nguvu na mtukufu.

- WALA USIOMBE: Dua ya ibada na maombi mengine kile ambacho hakuna mwenye uwezo nacho isipokuwa muombe Allah tu .
- MBELE YA ALLAH: Pametangulizwa kitu ambacho hiki yake ni kuchelewa, ili ipatikane HASRI (husisho) kwa maana tafuteni riziki kutoka kwa Allah tu na siyo kwa mwingine asiye kuwa Allah, basi wao wanawaabudu hayo masanamu na hali ya kwamba hawana uwezo wa kumiliki riziki milele.
- MAUMBUDUNI YEYE: Ishara ya kwamba kudumisha ibada ni katika kutafuta riziki na sababu zake.
- MSHUKURUNI YEYE: Hii kwa sababu ya neema ni mtihani na inahitaji kushukuru katika moyo na ulimi na viungo.
- ANAJIBU: Hataki kwa mtu yeyote amuondoshee dhiki zake na amuondoshee mabaya yake naye akiwa hawezi.
- MUNAAFIQ: Mnafiki ni Yule ambaye anadhihirisha uislamu na anaficha ukafiri na kuudhi watu ndiyo kawaida yake.

VIGAWANYO VYA RIZIKI

- Kiujumla: kila kiumbe anayo ima iwe halali au haramu
- Maalum kwa waumini: Nayo ni imani na uchamungu na matendo mema.

MAS-ALA MBALI MBALI

1. Hakika kuinganisha dua kutika kutaka msaada ni miongoni mwa kuunganisha chenye kuenea katika kitu.
2. Tafsiir kauli yake (Na wala usiwaabudu badala ya Mwenyezimungu wale ambao hawakunufaishi wala hawakudhuru)
3. Hakika ya hili ni katika shirki kubwa.
4. Hakika mzuri katika watu laiti angefanya ili aridhie mtu mwingine itakuwa katika wale walio dhulumu nafsi zao (Na makatazo yameelekeza Yule ambae hawezi kudhihirisha hilo kwa kuzingatia hali yake itakuwa kwa Yule mwenye kuweza ni katika milango iliyokuwa bora.
5. Tafsiri ya aya iliyokuja baada yake (Na kama Mwenyezimungu akikugusisha dhara basi hakuna yeyote awezae kuondoa isipokuwa Allah mwenyewe) ikiwa sasa akuna awezae kuondoa madhara isipokuwa Allah ni wajibu ibada iwe yak wake yeye na kumtaka msaada yeye pekee.
6. Kuwa hivyo hainufaishi katika dunia pamoja na kuwa hivyo ni ukafiri (atapata khasara katika dunia na akhera)
7. Tafsiri ya aya ya tatu (tafuteni riziki kwake yeye Allah na Mumuabudu)
8. Hakika ya kutafuta riziki haifai isipokuwa kwake Allah. Kama ilivyo pepo haiombwi isipokuwa kwake Allah.
9. Tafsiri ya aya ya nane (Na wapotofu wakubwa ni kina nani kuliko wale wanao waomba asiye kuwa Allah)
10. Hakika kuna upotevu kwa Yule atakae omba kwa asiye kuwa Allah (kwa sababu ya kiulizo cha kukanusha)
11. Mwenye kughafilika kutokana na maombi ya muombaji , hata mfahamu amuombaye .
12. Hakika ya yale maombi ni sababu ya kuchukiwa muombaji na Yule anaemuomba na kumfanyia uadui.
13. Kuita yale maombi ni ibada kwa anayeomba.
14. Anakuwa kafiri Yule anaeombawa kwa hizo ibada (kumrejesha na kumpinga)
15. Hiyo ndiyo sababu ya kuwapoteza watu (1) kwa sababu yeye anaomba kwa Yule asiyeweza kumjibu (2) kwamba wenye kuombwa wamejisahau katika maombi hayo (3) hakika yeye ni amekufuru katika ibada zake.
16. Tafsir ya aya ya tano: (au nani yule anaemjibu aliye na dhiki anapo anapomuomba)
17. Jambo la kushangaza: Nalo ni kukubali wenye kuabudu masanamu ya kwamba wao hawawezi kuwajibu dua zao isipokuwa Allah. Na kwa sababu hii wanamuomba katika shida wakiwa ni wenye kumtakasia dini yake.
18. Kulinda kwake mtume wetu (s.a.w) kwa kuihami na kuitetea Tawhid na kua na adabu kwa Allah (basi yeye anaufundisha umma kukimbilia na kuelekea kwa Allah peke yake katika shida na wala asitake mtu msaada isipokuwa kwake yeye Allah pekee

(15) MTIHANI WA KIGAWANYO CHA PILI (MILANGO -9)

SWALI LA KWANZA:

Taja tofauti kati ya aina za nadhiri zinazokuja :-

Nadhiri ya kutii Nadhir ya maasi Nadhiri kwa asiyekuwa Allah.

_____ _____ _____
_____ _____ _____
_____ _____ _____

SWALI LA PILI :

Bainisha hukumu za matendo yafuatayo kwa kuchagua namba yenye kunasibiana katika kila kazi :-

1) Inajuzu 2) lenye kuchukiza 3) Ndogo 4) kubwa 5) Shirki ndogo 6) Shirki kubwa 7) ndani yake kuna ufafanuzi 8) wajibu 9) Inapendeza.

Mapenzi kwa mke_____. Mapenzi kwa mtume (Rehma na amani ziwe juu yake)_____ . Mapenzi kwa Allah _____ . Shaka katika kukufuru kwa watu wa kitabu _____ .khofu Mas-hafu huondoa kijicho _____. Dua kwa ambaye ameshikamana na vifundo _____kwakitu

Kulaani mtu maalum _____. Pete ya uchumba _____. Kujifuta katika chumba cha mtume _____

Kujisafisha kwa kutumia vinyesi na mifupa _____. Kuihusisha sehemu ya kufanyia Nadhiri _____

Kutaka Baraka kwa kusoma Qur-ani_____. Kuhudhuria sikukuu za makafiri _____ ___. Kutaka msaada kwa viumbe _____. Khofu kutokana na majini _____

Kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Allah. _____ . Kunig'iniza Aya za Qur-ani _____

Ahadi ya muasi _____. Hirizi kutokana na Qur-ani kuuambatanisha kamba au ndala _____ . Kufanya Ruqya pasipo kutumia lugha ya kiarabu _____.

Kushika jiwe jeusi _____. Kunywa maji ya zam zam kwa ajili ya tiba_____. Kufahamu sehemu ya msikiti wenye madhara _____.

Kusema tunaomba mvua kwa kutumia mtume wa Allah (Rehma na amani ziwe juu yake)_____

Kutaja majina ya Allah kwa lugha isiyo ya kiarabu _____

Kuharibu mali kwa maslahi _____

Kuvaa kamba kwa ajili yap ambo _____ kuning'iniza kitambaa au kitu _____

SWALI LA TATU

Weka alama ya (x) katika sehemu yenye kustahiki au kamilisha

1. Tafsiri ya Tawhid ni ☐ kigawanyo cha pili ☐ mlango wa ujumla . ☐ vyote .
2. Sherhe yahii ya tarjama ni milango inayokuja baadae kuelekea. . ☐
3. Mtunzi Allah amrehemu ameitafsiri Tawhid ☐ kwa kinyime chake ☐ kwa mambo ya wazi ☐ vyote.
4. Kigawanyo cha pili cha kitabu hiki kinakusanya ☐ 5 ☐ 9 ☐ 7 milango .
5. Wanawapenda kama wanavyompenda Allah (kwa maana)_____
6. Mapenzi yameganyika kama ifuatavyo 1,_____ na hukumu yake ni _____ 2,_____ na hukumu ni _____3, na hukumu ni _____
7. Mapenzi kwa Allah yanakuwa kwa _____ na _____na _____ Na _____
8. Sababu za kuharamishwa hirizi zitokanazo na Qur-ani 1- _____ 2_____3_____ 4- _____
9. Masharti ya kufaa kusoma ruqiya 1,_____2,_____ 3, _____
10. Sababu ya kuleta aya { Na wala msisimame ndani yake milele} katika mlango (Asichinjwe kwa jina la Allah katika sehemu kinachinjwa ndani yake kwa asiyekuwa Allah ni _____
11. Sababu ya kutaka { wanaotimiza wajibu wao } katika mlango (miongoni mwa shirki ni kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Allah _____
12. Nadhiri kisheria ni _____
13. { kaika asiyoyamiliki mwanadamu } maana yake ni _____
14. Kufungamana na nadhiri maana yake ni_____
15. { Buwaanat) maana yake _____{ Haijuzu kwake) maana _____
16. Umejengwa misikiti wa madhara kwa ajili ya ukafiri na _____na kwa ajili ya _____ na kwa ajili ya _____
17. Kwa nini haijuzu kuchinjia kwa ajili ya Allah sehemu inayochinjiwa kwa asiyekuwa Allah ? 1._____ 2_____ 3._____
18. Kwa nini Mtume alisema { mimi siombwi msaada } _____
19. {kumuhifadhi} kwa amana ya _____, { mzushi} kwa maana : katika _____au _____
20. { kulaani wazazi wake } maana yake _____au _____
21. { Na mimi ni miongoni mwa waislamu }maana yake _____ au _____
22. { Je,mmemuona } maana yake _____ { Allaata }kwa maana _____
23. {Na uzza } kwa maana _____{ Manaata } kwa maana _____ Au katika _____

24. (Najilinda)maana yake ……(Kwa maneno ya Allah) maana yake ……..
25. Kutaka Baraka inagawanyika katika: 1 …….. 2 ……. Tunatofautisha katika hivyo vigawanyo ya kwamba …….
26. Vigawanyo vya watu wenye kupewa udhuru katika ujinga 1…… ……. 2 ……..
27. Hupatikana Yule mwenye kusali na anatoa sadaka na anafunga na anaenda kwenye makaburi anayasujudia huyu hukumu yake :
    ☐ Kufuru kubwa ☐ kufuru ndogo ☐ madhambi makubwa ☐ mnafiki
28. Inagawanyika shirki kubwa katika: ☐ vigawanyo 3 ☐ vigawanyo 4 ☐ vigawanyiko 2
29. Kuchinja kumegawanyika katika: ☐ vigawanyo 3 ☐ vigawanyo 4
30. (Bila shaka mimi nimejitenga mbali na hayo mnayoyaabudu (26) isipokuwa Yule aliyeniumba)
31. kwenye aya hii : ☐ kuna maana ya(hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezimungu) ☐ muumbaji ndie ambaye anastahiki kuabudiwa ☐ kushinda masanamu ☐ yote.
32. (AHBAARAHUM): ☐ Wasomi wao ☐ waabudiaji wao
33. (WARUHBAANAHU): ☐ waabudiaji wao ☐ wasomi wao
34. (ARABAABA) shirki katika: ☐ mapenzi ☐ kutii
35. Vigawanyo vya watu katika kuchukua sababu ni ☐ makundi mawili na wakati na kati ☐ sahihi na shirki kubwa na ndogo
36. Kuchinja ni katika ibada kubwa za kimwili: ☐ sahihi ☐ kosa
37. Haifai kuwalaani watu wenye kufanya maasi isipokuwa kwa njia ya wote ☐ sahihi ☐ kosa
38. Ni juu ya mwislamu kuhifadhi ulimi wake kutokana na kulaani na kulaaniana basi asilaani isipokuwa mwenye kustahiki kulaaniwa kwa dalili ☐ kwa wote kama vile makafiri ☐ kwa mtu maalum kama walao riba ☐ kwa wote
39. Ikiwezekana kubadilishwa sehemu hizo na zikawa za ibada zibadilishwe : ☐ sahihi ☐ kosa
40. Ikikubali kubadilishwa kwake ingewezekana kutii ingebadilisha: ☐ sahihi ☐ kosa
41. Inasihi kufunga safari kwa ajili ya sala katika msikiti wa qubaa: ☐ sahihi ☐ kosa
42. Kwenda katika sehemu za shirki zilizojificha inasihi ikiwa ni katika upande wa kukumbusha ☐ sahihi ☐ kosa
43. Inasihi kwenda katika pango la hiraa kwa kujua yale ambayo alikuwa anafanya mtume (s.a.w) katika kuabudu: ☐ sahihi ☐ kosa
44. Miiraji ni safari yake mtume (s.a.w) kutoka Makka mpaka baytil-maqdis: ☐ sahihi ☐ kosa
45. Mwenye kubadilisha alama ambazo zinamuongoza mtu katika njia: ☐ mwenye kulaaniwa ☐ Mwenye kufanya madhambi
46. Wanawatia kasoro watu wema na wanapinga ubora wao: ☐ kuchupa mipaka ☐ kuzembea ☐ kati na kati

Swali la nne: taja hukmu za kuweka nadhiri kwa kuchanganua

Kutia nadhiri kwa ajili Allah…….....

Kutia nadhiriKwa asie kuwa Allah (shirki kubwa) ……...

……

…….....

Baada ya kuitamka ……..

Kabla ya kuitamka. …….

Kutii: ……..

Maasi: ……..

Jambolahalali:……..……

Ya kung'ang'niza:……...……..

Ya kuchukiza ……..

Isiyofungamana na chochote……..

Swali la tano: weka katika kifungu (A)kile kinachoendana na kifungu (B)

M	A	B
1.	Nadhiri	Inaitwa hirizi na ikawa ina dalili maalumu iliyo mbali na shirki
2.	Mnafiki	Kitu wanakitengeneza na wanadai ya kwamba atapendwa mwanmke kwa mume wake na mwanaume kwa mke wake
3.	Ruqiya isiyo ya kishirki .	Ni kitu kinafungwa kwa watoto kwa ajili ya kijicho Kutoka kwa Allah ni kufukuzwa na kuwekwa mbali na rehma ni kutolewa na kuwekwa mbali na rehma ya Allah
5	Limbwata	Mtu aliyebaleghekulazimishwa nafsi yake kitu chochote kisichokuwa lazima
6.	hirizi Laana	Ni Yule ambaye anadhihirisha uislamu alafu anaficha ukafiri na mwenye tabia ya maudhi

TATU: KUBATILIKA KWA IBADA ZA ASIE KUA ALLAH- MILANGO 4

Baada ya kutaja tafsiri ya Tauhid zimetajwa dalili zinazoonyesha ubatilifu wa ibada za asie kua Allah ndani ya milango mine:

- Ubatilifu wa ibada za masanamu na chochote kisichokua Allah na kuwaabudu mitume
- Ubatilifu wa kuwaabudu malaika, na wao wako karibu zaidi na Allah tofauti na binadam makhsusi (mawalii)
- Ubatilifu wa maombezi yaliyo kataliwa kinyume na Allah, na kuomba uombezi ni haqi ya Al;lah mtukufu
- Ubatilifu wa muongozo wa kuwafikishwa na Allah kwa asie kua Allah, na kwamba haumiliki muongozo huo yoyote asie kua Allah.

(15) MLANGO UNAOZUNGUMZIA QAULI YA ALLAH: (Aati wanawafanya viumbe kuwa washirikina wa Allah , nao hawaumbi wao ndio wameumbwa wala hawana uezo wa kuwanusuru (191) Aya)

- Allah amebainisha udhaifu wa masanamu haya, na kwamba hayafai kuabudiwa kwa namna (sababu) nne:
  [1] kwamba hayana uwezo wa kuumba, na asieweza kuumba hastahiki kuabudiwa.
  [2] ya kwamba wao wameumbwa baada ya kutokuwepo kwao, na wao wanahitajia kutoka kwa wengine msaada daima na milele
  [3] ya kwamba haya masanamu hayawezi kuwasaidia wale wanaoyaomba
  [4] ya kwamba hayo masanamu hayawezi kujisaidia yenyewe

DALILI YA PILI.

Na kauli yake Allah: (Na wale mnaowaabudu kinyume na Allah, wao hawamiliki hata punje ya tende au (utando wa punje ya tendo)

- (Qitmir) ni utando mwembamba laini ambao hufunika mbegu ya tende .
- Allah amebatilisha ibada za asiekua yeye kwa mambo yafuatayo:-
  [1] kwamba hivyo vinavyoabudiwa kinyume na yeye hauna umiliki wa kitu chochote.
  [2] pia havisikii
  [3] Na hata vikisikia haviwezi kujibu
  [4] Siku ya Qiyama Allah atavileta vilivyokua vikiabudiwa kinyume nay eye viwakanushe waliokua wakiviabudu.

DALILI YA TATU MPAKA YA SITA:

[3] Na kauli yake Allah (Na wale mnaowaomba kinyume na Allah hawaumiliki hata punje ya kokwa la tende)

[4] Na katika kitabu cha sahihi, hadithi kutoka kwa Anas amesema. (Alijeruhiwa Mtume rehma na Amani ziwe juu yake , siku ya vita vya Uhudi na akavunjwa meno yake ya mbele akasema " vipi watafaulu watu hali ya kuwa wamemjeruhi Mtume wao ? ") ndipo ikashuka aya isemayo " wewe huna lako jambo katika haya "

[5] Na katika riwaya nyingine Mtume alikuwa anamuapiza (kuomubea duwa mbaya) Swafuwani bin Umaiyah na Suhaila bin Amry na Harith bin Hishaam . ikateremka aya isemayo (wewe hauna lako katika shauri hili)

[6] Na kutoka katika kitabu cha swahihi hadithi kutoka kwa Abii Hurayrah (R.a) alisema: Alisimama mtume (s.a.w) pindi aliposhushiwa aya hii (Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe) – akasema (Enyi makurayshi – au mfano wa neno hili – ziuzeni nafsi – kwa Allah – sitokutoshelezeni kwa Allah na chochote,ewe Abbas bin Abuu TwalIbsikutoshelezi kwa Allah na chochote, Ewe swafiyya – shangazi wa mtume – sikutoshelezi kwa Allah na chochote, na ewe Fatwima binti wa Muhammad, Niombe chochote utakacho katika mali zangu, kwani

- (shujaa): Jeraha la kichwa hasa hasa usoni
- (Rubaaiyyatuhuu): Meno mawili ya kati yanaitwa thanaayaa, na meno mawili ya chini yake yanaitwa rubaaiyyatayn.
- Na katika hadithi kuna dalili ya kwamba mtume (s.a.w) ni mtu na anapatwa na yawapatayo watu na kubatilisha kumuabudu yeye .
- Ndani yake kuna mazingatio kwa mwenye kuzingatia ya kwambatusiweke mbali rehma za Allah kwa mwanaadamu yeyote hata kama ni muasi
- (Swafwan bin Umayya na Suhayl Ibn Amni bin Hilhaam) Na watatu hawa walisilimu na ukapendeza uislamu wao, tambua sasa ya kwamba uadui unaweza kugeuka kua unafiki.
- Kilichokatazwa ni;

  [1] Kuwalaani makafiri kwa kuwaainisha – kwa majina yao – ama kuwalaani kwa ujumla hakuna ubaya, Na hakuna ubaya kumuombea mabaya kafiri kwa kusema: Ewe Mwenyezimungu! Wastareheshe waislam kutokana na shari zake.

  [2] Kuwaombea maangamizi makafiri kwa ujumla, mtume hakuwaombea hilo, na Allah amekadiria kubaki kwao.

MAS-ALA MBALI MBALI.

Jambo la kwanza : Tafsiri ya mbili na ndani ya aya hizo kun kubatilisha ibada ya masanamu , ibada ya asiyekuwa Allah .

Jambo la pili : kisa cha vita vya Uhudi na ndani yake kuna kubatilisha kumuabaudu mtume Rehma na amani ziwe juu yake . basi kwa mwingine ndiyo haifai kabisa kumuabudu .

Jambo la tatu :kukunuti (dua) kwa bwana wa Mtume na nyuma yake akwa na mabwana wa vipenzi Allah wakiitikia dua yake ndani ya swala. Hakuna mtu yeyote yulu katika umma huu alie karibu zaidi na Allah kuliko Mtume Rehma na amani ziwe juu yake na maswahaba wake lakini pamoja na hayo wanamuelekea Allah na kumuomba .

Hivyo kwa wtu wengine kufanya hivyo ndiyo bora zaidi .

Jambo la Nne : Kwa hakika wale walio apizwa na kuombewa dua mbaya ni makafiri , na Mtume rehma na amani ziwe juu yake hamilik chohte kwao .

Jambo la tano : Hakika wao wamefanya yaliyofanywa na wengi katika makafiri miongoni mwa hayo ni kumjeruhi mtume , na kuwa na pupa ya kumuua , na miongoni mwa hayo kuwakata kata wafu , pamoja na kwamba hao wafu ni watoto wa baba zao wadogo.

Jambo la sita: Allah alimteremshia Mtume kwa hilo aya isemayo : " wewehuna laki jambo kaitka shauri hili " mambo yote ni kwa Allah .

Jambo la saba : Ni kauli ya Allah isemayo " Ama atawahurumia au atwaadhibu kwani wao ni madhalimu "Allah akawhurumia kasha wakaamini .

Jambo la nane : kukunuti (Dua) kutokana na mabalaa au matatizo hakutakiwai isipokuwa katika mambo ambayo ameteremsha Allah kama vile tetemeko la Ardhi .

Jambo la tisa : kutaja mjina y wale wanoombewa duwa mbaya au majina ya baba zao ndani ya swala jambo linafaa kisheria .

Jambo la kumi : kuwalaani watu maalum katika kunuti jambo hilo lilitokea kipindi cha mtume Rehma na amani ziwe juu yake kasha likakatazwa .

Jambo la kumi na moja :kisa cha Mtume Rehma na amani ziwe juu yake pale alipoteremshiwa aya isemayo " Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe "basi akatekeleza amri ya Allah. "

Jambo la kumi na mbili : juhudi zake Mtume Rehma na Amani ziwe juu yake katika jambo hili la Da-awa ni kubwa , kwa namna alivyofanya mambo ambayo yalisababisha atwe mwenda wazimu , hivyo hivyo kama atakavyofanya hivi sasa mtu yeyote , hivyo ni wajibu kutoa juhudi katika kulingania kwa njia ya hekima.

Jambo la kumi na tatu :pale alipowaambia jamaa zake wa karibu na wa mbali (sinto watosheleza kutokana na Allah kwa kitu chochote) mpaka akamwambia binti yake Fatma (ewe Fatma binti Muhammad sintokutosheleza kutoka kwa Allah kwa kitu chochote) ikiwa Mtume Rehma na amani ziwe juu yake ameweka wazi ya kwamba , hatomtisheleza kwa Fatma kitu chochote bibi wa wanawake wa kiislamu ulimwenguni hali ya kuwa yeye ni bwana Wa Mitume wote, na wanaadamu wamemuamini ya kwamba , hasemi ispokuwa ni kweli,kasha akatazama yaliyopo kwenye vifua vya watu leo hii itabainika kwake kwa tawhidi imeachwa , na dini imekuwa ngeni :

(ambacho kitacho nufaisha kwa munasaba wa Mtume Rehma na amani ziwe juu yake ni kumuamini na kumfuata kasha mapenzi na huruma ya muumini kwa Mtume Rehma na amani ziwe juu yake ni jambo lisilopingika lkini hatakiwa kwa mwanadamu kuyapa nafasi na kutawaliwa na mapenzi yake , bali ni wajibu kwake kufuata yale yaliyojulishwa na kitabu(Qurani) na snna (Hadithi) na yakatiwa nguvu na kuungwa **mkono na akili iliyo wazi** , yenye kusalimika na shubha na matamanio yake)

16. MLANGO WA KAULI YAKE ALLAH:(Mpaka itakapoondolewa hofu nyoyoni mwao husema mola wenu amesema nini nao huambiwa amesema maneno ya haki naye aliye juu mkubwa)

- Hii ni katika dalili zinazojulisha juu ya kwamba astahiki yeyote yule awe mshirika pamoja na Allah kwa sababu malaika wao wapo karibu sana katika viumbe kwa Allah miongoni mwa viumbe tofauti na wengine katika wanadamu na pamoja na hivyo hakika inawafikia kwao wao hofu wakati wa kusikiliza maneno ya Allah.

NI KIPI KINAKUSANYA IMANI KWA MALAIKA.

- Inakusanya imani kwa malaika kwamba wao ni ulimwengu uliofichika amewaumba Allah mtukufu kutokana na nuru na wanamtii Allah na wala hawamuasi wao wana roho na akili na miili na nyoyo tunawaamini na yale aliotupa habari Allah kuhusu wao katika matendo yao na sifa zao na majina yao na habari zilizokuja ziliwazungumzia.
- **FUZZIA:** Imeondoshwa khofu iliyoingia katika nyoyo zao (na yeye ndiye aliye juu) watu wa sunna wanamthibitisha Allah (1) kuwa juu kwa dhati yake (2) kuwa juu kwa sifa (3) kuwa na nguvu ya juu ya kuwashinda viumbe wote.

FAIDA ZA AYA

- Hakika ya malaika wanamuogopa Allah amesema Allah mtukufu (na wanamuogopa mola wao aliyeko juu yao)
- Kuthibiti kuwa malaika wana mioyo amesema Allah mtukufu (mpaka inapoondolewa khofu katika nyoyo zao)
- Kuthibiti ya kwamba wao wana miili na si roho peke yake bila ya mwili amesema Allah mtukufu (aliyewafanya malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili mbili, tatu tatu na nne nne)
- Ya kwamba wao wanaakili hivyo basi nyoyo zao zimebeba akili.
- Kuthibitisha kauli ya Allah mtukufu ya kwamba yeye amefungamana na matashi.
- Kuthibitisha kauli zake Allah ni kweli na ukweli wa maneno huwa: (1) ukweli katika kutoa habari (2) Na uadilifu katika kutoa hukumu amesema Allah mtukufu (Na yametimia maneno ya mola wako mlezi ukweli na uadilifu)

DALILI YA KUTHIBITSHA DHATI YA ALLAH IPO JUU KWA UJUMLA '5'

- Kitabu
- Sunna
- Makubaliano
- Akili
- maumbile

DALILI YA PILI.

Katika sahihi ya Bukhari kutoka kwa Abu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake, kutoka kwa mtume rehema na amani ziwe juu yake. Amesema Pindi atakapolihukumu Allah jambo lake mbinguni malaika hupiga mbawa zao kwa unyenyekevu kwa kauli yake Allah kama vile sauti tukufu inayotoka kwenye jiwe gumu, inawfikia wao hiyo sauti, mpaka inapoondoshwa khofu utakapoisha katika nyoyo zao. husema malaika (wakiulizana wao kwa wao) Nini kasema Mola wenu mlezi? Wanasema : amesema kweli , na yeye ni wajuu na mkubwa. Basi wanalisikia neno hilo wezi wa kusikiliza (mashaitwan)wao kwa wao, hivyo hivyo baadhi yao juu ya wengine (SUFYANI BIN UYAINA : ameelezea namna walivyokuwa wakifanya kwa kutumia viganja vyake) basi wanalisikia neno (la Allah)na wanalifikisha walio chini yake , kisha wengine walikisha kwa walio chini yao mpaka wnalifisha kwenye ulimi wa mchawi ao kohani , baadhi ya muda hupigwa na vimondo kabla ya kufkisha , na wakati mwingine hufikisha kabla ya kupigwa na vimondo, huyachanganya maneno hayo nay a uongo mia moja . Basi husemwa hivi hakutuambia sisi siku kadhaa maneno kadhaa na kadhaa ? hapo huonekana kuwa mkweli (shetani) kwavile neno moja la kweli alilisikia mbinguni na kuliachanganya na uongo .

- **SWAFUANI:-**
  Ni jiwe gumu lenye kuteleza na myororo juu yake unakuwa na sauti kubwa na kinachokusudiwa hapa ni kuelezea mfadhaiko wa Malaika unaopatikana pale wanaposikia maneno ya Allah.

- **INAWAFIKIA:kwa maana inawafikia malaika hii sauti ufkiaji wa kusikia .**

MIONGONI MWA FAIDA ZA HII HADITHI .

- Uthibitisho kuwa Allah ana kauli , pia kuthibitisha ukubwa wa Alla wala halitoki kwa Allah isipokuwa la haki .
- Kuthibitisha kuwa malaika wan mbawa ,wanaongea na wana akili , wanaogopa na humyenyekea Allah .
- Allah anawewezesha hawa Majini kufika mbinguni ikiwa mtihani kwa wanaadamu.
- Majini ni wengi miili yao ni myepesi wanaruka na kupaa .
- Hakika Mkohani (wapiga ramli) ni watu waongo mno , kwa sababu hiyo wanaongeza katika walichosikia uongo mwingi .
- Hakika mchawi humpambia na kumdanganya alierogwa vitu ambavyo siyo vya uhakika , hivyo ni wajibu kuchukuwa tahadhari .

DARAJA YA USIKIVU WA KUIBA KWA MAJINI .

1- Kabla ya kutumwa Mtume wizi wa kusikia ulikuwa mwingi .
2- Baada ya kutumwa Mtume(Rehma na amani ziwe juu yake) walizuiliwa kusikiliza.
3- Baada ya kufa Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) walitarajia tena kusikiliza kwa kuiba , lakini kwa uchache .

DALILI YA TATU:

Na kutoka kwa Nnawasi bin Samaana radhi za Allah ziwe juu yake amesema mtume rehema na amani ziwe juu yake: (Pindi anapotaka Allah mtukufu kulifikisha jambo hulifikisha kwa wahyi, mbingu hupatwa na mtetemeko kutokana huo wahyi. au akasema:

RIIDATU – Khofu kali kwa kumuogopa Allah mtukufu, basi watakapo sikia hilo mbinguni (Malaika)huzimia na kuporoka hali ya kumsujudia Allah, basi atakua wa kwanza kunyanyua kichwa chake, Jibril, atazungumzishwa na Allah kutokana na wahyi wake kwa vile atakavyotaka, kisha atapita Jibril kwa malaika, kila mbingu anayo pita humuuliza malaika wake: (Kitu gani amesema mola wetu ewe Jibril? Atasema Jibril: Amesema haki na yeye ni wa juu na ni mkubwa, watasema wote mfano alicho kisema Jibril, ataishia Jibril kwa wahyi mpaka pale alipo mwamrisha Allah mtukufu.

FAIDA KUTOKA KWENYE HADITHI.

- Kuthibiti matakwa ya Allah nayo yapo katika vigawanyo viwili:-
  i. Matakwa ya kisheria
  ii. Matakwa ya kiulimwengu (yaani namna alivyoupangilia)
- Hakika viumbe na hata kama ni vitu vigumu vimetokana na uwezo wa muumbaji
- Kithibiti idadi ya mbingu, na kila mbingu ina malaika muhusika.
- Ubora wa Jibrili pale ambapo yeye ni maarufu kwa maana ya wahyi na hakika yeye ni mwaminifu.
- Kuthibiti uwezo na utukufu kwa Allah

UWEZO NA UTUKUFU.

JALLA: Utukufu kwa maana utukufu ambao hakuna juu yake utukufu.

AZZA: Kwa maana ya kushinda kuwa na nguvu.
Na uwezo una maana tatu:-

- Mwenye nguvu, kushinda na alie juu
- Mwenye nguvu na cheo hana wakushirikiana naye katika hilo yeyote.
- Mwenye nguvu , haiwezekani yeyote kumpata kwa mabaya.

MAS-ALA MBALI MBALI:

Ya kwanza: Tafsiri ya aya (Mpaka inapo ondoshwa khofu katika nyoyo zao, malaika husema kwa uliza nini amesema Mola wenu? Watasema amesema kweli mola wetu.

Ya pili: Hoja zilizomo ndani ya aya katika ubatilifu wa shirki hasa hasa yale yanayofungamana kwa watu wema na hiyo aya ambayo inasemekana ya kwamba inakata mizizi ya mti wa ushirikina ndani ya moyo.

Ya tatu: Tafsiri ya kauli yake Allah (Watasema amesema ukweli mola wetu na yeye ni wa juu mkubwa)

Ya nne: Sababu ya malaika kuuliza juu ya hilo (Ni wingi wa khofu yao)

Ya tano: Ya kwamba Jibril A.S anawajibu baada ya swali lao hilo (Mola wetu amesema kadha wa kadha)

Ya sita: Hadithi imetaja ya kwamba wa kwanza kuinua kichwa chake ni Jibril (Na hapa kuna fadhila na ubora wa jibril)

Ya saba: Ya kwamba Jibril anawaambia walioko mbinguni wote alichoambiwa na Allah kwa sababu humuuliza (Ni dalili ya cheo chake baina yao)

Ya nane: Ya kwamba kiwewe kinawapata walioko mbinguni wote.

Ya tisa: Kutetemeka kwa mbingu kwa ajili ya maneno ya Allah (kwa kumtukuza Allah)

Ya kumi: Ya kwamba Jibril ndiye ambaye anaupeleka wahyi mpaka pale alipo amrishwa na Allah (kwa sababu yeye ni mwaminifu)

Ya kumi na moja: Hadithi inataja jinsi wanavyosikiliza kwa wizi mashetani (wahyi)

Ya kumi na mbili: Sifa ya mashetani kubebana au kupandiliana wao kwa wao

Ya kumi na tatu: Kuachiwa kwa vimondo vya Moto (ambavyo vinawachoma mashetani wanaosikiliza wahyi)

Kumi na nne: Ya kwamba mara nyingine vimondo vya moto huwapata mashetani hao (wanaosikiliza wahyi kwa wizi) kabla hawajaufikisha wahyi huo ardhi kwa mawalii wao katika watu, Na mara nyingine hufikisha wahyi huo kwa watu kabla vimondo hivyo vya moto havijawapata.

Ya kumi na tano: Ya kwamba kohani wa kienyeji husema kweli baadhi ya nyakati

Ya kumi na sita: Kuwa ya kwamba kohani hudanganya pamoja na ukweli huo uongo mia moja (Na uongo mia ni kuonesha wingi wa uongo na sio ukomo wa idadi)

Ya kumi na saba: Ya kwamba hausadikishwi uongo wake ila lile neno lililosikika mbinguni.

Ya kumi na nane: Nafsi kuukubali batili kwanini wanang'ang'ania ukweli mmoja na hawazingatii udanganyifu mia.

Kumi na tisa: Ya kwamba wao wanapokezana neno hilo na wanalihifadhi na kulitolea dalili (kwa sababu neno hilo linawaletea faida na lau ingekuwa ni uongo mtupu usingeleta faida.)

Ya ishirini: Uthibiti wa sifa za Allah lau ingelikuwa na madhehebu ya Al- ash ariyah wenye kukanusha sifa za Allah.

Ya ishirini na moja . Hadithi imeweka wazi kuwa kutetemeka na kuzimia kwa Malaika ni kwa kumuogopa Allah (azza wajalla)

Ya ishirini na mbili : Hakika Malaika huporomoka n kusujudu kwa ajili ya Allah (kwa kumtukuza na kujikinga na kile wanachokikhofu.)

(17) MLANGO WA UOMBEZI (SHAFAA)

Kwanini mtunzi ameleta mlango huu?(Allah amrehemu)

- Kwa sababu ya ubatilifu wa uombezi (shafaa) wa masanamu, kwa sababu ya makafiri wanaitakidi kuwa masanamu yatawaombea uombezi mbele ya Allah.
- Kwa sababu Allah ni mkamilifu wa elimu na kiuwezo na ufalme hayupo kama wafalme wa duniani kwani wao wanahitaji waombezi kwa upungufu wa elimu zao na ufalme wao na uwezo wao.basi husaidiwa na waombezi katika mapungufu hayo , ufanya jasiri kwao waombezi na huwaombea bila ya ruhusa .

DALILI YA KWANZA HADI YA TANO

(1) Na kauli yake Allah: (Na uwaonye kwa qur'an hii wale wanaoogopa ya kwamba watakusanywa kwa mola wao, hali ya kuwa hawana mlinzi yeyote, isipokuwa yeye wala muombezi.

(2) Kauli yake Allah: (sema uombezi wote uko katika amri ya Allah)

(3) Kauli yake Allah: (Na nani huyo awezae kuombea mbele yake bila tahim yake)

(4) Na kauli yake (wako wangapi malaika mbinguni ambao huombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezimungu kutoa idhini kwa amtakae na kumridhia)

(5) Na kauli yake Allah (sema waiteni mnao wadaia uungu kinyume na Allah hawamiliki hata uzito wa mdudu chungu mbinguni na ardhi ni wala hawana ushirika na Mwenyezimungu katika hizo mbingu na ardhi wala yeye hana msaidizi miongoni mwao. Aya(22) Na wala hautafaa uombezi mbele yake Mwenyezimungu ila kwa Yule aliempa idhini.

- (Na uonye kwa hiyo): Kuonya ni maelekezo yaliyo fungamana na kuogopesha na maana yake mtume awaonye kwa qur'an.
- (Ni malaika wangapi): Yaani Ni wingi ulioje wa malaika walioko mbinguni, na pamoja na wingi huo hautafaa uombezi wao kwa chochote ila baada ya idhini ya Allah na radhi zake kwa muombezi na muombewa.
- (waiteni): Amri hii ni kushindisha , kwa maana waleteni (hao washirika)
- (ushirika): Hawamiliki chochote wakiwa pekee yako au wakiwa na mshirika
- (Msaidizi): kati kipande hiki cha aya Allah anakanusha masanamu kuwa si wasaidizi.
  Neno DHWAHIIR. Maana yake ni msaidizi .

- Yanakanushika kwa hayo masanamu yote wanayoitakidi na kyaabubudu , kwa hiyo hayamiliki chochote kwa njia ya mmoja mmoja , hata kwa kushirikiana , wala kwa kusaidiana . kwani anayekusaidia hata kama sio mshirika wako hua aanakuwa muhisani wako , huenda akapendelea kumpa anachokitaka .

Kwa kuwa haya yote matatu hayapo kwa masanamu hakuna kilichobaki isipokuwa uombezi (shafaa) nao pia Allah ameubatilisha kwa hayo masanamu , hivyo haunufaishi uombezi wao .

Na aya hii na inayofuatia . amesema Ibnul- Qayyim Allah amrehemu " ndiyo aya ambayo inakta mizizi ya mti wa ushirikina kwenye moyo."

ViGANYO VYA UOMBEZI (SHAFAA) AMBAYO NI KUWEKA MTU AU KITU KATIKATI KWA AJILI YA KULETA MANUFAA AU KUONDOA MADHADHARA .

ILVYOTHIBITISHWA.

Amethibitisha Allah yeye mwenyewe na huombwa kwa masharti yafuatayo :-

- Atoe idhini ya kuomba .
- Amridhie muombaji.
- Amridhie muombewa .

ILIVYOKANUSHWA.

Ni ile ambayo-Qur'ani Nayo ndo ile ambayo inayoombwa kwa asiye kuwa Allah kwa kile asichokiweza yeyote isipokuwa Allah pekee. Nayo ndiyo ile ambayo ndani yake kuna shirki kubwa.

ILIYO KATIKA UWEZO WA MWANADAMU

Hii inasihi kwa sharti muombaji :-

- Awe hai
- Awe ana uwezo wa anachoomba.
- Awepo mahali husika
- Awe ni sababu tu

Na wako malaika wengi mbinguni ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Allah kutoa idhini kwa amtakae na kumridhia.

Utetezi maalum kwa Mtume Rehma na amani ziwe juu yake , hatoshirikiana na yeyote katika uombezi huo.

- Utetezi uliyokuwa mkubwa nao ni kila kisimamo kilichoshukuruwa ambacho Allah amuahidi Mtume wake .
- Utetezi yake Mtume Rehma na amani ziwe juu yake kwa baba yake mdogo Abu Twalibi ili apunguziwe adhabu.
- Utetezi wake Mtume Rehma na amani ziwe juu yake katika kufunguliwa milango ya pepo kwa ajili ya watu wake.

Utetezi wenye kuenea wote kwa Mtume Rehma na amani ziwe juu yake na kwamitume wote na malaika na wenye kumpwekesha Allah na watoto wadogo.

- Utetezi na uombezi katika kuwanyanyuliwa daraja za waumini.
- Utetezi kwa wale waliostahiki kuingia motoni katika wale wenye kumpwekesha Allah ili wasiigie motoni.
- Utetezi kwa wale walioingia motoni miongoni mwa wale wenye kumpwekesha Allah awtoe humo motoni.

Amesema Abul-Abbass (Amekataa Allah kile kilicho kinyume nae.

Kila wanachoambatana nacho washirikina ,akapinga kwa mwingine ufalme au sehemu katika ufalme au awe msaidizi kwa Allah, na wala hakuna kilichobaki isipokuwa utetezi, na akabainisha ya kwamba haunufaishi isipokuwa kwa aliyempa idhini Allah kama alivyosema (Na wala hawamuombei yeyote ila Yule anaemridhia Allah) huu utetezi ambao wanaudhania washirikina ni ule utakao kataliwa siku ya kiyama kama ulivyo ukataa katika Qur'an na akatukhabarisha mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) ya kwamba yeye atakuja na atasujudu kwa mola wake na atamsifu haanzi kwa utetezi kwanza – kisha ataambiwa na Allah: (Nyanyua kichwa chako na sema utasikilizwa na omba utapewa na omba utetezi utakubaliwa)

Na akasema Abu hurayra kumwambia mtume (Rehma na amani ziwe juu yake): nani atakae fanikiwa zaidi katika watu kwa utetezi wako? Akasema mtume(s.a.w) (Mwenye kusema: (hakuna mola apasae kuaudiwa kwa haki isipokuwa Allah) ikiwa ni kweli kutoka moyoni mwake) basi ule utetezi ni kwa watu wenye kumtakasa kwa idhini yake na wala hajiwi kwa mwenye

MAMBO.

1. Tafsiri ya aya (Nazo zipo tano)
2. Sifa ya utetezi uliokataliwa (Naona ule ambao ndani yake kuna shirki).
3. Sifa iliyothibitishwa (Nayo ni utetezi wa watu wenye kumpwekesha Allah baada ya idhini yake Allah mtukufu na aliye juu na radhi zake kutoka kwa muombaji na muombewa
4. Kutaja utetezi uliokuwa mkubwa nayo ni sehemu iliyokuwa nzuri (kwa watu wanaosimamia kuhukumu baina yako)
5. Sifa anayoifanya mtume (s.a.w) ya kwamba hatoanza kwa utetezi bali atasujudu atakapoewa idhini na Allah ya utetezi (Na hili linajulisha juu ya ukubwa wa mweyezimungu mtukufu na ukamilifu wa adabu yake mtume(s.a.w)
6. Atakae furahi kwa hilo katika watu? (watu wenye kumpwekesha Allah na kumtakasa)
7. Ya kwamba hauwi huo utetezi kwa Yule mwenye kumshirikisha Allah.
8. Kubainishwa uhakika wake (Hakika ya Allah aliyetakasika yeye ndiye ambae anawafadhilisha wale watu wenye kumtakasa atawasamehe kati ya dua za Yule ambae aliyepewa idhini kwao wao aweze watetea ili amkirimu na apate sehemu iliyo kuwa nzuri.

[18] MLANGO KAULI YA ALLAH MTUKUFU "KWA HAKIKA WEWE HUMUONGOI UMPENDAE"

DALILI YA PILI.

Katika sahihi Bukhari imepokelewa na ibn Musaybu kutoka kwa baba yake amesema pindi alipofikwa na umauti.abtwalibu akamuijia mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) pembeni yake akiwepo Abdillah ibn Abii Umay na Abbu jahali akamwambia mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) (Ewe ami wangu) sema Lailaha ila lallah neno ambalo nitakutetea kwa neno hilo mbele ya Allah "Akamjibu: Unapinga mila ya Abdul mutwalibu? Akawa anarudia mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) kurudia rudia akawa amesema mwingine ni katika mila ya Abdul mutwalibu. Akakataa kusema (laaila hailalah) akasema mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) "nitakuombea msamaha kama nisipokatazwa" Allah akaremsha aya (Haimpasii nabii na wale walio amini kuwatakia msamaha washirikina.) Allah akateremsha aya kwa Abuu twalibu " Kwa hakika wewe humwongoi umpaendae, lakini Mwenyezimungu humwongoa amtakae"

VIGAWANYO VYA HIDAYA (UONGOFU)

UONGOFU WA KUWAFIKISHWA KATIKA KHERI.

Na uongofu huu hakuna anaeumiliki ispokuwa Allah pekee. " Hakika wewe humuongoi umpendae "

UONGOFU WA KUMUONGOZA MTU NA KUMJULISHA KHERI.

Uongofu huu anamilki Mtume(Rehma na amani ziwe juu yake) " Na Hakika wewe unaongoza kwenye njia iliyonyooka"

- Ameleta mtunzi radhi za Allah ziwe juu yake huu mlango atubainishie hakika hawezi hata mmoja kumuongoza yeyote muongozo wa tawfiq, asimame katika amri za Allah (s.w)
- **TATIZO:** Vipi Mtume anampenda Abutwalib wakati ni kafiri? Yawezekana katika hilo kuna maneno yaliyokadiriwa :-[1] ni yule uliempenda kuongoka kwake si uliempenda yeye kama yeye na (hii ni kauli yenye nguvu [2] Ama utakae mpenda upendo wa kimaumbile tu nayo inafaa. [3] Au utake mpenda kabla ya makatazo ya kumpenda kafiri.
- Mtume Rehema na amani ziwe juu yake alimuendea Abuutwalib, hapa kunajuzu kumtembelea kafiri ikiwa atatarajiwa kuwa muislamu
- Ewe Ami "alileta tamko hili ikiwa ni kinaya lenye kujulisha huruma na hii ndio hekima ya da'awa
- Vipi tunakusanya kati ya hadithi na kauli ya wanachuoni ni kuwa sunna kumtamkisha mtu bila katumia neno: sema? Jawabu hakika ya Abutwalibu alikuwa kafiri pindi alipoambiwa sema na akakataa basi amebakia kwenye ukafiri. Haikumdhuru Taliqiini kwa hili kinyume na muislamu hatari kwa sababu huenda ikamdhuru taliqiini.

UKIMFIKIA UMAUTI: Yaani alama za umauti na hazikumtoka kwa namna hii je anakubaliwa toba yake? Ukweli hakubaliwi [1] kwa sababu aya "Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti imefungamana kiukamilifu na hadithi [2] kwa sababu amesoma: "litakuokoa wewe" na hayakufaa manufaa yake.

- Hii amri ni maalum kwa mtume (s.a.w) kumuomba Ami wake pamoja ukafiri wake.
- Alimswayibu na Abdillah ibn ummaya walisilimu radhi za Allah ziwaendee kinyume na Abutwalibu na Abajahali
- "nayo ni mila yake" ameweka sehemu ya (mimi) thamiri (ya yeye) kuna hakika za mapokezi ya Tawhid.

MOJA: tafsiri ya kauli "kwa hakika wewe humwongoi umpendae lakini Mwenyezimungu humwongoa amtakae" aya

MBILI: tafasiri ya kauli "kwa kuwa nabii Aya (ni haramu kudhihirisha huzuni ya umauti wao na utukufu wao

TATU: ni masiara makubwa, tafasiri ya kauli (laailahailalah) kinyume na aliyonayo anaidai elimu kwasababu hii imekataa kuyasema

NNE: Hakika ya Abajahali na aliyokuwa nao wajua makusudio ya mtume (s.a.w) pindi akisema Kumwambia mtu sema (laahilaahaillah) Allah amchukue Abajahali amejua asili ya uislamu

TANO: Babu yake Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) na kufanya pupa juu ya kusalimu amri yake [1] kwa ukaribu [2] pindi alimsaidia mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) katika uislamu kwa wema katika hili ni la kushukuriwa hata kama alikuwa ni kafiri anapewa udhuru

SITA: Majibu kwa wanaodai kusilimu kwa Abatwalibu na kuacha (mila ya ukafiri)

SABA: Kauni ya mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) kumuombea na hakufanikiwa msamaha isipokuwa alikatazwa jambo hili (ni jambo la Allah)

NANE: Madhara ya wtu waovu juu ya mwanadamu.

TISA: Madhara ya kuwatukuza wanaopingana na viongozi (pindi wakiwa wamepotea)

KUMI: Utata wa wabatilishaji katika jambo hili kwa usahihi wa Abajaliah

KUMI NA MOJA: Kushuhudia mwisho wa matendo kwa sababu angesema lingempa manufaa

KUMI NA MBILI: Kuamiliana na wakubwa wa shubuha wa nyoyo za wapotofu kwa sababu katika kisa hawa kujali ila hilo tu pamoja pupa mtume Rehma na amani ziwe juu yake) na kurudia rudia. Kwa ajili ya ubora wake na uwazi wake juu yao na uakoaji wake. "Nayo ni shubuha kuwatukuza wanaopinga na wakubwa wao"

MTIHANI WA KIGAWANYO CHA TATU MILANGO NNE

SWALI LA KWANZA:-

Taja milango ya hiki kigawanyo na sababu ya mtunzi kuleta kila mlango:-

	Anwani yake	SABABU YA KULETA MTUNZI amrehemu KILA MLANGO
1.	_____	_____
2.	_____	_____
3.	_____	_____
4.	_____	_____

SWALI LA PILI:

Bainisha hukumu za matendo yafuatayo;-

Inajuzu (1) haijuzu (2)shirki kubwa (3) inapendeza (4) sunna

Kutaka uombezi kwa waliokufa _____ kutaka kujikulubisha kupitia cheo cha mtume

Kumtembelea mgonjwa mshirikina _____ rehema na amani ziwe juu yake _____

Kumtamkisha alie katika sakaratul mauti _____ Laana kwa mtu maalumu _____

Laana kwa ujumbe wa makafiri _____

SWALI LA TATU:

Weka alama [x] katika sehemu inayo nasibiana au ukamilishe sehemu ya wazi:

1. Kigawanyo cha tatu katika kitabu cha kumpwekesha ni:- ☐ Tafsiri ya kumpwekesha ☐ kufanya ibada kinyume na Allah
2. Kinazingatia kigawanyo cha tatu katika: ☐ 5 mlango ☐ ne mlango ☐ mlango
3. Kuuliza katika [Wanashirikisha] kwa kukataa na kuhofisha: ☐ hihi ☐ sa
4. Alibainisha Allah kushindikana na kukabatilika ibada ya masanamu katika: [Je wanashirikisha] kutokana: ☐ Namna 4 ☐ Namna 3
5. [Na wale wanaoomba kinyume na yeye] dua: ☐ ibada ☐ masiara ☐ inakusanya ujumbe
6. Tusiweke mbali rehema za Allah kwa mwanadamu yeyote atakaye kuwa muasi isipo kuwa uma uliokufuru; ☐ sahihi ☐ kosa
7. Neno la mtunzi hakika mwenye kuombwa kwa wao makafiri makusudio yake kufahamu kwa ukafiri wao: sah ☐ kosa ☐
8. Neon la mtunzi [QUNUT SAYIDU ALMURSALINA] makusudio yake ☐ kujuzu kunuti ☐ Hakuna yeyote ambaye yupo katika uma ambao upo karibu na Allah kuliko mtume na maswahaba, na pamoja na Hivyo wanarejea kwa Allah
9. Vipi tunaomba kwa makafiri? _____

10. [Kufazaika] kuondosha khofu [ ] Mwenye kughafirika [ ] Mwenye kuendelea kutoka kwenye nyoyo zao
11. [Kuwa kwake anakadhibisha pamoja naye uongo mia moja] kwa njia: [ ] ya kufikia [ ] kikomo
12. [Na wako malaika wangapi mbinguni] imekusanya masharti ya uombezi matatu [ ] sahihi [ ] kosa
13. Kila uombezi ndani yake kuna shirki basi ni waombezi: [ ] wenye kukataza ku[ ]kisha kwa wote [ ]
14. Uombezi hautaki msaada kwa Allah katika chochote kwa kila alichokiombea kwacho na hili limezaliwa [ ]ahihi [ ]kosa]na kwa hilo inakusaidia kwayo [kumkirimu muombewa kunufaika mw[ ]e kuombewa kwake ujumla] [ ]
15. Aya ambayo imesemwa kwayo inakata mizizi ya shirki katika nyoyo: _____
16. Uongofu wenye kuthibiti ni _____
17. Maana ya aya [Hakika wewe humuongozi umtakae] yaani unaemtaka [ ]ofu wake mapenzi ya kitabia [ ]abla ya kukataza kutoka na mapenzi ya makafiri k[ ]umla
18. [Yalihudhuria mauti ya Abutwalibu] yaani _____, au _____
19. Mila ya AbdulMutwalibu ni: [ ]hirki na kuabudu masanamu [ ]wara wanaoabudu moto
20. [UHAJU] yaani [ ]iitaje hoja kwako wewe mbele ya Allah [ ]ta magonvi na naleta mjadala kwako wewe mbele ya Allah
21. Kwanini alisema mpokezi: [Yeye yupo katika mila] na hakusema [mimi]? _____
22. Imesuniwa kumtamkisha mwenye kufikwa [Hakuna mola isipokuwa Allah] kwa kauli yetu kwake [sema] na dalili kitendo chake mtume rehema na amani ziwe juu yake pamoja na baba yake mdogo sahihi [ ] kosa na ni vipi u[ ]tsanya kati \yake na kati ya kauli ya maulamaa: [Imesuniwa kumtamkisha mwenye kufikikwa hapana mola isipokuwa Allahpasina kusema: sema]

    _____
23. Pupa ya mtume rehem na amani ziwe juu yakekunako kusilimu kwa baba yake mdogo Abu Twalibu kwa sababu yeye: [ ]ukaribu wake [ ] hakumwacha yeye na uislamu ukiwa wenye kufahamika wote [ ]
24. Kuwatukuza waliotangulia na wale wenye kujifukiza ni vibaya: [ ]moja kwa moja [ ]ukiwa ni katika batri

SWALI LA NNE: KAMILISHA VIGAWANYO VYA UOMBEZI

_____: inaswihi kwa sharti:

1. _____.
2. _____.
3. _____.
4. _____.

_____: Niile ambayo imekatazwa qur'an moyoni ambayo _____ na hakika yenyewe _____.

_____: Amethibitisha Allah mwenyewe na inatoka kwake yeye kwa masharti;-

1. _____.
2. _____.
3. _____.

Kwa ujulma inakusanya _____ na miongoni:

1. _____.
2. _____.
3. _____.

Maalumu kwa mtume rehema na amani ziwe juu yake:

1._____.
2._____.
3._____.

NNE: SABABU YA KUKUFURU WANADAMU (4 MILANGO)

- Ametuletea ili kutubainishia sababu za kukufuru ili tujiepushe nazo lazima Kwanini kufuru hupatikana katika baadhi ya umma? Amejibu katika milango mitatu na wanne Hakika mtume (s.a.w) amefunga kila kinachopelekea katika shirki

[19] MLANGO ULIOKUJA KUELEZA HAKIKA SABABU YA KUKUFURU WANAADAMU NA KUACHA DINI YAO NI KUCHUPA MIPAKA KWA WATU WEMA.

- Hii ni katika sababu kubwa ni hatari zaidi na ni shirki ya kwanza kuzuka sababu yake ilikuwa ni shubha ya kuchupa mipaka kwa watu wema.

DALILI YA KWANZA NA YA PILI.

[1] Kauli ya Allah (s.w) "Enyi watu wa kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu.

[2] katika sahihi kutoka kwa Abbas radhi za Allah zimwendee – katika kauli ya Allah (s.w): "Na wakasema: msiwaache miungu yenu, wala msimwache wadda wala suwaa wala ya ghutha, wala yauqa, wala Nasra" Amsema: "Haya majina ni ya wanaume wema walikuwa zama za Nuhu, pindi walipokufa shetani wakawapa wahyi watu wao. Kwamba wekeni masanamu , katika maeneo ambayo walikuwa wanakaa na kufanya ibada, na yaiteni kwa majina yao wakafanya hivyo lakini hawakuabudu hadi walipo kufa hawa na elimu ikapotea wakaanza kuabudu hayo masanamu"Amesema ibn qayimu wamesema zaidi ya mmoja katika wema waliopita : pindi walipokufa wakawa wanakaa kwenye makaburi yao na kufanya ibada. Kisha wakatengeneza picha zao au masanamu kisha ukapita muda mrefu kwao na baadae wakayaabudu.

- Enyi watu wa kitabu); nao ni mayahudi na kitabu chao ni tawrati na manaswaara kitabu chao injili.
- "Msipite kiasi katika dini yenu" yaani msijevuka mipaka zaidi na zaidi katika kusifu au kukosoa . Manaswara walivuka mipaka kwa nabii Issa zaidi wakasema ni moto wa Allah, na watatu katika utatu, na mayahudi walichupa mipaka kwake kwa kukosoa na kumpa sifa mbaya.
- (halaku) yaani walikufa
- Shetani aliwapa wahyi : mana aliwatia wasi wasi .

- "wekeni sanamu" kila kinachowekwa kama vile fimbo au jiwe, hivyo aliwaambia kufanya hayo ili wanapowaona wapate uchangamfu katika ibado zao ,lakini walienda kinyume na sheria kwani nia haitoshelezi peke yake lazima ipatikane matendo yanayo afikiana na sheria hivyo kusudio ni sahihi matendo ni batili.
- "mpaka walipo kufa hao ambao walichonga masanamu" sura zao zikafananishwa
- Umma ambao umemtangulia Nuhu (A.s) walifanya vitu vitatu!
    - "walichonga picha" wakawafananisha nao, na hapa kuna hatari ya kutunza picha na masanamu.
    - "walikaa " kufanya ibada juu ya makaburi yao.
    - "muda ulikuwa mrefu" ukawa mbali baada ya mda wa utume elimu ikakosekana ikatokea shirki kubwa wakawaabudu kinyume na Allah. Asili ni kuishughulika elimu na kuifanyia kazi ili yasije kutokea kama mfano huu.

MADHARA YA KUVUKA MIPAKA KATIKA DINI .

- Hakika kuna kumuweka msifiwa zaidi ya mahala anapostahiki ikiwa ni katika kusifia na itakuwa ni kushusha chini kama itakuwa ni kumkosoa .
- Hakika inapelekea kuabudiwa huyu mwenye kuchupwa mipaka
- Hakika inazuia kumtukuza Allah kwa sababu nafsi hushughulika na batili au haki.
- Hakika ya mchupa mipaka akiwa yupo. Hakika atajifaharisha kwa nafsi yake na hii ni madhara kwa mwenye kuchupwa mipaka ikiwa anasifiwa sifa nzuri na italeta uadui na fitna ikiwa ni sifa mbaya.

VIGAWANYO VYA WATU KUHUSU WAJA WEMA.

- kuna kigawanyo kinachupa mipaka katika kusifu. Kama vile wakiristo kwa nabii Issa amani ziwe juu yake
- Kuna kigawanyo kinachupa mipaka katika kukosoa (sifa mbaya) kama vile mayahudi kwa nabii Issa amani ziwe juu yake .
- Kuna kigawanyo cha kati na kati hikichupi mipaka wala kuzembea na hao ndiyo (Ahlu sunna) watu wa sunna.

DALILI YA TATU HADI TANO.

[3] Kutoka kwa Ommary. Hakika ya mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesoma: "msinisifie sana kama walivomsifia manaswara motto wa Marymu (Issa) hakika mimi mja wa Allah semeni mja wa Allah na mjumbe wa Allah.

[4] Kutoka kwa Ibn Abasi radhi za Allah ziwaendee Amesema: “ amesema mjumbe wa Allah Rehma na amani ziwe juu yake” “Jiepusheni na kuchupa mipaka hakika waliangamia wale walikuwa kabla yenu”

[5] Na kutoka kwa Muslimu kaipokea Ibnu Masood hakika mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema: “waliangamia wavuka mipaka” alisema mara tatu

- “msinisifie” kusifia hadi kwenda juu katika sifa kama walivyofananishwa wakiristo na wengineyo.
- “mja wa Allah na mjumbe” hizi sifa mbili sahihi ni sifa na sharafi kwa mtume (s.a.w)
- “kuvuka mipaka” ni kuzidisha zaidi katika kusifia kwenye ibada na matendo
- Ni kwanini waliangamia walio chupa mpaka? Waliangamia [1] katika dini [2] katika miili yao
- Kuchupa mipaka kuna aina nyingi: kuchupa mipaka kwenye akhida na ibada na miamala na ada na dini ya Allah (s.w) ipo kati kwa kati baina ya juu na chini
- “walmutwanafighuna”: Alimutanatigha ni aliyezidi na kuzama zaidi hana mwenye kumshikilia maneno na matendo pindi anapoona uzembe wa nafsi yake na mantwighu, katika dini inafanana na kuvuka mipaka na sababu katika sababu za kuangamia.

MAS-ALA - MBALI MBALI

Moja: Hakika mwenye kuufahamu mlango huu na milango miwili baada yake itambainikia ugeni katika uislamu na kuona uwezo wa Allah (s.w) na nmna anavyoziegemeza nyoyo ni mambo ya ajabu .

Mbili: Kujua mwanzo wa kutokea shirki katika ardhi ilikuwa utatanishi kwa waja wema.

Tatu: Kufahamu kitu cha mwanzo kilichobadilisha dini ya manabii (ni shirki) na ipi sababu yake? “kuchupa mipaka kwa waja wema” pamoja na kujua hakika Allah ndie amewatuma wao.

Nne: kukubalika kwa bid’aa pamoja na kuwa sheria na maumbile inakataa na kuipinga.

Tano: hakika sababu hayo yote ni kuchanganya haki kwa batili, mwanzo ni kuwapenda waja wema, pili ni kufanya watu wenye elimu na dini walitaka kheri, wakadhania waliokuja baada yao hakika wao walitaka kingine “mwenye kutaka kusimamisha dini kwa jambo la bid’aa hakika madhara yake ni makubwa kushinda manufaa”

Sita: tafasiri ya aya ambayo ipo katika surat Nuhu “hakika hao walikuwa wakihusiana katika batili”

Saba: maumbile ya mwana adamu ni kamba haki hupungua moyoni na batili huzidi “isipokuwa aliyeongozwa na Allah”

Nane: kuna ushahidi kwa yaliyopokelewa kwa wema waliotangulia hakika ya bid’aa ni sababu ya ukafiri (hakuna kiziwizi kutokana na sababu zake).

Tisa: kumjua shetani jinsi alivoanza na kuwaletekea bid’aaa pamoja uzuri wa makusudio ya mtendaji.

Kumi: kujua kanuni kuu nayo ni makatazo juu kuchupa mipaka na kujua yanayopelekea hulo.

Kumi na moja: madhara ya kukaa juu ya makaburi kwa ajili ya matendo mema hupelekea katika kuwaabudu wao.

Kumi na mbili: kujua makatazo juu ya kutengeneza sanamu na hikma ya kuyaondoa ni kuziba mianya shirki .

Kumi na tatu: ukubwa wa kisa hiki na kuna hoja kubwa ya kukihitaji pamoja na kuwa watu wameghafilika nacho .

Kumi na nne: Ajabu ya maajabu ni wao kukisoma kisa hicho kwenye vitabu vya tafsiri na hadithi na wanatambua maana ya hayo maneno , na kuwa Allah amezidi kati yao na kati ya mioyo yao , mpaka wakaitakidi ya kwamba kitendo cha watu wa nabii Nuhu ndio ibada bora .na wakaitakidi ya kwamba aliyo kataa Allah na Mtume wake ni ukafiri wenye kuhalalisha damu na mali .

Kumi na tano: kuweka wazi ya kwamba wao hawakutaka chochote isipokuwa uombezi (pamoja na hayo , lakini waliingia kwenye shirki)

Kumi na sita: Dhana yao ni kwamba wanachuoni waoambao walitengeneza picha za masanamu walikusudia kutaka uombezi wao (na hii ni dhana mbaya)

Kumi na saba: ubainifu mkubwa katika kauli yake mtume .(msichupe mipaka katika kunisifu kama walivyochupa mipaka wakiristo kwa mtoto wa Mariam (Nabii Issa) mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) amefikisha ujumbe kwa uwazi (akakataza kuchupa mipaka katika kumsifu na kuzidisha hilo na katika hilo wamelifanya baadhi ya watu wa umma huu , bali bali wamefanya mbaya zaidi)

Kumi na nane: Nasaha zake kwetu kuwa wameangamia wenye kuchupa mipaka (ni kwa ajili ya kutahadharisha hilo)

Kumi na tisa: Ni kuweka wazi ya kwamb masanamu hayakuabudiwa mpaka pale iliposahaulika elimu , katika hilo kuna ubainifu wa kutambua wsa kutambua thamani ya kuwepo elimu na madhara ya kukosekana kwake .

Ishirini: Hakika sababu ya kukosekana kwa elimu ni kufa kwa wanachuoni (hii ni katika sababu kubwa " pia watu kughafilika na kuipuuza elimu na kushughulika na mambo ya dunia na kutojali .

[20] MLANGO UNAOELEZEA UZITO KWA YULE ANAEMUABUDU ALLAH KWENYE KABURI LA MTU MWEMA ,VIPI ITAKUWAJE AKIMUABUDU HUYO MTU ?

Ameleta mtunzi mlango huu kutubainishia ugeni wa dini na kuacha watu Tauhid na yaliyokuja katika makatazo juu ya ibada ya Allah juu ya makaburi ya waja wema ili isije ikawa ni sababu Ya shirki (kumshirikisha Allah)

DALILI YA KWANZA

Katika sahihi ya Bukhari kutoka kwa Aisha radhi za Allah zimwendee. Hakika ya unmu salama alimtajia mtume (s.a.w) kanisa alioliona katika ardhi ya habeshi ndani yake kuna picha (sanam) akasema: hao ni wale anapokufa kati yao mtu mwema au mja mwema walijenga juu ya makaburi yao msikiti na kuwapiga picha zile picha zao hao ni viumbe wabaya " hawa walikusanya bainu ya fitina mbili fitina mbili fitina ya makaburi na fitina ya kufananisha.

- Hawa walikusanya baina ya fitina mbili haya ni maneno ya Ibn Taymia Allah amrehemu ameita hivi " hii ni fitina kwasababu Kuwazuia watu kwenye dini yao
- Asili katika makaburi iwe nje ya majengo hadi isije ikapatikana upenyo sababu ni shirki
- Makaburi ni fitina kubwa kuliko masanamu na hii ni kwa sababu ya mambo mawili :
    - Makaburi yapo kila sehemu kinyume na masanamu
    - Kwenye kaburi vinatokea vitu vingi ambavyo ni havitoki sehemu nyingine mfano kukhofu (woga)

DALILI YA PILI

Kutoka kwa Aisha na Ummu salama: amesema "pindi alipofikwa Mtume (Rehema na amani ziwe juu yake)hali ya umauti , akawa anatupa shuka lake kwenye uso wake anapozidiwa na hali ya uchungu na kifo huifunua kasha akasema hali ya kuwa yupo katika hali hiyo " laani ya Allah juu ya mayahudi na manaswara. Wameyafanya makaburi ya manabii wao misikiti kinyume na kuogopa kuyajaalia misikiti"

Ameipokea.

DALILI YA TATU.

Hadithi kaipokea Muslim kutoka kwa Jundabi ibn Abddallah amesema: nilimsikia mtume Rehma na amani ziwe juu yake siku tano kabla ya kifo hake akisema (hakika mimi najiepusha kwa Allah asije akanifanya ni kipenzi, hakika Allah amenifanya ni kipenzi kama livyomfanya Ibrahim kipenzi laiti ningekuwa ni wakufanywa katika umma wangu kipenzi basi ningemfanya Abu Bakari kuwa kipenzi wa ndani tambueni hakika walikuwa kabla yenu walikuwa waliyafanya makaburi ya manabii wao misikiti tambueni msije mkayafanya makaburi ni misikiti hakika mimi nimewakataza jambo hilo.) Mtume amekataza mwisho wa maisha yake kisha akamlaani mwenye kufanya hayo na kuswqali mbele ya mkaburi ni katika kufanya misikiti hata kama haikujengwa misikiti , na ndiyo maana ya kauli yake . (Alihofia kufanywa kuwa ni sehemu ya kuabudia hakika maswahaba hawakuwa ni wenye kujenga msikiti. pembeni ya kaburi la mtume na kila

sehemu au mahali ambapo pamekusudiwa kusaliwa, basi pameishakuwa ni msikiti wameshafanya . Bali kila mala panaposaliwa huitwa msikiti kama alivyosema mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) " imefanywa ardhi kwangu kuwa ni msikiti na kitu cha kujsafishia . "

- "pindi aliteremkiwa mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) na malaika wa kifo ili kuchukua roho ya mtume.
- "Khamiswa " shuka au vazi lenye mistari mistari .
- "laana ya Allah" yaani kutolewa na kuwekwa mbali, hii habari ya Allah , na pia yawezekana mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) aliwaombea mabaya
- "wamefanya makaburi ya manabii wao kuwa ni misikiti ima kwa kuyasujudu au kwa kujenga misikiti juu yake .
- "kudhihiri kaburi " kwa maana lingetolewa kutoka katika nyumba yake na kuzikwa katika makabari yaliyopo Baqiyu au sehemu nyingine .

  Kwa nini Mtume Rehma na amani ziwe juu yake amezikwa ndani ya chumba , wala hakuna yeyeto anaekiona , pia mchanga wa kaburi ?

  Ni kwa sababu ya kauli yake Mtume Rehma na amani ziwe juu yake " Hajapata kufa nabii yeyeote isipokuwa huzikwa pale alipofia ".
  - "Alikhofia " Mtume Rehma na amani ziwe juu yake kaburi lake kufanywa kuwa ni mzimu, au sanamu lenye kuabudiwa .
  - " Palikhofiwa " kwa maswahaba kufanywa kaburi la mtume kuwa ni wathani (mzimu) hii ni kwa sababu ya kkuwana pupa ya kuithibitisha Tawhidi .

Vipi tutamjibu Yule anaedai kuwa kaburi la mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) lipo ndani ya msikiti?

A. JIBU LA KIUJUMLA . " ni kwamba hayo ni maelezo yenye kutatiza ambayo hayajafafanuliwa , lililokuwa ni wajibu ni kuchukuwa maelezo yaliyokuwa fafanuliwa katika kitabu na sunna na wewe ni miongoni mwa wale wenye kufuata maelezo yenye kutatanisha , yasiyofafanuliwa , na kuacha yale yaliyokuwa wazi, hatuto kusiliza kamwe .

- **B. JIBU LA UFAFANUZI :**

1. Hakika msikiti haukujengwa baada ya kaburi bali umejengwa msikiti katika uhai wa mtume (Rehma na amani ziwe juu yake)
2. Hakika Mtume(Rehma na amani ziwe juu yake) hakuzikwa msikitini bali alizikwa nyumbani kwake, ilikuwa nje ya msikiti.
3. Kuingizwa vyumba vya mtume msikitini haikuwa kwa makubaliano ya maswahaba wote, bali ni baada ya kufariki wengi wao,na baadhi ya waliobakia walipinga, kama alivyopinga Said ibn Musaybu.
4. Kaburi halipo msikitini bali lipo katika chumba kilichotengwa. msikiti haujajengwa juu yake bali kaburi limekingwa na kuta tatu. Umewekwa ukuta pembeni hujaelekea kibla ili asije kuelekea mwenye kusali.
5. Msikiti wa Mtume una fadhila zake katika sala, na kufunga safari kwenda kufanya ibada, na mengineyo
6. **TANBIHI:** " Khulatun" ni mapenzi ya ndani ya moyo ni katika aina kubwa ya mapenzi na ni ya juu zaidi, Allah hakuyathibitisha tunavyotambua isipokuwa kwa viube wake wawili tu . ambao ni Ibrahim (Amani ziwe juu yake) na Muhammad (Rehma na amani ziwe juu yake) kwa maelezo haya utatambua ujinga mkubwa katika kauli za watu wa kawaida wasiokuwa na elimu wakisema : hakikika nabii Ibrahim ni mwana ndani wa Allah na Muhammadi ni kipenzi cha Allah , huku ni kupunguza haki yake . kwani wao wamefanya daraja la Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake)kuwa ni chini ya daraja la Nabii Ibrahim, na hawakutofautisha kati ya Mtume na mtu mwingine . kwani Alla ni mpenzi wa watu wema pia . Atakaemsifia Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) kuwa yeye ni mpenzi wa Allah,itakuwa amekosea.

DALILI YA NNE.

Hadithi kailezea Ahmadi kwa mapokezi mazuri – kutoka kwa ibn Masood radhi za Allah zimwendee. Hadithi ni marfuu . (Hakika miongoni mwa watu waovu zaidi ni wale ambao watakutwa na kiyama wakiwa hai. Na wale ambao wanafanya makaburi kuwa ni misikiti.)

Kaipokea Abuu hatim (katika sahihi yake)

- "Watu waovu zaidi " hakika watu wanatofautina katika maovu na shari, na hakika baadhi yao ni wabaya zaidi kuliko wengine .
- Ufupisho wa mlango.

  Ni lazima kujiepusha na shirki na vinavyopelekea au sababu zake . na hutiliwa nguvu zaidi kwa yale anaemuabudu Allah kwenye kaburi la mtu mwema, pia hujumuishwa kuswali na kufanya ibada zingine . atakaedai kwamba kutoa sadaka mbele ya kaburi hili ni bora zaidi kuliko sehemu nyingine basi kufanya hivyo ni mfano wa kufanya kaburi hilo ni msikiti wa kufanyia ibada

MAS-ALA MBALI MBALI

7. Moja: Kile alichotaja mtume ((Rehma na amani ziwe juu yake) kwa Yule atakaejenga msikiti

Ambao Allah anabudiwa ndani yake ,mbele kaburi la mtu mwema, hata kama nia ya mfanyaji ilikuwa sahihi ."jambo hili halihitaji nia" kwani hilo limefungamana na kitendo chenyewe , pia kujifananisha na washirikina , hakuhitaji nia .

Mbili: Makatazo ya kuweka masasnamu , na uzito wa jambo hilo (na hasa zinapokuwa picha na masanamu ya watu wenye kutukuzwa , mfano wa picha za viongozi na wazazi. Au picha za mawlii na watu wema).

8. Tatu: kuna mazingatio katika kuzidisha kwa Mtume ((Rehma na amani ziwe juu yake)

Kubainisha jambo hili , namna gani aliwabainishia kwanza hili . kasha kabla ya kufa kwake kwa siku tano alisema aliyoyasema , kasha alipokaribia kufa hakutosheka kwa yale aliyotanguliza kusema .

Nne: Mtume alikataza hilo kwa kufanyika katika kburi lake, kabla ya kuwepo kaburi lake.

Tano: Hakika huo ndiyo mwenendo wa mayahudi na manaswara, kwa makaburi ya manabii wao.

Sita: Mtume amewalaani mayahudi na manaswara kwa kosa hilo .

9. Saba: Hakika Mtume ((Rehma na amani ziwe juu yake)alikusudia kututahadharisha sisi kuhusu kaburi lake .

Nane: sababu ya kutodhihirishwa kaburi lake ni "kuhofia kuabudiwa, na kila Mtume huzikwa mahala alipofia"

Tisa: Miongoni mwa maana ya kuyafanya makaburi kuwa misikiti ni " kujenga misikiti juu yake , na kuifanya ya kusalia ."

Kumi: Hakika Mtume amelinganisha kati ya Yule mwenye kufanya hayo makaburi kuwa ni misikiti na kati ya Yule ambae kiama kitasimama kwao , wakiwa hai . Akataja sababu ya kupelekea hilo ni shirki kabla ya kutokea , pamoja na mwisho wake .

Kumi na moja: alitaja jambo hilo katika hotuba yake , kwa siku tano kabla ya kifo chake, ikiwa ni kuyakemea na na kuyajibu makundi mawili ambayo ndiyo makundi mabaya zaidi katika watu wa Bid-aa, bali baadhi ya watu wenye elimu wametoa makundi sabini na mbali kwenye hayo makundi mawili nayo ni Raafidhwa (Shia) na Jahmiya . kwa sbabu ya hawa Raafidhwa, ndiyo ikazuka shirki na kuabudu makaburi , na hawa ndiyo wa mwanzo kujenga msikiti katika makaburi

10. Kumi na mbili: Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alipewa mtihani katika kuzidi mamivu ya kutoka roho .
11. Kumi na tatu: Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) alikirimiwa kwa kuwa ni mwanadani wa Allah

Kumi na nne: kuwekwa wazi kwamba kuwa mwanandani wa Allah ni daraja la juu zaidi kuliko kuwa HABIB. (mpenzi)

Kumi na tano: kuwekwa wazi kwamba Abubakari Swidik ni swahaba bora (ubora kaika imani na matendo mema ni zaidi ya ubora wa nasabu kwa hiyo akatangulizwa Abubakari dhidi ya Alli.

Kumi na sita: Hii ni ishara yeye kuwa khalifa wa Mtume .

[21] MLANGO WA YALIYO KUJA. HAKIKA NI KUVUKA MIPAKA KATIKA MAKABURI YA WATU WEMA, KUYAFANYA KUWA NI MASANAMU YENYE KUABUDIWA KINYUME NA ALLAH.

- Hii sababu ya tatu kutokea kwa shirki, jambo hili hurejea kwa wale wenye kuvuka mipaka ,mpaka kupelekea kuabudiwa makaburi au kuabudu wenye makaburi .
- Neno (GHULUWU)maana yake ni kuvuka mipakak katika kusifia na kuponda .
- Vigawanyo vya watu katika kuyaelekea makaburi ni viwiwli, na cha kati na kati :
  Kiganyo cha kwanza ni kwa wale waliovuka mipaka kuyabudu na kujengea makubba juu yake .
  Cha pili ni wale waliozembea kuruhusu makabui, katika haki zake kama vile kuyaheshimu, na kukaa juu yake, na kuyafukua na haki ni kuwa kati na kati, kwa kuhifadhi heshima na utukufu wake ,na kutovuka mipaka ndani yake , mpaka yakafia hatua ya kuabudiwakinyume na Allah .

DALILI YA KWANZA HADI YA NNE

[1] Hadithi kailezea Imamu Malik katika kitabu (Almuwatwaa) Hakika mjumbe wa Allah Amesema: (Ewe mola wangu usijaalie kaburi langu sanamu lenye kuabudiwa, (hasira za Allah zimezidi juu ya watu wenye kufanya makaburi ya manabii wao kuwa misikiti(sehemu ya kuwabudu)

[2] Na pia kailezea ibn Jariri kwa mapokezi kutoka kwa Sufian,kutoka kwa Mansour, kutoka kwa Mujahid : “Je! Mmemuona Lata na Uzza?” Amesema: “Alikuwa akiwaadalia uji , akafa , wakakaa wakifanya ibada katika kaburi lake)

[3] pia amesema Abu-jawzaa, kutoka kwa ibn Abas (alikuwa akiandaa uji kwa mahujaji)

[4] kutoka kwa ibn Abasi (R.a) Amesema: “Amewalaani mjumbe wa Allah wanawke wenye kuzuru makaburi,na wale wanaofanya makaburi misikiti nakuwasha makandili (taa za kufanyia ibada zao) wameipokea watu wa Sunna.

- “imezidi hasira ya Allah“: Sifa yake ya ukweli imethibiti kwa Allah si mfano wa hasira za viumbe.
- “wameyafanya makaburi ya manabii wao kuwa ni misikiti ima kwa kuya sujudia au kujenga misikiti juu yake .
- Je! Kujibiwa dua ya mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) isije ikafanywa kaburi lake kuwa ni sanamu la kuabudiwa, au hekima za Allah zimehukumu kinyume na Hivyo? amesema ibn Qayyim Allah amrehem : hakika Allah alijibu dua yake na haikutajwa kuwa kaburilake limefanywa kuwa au mzimu , bali liliwekewa kuta tatu. Hivyo mola mlezi wa viun\mbe amejibu dua yake na akalizungushia kuta tatu . ni sahihi kwamba hupatikana badhi ya watu huvuka mipaka katika hilo kaburi , lakini hawakufikia hatua ya kulifanya kuwa ni kaburi pia ni sanamu lenye kuabudiwa

- "je umemuona ?": Ni nini mnasaba wa haya masanamu kwenye hizi aya kubwa ambazo aliziona mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) usiku wa miiraji .
- "SAWIQA":NI ngano ambayo hukaangwa kasha husagwa kasha huchanganywa na tende na hupewa mahujaji .
- "SURUJU "ni taa zilizokuwa nyingi zinzowashwa juu ya makaburi usiku na mchana, kwa aji ya kuyatukuza, na kuchupa mipaka kwenye makaburi .]
- Wanawake kutembelea makaburi ni katika madhambi makubwa na hivyo kuyafanya kuwa ni misikiti, na kuwasha mataa juu yake ni laana kwa wenye kufanya .
- VIGANYO KATIKA KUZURU MAKABURI; [1] Kiheria: hairuhsiwi kufunga msafara na kwenda kwenye hayo makaburi,na anuie kwa ziara hiyo kujikumbusha akhera na kuwaombea maiti . [2 Ikiwa atanuia kuwaombea maiti tu , basi itakuwa ziara ya kishirikna, [3] na akiwa amenuia kumuomba Allah mbele ya makaburi na maiti basi ziara hiyo itakuwa ni ziara ni bidaa.

MAS-AIA YANAYOHUSIANA NA SOMO HILI .

Moja: Tafsiri ya neno (AUTHAN) "chochote chenye kuabudiwa kinyume na Allah ,sawasaw iwe ni sanamu, au kaburi, au kitu kingine"

Mbili: Tafsiri ya neno (IBADA) "kujidhalilisha na kunyenyekea mwenye kuabudiwa (Allah) kwa kumuogopa na kutarajia, na kumpenda, na kumtukuza "

Tatu: Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) hakujilinda ispokuwa katika jambo ambalo anakhofia litatokea .

Nne: Mtume (Rehma na amani ziwe juu yake) amekutanisha hukumu ya wanawake kutembelea makaburi , na hukumu ya kufanya makaburi ya manabii kuwa ni miiskiti.

Tano: pametajwa kuzidi ghadhabu za Allah, kwa wenye kufanya makaburi ya manabii kuwa ni misikiti .

Sita: nayo ni katika mambo muhimu kufhamu sifa ya ibada ya Laata, ambayo ni miongoni mwa masanamu makubwa.

Saba: kufahamu ya kwamba hilo ni kaburi la mtu mwema.

Nane : ni kwamba (LAATA) ni jina la mwenye kaburi , na imetajwa sababu ya kitwa jina hilo .

Tisa : Mtume amewalaani wenye kuzuru makaburi kwa wanawake .

Kumi: Mtume amewalaani wenye kuwasha taa kwenye hayo mkaburi .

- MAS-ALA MUHIMU: kuchupa mipaka kwenye makaburi ya watu wema,huyafanya makaburi hayo kuwa ni masanamu , kama ilivyokuwa kwenye kaburi la Laata .
- MAS-ALA: pindi Mwanamke anapoenda rawdhwa (kiwanja cha peponi) katika msikiti wa mtume, kwa ajili ya kuswali, kaburi la Mtume lipo karibu na maeneo hayayo basi atasimama na kusalimia, hakuna tatizo hilo . lakini ni bora ajiweke mbali na msongamano na kuchanganyika na wanaume na ili wanamuona wasije kudhania kwamba inafaa kwa mwanamke kukusudia kuzuru makaburi .

[22] MLANGO UMEKUJA KATIKA KULINDA UTUKUFU WA MTUME (Rehma na amani ziwe juu yake) UPANDE WA TAWHID NA KUZIBA KILA NJIA INAYOPELEKEA KWENYE SHIRKI.

30. Sahihi: kutoa dalili kisha msimamo ☐ msimamo kisha dalili ☐
31. Nabii (swalallahu alaiyhi wasalam) ni sharafu: mja wa Allah na mtume wake ☐ Muhammah bin Abdillah ☐
32. Ndoto njema nayo ni: imefungamana na mazuri ☐ inakuja kinidhamu ☐ yote
33. Ndoto ikiwa kinyume na nidhamu nayo ni habari mbaya. Ndio ☐ hapana ☐
34. Malaika ni machukizo kwa shetani. Ndio ☐ hapana ☐ ni suna iwe
35. Ikijulisha kanuni juu ya kupinga ndoto ya kisheria kuzingatia ☐ sio kuzingatia ☐
36. Kauli ya mmeo: “weusi wa siku katika siku niliyokuoa : inafaa ☐ haifai ☐
37. Sahihi ni: haifai mauzi ya dharura ☐ inalazimu mauzi ya dharura ☐
38. Majina ya Allah mazuri na mwaka ni jina halibebi maana isipokuwa jina la wakati. Ndio ☐ hapana ☐ “ na mimi ni katika mlango wa habari
39. Kauli “zama mbaya”: haramu ☐ inafaa kwasababu ni katika mlango wa habari ☐
40. Kauli: “mtoto wa Fulani ni mwaka wa njaa: haramu ☐ inafaa kwa sababu ni katika mlango wa habari ☐
41. Kauli yake aridhi hifadhi uliyonayo ni dua kinyume na Allah shirki ☐ inafaa ☐
42. Aina za kutukana mwaka: 1. …… na hukumu yake ……..
    2……hukumu yake ……
    3……..hukumu yake ……..

43. Kauli: (Tabia ina maajabu na siri) au: (hii ni katika vitendo vya kimaumbile. Ndio ☐ ☐
44. Hakimu (Qadhi) amekusanya baina ya kulazimiana na kutoa fatwa. Ndio ☐o ☐
45. Kauli (amehukumu hukumu ya kane ya saba) Inafaa ☐i bora kuiacha ☐
46. Shaykhul –Islaam ni: shekh yeyote amerejea katika wislamu. ☐Ni Yule inayopatikana kwake athari nzuri katika kulinda uislam ☐
47. (Inatakiwa ☐ Haitakiwi ☐) Kuchunga upande wenye kusifiwa kwamba asije akadanganyika na akadanganya ☐
48. Jina linalopendeka kwa Allah ni lile linalo julisha kujidhalilisha na kunyenyekea. Mfano (shahan shaha ☐ Abdul-rahman ☐)
49. Kujiita mfalme wa wafalme na hakim wa mahakama. Inafaa ☐Ni haram ☐i dhambi kubwa ☐
50. Kumlani jina ambalo linaanzia kwa (Ab) au (umm) au (Akh) au (Amm) au (Khal) na inakuwa kwa lengo la: kuishi ☐ kutia dosari ☐ kuwa karibu na kitu na kulazimiana nacho ☐ kilimwengu ☐ yote ☐
51. Anapatikana katika maswahaba anayeitwa Hakiim, Na hakulibadili jina hilo mtume (swalallahu alaiyhi wasalam) kwa sababu halikukusudiwa isipokuwa jina lenye kuainisha mwenye kuitwa moja kwa moja (Ni sahihi ☐sio sahihi ☐) Na ina katazwa katika majina yake Allah (yanayo muhusu yeye pekee) ☐ yanayokusudiwa kuchunga sifa ☐ote ni sahihi ☐
52. Kufanya kunai (jina linaloanza na Abu au Umm) hokum yake ni Inaruhusiwa ☐apendeza ☐
53. Atakae fanya matani kwa kitu ambacho ndani yake kwa utajo wa Allah au Qur'an (mtume) makusudio ya mtume ni: Muhammad (swalallahu alaiyhi wasalam) ☐tume ☐e
54. Kukataa kwa istilizai katika imani nikukataa kukubwa na haiwezi kupigiwa taswira kwamba muislam hajui jambo hili. Ni sahihi ☐io sahihi ☐
55. Sharti za toba ya mwenye kufanya Istili zao (kucheza shepe)
    1) _____ 2) _____ 3) _____
56. Hakuna budi kufanya mlango wa istihizaai na kuto kupuuzia. Sahihi ☐o sahihi ☐
57. Kuna wanao walinda wanao mtukuza Allah hata kama ataitukana yeye au mama yake au kumchukua izza. Ni sahihi ☐sio sahihi ☐
58. Ni wajibu awabainishie watu hatari ya mlango huu. Na ni ukafiri unao mtoa mtu katika uislam na wala hatusubiri mpaka ipatikane tusi na istilizai ☐ sahihi ☐o sahihi
59. Kuna wanaosema: Tuna muuliza mwenye kutukana na mwenye kufanya istilahi je anakusdia kutukana au laa, Na kauli hii ni: batili ☐ahihi ☐
60. Katika kutukuza haki ya kiumbe kwa muumbaji ni kauli kwamba mwenye kutukana anapewa udhuru kwa gadhabu, pamoja na kutokuwa na udhuru katika kumtukana raisi au baba au kutaka (kuchukua) pesa dhulma mfano; Ni sahihi ☐io sahihi ☐

61. Fungu katika huu mlango, una faida sana na shukrani ni za Allah katika baadhi ya nchi Na haki kupuuza kuifanya mkubwa na mdogo wanatukana katika nchi zingine. Sahihi ☐ o sahihi ☐
62. Mwenye kupuuza ni bora kuliko mwenye kusujudia sanam. Sahihi ☐ o sahihi ☐
63. Unaweza usisikie kutoka kwa mayahudi na wakiristo wanao mtusi mola au musa au Issa au dini na lakini unaweza ukasikia hilo kwa wenye kudai kuwa ni waislam. Sahihi ☐ o sahihi ☐
64. Muumini ni haki pindi inapotajwa qur'an au hadithi anaogopa na inazidi imani yake ama kwa mnafiki anazidisha zarau na kupuuza na anacheza na anasema maneno ili awachekeshe watu. Ndio ☐ sio ☐
65. Je unatuma video ndani yake kuna anae mtukana mama yako? Au unamsikiliza? Vipi kwa mwenye kumtusi mama wa kila muumini? Ndo ☐ apana ☐
66. Ni wajibu pale inapokuja video ndani yake kuna matusi au shutma, kusikiliza na kuieneza ☐ kuifuta palepale ☐
67. Kukusanya video za matusi na upuuzi ni njia ya: wema waliotangulia ☐ anafiki ☐
68. Kurejesha na kutukana na istilizai jambo lake ni kubwa na kuna wanazuoni wamesema jambo hilo halina toba na hakuna budi kadhi amuue na wala hatosaliwa na wala hatoombewa dua na wala hatozikwa pamoja na waislam ☐ ahihi ☐ o sahihi
69. Mwenye kutukana anaposema kuwa yeye ametubia kisha akarejea katika kutukana kwa mara nyingine hii ni dalili ya uongo wake. Ndio ☐ o ☐
70. Mnafiki anapotukana anasema: sijakusudia na haya ni maneno kwa ulimi tu. Ndio ☐ ☐
71. Katika mambo yanayo julisha juu ya ukweli wa toba ya mpuuziaji kauli yake kunako kutukana na kupuuza kwamba ni ukafiri na Allah anajitenga naye. Ndio ☐ o ☐
72. Ambae anasikiliza matukano (matusi) na kupuuza na wala haipingi au kugeuka hukmu yake mfano wa mpuuziaji. Ndio ☐ sio ☐
73. Shetani anaweza akafungua milango ya kheri ili akuweke katika ukafiri na huyu mtu alikuwa katika taabuki. Ndio ☐ sio ☐
74. Inapatikana faida kutokana na hadithi (mazungumzo) ya mwenye kucheza shere ni ukafiri kwa mwenye kutukana maswahaba. Ni sahihi ☐ sio sahihi ☐ kwa sababu kuwatia dosari (kuwaponda) maswahaba, ni kutia dosari kwa Allah ☐ mtume (swalallahu alaiyhi wasalam) ☐ dini ☐ katika swahaba ☐ yote
75. Atakae kuwa kusamehe kwake ni uharibifu na sio kutengeneza. Hakika (anapata dhambi ☐ hapati dhambi ☐)
76. Mwanadamu anapo egemeza neema kwa matendo yake na dhima yake ndani yake kunakuwa na shirki katika (matendo ya Allah ☐ ibada ☐) na anapo iegemeza hio neema kwa Allah, lakini akidai kuwa anastahiki hio neema, basi ndani yake kuna aina ya kujikweza na kujinyenyua (Ndio ☐ sio ☐)

52. MLANGO ULIOKUJA KUELEZEA KUA HAIFAI KUSEMA: SALAM (AMAN) ZIMWENDEE ALLAH (UHARAMU)

KWANINI?

Kwasababu hicho kinapingana na uhakika kwani Allah anaombwa na haombewi kwa kuwa yeye ni tajiri, lakini husifiwa Allah kwa sifa za ukamilifu

Kwa sababu kamwombea Allah dua kama hii kunapelekea mtu kufikiria kua kuna mapungufu katika haki ya Allah, kwani hatuna kinachoombewa salamu isipokuwa kitu hicho kinasifika na sifa ya upungufu na Allah ametakasika na mapungufu

DALILI YA KWANZA:

Katika kitabu cha sahihi kutoka kwa ibn Masud radhi za Allah zimfikie, amesema: ilikuwa tukiwa na mtume katika swala tunasema: salam (amani) zimwendee Allah kutoka kwa waja wake salam (aman) zimwendee Fulani na Fulani mtume akasema; msiseme salam (aman) zimwendee Allah kwani Allah ndie (Asalaam) amani.

- Assalaam ni jina lililothibiti linapinga mapungufu yote na aibu ambayo mwanadamu ana fikiria akili yake kuhusu Allah, kwani Allah hana mapungufu katika dhati yake au sifa yazake au vitendo vyake au hokum zake na maana ya jina lililothibiti ni uthibiti wa jina hilo kwa Allah na sifa zilizobebwa ndani ya jina hili ambayo ni amani na jina Assalaam lina maana nyingi.

Maamkizi: kama inavyosemwa msalimie fulani

Kusalimika kutokana na mapungufu na maafa kama kusema (salam ziwe juu yako ewe mtume)

Assalam ni jina katika majina ya Allah.

MAS-ALA MBALI MBALI.

Moja: Tafsiri ya jina Assalaam (jina la Allah) na maana yake Allah amesalimika na kila mapungufu na aibu

Mbili: Ya kwamba ni maamkizi.

Tatu: Ya kwamba haifai kumtakia salaam Allah (na kwa hali hiyo inakuwa haraam)

Nne: tatizo katika hilo (au sababu ya katazo) ni kwamba Allah mwenyewe ndie Assalaam (amani)

Tano: kuwafundisha mtume maswahaba maamkizi yanayofaa kwa Allah (katika tashahhud (kikao katika swala) hatusemi kwa kiumbe, Attahiyyaatu).

[53] MLANGO KAULI (EWE MOLA WANGU NISAMEHE MIMI UKITAKA) "UHARAMU WA KUTENGANISHA KATIKA DUA"

huu mlango unabainisha ukamilifu na ufalme wa Allah (subhanahu wataala) uwepo wake na fadhila zake na mahadhura katika huu umewekewa zingatio

Hakika unafungamana na kutosheka kwa mwanadamu juu ya Allah nah ii kinyume uhalisia na sio katika adabu	Hakika unafungamana kwa kuwa hili jambo ni kubwa juu ya Allah huenda ikampunguzia na akashindwa na sio hivyo	Hakika unafungamana kuwa Allah ni mukaratu na jambo sivyo kilivyo

DALILI YA KWANZA

Katika sahihi kutoka kwa Abbu hureyra. Hakika mtume(swallalahu alaiyh wasalam) amesema: asisema mmoja wenu: ewe mola nisamehe mimi ukitaka, ewe mola wangu nihurumie mimi naazimia kuomba hakika Allah hakuna wa kumlazimisha yeye.

Na kutoka kwa muslimu "na waombe kwa wingi, kwani hakika Allah hakiwi kikubwa kwake alichotoa.

Kuweka matarajio katika dua ya istikhara, si kuweka matarajio katika matakwa na hakika ni katika mambo yasio julikana kwangu mimi sikjui je hilo ni kheri kwangu, au sio kheri? Hivyo imekuja kwa mnasaba hadithi (nihuishe, madamu uhai ni bora kwangu)

Mas-ala.

Moja: makatazo katika kufanya :"istithnai" kutenganisha katika maombi

Mbili: kubainisha sababu katika hili

Tatu: kauli yake: (Aazimie kuomba) (Pindi unapoomba azimia, wala usibabaike)

Nne: (Kuomba kwa wingi) "yaani anaomba anachotaka, hakuna kitu kigumu au kinacho zuilika juu ya Allah

Tano: Sababu ya hili jambo: [1] kubainisha utukufu wa sharia [2] kuongezeka utulivu kwa mwanadamu [3] kiasi pindi itakapo kuwa kuomba ni hukumu.

[54] MLANGO WA: HASEMI MTUMWA WANGU WA KIUME NA MTUMWA WANGU WA KIKE

HUKUMU YA KUSEMA. "MTUMWA WANGU WA KIUME" "MTUMWA WANGU WA KIKE)

Utegemezi katika nafsi yake: ina muonekano wa aina mbili

Ategemeze kwa mwingine: mfano, aseme: huyu ni mtumwa wa Fulaniau huyu ni mtumwa wa kike wa Fulani, Basi hiyo ndo inafaa

Akiwa anasema kumzungumzia mtumwa wake kwa wakati uliyopo au kumzungumzia mtumwa wa kike. Tuangalie je inapangika kuwa sentensi yenye faida, inafungamana namtumwa au boss endapo ikipatikana kitu cha kuharibu itazuilika au isipopatikana basi itafaa kutumika.

Iwe kwa matamshi ya khabar: kama kusema: nimemlisha mtumwa wangu wa kiume au nimemuacha huru mtumwa wangu wa kium, na hapa ndani yake kuna ufafanuzi.

Iwe kwa matamshi ya wito: kama kusema: Ewe mtumwa wangu basi hiyo inakuwa imekatazwa.

Ikiwa nasema kumzungumzia mtumwa wake asiye kuwepo au kumzungumzia mtumwa wake wa kike, basi hiyo inafaa

DALILI YA KWANZA.

Kaika hadithi sahihi ya Abiy Hureyira radhi za Allah ziwe juu yake. Anasema rasulullah (subhanahu wataala) anasema: "asiseme mmoja wenu: mlishe mola wako, muoshe mola wako na aseme: (bwana wangu na mola wangu), wala asiseme mmoja wenu mtumwa wangu wa kike na wa kiume, na aseme mtoto wangu wa kike na wa kiume anasema: (Kijana wangu wa kiume na wakike)

- Asiseme mmoja wenu: mrishe mola wako muoshe mola wako": kwa sababu inarudi katika upande wa umungu.
- Na aseme: "bwana wangu na mola wangu: "na haya mazungumzo ni ya mtumwa, na hayo maneno sio ya lazima bali ni ya mwongozo wa halali: kwa sababu maulamaa wamesema: hakika ya maamrisho yakija, inatanguliza kitu cha makatazo: itakuwa ni kitu cha halali, na miongoni mwake kauli ya Allah: mkisha maliza ibada za Hajji basi mfanye yale mlozuiliwa kuyafanya kabla ya ibada
  "wala asiseme mmoja wenu": makatazo Ikiwa ni katika uharamu au machukizi, wala isidhaniwe kua ni miongoni mwa Ibada ambayo haiwi isipokuwa ni ya Allah aliye tukuta. Neon Abdi Anakuwa mtumwa wa kiume na neon Ammaty anakua ni mtumwa wa kike.
- Na aseme: mtoto wa kiume na mtoto wa kike na kijana wangu hayo mazungumzo ni ya bosi wao yaani mtu mwenye cheo kwao na hapo inapatikana sheria iliyopangwa.

Mlango wa haramu, hufungua mlango wa kufaa, na ndani yake kuna tanbihi katika kuthibitisha tawhid mpaka katika matamshi .

MAS-ALA MBALI MBALI

Ya kwanza : Makatazo katika kusema (mtumwa wangu)

Ya pili : Asiseme mtumwa (mola wangu) wala asiambiwe (mlishe mola wangu) .

Ya tatu : kumfundisha wa kwanza kusema (kijana wanngu msichana wangu) .

Ya nne kumfundisha wa pili kusema (bwana wangu na mola wangu)

Ya tano : kuzindua katka makusudio , nayo kuthibitisha tawhid mpaka kwenye matamshi .

[55] MLANGO HUU NI UNAOBAINISHA HAREJESHWI KWA MWENYE KUOMBA KUPITIA JINA LA ALLAH KWA UHARAMU AU KARAHA.

AINA ZA KUOMBA KWA JINA ALLAH

Kuomba kwa sheria ya Allah: yaani anayeomba ombi ambalo sheria imeliruhusu kama kuomba fakiri sadaka.

Kuomba kwa jina la Allah kwa maneno: mfano mtu aseme: Nakuomba kwa kwa jina la Allah.

JE INAFAA MTU KUOMBA KWA KUTUMIA JINA LA ALLAH AU HAIFAI?

Kuomba kwa jinsi kulivyo ni machukizo au haramu ila kwa haja au dharura kwa ajili hii mtume alifunga ahadi na maswahaba zake wasije wakawaomba watu chochote, ama jibu la muombaji haiwi kinyume kwa muombaji kwa Yule mwenye kuomba.

Kuomba kupitia jina la Allah: hii ni wajibu kumpa hata kama haikuwa ni mweye kustahili kwa sababu ameomba kwa jina la mtukufu kujibiwa kwake ni utukufu wa kutukuza utukufu. Lakini akiomba uovu au kujibiwa kwake ni dhamira juu ya masuulu hatojibiwa.

Kuomba moja kwa moja: kama vile aseme "ewe Fulani nipe, ikiwa ni kile anachokiomba katika vitu ambavyo ni halali kupewa kisheria basi atampa kitu hicho

DALILI YA KWANZA.

Kutoka kwa ibn Omari (radhi za Allah zimwendee: amesema: amesema mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake "mwenye kutafuta msaada kwa Allah msaidieni ila mwenye kuomba kwa Allah mpeni na mwenye kukuiteni mwitikieni na mwenye kukufanyieni jambo jema mshikilieni ikiwa hamtopata cha kumlipa basi muombeeni dua hadi awaone nyinyi kuwa mmemlipa (wema wake)"

Amepokea Abbu Daudi na Nasai kwa sanadi sahihi

- "mlindeni": Isipokuwa akitaka msaada jambo la hekima kwake au kuaminina katika maovu na uadui.
- Je kuitikia mwito ni katika haki ya Allah au ya mwanadamu? Ni haki ya mwanadamu na kwa ajili hii laiti ukitaka kwa mwenye kuita akusamehe kuitikia wito akakubali. Hakuna madhambi kwako lakini ni lazima kwa amri ya Allah, lakini ikiwa amekusamehe kwa sababu ya kukuonea haya au fedheha hali ya kuwa nafsini mwake hajaridhika hapo itakuwa ni wajibu kutakia wito wake.

- "mwitikieni (wito wake)": makusudio yake ni wito ambao inaikiramu sio wito tu na kongamano la wanachuoni wa elimu ya juu, hakika kuitikia wito ni jambo la sunna isipokuwa wito wa harusi huo ni wajibu kwa masharti (6)

1. Isiwe kwa mwitaji ambayo sio wajibu kwenda au sunna
2. Isiwe kuna jambo baya katika sehemu ya witoikiwa kule kuna jambo baya ikiwa anaweza kutoa ni lazima kwenda kuitikia mwito au kupandilisha baya.
3. Awe anaita mwito awe mwislamu kinyume na hivo hakuna kuitikia mwito
4. Usiwe mwito wa haramu
5. Usifungamane mwito kuangusha uwajibu au kilicholazimishwa
6. Usifungamane dharura juu ya aliyewajibishwa kama safari au makundi ya watu wenye kuhitajia

- Je mwito ambao ni wa kugawiwa ni kama mwito wa kuongeleshwa? Pindi atakapo juu au ikamfunika dhana hakika ambaye ametumwa kwake makusudio yake ni mwaliko basi itakuwa na hukumu ya wito wa kuzungumza.
- "na mlipeni na malipo yako maana mbili (2)
  1. Kuhamasisha mwenye wema juu ya kufanya mema
  2. Hakika mwanadamu anavunja unyonge ambao inampelekea kwake katika mema.

MAMBO YANAYO AMBATANA NA MLANGO HUU.

Jambo la kwanza: kutaka msaada katika msaada wa Allah "atakae taka msaada kwa Allah ni wajibu kupata isipokuwa katika kitu lazima kufanya kitendo au kuacha hakika hapewi msaada.

Jambo la pili: kupewa kwa aliye muomba Allah

Jambo la tatu: kuitikia mwito

Jambo la nne: kutoa maipo juu ya jambo jema, "yaani kuulipa wema aliyekuanyia jambo jema

Jambo la tano: hakika dua ni malipo kwa hakuwa na uwezo wa chochote isipokuwa dua, basi dua hiyo ndio itakuwa malipo ya wema huo katika wema amao mtendaji wake haipwi kidesturi basi ataombewa dua.

Jambo la sita: kauli ya mtume: "hadi mtakapo ona hakika nyinyi mmemlipa asizembee katika dua yake isipokuwa aombe sana hadi ajue au anafunikwa na dhana yakuwa tayari amemlipa (kwa dua).

(56) HUU NI MLANGO "UNAOFAFANUA KAULI YA MTUME HAIOMBWI KWA KUTUMIA THATI YA ALLAH(USO) ISIPOKUWA PEPO.

MAANA YA TAFSIRI YA MLANGO HUU

Au: pindi ukiomba kwa dhati ya Allah basi omba pepo wala usiombe chochote katika mambo ya duniani

Yaani usimuombe yeyote katika viumbe kwa dhati ya Allah na viumbe hawawezi kukupa pepo.

Ndani ya maelezo hayo kuna kumtukuza Allah, pindi haombwi Allah kwa dhati yake tukufu (uso) mkarimu isiopokuwa pepo au yanayopelekea kupata pepo.

DALILI YA KWANZA.

Kutoka kwa Jabiri amesema: amesema mjumbe wa Allah rehema na Amani ziwe juu yake: hapaombwi kwa kutumia dhati ya Allah isipokuwa pepo.

Amepokea Abu daudi.

- "uso wa Allah" kuna kuthibitisha uso wa Allah, nao umethibiti kwa dalili za quran na sunna na jamaa na uso wa uhakika haulinganishwi na nyuso za viumbe.

MAMBO YANAYOAMBATANA NA MLANGO HUU.

Jambo la kwanza: Katazo juu ya kuombwa kwa uso wa Allah isipokuwa kiwe ni maombi ya juu mno hakika ni katika adabu usiombe kwa uso wa Allah isipokuwa iwe ni jambo la akhera: kufaulu kuingia peponi au kuokolewa na moto.

Jambo la pili: kuthibitisha sifa ya uso (kwa Allah)

Hukumu ya kuomba kwa sifa za Allah.

Hiafai kuomba sifa kama kauli za baadhi: ewe rehema za Allah, Ewe uso wa Allah, Ewe nguvu za Allah! Maombi haya ni uzushi hayatambulikani kwenye dalili za kisheria, wala hayakupokelewa kwa waja wema waliotangulia Na amesema Sheikhul-Islam Ibn Taimiyah maombi ya namna hii ni kufru.

(57) HUU NI MLANGO ULIOKUJA KUFAFANUA KUHUSU (NENO) LAITI!

VIGAWANYO VYA KUTUMIA NENO LAITI

Laity iliyoharamishwa na inaeweza kufikia kwenye kufru. Ni kutumia neno hilo kupinga sheria ya Allah	(Lau tungelikuwa tuna lolote katikajambo hili kusingelikuwa hapo): Huu ni upingaji wa wanafiki katika sheria ya mtume, na wakasema, lau wangelitutii na wakarudi (wakaacha kupingana vita vya uhuru) kama sisi tulivyorudi wasingeliuwawa, basi maoni yenu ni bora mno kuliko sheria ya mtume.
Laity iliyo haramishwa. Ni kutumiwa neno hilo katika kupinga Qadar ya Allah.	(Lau (laiti) wangelitutii (wakatusikiliza) wasinge liuwawa): Yaani laity wao wangelibakia (majumbani): wasingeuwawa, basi hao (wanafiki) wanaipinga Qadar ya Allah (aliyokwisha ipitisha)
Laity iliyoharamishwa ni kutumiwa neno hilo kwa ajili ya majuto	(kama mtu akisema) "Laiti ningelifanya hivi ningelikuwa hivi na hivi" kwa sababu majuto huipa nafsi huzuni na majonzi na ili hali Allah anatutaka tuwe katika uchangamfu (wa nafsi)
Laiti iliyo haramishwa ni kutumiwa neno hilo katika kujitetea kupitia Qadar katika kufanya maasi.	(Lau angelitaka Allah tusingeli shiriki) nah ii ni kauli ya batili, lakini inasihi kujitetea kupitia Qadar katika kupata misiba (matatizo) si katika mambo maovu, na itafahamika kwa mtu kutubia na kuyatoa kwenye maasi yote.
Ni kutumiwa neno laiti katika kutamani jambo: Ikwa jambo hilo ni la kheri basi itakuwa ni kheri na ikiwa jambo hilo ni shari basi itakuwa ni shari.	"Laiti ningelikuwa na mali mngelifanya kama anavyofanya Fulani" Mtu huyu ametamani kufanya kheri, mtume akasema, mtu huyo atalipwa kwa kuzingatia nia yake, basi malipo yao yako sawa (aliyetoa na aliyetamani) na mtume akasema kumuhusu Yule aliyetamani jambo baya (ovu) basi atalipwa kwa kuzingatia nia yake, madhambi yao yako sawa (Yule aliyefanya ovu na yule aliye mtania kwenye ovu hilo kulifanya)
Laiti inayofaa: Ni ile inayotumiwa kwenye mazungumzo ya kawaida tu.	Lau ningelitambua kwenye amri yangu hii, ningelimwamrisheni toka mwanzo na msingechukua mnyama (kwa ajili ya hija) haya ni mazungumzo, kwa sababu mtume hatamani kitu chochote ambacho Allah amekadiria kinyume chake, mfano wake ni kama kusema. Laiti lingetuhudhuria darsa ningepata faida.

DALILI YA KWANZA MPAKA YA TATU.

1. Ni kauli ya Allah wansema: Lau ingelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusingeliuliwa hapa……..
2. Na kauli yake Allah: Hao ndio walio waambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wangelitutii wasingeliuliwa……
3. Na hadithi iliyo kwenye sahihi ya Bukhar, kutoka kwa sahaba Abu Huraira, Hakika mtume wa Allah amesema: Pupia (kufanya(matendo yatayo kunufaisha na utake msaada kwa Allah wala usizembee na ikiwa litakufika jambo (dhara) lolote usiseme: Lau mimi ningelifanya hivi igelikuwa hivi na hivi, lakini sema: Allah ndio aliyepanga na lile alilolitaka ndio amelitenda kwa sababu neno lau (laiti) hufungua kazi za shetani.

- (Wanasema: Lau tungelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusingeliuliwa hapa). Kauli hizi ni katika kupinga wanafiki sheria ya Allah, kwa sababu (wanafiki) walimlaumu mtume pale alipotoka kwenda vitani bila kukubaliana nao (katika rai yao)
- Inawezekana pia kauli hizo zinapinga Qadar ya Allah, kwa maana (sisi hatukutaka tuje tuuwawe)
- (Hata ndio waliowaambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wangelitutii wasingeliuliwa) ndani ya haya maneno ya wanafiki kuna kuwapinga waumini, (kufuata dini yao) na kuipinga Qadar ya Allah na hukumu zake, pia kama uoga wa kupigana jihadi.

- Yeyote mwenye kuipinga Qadar ya Allah huyo hajamridhia Allah kuwa mola wake mlezi na wala hajaikubali tawhid ya rububiyah (utawala wa Allah kwa viumbe vyake)
- Kwenye hadithi hii kuna mafundisho yafuatayo
  1- Kupupia kutenda matendo yenye kunufaisha na kuacha yenye madhara
  2- Kutaka msaada wa Allah
  3- Kuendelea kutenda matendo ma kutokata tama (ya kutenda)
  4- Itakapo tokea kinyume na makusudio (aliyoyatarajia) hali hiyo haipo kwenye uamuzi wako bali ni katika mopango ya Allah basi yategemeze mambo yote kwa Allah

MAMBO YANAYOAMBATANA NA MLANGO HUU (WA QADAR)

Jambo la kwanza: Tafsiri za aya mbili katika sratul – Imram, (Aya ya kwanza inafafanua kupinga sheria ya Allah, na aya ya pili inafafanua kupinga Qadar ya Allah.

Jambo la pili: katazo la wazi kuhusu kusema (Lau (laiti) mimi) pete linapokufika jambo lolote (baya)

Jambo la tatu: imetolewa sababu ya jambo hili kuwa linafanyiwa kazi ya shetani (kwa kuwa mtu manajuta)

Jambo la nne: maelekezo katika kutamka maneno mazuri (Allah ndio aliyepanga na amefanya alilolitaka yeye)

Jambo la tano: Maamrisho ya kupupia kutenda matendo yenye kunufaisha pamoja na kuomba msaada kwa Allah

[58] huu ni mlango katazo la kutukana upepo (kuridhia Qadar ya Allah.)

DALILI YA KWANZA.

Kutoka kwa baba yake kaabi Allah amrizie: Hakika mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema: “msitukana upepo, pindi mtakapo ona kinachokuchukizeni semeni “ewe mola wetu tunakuomba kheri katika huu upepo na kheri iliyopo na kheri uliyoamrisha na tunajikinga katika huu upepo na kheri iliyopo na shari uliyoamrisha.

Ameisahihisha tirimizuyu.

- Kutukana upepo ni katika upambanuzi ambao umetanguliwa katika kutukana mwaka ametofautisha mtunzi hapa kwa wingi wa kutokea. Yamepokelewa makatazo ya kulaani na kutukana kiujumla. Amesema mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake “si muuni mwenye kulaani wala mlaaniwa wala mfanya maovu na akasema mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake: “ haiwi kwa wanaolaani uombezi wa ushahidi siku ya mwisho”
- Katika kutukana uislamu: amesema mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yak: kumtukana muislamu ni uovu na kumuuwa ni ukafiri.
- Katika kuwatukana mauti amesema mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake “msiwatukane mauti, hakika wao huenda yakawa mbora yale yaliotangulia.
- Katika kutukana wanyama: amesema mjumbe wa Allah rehema na amani ziwe juu yake “msitukane homa”

MAS-ALA.MBALI MBALI

Moja: Katazo juu ya kutukana upepo “uharamu kwa sababu anaemtukana Yule ambae ameumba na ameutuma.

Mbili: Muongozo katika mamneo yenyekufaa pindi atakapoona mwanadamu upepo anauchukia “kwa kusema “ewe mola wetu tunakuomba ……..” na afanye sababu za kuhisia kama vile kujikinga na shari zake kwa ukuta.

Tatu: muongozo wa kuwa ni wenye kuamrishwa.

Nne: hakika hutumwa kwa kheri au hutumwa kwa shari “yanayotokea hakika kuna kheri au kutumwa kwa shari yanayotokea”. Hakika kuna ulazima juu ya mwanadamu asije akapiga juu ya hukumu za Allah na khadari zake na wala asimtukane na awe ni mwenye kumnyenyekea kwa amri za ulimwengu kama ulazima wa kumnyenyekea kwa amri za ulimwengu kama ulazima wa kunyenyekea amri za kisheria, kwa sababu hivi ni viumbe haviwezi kufanya chochote isipokuwa kwa amri ya Allah.

(59) **HUU NI MLANGO UNAOFAFANUA KAULI YA ALLAH** ***" Na wakamdhania Allah dhanna isiyokuwa ya haki , dhana ya kijinga wakasema : Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili ? sema mambo yote ni ya Allah ."***

(Wakamdhania Allah) "Wanafiki" dhana ya mila ya kijahili ambayo mwenye dhana hajui heshima ya Allah na utukufu wake basi hiyo ni dhana mbaya iliyojengwa kwenye ujinga. Na kumdhania Allah kuko namna mbili:-

[1] Kumdhania vizuri Allah nako kuna viambata viwili;

a) Kiambata kinachofungamana na matendo anayoyafanya Allah kwenye huu ulimwengu, Ni lazima kwenye kiambata hiki umdhanie Allah dhana nzuri

b) Kiambata chenye kufungamana na matendo anayokutendea Allah (wewe binafsi), Ni lazima kwenye kiambata hiki umdhanie Allah dhana nzuri zaidi, kwa sharti uwe nayo mambo yenye kuwajibisha dhana nzuri – nayo ni Ikhlasi (kumtakasia Allah nia njema) na Ufuasi (Kumfuata mtume kwenye ibada zote)

[2] Kumdhania Allah dhana mbaya, mfano mtu kumdhania kwenye utendaji wa Allah kuna upumbavu au dhulma au mfano wa hayo, kwa sababu dhana hizo ni katika maharamisho makubwa sana na ni miongoni mwa madhambi mabaya mno, kama walivyomdhania Allah wanafiki na wengine dhana isiyokuwa ya haki.

DALILI YA PILI.

Na kauli ya Allah: Wanaomdhania Allah dhana mbaya, utawafikia mgeuko mbaya makusudio ya hao wenye dhana mbaya ni wanafiki na washirikina ubaya umeporomosha matendo yao yote.

Ibnu Qayyim amesema kufafanua aya ya kwanza "Dhana hii imetafsiriwa kuwa Allah Subhanahu wataala hatomnusuru mtume wake, na dini yake itafutika tu, na ikatafsiriwa kuwa yote yaliyompata hayakuwa kwenye mipango (Qadar) ya Allah na hekima zake ikatafsiriwa huko ni kuipinga hekima na Qadar za Allah, na kupinga Allah kulitimiza jambo la mtume wake (dini) na kuipa ushindi dini hiyo dhidi ya dini zote nah ii ndio dhana mbaya ambayo ndio walio idhania wanafiki na washirikina iliyoelezwa kwenye suratul fat-h.

Na bila shaka dhana hii imeluwa mbaya kwa sababu ni dhana isiyostahiki kudhaniwa kwa Allah na wala haistahiki pia kwenye hekima zake, sifa na ahadi zake zilizo kweli. Basi atakae dhania Allah ataipa ushindi batili iishinde haki ushindi wa daima utakaozifuta kabisa haki (itoweke), au akapinga kuwa yake yaliyotokea (katika vita Uhud) hayakutokana na hukumu ya Allah na mipango yake, au akapinga kuwa Allah hakuyapanga hayo kwa hekima yake iliyotukuka na anastahiki kwayo sifa na shukrani, bali alidai tu kuwa hayo yametokea kwa matakwa tu yalivyo, basi hizo ndio dhana walizodhania makafiri.

Ole wao waliokufuru kwa moto utaowapata, wengi katika watu wanamdhania Allah dhana mbaya kwa yale yanayowakuta. Na kwa yale aliyoyafanya kwa wenzao na hatosalimika kwa hili isipokuwa aliyemjua Allah kwa majina yake na sifa zake na kila linalowajibisha hekima zake na utukufu wake, kila mwenye akili mwenye kuitakia kheri nafsi yake ashulikie hili amuombe msamaha Allah katika dhana mbaya kwa mola wake. Na laiti angemkagua yeyote atakae mchagua utaona kwake kuna Allah kupata tabu juu ya Qadari ya tawama zake kwenye Qadar na atasema hakika inatakiwa liwe hivi na hivi, amesimama na mwenye wingi na aiangalie nafsi yake je wewe ni salama? Ikiwa hutofaulu utafaulu kwa uwezo na utukufu wa Allah ….. kinyume na hivo hauna msimamo wenye kutuliza.

- Haya maneno aliyataja ibn Khaymu (radhi za Allah ziwe juu yake) katika "zadul- maadi" baada ya kuelezea vita vya uhudi chini ya kutafiti hekima na malengo mazuri ambayo yalikuwa ndani ya vita hivyo. Akafundisha katika kutaja dhana mbaya.

  Na huu ni ufupi wa maelezo aliyoyatoa kuhusi dhana mbaya (kwa Allah)

1. Kumdhania Allah anaweza kumpa nguvu batili juu ya haki, nguvu ya kipekee itayoitoweza haki
2. kuchukia yote yaliyotokea kwa hukmu ya Allah na qadari zake vipi yanatokea katika miliki yake mambo ambayo hataki.
3. Kupinga kuwa qadari za Allah huja kwa hekma kubwa ambazo zinastahiki kushukuriwa.

- Ufupisho wa maelezo aliyotaja katika kutibu dhana mbaya:

1. Kuyajua majina ya Allah na sifa zake. Kujua kwa haki si kujua kwa kuharibu majina hayo na kuyageuza.
2. Ashughulikie hili mwenye akili timamu ili amdhanie Allah dhana ya haki si dhana mbaya wala dhana ya wajinga.
3. Kurejea kwa Allah kwa kutubu katika maasi hadi kutii na kuomba msamaha.
4. Kudhania nafsi yako dhana mbaya basi mwanadamu ni mwenye hali ya upungufu na muovu wa dhana.

MAMBO YANAYO AMBATANA NA MLANGO HUU.

Jambo la kwanza: Tafsiri ya aya ya al-imran " wakamdhania Mwenyezimungu dhana isiyo kuwa ya haki" na dhamiri inarudi kwa wanafiki"

Jambo la pili: Tafsiri aya ya suratul-fathi "Wanaomdhania Mwenyezimungu dhana mbaya dhamiri inarudi kwa wanafiki

Jambo la Tatu: Habari kuwa aina ambazo hazitokea na kudhibiti atakae mdhania Allah ambayo hayaendani naye.

Jambo la Nne: Hakika hatasalimika kwa hili (dhana mbaya) isipokuwa kwa mwenye kujua majina ya Allah na sifa zake na kuijua nafsi yake " na hakika wa wa kuwa mwanadamu ni mwenye mapungufu na muovu ama mja aliyetukuka hana mapungufu na katika ukamilifu wake moja kwa moja ambayo wanampelekea katika upungufu kwa uwezo na uwepo wake.

(60) MLANGO ULIOKUJA KUELEZEA WENYE KUPINGA QADARI "NI MIONGONI MWA KUFRU KUBWA"

- QADARI: Ni siri ya Allah kwa viumbe wake wala hatuijui isipokuwa baada ya kutokea na inahusiana hasa hasa uumbaji na tawhid na Tawhidi ya majina na sifa za Allah watu katika kuamini Qadari wamegawanyika katika makundi matatu

1. Kundi la JABRIA. Hawa walithibitisha Qadari na wakachupa mipaka ndani yake na mpaka wakamuondoshea mtu sifa ya kua na uwezo na kufanya maamuzi wakasema: mwanadamu hana uamuzi wala uwezo
2. Kundi la QADARIA MUUTAZILA: Hawa walithibitisha kwa mja kuwa na khiari na uwezo katika matendo yake, na wakachupa mipaka katika swala hilo mpaka wakakanusha ya kwamba Allah hana matakwa katika matendo ya mja wala uumbaji.
3. Kundi la tatu ni AHLU NA SUNNA WAL-JAMAA, Walizikusanya dalili zote na wakapata katika njia yao ambayo ndio dini bora wakaamini aliyohukumu za Allah na Qadar zake na wakathibitisha kwamba mja anamatakwa yaliyofungwa kwenye matakwa ya Allah

KATIKA KUAMINI ALIYOYAHUKUMU ALLAH NA QADARI ZAKE KUNA FAIDA NYINGI. MIONGONI MWAZO;

- Ni moja katika ukamilifu wa tawhidi ya malezi (uumbaji)
- Ya kwamba imani hiyo inawajibisha ukweli wa kutegemea Allah
- Hakika huleta utulivu katika moyo utulivu, unapotambua kwamba kilichokupata hakikuwa ni chenye kukukosa na kilichokukosa hakikuwa ni chenye kukupata, utapata utulivu kwa yalio kusibu, baada ya kuwa umefanya matendo yenye kunufaisha
- Inamzuwiya mtu kujiona kwa amali azifanyazo, pale afanyapo matendo mazuri yenye kushukuriwa, kwani Allah ndiye aliye mneemesha kufanya hivyo.
- Hatahuzunika kwa yaliyomsibu, kwakuwa yanatoka kwa mola wake azza wa jala. Yametoka kwa rehema na hekima zake.
- Mwanadamu anatakiwa kufanya sababu mbalimbali kwani yeye huamini hekima za Allah, hakika Allah hakadirii mambo isipokuwa huyafungamanisha na sababu zake.

DALILI YA KWANZA.

Amesema Ibn Omari. Namuapia yule ambaye nafsi ya Ibn Omari ipo mikononi mwake. Lau mmoja wao alikuwa na dhahabu mfano wa mlima wa Uhud. Kisha akaitoa katika njia ya Allah. Allah asingeikubali mpaka aiamini qadari. Kisha akatoa dalili kwa mtume (swalallahu aleiyhi wasalam): (Imani ni kumuamini Allah na malaika wake na vitabu vyake na mitume wake na siku ya mwisho na kuamini qadari kehri na shari yake

(kaipokea muslim)

Imani: ni kusema kwa ulimi na kuitakidi kwa moyo na kufanya kazi kwa viungo na nguzo. Inazidi kufanya utiifu na inapungua kwa kufanya maasi na ina nguzo sita

- Kumuamini Allah
- Kuamini malaika
- Kuamini vitabu vyake
- Kuamini mitume wake
- Kuamini siku ya mwisho
- Kuamini qadari, kheri yake na shari

"Kumuamini Allah": Kuna lazimisha uamini mambo manne

- Kuamini uwepo wa Allah anakuwa kwa
  - Akili: huingia akilini kuwepo viumbe bila ya muumbaji (au wao wameumbwa pasipo kutokana na kitu chochote au ni wao ndio waumbaji.
- Tawhid ya malezi
  - Hisia: Mnaweza mkawa katika tatizo na shida kisha unamuomba Allah unakuta hiyo shida inaondoka kwa kumuomba Allah kama alivyoomba mtu (rehema na amani ziwe juu yake) Vita vya uhudi
- Tawhid ya ibada
  - Kwa maumbile: Amesema mtume (rehema na Amani ziwe juu yake) kila mtoto huzaliwa katika maumbile ya kumtambua Allah, hivyo wazazi wake wanampeleka katika dini ya myahudi unaswara
- Tawhid ya majina ya Allah
  - Kisheria: ametaja ibn Qaym Allah amrehemu ya kwamba hakuna aya yoyote katika kitabu cha Allah isipokuwa ndani yake kuna dalili ya kumpwesha Allah.

- (Na malaika wake) wao ni ulimwengu uliofichikana Allah amewaumba kwa nuru, wanamtii Allah wala hawamuasi, wao mwana roho (roho ya utakatifu) wana wiwiliwili (aliyewafanya malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbilimbili na tatu tatu nan ne nne. Huzidisha katika kuumba apendavyo) wao wana akili na mioyo (hata atapo ondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: mola wenu mlezi kasema nini) tunawaamini wao, na wale aliotufahamisha Allah majina yao mfano (jibril, mikaili na israfil) na sifa zao (hawamuasi Allah kwa anayowaamrisha na wanatenda wanayoamrishwa) na kazi zao, mfano; (wenye kubeba arshi ya Allah) kwa habari zilizokuja kuwaeleza.
- Na vitabu vyake) Inapaswa tumuamini kuwa hayo ni maneno ya Allah, hakika au kiuhalisia sio kama jazi, na hakika hayo ni maneno yameteremshwa hayakuumbwa na hakika Allah ameteremshia kila mtume kitabu kwa maana tuviamini na vile vilivyotuelezea Allah na miongoni mwa vitabu hivyo na habari zake

Na hukumu zake moja moja au kwa ujumla, muda wa kuwa hazikufutwa na tunaamini hakika ya Qur'an imefuta vitabu vyote vya kabla yake nayo ni Taurat, Injili, Zaburi, wahifa ya Ibrahimu na Mussa (s.a)

- "Mtume wake": lazima tuamini wao ni wanadamu hawana chochote katika mambo makhsusi tofauti katika ya uungu hakika wao ni waja tu sio waabudiwa. Hakika ya Allah amewatuma na amewapa ufunuo na amewapa nguvu za miujiza hakika wao wamefikisha amana na wameunasihi umma na wamefikisha ujumbe wamepigania dini ya Allah ukweli wa kuipigania tunawaamini wao, na yote aliyotueleza Allah katika majina yao na sifa zao na habari zao na wa kwanza wao katika manabii ni Adamu na wa kwanza katika mitume ni Nuhu na wa mwisho katika manabii na mitume ni Muhammad (swalalahu alayhi wasalam) na sheria zilizotagulia zote zimefutwa kwa kuja sheria ya Muhammad (swallalahu alayhi wasalam) na walio bora ni watano waliotajwa katika sura ya shuura na Ahzabi " Muhammad, Nuhu, Ibrahimu, Mussa, Issa.
- " na siku ya mwisho: inafungamana na kuamini kila alichokielezaNabii Muhammad (swallalahu aleiyhi wasalam) yanayotokea baada ya kufa, mfano; adhabu za kaburini, pulizo la kwanza na kufufuliwa watu kwenye makaburi yao na mizani za matendo na vitabu vya amali na haudhi na shafaa na pepo na moto na waumini thimuo na mola wao siku ya kiyama na peponi na mengineyo katika mambo yaliyo jificha.
- "na kuamini qadari" amerudia kitendo "tunaamini" kwa sababu imani ya qadari ni muhimu na ina daraja nne: elimu na kuandika mola wetu na matakwa yake**** na kuumba (nako ni kukiumba kiumbe na kukifanya kuishi).

Elimu: kuamini hakika ya Allah (subhanahu wataala) amejua kila kitu yote na mkusanyo dalili kauli yake Allah (subhanahu wataala) yeye anajua yalio mbele yao na yalio nyuma yao.	Kitabu: kuamini ya kuwa Allah ameandika qadari kila kitu hadi kusimama kiyama. Dalili: "na hakuna siri katika mbingu na ardhi ila imo katika kitabu kinachobainisha"	Matakwa: kuamini ya kuwa Allah akitaka linakuwa na asilotaka haiwezi kuwa hakika ya mja anamatakwa ya ndani chini ya matakwa ya Allah wala hawezi kutaka ila atakapo taka Mwenyezimungu.	Muumba: hakuna kitu isipokuwa ameumba Allah na analiendesha na ni mfalme hadi akafanya viumbe ni viumbe "na hali Mwenyezimungu ndiye aliye kuumbeni nyinyi na hivyo mnavyovifanya"

DALILI YA PILI MPAKA YA NNE

2. Kutoka kwa Ubada mtoto wa swaamit; amesema kumwambia mtoto wake: ewe mtoto wangu hutapata ladha ya Imani mpaka utambue kilicho kusibu hakikuwa chenye kukukosa na kilicho kukosa hakikukadiriwa kukupata (kukufikia) nimemsikia mtume (swalallahu aleiyhi wasalam) akisema "kitu cha kwanza alichoumba Allah ni kalamu akasema kuiambia kalam: andika na ikasema kalamu kumjibu Allah niandike kitu gani? Akasema Allah kuiambia kalamu: andika makadirio ya kila kitu mpaka kisimame kiyama. Ewe mtoto wangu je umemsikia mtume wa Allah(subhanahu wataala) akisema: mwenye kufa pasina kuamini hili jambo hatokuwa pamoja nami. na katika mapokezi ya hadithi tofauti kutoka kwa Ahmad: hakika kitu cha kwanza alichoumba Allah ni kalamu na akasema Allah kuiambia kalamu: andika andika kila kitu kinachotokea na kufanyika duniani mpaka kusimama kiyama.
3. Na katika mapokezi tofauti katika hadithi ya Ibn Wahabi anasema: Rasulullah (subhanahu wataala) "kwa mtu asie amini qadari na kheri zake na sharia zake Allah atamchoma moto.
4. Katika musnad na sunami kuna hadithi kutoka kwa mtoto wa dailami, akasema: nimemuijia (nimemfata ubaya mtoto wa kaab) na nikasema: katika nafsi yangu kuna kitu kuhusu qadari basi nielezee, na kitu huenda Allah ataniondolea shaka katika moyo wangu, na akasema hata ungetoa zaka mfano wa mlima wa uhud. Allah hata kubali mpaka uamini qadari na utambue kuwa kila kilicho kukuta hakijawa cha kupia(yaani kukosea kukupata) na kilicho kukosa hakikuwa ni cha kukupata na ukifa bila kuamini qadari jambo hilo utaingizwa motoni. Akasema: nikamfuta Abdullah mtoto wa masudi na Khudhaifa mtoto wa yaman na zaid mtoto wa Thabit na wote amenielezea mfano wa hayo pia mtume wa Allah amenielezea tena katika hadithi iliyo sahihi imepokelewa na Hakim katika hadithi sahihi.

- Mpaka utambue: na ameashiria Allah mpaka kwenye maana hiyo katika kauli yake.
  "hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu kabla hatuja uumba hakika hayo kwa Allah ni mepesi (22)
  Ili msihuzunike kwa kilicho kupoteeni wala msijitape kwa alicho wapatieni na Allah hampendi kila anae jivuna na akajifaharisha (23) – suratul-hadid (23)
- Ewe mtoto wangu: katika kuwaongelesha watoto kwa huruma kupitia mawaidha. Na wao wanafaa wawatamkishe watoto wa maneno wenyewe wanawafunza kwa hokum na dalili za vitabu: (1) kuwezesha watoto wa kufata dalili za vitabu vya Allah (2) na kuwalea na kuwafunza kwa mapenzi na kumpenda mtume (swalallahu aleiyhi wasalam)
- "Katika nafsi kuna kitu": na haikutokea kwenye nafsi yangu ubabaifu wa dalili na shaka juu ya qadari ya kukaa katika makazi ya watu wa bidaa ambao wanazusha kitu kwenye dini watu ambao wanakuwa na shaka katika jambo la qadar na kutia shubha yaani dosari basi yote hayo yanaondolewa endapo ukiingiza dalili inaondosha yote na shaka ziliyopo wala haitolewi kwa kutumia akili isipokuwa aliki inazidisha upotevu.
- Kalamu: kuna mapokezi mawili (aina mbili) ambayo inakuwa katika haraka ya dhama na fatha.

1. Kuweka haraka ya dhama: inakuwa kwasababu ya 1 ya kitu alichokiumba Allah ni kalamu ndio ya kwanza kuumbwa kwa sababuj imetengenezwa kwa kila tunachokiona katika viumbe alivyo viumba kama alivyoumba mbingu 7 na ardhi 7 ni vitu vya kwanza vilivyotengenezwa kuwa vyenyewe ndio vya kwanza kuumbwa. Anasema Ibn Qayim Rehema za Allah ziwe nae.

Shairi lake.

1. Na watu wanatofautiana katika kalamu ambayo imeandika qadhaa zake katika madeni.
2. Je hiyo kalamu ilikuwepo kabla ya arshi au baada ya kuumbwa arshi. Kauli mbili kutoka kwa Abdul-gh'alaal-hamathaini:
3. Na ukweli ni kuwa hiyo arshi ni ya kitambo kabla ya kalamu kwa sababu hiyo arshi kabla ya kuumbwa kila kitu yenyewe ilikuwa ni nguzo ya kwanza.

Yaliyomo.

1. Kubainisha ulazima wa kuamini na kuwa na Imani na qadari (makadirio)
2. Kuharibu matendo mema kwa yule asiyemuam
3. Kubainisha jinsi gani inakuwa hiyo Imani (Imani ya kuamini makadirio ya Allah kwa sababu tunaamini mipangilio yake minne)
4. ini Allah (basi atakuwa kafiri)
5. Utajo wa kwanza aliyo uumba Allah (hakuna sha kua uumbaji wa kalamu ni baada ya uumbaji wa arshi, hiyo kalamu ni kitu cha kwanza ambacho kimeumbwa kunasibisha au kupatikana hivi tunavyo viona nayo kalamu imeumbwa ya kwanza kabla ya uumbaji wa mbingu na ardhi, navyo vinakuwa ni vitu vya kwanza kutengenezwa na kunasibishwa)
6. Na yenyewe kalamu inapitia na kupita kuandika kila kadirio lililokadiriwa katika mda huo mpaka kusimama kiyama,yenyewe inaandika kila kitu (na kuna kuelekeza mazungumzo ya Allah, kuongelesha vitu vikavu ambavyo haviongei (vimekauka) na wao w anatumia akili na wanakuwa na akili ya kutambua maamrisho ya Allah kawa sababu Allah ameeleza mazungumzo kwa kalamu na hio kalamu haina roho isipokuwa ikamuelewa Allah na ikatekeleza
7. Mtume wa Allah kujiweka mbali na watu wasio na Imani ya Qadar (na huyo asieamini anakuwa ni kafiri aliyetoka katika mila ya kiislamu)
8. Mambo wanayoyafanya watu wa salafi mambo ambayo ni kawaida kwao katika kuondosha shubha yani shaka zinazopatikana kwa kuwauliza maulamaa (watu wenye elimu) (na mambo yanayo faa katika maswali waliyouliza maulamaa pia ikawa majibu yalotolewa ni bora saana kwa mtu mwenye elimu kuthibiti pasina kufatana hiyo ni rukhswa)
9. Pia maulamaa walijibu vitu ambavyo vinaondosha shubha na vile vile imenasibiana na kalamu mpaka kwa mtume Muhammah (swalallahu aleiyhi wasalam) basi (na hiyo ndio inaondosha shubha yaani kushuku) inaondosha shubha yote kwa watu wenye imani. Wala haikatazi ije kwa dalili ya kutumia akili au kutumia hisia kwa sababu ya kukinaisha kuondosha ugonvi na malumbano na kutulia na kupata makubaliano. Na kuna dalili ya 4 nayo ni dalili ya kimaumbile.)

(61) MLANGO ULIOKUJA KUELEZEA JUU YA WENYE KUCHONGA MASANAMU

1. Katika kutengeneza picha kama kiumbe cha Allah na kuanza kutengeneza picha na kumshirikisha Allah katika uumbaji wake
2. Kitu cha kwanza ni shirki ambayo imeanza ardhini katika "qaumu" watu wa Nuhu ilikuwa ni sababu na kuchonga na kutengeneza picha na masanamu

DALILI YA KWANZA HADI YA TANO

1. Kutoka kwa Abu Hureirah radhi za Allah ziwe juu yake amesema: amesema mtume wa Allah (subhanahu wataala) amesema Allah aliyetukuka: na yule ambaye amepotea ni yule ambaye ameelekea kuumba kama uumbaji wa Allah. Basiu aumbe chembe au aumbe mbegu au aumbe ngano.
2. Na imepokewa na Aisha radhi za Allah ziwe juu yake anasema mtume wa Allah (subhanahu wataala) watu wenye wataadhibiwa adhabu kali siku ya qiyama: wale ambao wanafananisha kama alivyoumba Allah.
3. Na imepokelewa na mtoto wa Abas: nimemsikia mtume (swalallahu aleiyhi wasalam) akisema: kila mwenye kuchonga sanam ataingia motoni: akawekewa kila picha aliyotengeneza awekee roho asipo muwekea basi ataadhibiwa katika moto wa jahanam.
4. Na imepokelewa pia ni hadithi sahihi: "mwenye kuchora picha duniani atalazimishwa aipulizie roho wala hatoweza kuipulizia"
5. Kutoka kwa muslim imepokelewa na baba halaja amesema: "je nikuagize alipo agizwa mtume Muhammad (swalallahu aleiyhi wasalam)? Usitengeneze sanam lolote isipokuwa uwe na uwezo wa kuliwekea roho, wala kaburi la kafiri kuliweka sawa na kulisawazisha.

- Adhabu za kutengeneza picha (sanam): (1) Wao ni watu ambao wataadhibiwa adhabu kali na adhabu yao ni kali sana (2) Wao wamelaaniwa na Allah (3) atawekea kila sanam roho kisha atawaadhibu wailoyatengeneza motoni (4) wao wataingia motoni (5) Atalazimishwa aiwekee roho atashindwa na ataingizwa motoni (6) Hakuna mtu aliyepita katika huu mlango au anaingia katika kipindi cha dhulma.
- Kuishika na kuiwekea na kuipulizia: ikiwa ina rangi nyingi kwa kuweka rangi nyinginewe basi ataondosha kufahamika kwake. Na ikiwa ni sanam basi litakatwa kichwa chake na ikiwa imefufuliwa basi atafufuliwa kwa muonekano wake mpaka isibainike alama yake wala isifahamike na kupuliziwa inatofautiana na muonekano wa vitu vyote alivyokuwa anaabudu pasina allah au tofauti na hivyo.
- Kiongozi: au iliyoko juu (aliyo sawasawa) ina maana mbili.

- Nimeifanya kuwa nzuri juu ya kutokupingana na sharia
- Nimeiweka sawa na kilicho pembeni yake na kaburi

Vigawanyo vya: …….

1. Kutukuza sanam: basi hiyo ni haram kwa kila shari kwasababu na utukufu wa kutukuza saanam zao wangeingiza katika uumbaji na kutukuza kinyume cha ibada cha kutengeneza sanam lao basi hiyo ikwa naingia katika upande wa ulezi.
2. Kustarehe: kwa mtizamo wa kuangalia kwake au kwa kupata ladha kupitia hiyo basi hiyo ni haramu kwa yanayo patikana katika fitina.
3. Kwa mpole na mwenye utulivu: kama ile amabyo wanatengeneza sanam ndogo za watoto wao, basi hiyo ni haram.
4. Na kina haki kwa kilicho timia: kama kutengeneza sanam ambazo zinapatikana kwenye pesa au kitambulisho cha mtu basi hiyo haina dhambi ndani yake, kwa sababu haiwezekani kuziondosha katika hizo sehemu.
